Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 24 Juni 2010**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**KAIMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako naomba kuwasilisha Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**NAIBU SPIKA:** Kiongozi wa Kambi ya Upinzani simwoni, halafu nadhani Waziri Mkuu ameshinda sana maana sasa hata maswali kwake hakuna. Kwa hiyo, kuna maswali matatu tu kutoka chama kimoja hata Kiongozi wa Upinzani hayupo. Kwa hiyo, tunaendelea na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuna maswali matatu kutoka kwa Wabunge watatu.

Kwanza kabisa namwita Mheshimiwa Godfrey W. Zambi !

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi karibuni na zaidi siku ya jana tarehe 23 Juni, 2010 nimepata simu nyingi sana kutoka Mbozi. Wafanyabiashara wa maduka ya madawa wamelalamika sana kwamba wananyanyaswa kwa sababu wameambiwa sasa wafunge maduka yao kama yamekaribiana na sharti linalotolewa ni kwamba kuwe na umbali wa mita 300 kutoka duka moja hadi jingine. Sasa mimi nashangaa ni sheria gani hii ya ubaguzi ambayo inamlazimisha mfanyabishara wa duka la dawa asifungue biashara pale anapotaka ila afungue pale tu ambapo mamlaka inayostahili inataka. Nataka ufafanuzi wa Serikali kwa sababu hii imeonyesha kama kuna ubaguzi mkubwa sana.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabla sijamjibu ndugu yangu Godfrey W. Zambi, niwashukuru sana Wabunge, muendelee na kasi hii mpungue zaidi maana mnanipunguzia *pressure* mimi. Lakini hiyo ni ishara vilevile watu wa Rukwa wakati mwingine tukifanya vitu vyetu mambo si mabaya sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya ndiyo kwanza napata taarifa hii na bahati mbaya hapa katikati sikusaidiwa sana kwenye vyombo vya habari ili niweze kujua ni nini kinaendelea, mambo yalikuwa mengi!

Lakini kwa upande mmoja nataka niamini kwamba jambo hilo litakuwa limetokana pengine na taratibu zilizopo kuhusiana na masuala haya ya maduka ya dawa za binadamu, ni kama ilivyo tu kwa vituo vya mafuta, vituo vya mafuta navyo vina utaratibu kama huo ili kuweza kufanya pengine shughuli zifanyike vizuri zaidi.

Lakini linalonipa tatizo ni kwa kuwa hawa watu tayari walikwishaweka maduka hayo, kwa hiyo, kama kweli Serikali tungetaka kufanya kazi yetu iwe makini wakati wa kutoa leseni ndiyo tulitakiwa tufanye vilevile zoezi la kuhakiki na kuona duka hili liko

umbali gani kutoka duka lingine badala ya kungoja watu wameshaweka miundombinu tayari wanauza dawa baadaye tena mnakurupuka mnaanza kupambana na watu katika mazingira ambayo kusema kweli hayana tija sana.

Lakini Mheshimiwa Zambi nataka nikuahidi kwa sababu Waziri wa Afya yuko hapa tutalishughulikia jambo hili mapema na mimi nataka niwasihi sana ambao waliamua kufanya hivi wasubiri kwanza kidogo tuelewane nini hasa kimetokea kwa sababu ni mara ya kwanza tunasikia utaratibu kama huo unajitokeza. (*Makofi*)

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu yake.

Lakini kwa sababu pale Mbozi pia pamekuwa na malalamiko hasa miji ya Vwawa na Mloo na Mkoa wa Mbeya lilitokea hili kwamba wafanyabiashara wa kawaida ndiyo wanaokumbwa zaidi na msukosuko huu kuliko wafanyabiashara wenyewe ambao wako kwenye Sekta ya Afya kwa maana ya Madaktari na wengine wanaofanana nao.

Je, sasa utaagiza Mamlaka ya Mkoa wa Mbeya na Wilaya ya Mbozi kwa ujumla ili wahakikishe kwamba taratibu zinazingatiwa na ubaguzi hautokei katika suala hili?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kama nilivyosema Mheshimiwa Godfrey Zambi tupe nafasi tulifanyie kazi jambo hili, hata hilo unalolisema inawezekana lipo kwa sababu hatuwezi kukataa haraka haraka kabla hatujafanya uchunguzi. *(Makofi)*

Tukishabaini mambo yalivyo nadhani tutatoa maelekezo haraka sana ili kuweza kurekebisha kasoro ambayo inaweza kuwa imejitokeza na hiyo itawahusu hata Wataalamu wale wa eneo hili la Madaktari na watu wengine ambao wanahusika na jambo hili. *(Makofi)*

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kumwuliza Waziri Mkuu swali moja.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ya Kilombero ina eneo takribani la kilomita za mraba 15,000, lina watu wasiopungua 363,000, kutoka mwanzo wa Wilaya mpaka mwisho ni kilomita 300, lina kata 23, lina tarafa 5, vijiji 90, vitongoji 366.

Sasa ni kigezo kipi hasa tunachokosa sisi wana Kilombero kugawa hili jimbo au Wilaya hasa ukichukulia kwamba hii idadi ya watu 363,333 ni kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002.

Lakini kati ya 2002 na leo hii 2010 kuna watu wengi wameingia katika Wilaya ile takribani wanafika karibu 100,000 nzima kwa hiyo, watu kwa idadi tunaweza tukafikia lake nne na kitu.

Sasa jimbo hili hasa na sehemu uliyofika Mheshimiwa Waziri Mkuu pale kwenye Bonde la Kihansi ni nusu tu.

**NAIBU SPIKA:** Swali bwana!

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Ni kigezo kipi kilichofanywa katika kugawa Wilaya na Wilaya hii isigawanywe?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, anachokisema Mheshimiwa Castor R. Ligallama, kuhusiana na eneo au Jimbo lake ni kweli, ni Jimbo kubwa bahati nzuri mara ya mwisho nilitembelea kule niliona hali halisi.

Lakini kwa upande mmoja Mheshimiwa Mbunge, Serikali katika suala la ugawaji wa maeneo mapya kinachotokea kwanza ni maombi kutoka kwa wahusika wenyewe wanaoona kwamba iko haja ya kugawa eneo katika maeneo ama Jimbo ama Wilaya.

Sina hakika kwa upande wa Kilombero kama maombi haya yaliwasilishwa au hapana. Lakini kwa kawaida yaanzia huko, yanapita kwenye kikao chenu cha RCC, baadaye yanakuja huku kwa ajili ya kuona kama kuna vigezo vimezingatiwa au hapana.

Sasa vigezo kwa upande wa Wilaya ni vingi kidogo lakini mambo makubwa hasa huwa kwanza, ni ukubwa wa eneo, eneo ambalo tunadhani Mkuu wa Wilaya anaweza akaliongoza bila matatizo makubwa sana ni kilomita za mraba zisizozidi 5000.

Lakini ni idadi ya watu, Mkuu wa Wilaya ili aweze kutimiza wajibu wake vizuri ni vizuri idadi ya watu ikawa kati ya 200,000 – 250,000 katika eneo ambalo analiongoza, inaweza ikawa chini kidogo au kuzidi kidogo lakini iwe katika eneo hilo la wingi wa watu.

Kwa hiyo, kama eneo lako unataka ligawiwe mara mbili tutakachoangalia kwanza ni ukubwa lakini tutaangalia je tukiligawa mara mbili upande mmoja utakuwa na idadi ya watu wangapi na upande mwingine utakuwa na watu wangapi.

Lakini *formula* hiyo siyo kwamba ikishasemwa basi muda wote inafuatwa, hapana! sehemu nyingine tunakuwa kidogo *flexible* au tunakuwa laini kidogo kwa kuzingatia pengine hali ya jiografia ya eneo lilivyo maana maeneo mengine ni visiwa, maeneo mengine yanaweza yakawa na utata mkubwa sana kama milima na kadhalika, wakati mwingine Serikali inakubali jambo hili kutokana na uhalisia wa eneo lenyewe lilivyo.

Kwa hiyo, kwa kweli Mheshimiwa Castor Ligallama ni kwa sababu sina uhakika na maombi yenu kama yaliletwa au hapana, lakini tunaweza tukaangalia na Mheshimiwa Celina Kombani tuone kama yaliletwa tukueleze kwa nini yalikataliwa. (*Makofi*)

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, labda kwa kusaidia tu nijibu swali la Mheshimiwa Waziri Mkuu, maombi yetu tulileta.

**WAZIRI MKUU:** Basi ni vizuri, kama ulileta basi tutaangalia tuone sababu zake. Lakini huenda idadi ya watu pengine kwa upande wako pengine ndiyo kasoro moja kubwa maana kama ni laki tatu unataka kugawa mara mbili maana yake utakuwa na watu laki moja hivi, sasa lazima kuwe na sababu nyingine za ziada za kufanya Serikali ikubali. Lakini tutaliangalia na baadaye tutakupa majibu.

**MHE. COL. SALEH ALI FARRAH**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Lakini na mimi nina swali moja ambalo ilikuwa linanitatiza kila siku.

Suala lenyewe hasa ni neno kero, hili neno kero limekwenda au maana yake hasa ni jambo ambalo mtu analitegemea liweze kumwendeshea maisha yake au limsaidie lakini halipatikani kama lilivyo na ndiyo maana likaja moja kwa moja mpaka kwenye kero za Muungano.

Sasa mimi nataka niulize hivi, Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika masuala mazima ya kero za Muungano umechaguliwa uongozi wa juu, wewe pamoja wengine akiwamo Waziri Kiongozi mnakaa kitako na kuzungumzia kero, lakini zilizotoka kwa wananchi na wananchi wenyewe wawakilishi wake ni sisi Wabunge na Wawakilishi wa Zanzibar au Wabunge kwa upande wa Tanzania Bara.

Sasa swali langu, wakati kikao kile kinakaa kwa nini Wawakilishi na Wabunge hawashirikishwi katika masuala ya wananchi wao na hawa Wabunge na Wawakilishi ndiyo wawakilishi halali waliochaguliwa? Wanakaa tu pamoja na *technocrats* Viongozi wengine wa Kiserikali? Ahsante sana.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijaribu kutoa maelezo kidogo kwa Mheshimiwa Col. Saleh Ali Farrah kuhusiana na suala hili la kero za Muungano.

Hoja yake ni kwamba ni kwa nini basi Wabunge au Wawakilishi wasiwe ni sehemu ya vikao vyetu ambavyo tunavifanya ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni uamuzi uliofanywa kwa nia njema kabisa kujaribu kuona kwa sababu mambo mengi mmekwisha elekeza kupitia Bunge, kazi iliyobaki ni kwa Serikali zote mbili kuendelea kuzungumza na kuyapatia ufumbuzi. Sasa kama mnataka na ninyi muwe ni sehemu ya majadiliano hayo ni jambo ambalo linazungumzika na mimi sioni kwamba kuna tatizo kubwa kwa sababu mazungumzo yale ni ya kawaida wala hayana usiri wowote kama ikibidi kualikwa mnaweza kualikwa kuja kusikiliza ni kitu gani kinaendelea.

Lakini nadhani hapa ni kwa sababu jukumu mliloipa Serikali ni kuzungumzia masuala haya na kujaribu kuyapatia ufumbuzi.

Pengine jambo la msingi ambalo nadhani Col. Saleh Ali Farrah, ungeweza ukaomba na sisi tukakubali haraka ni kwamba basi angalau Serikali hapo mlipokwisha kufika leteni taarifa humu Bungeni tuweze kuona mmefikia wapi katika suala zima la kero mbalimbali, tungeweza tukalifanya hilo.

Lakini nafurahi tu kwamba juzi wakati Waziri wa Nchi, katika Ofisi ya Makamu wa Rais anawasilisha Bajeti yake mliona maelezo marefu sana katika eneo hili na hiyo ni namna nyingine vilevile ya kuwasilisha taarifa kwa upande wa Bunge ili muweze kuona kinachojadiliwa huko ni nini na tumefikia wapi.

Lakini mimi sioni ugumu sana katika jambo hili kama kinachoombwa ni kwamba tupate nafasi ya kuwakaribisha baadhi kuja kushiriki pale au kusikiliza tu na kuona ni nini kinaendelea. Tunaweza tukalizungumza na Waziri wa Nchi pamoja na Makamu wa Rais kama itaonekana inafaa, mimi sioni kama kuna ugumu sana katika jambo hili. (*Makofi*)

**MHE. COL. SALEH ALI FARRAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi tena. Nimefurahi sana na majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, ninaliomba hilo alilolisema lifanyike.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru kwamba ameona kwamba tumekuwa wasikivu kidogo.

Lakini labda nitoe angalizo tu maana wakati mwingine mnasahau kwamba hata sisi tunaokwenda kule ni Wabunge vilevile, mimi ni Mbunge, Waziri Kiongozi naye ni

Mwakilishi ndani ya Baraza la Wawakilishi ametokana na watu. Kwa hiyo, msije mkadhani kwamba tukienda pale sisi hatujali sana maslahi ya wananchi kwa sababu tunajua kwamba tunao wajibu vilevile kama Wabunge wa kusaidia kujaribu kuhakikisha kwamba yale yanayogusa watu yanakuwa ni sehemu ya maisha yetu kama watumishi lakini vilevile kama Viongozi tunaowawakilisha watu. Lakini nitaliwasilisha hilo jambo mbele ya chombo chetu tuone uwezekano wa kuweza kuli-*accommodate* kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU S PIKA:** Tatizo litakuwa Wabunge nani au wote sisi na kama tukiwa wote sisiushauriano utakuwa haupo na utakuwa ni mkutano wa hadhara.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, maswali ya wale waliojitokeza wamemaliza watatu yamekwisha. Tunakushukuru sana na kama nilivyosema ni kwamba Waheshimiwa Wabunge naona mmeridhika ndiyo maana hamkuona sababu ya kuuliza maswali mengi zaidi. Najua wengine wameleta vikaratasi hapa lakini kwa kweli lazima tufuate utaratibu maana tukianza kuruhusu wale ambao hawakwenda kule tena tukaanza kuruhusu vikaratasi hapa mwisho wake itakuwa utaratibu wote hauna hata maana. Kwa hiyo, nimepata vikaratasi hapa lakini nimeamua kwa misingi ya utaratibu hapana!

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tunaendelea! (*Makofi*)

## MASWALI NA MAJIBU

**MHE. DR. FEUSTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niliondoe swali langu Na.106, ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Kanuni inaruhusu hiyo. Tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni na michezo, Mheshimiwa Salim Hemedi Hamis.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya swali langu kujibiwa ningeomba yafanywe masahihisho yafuatayo. Katika jibu la Mheshimiwa Waziri amenitaka kuwa mimi ni Mheshimiwa Salim Hemed Hamis, lakini jina langu hasa ni Salim Hemed Khamis.

**NAIBU SPIKA:** Jina lako ni?

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni Salim Hemed Khamis, with k, siyo Hamis. Lakini vilevile katika sehemu nyingine ya jibu lake amesema Mheshimiwa Salim Hemed Salim. Kwa hivyo, ni Salim Hemed Khamis, siyo Hamis wala Salim Hemed Salim. *(Makofi)*

Na. 107

**Vilabu vya mpira nchini Kuanzisha ACADEMY**

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa, vilabu vingi vya mpira wa miguu Duniani kama *F.C Barcelona,* vimepata mafanikio makubwa kwa kutumia vijana wake kutoka *"Academy"* badala ya kuendelea kununua wachezaji kutoka nje:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia uzoefu huo kuvishawishi vilabu vyetu vya mpira hapa nchini kuanzisha *Academy?*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba vituo vya michezo mbalimbali husaidia sana katika kuibua na kukuza vipaji vya wanamichezo vijana. Utaratibu huu wa kuanzisha vituo vya michezo umesaidia sana katika kukuza soka katika nchi mbalimbali duniani.

Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirikisho la Soka Nchini *(TFF)* ilikubaliana kutoa agizo kwa kuanzia na vilabu vinavyoshiriki ligi kuu ya *Vodacom,* kuhakikisha kuwa vinaunda timu za vijana chini ya umri wa miaka 21. Agizo hili limo pia kwenye Kanuni za ligi kuu nchini.

Aidha, Serikali imetoa ushauri wa jinsi ya kuanzisha shule za michezo nchini, kwa kutoa miongozo na masharti muhimu wakati wa usajili wa shule hizo. Miongozo au masharti hayo ni pamoja na:-

(i) Kuwepo na walimu wenye vyeti sahihi vya kufundisha soka.

(ii) Viwepo vifaa sahihi na bora vya michezo pamoja na miundombinu inayohitajika katika mchezo/michezo husika.

(iii) Walimu/Madaktari wenye vyeti vinavyokubalika katika kutoa elimu na matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Serikali kupitia chuo chake cha michezo kilichopo Malya mkoani Mwanza, kinatoa walimu wa michezo mbalimbali. Napenda kutoa wito kwa wadau wa michezo wanaotaka na wenye nia ya kutaka kuanzisha shule za michezo nchini kuwatumia wahitimu wa chuo hicho katika kufundisha kwenye vituo vya michezo vitakavyoanzishwa.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa, mashindano ya UMISETA na UMITASHUMTA yanafanana fanana na *Academy* kwa sababu yamesaidia kuibua vipaji mbalimbali ikiwemo mpira wa miguu.

Je, Waziri haoni kwamba sera zile za kupiga marufuku michezo mashuleni zimeua michezo na kuifanya hata timu yetu ya Taifa *Taifa Stars* isiweze hata kufuzu kwa ajili ya michezo ya *CHAN* mwaka huu, na kwamba zile zilikuwa ni sera za kishetani? (*Makofi*)

(ii) Kwa kuwa, *Twiga Stars* mara hii imefanya vizuri sana kiasi kwamba imefuzu kuiwakilisha nchi yetu katika mashindano makubwa ya kimataifa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuibua vipaji mbali mbali vilivyopo vijijini ili kuifanya *Twiga Stars* iwe imara zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, kama ifuatavyo:-

,

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza kabisa nikubaliane naye kabisa kwamba, mashindano ya UMISETA pamoja na UMITASHUMTA na Vyuo ni muhimu sana kwa kuibua vipaji nchini. Kwa bahati nzuri napenda kutamka mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali ya Awamu ya Nne nataka kuhakikishia Wabunge kwamba, imeishafufua mashindano hayo na yanafanyika.

Mheshimiwa Rais wetu, Jakaya Mrisho Kikwete yeye alikwenda kufungua mashindano haya Kibaha mwaka jana, na mwaka huu mwezi ujao UMISETA inafanyika na tayari TAMISEMI, Wizara yangu pamoja na Wizara ya Elimu tunashirikiana kuhakikisha kuwa tunafufua mashindano ya *Primary School* “UMITASHUMTA” Kwa hiyo, tumeishaanzisha na tunajua kabisa huko ndiko kwenye vipaji, kwa sababu ukitaka ufanikishe masuala ya michezo lazima uanzie katika umri wa utotoni. Kwa hiyo, hilo liko tayari tumeishalishughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la pili ni swali zuri. Kwa kweli, tunafarijika sana, na kipindi kilichopita nilisimama hapa kutoa hongera kwa timu yetu ya Twiga, timu yetu ya Twiga ya akina mama imefuzu kucheza fainali mwezi wa Kumi, kule *South Africa* zitakazoshirikisha timu nane bora katika Afrika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo kubwa na sisi kama Serikali tumeweka mkakati wa kuhakikisha kwamba, kocha wetu Charles Boniface Mkwasa na msaidizi wake Adolf Rished, wanatembea nchi nzima kuibua vipaji vingine zaidi ili kuongezea nguvu timu ile ili iwe nzuri zaidi. Pia tumeomba Chama cha Mpira wa Miguu wa Wanawake, kiimarishe ligi yao katika nchi nzima ili isiwe kwa Dar es Salaam na mikoa michache, ili vipaji vingine vionekane. *(Makofi)*

**MHE. NURU A. BAFADHIL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa, hivi karibu *Taifa Stars* walicheza na Brazil na kwa kuwa, nilisikia kuna Mashabiki waliosema kwamba, akitokea mtu ambaye atafanya dawa ili *Taifa Stars* iweze kushinda atapata shilingi milioni 10;

Je, hamwoni kama tunalipeleka taifa kwenye utamaduni ambao siyo? (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Haya Naibu Waziri, mambo hayo. Nani anapeleka huko siyo wewe uliyesema? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la nyongeza la Dada yangu, Nuru kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiutalam kwa kweli mpira hauna mambo hayo ya uchawi, au michezo haina uchawi na ukijiingiza katika masuala haya utakuwa umepotea kwa sababu unaweza ukazungusha waganga kwenye uwanja, kama uwezo wako ni mdogo utakung'utwa magoli tu. Kwa hiyo, huyu ni mtu aliropoka akajisema mwenywe, sisi kama Serikali hilo hatulifahamu na hatuwezi kulisemea. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Eti ingekuwa ipo dawa hiyo, wangepeleka kule Afrika Kusini ili timu zote za kiafrika zishinde. (*Kicheko*)

**MHE. DIANA M. CHILOLO**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kabla sijauliza swali la nyongeza naomba nitumie nafasi hii kuipongeza timu ya Kindai *Shooting Stars* kwa kuwa mabingwa wa *Kili Taifa Cup. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo sasa naomba kuuliza swali langu kama ifuatavyo. Kwa kuwa, tatizo la vijana wanaoibua vipaji vyao na kuonekana wengi hununuliwa kwenye timu za kitaifa au za kimataifa; na kwa kuwa, sababu kubwa ni ukata na ukata huu unatokana na Sekretarieti ya mkoa kukosa maafisa utamaduni wa mkoa.

Je, Serikali itakuwa tayari kuajiri Maafisa Utamaduni katika ngazi ya Mkoa ili waanze kupata Bajeti ya kulea wachezaji wao ili wasinunuliwe kwenye timu kubwa?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na mimi nirudie kuipongeza Kindai Shooting Stars kwa ushindi mkubwa walioupata wa kubeba kombe la Taifa katika nchi nzima, tunawapongeza sana kwa sababu tumezoea kila wakati wanashinda Dar es Salaam, lakini safari hii Singida wanapewa hongera kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hili alilozungumza ni kweli tuna matatizo ya Maafisa Utamaduni katika wilaya na mikoa yetu. Napenda kutamka mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba Serikali tayari imekubali kupitia Wizara yetu ya Utumishi kwamba sasa mikoa yote na Wilaya zote ziajiri Maafisa Utamaduni na Maafisa Michezo.

Hivi karibuni nilikuwa kwenye ziara ya karibu mikoa yote na nimeona baadhi ya mikoa tayari wameishaajiri Maafisa Utamaduni na Maafisa Michezo.

Kwa hiyo, napenda kutoa wito, wale ambao hawajafanya hivyo Serikali imeishatoa ruksa kwa hiyo, ninaomba tuajiri ili Maafisa hao na kama alivyozungumza Mheshimiwa Chilolo, michezo sasa hivi ni ajira ili waweze kuibua vijana kwa lengo la kuendeleza michezo katika nchi yetu. (*Makofi*)

Na. 108

**Sababu za Matetemeko Maeneo ya Bonde la Ufa**

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kipindi cha mwezi Desemba, 2009 hadi Januari, 2010 kiliambatana na matetemeko ya nchi makubwa sana *(Magnitude)* na kujirudia katika muda mfupi *(high frequency)* kwenye maeneo ya Bonde la Ufa hususan Bonde la Ziwa Nyasa na hivyo kuleta hofu kwa wananchi wa maeneo hayo.

Je, ni sababu zipi za kisayansi zinazosababisha matukio haya?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Desemba, 2009 hadi januari, 2010 kulitokea mitikisiko ya ardhi katika maeneo ya Kusini Magharibi mwa Tanzania, hususan katika Mikoa ya Mbeya na Iringa. Mitikisiko hiyo ilisababishwa na matetemeko ya ardhi ambayo vitovu vyake vilikuwa nchini Malawi. Kulingana na taarifa kutoka katika kituo cha kufuatilia matetemeko ya ardhi duniani kinachomilikiwa na Marekani (*United States Geological Survey Seismic Centre*) vitovu vya matetemeko hayo vilikuwa katika kina cha kilomita 10 chini ya ardhi na umbali kati ya kilomita 125 na 160 Kusini Mashariki mwa Manispaa ya Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitovu vya matetemeko haya vinaangukia karibu na makutano ya mabonde ya ufa matatu (*Triple Junction* -Mbeya). Mabonde ya ufa hayo ni ya Mkondo wa Msahariki unaopitia Mikoa ya Iringa, Dodoma na Arusha, Mkondo wa Magharibi unaoambaa sambamba na Ziwa Tanganyika unaopita katika Mikoa ya Rukwa na Kigoma na Mkondo unaoelekea Kusini uambaao sambamba na Ziwa Nyasa unashuka chini ukipitia Mikoa ya Mbeya na Iringa kuelekea nchini Malawi. Matetemeko hayo yanatokana na muendelezo wa msuguano wa matabaka ya miamba katika mipasuko ya mabonde ya ufa yaliyotajwa (*reactivation of rift faults*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida kabla ya tetemeko kubwa kutokea hutanguliwa na matetemeko madogo (*fore shocks*) na baadaye kufuatiwa na mtikisiko mkubwa *(main shocks*) na baadaye (*after shocks*) na hii ndiyo sababu iliyofanya wakazi wa maeneo hayo wasikie mitikisiko mingi iliyofuatana. Hata hivyo, mtandao wa kuratibu matetemeko wa *USGS* huwa hautoi taarifa ya matukio ya matetemeko madogo yenye ukubwa chini ya nne (4) katika kipimo cha *Richter* na ndio sababu baada ya mtikisiko mkubwa hakuna tukio lililonukuliwa (*aftershocks*)

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ya Naibu Waziri ni mazuri na ya kisayansi vya kutosha. Naomba niulize maswali madogo mawili yanayofanana.

(i) Kwa vile, maeneo hayo uliyoyataja kwenye Bonde la Ufa, mimi ningeyaita ni *high riskareas* na yanakaliwa na binadamu, wapiga kura wetu na kuna shughuli za kimaendeleo ya kiuchumi hapa nchini.

Je, Serikali imeweka utaratibu gani kuwa *prepared* hasa kama kunatokea maafa makubwa?

(ii) Kuna sera gani ambayo inaelekeza makazi au shughuli zinazotakiwa kufanyika katika maeneo kama hayo nikizingatia kwamba, nchi nyingine nyumba za aina fulani tu ndizo zinatakiwa zijengwe kwa kutumia vifaa fulani, au shughul fulani haziruhusiwi. Sisi tuna sera au utaratibu gani wa kuwasaidia watu wanaoishi kwenye maeneo haya?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimwambie Prof. Mwalyosi kuwa, nadhani kulitambua eneo la Bonde la Ufa hili tulilonalo kama *high risk areas* ni sawa kwa sababu kwenye kipimo cha *Richter* cha kuanzia 1 - 10 kile sisi matetemeko yetu. Labda niseme kwamba tumekuwa tunakusanya takwimu za matetemeko kuanzia mwaka 1900.

Kwa hiyo, tumekuwa tukifanya hivyo kwa miaka 110 na katika kipindi chote hiki matetemeko yote haya katika maeneo ya Sumbawanga, Mbeya, Ludewa kwako, Dodoma hapa, Arusha, Morogoro na Mikindani yana nguvu ya kiwango cha matetemeko kati ya kipimo cha richter 3 hadi 4.9.

Baadhi ya matetemeko yamekwenda mpaka kipimo cha 5.5.9. Kwa hiyo, bado katika kipimo hicho kwa *scale* hiyo ni kiwango ambacho kinasababisha madhara, lakini kitasababisha madhara kwa sababu ya hali zetu.

Kusema kweli kama ikiwa ni nyumba ya udongo na matengenezo yake yakawa dhaifu kidogo basi kimtetemeko kidogo tu cha *richter 2* au 2.5 kitaiangusha.

Kwa hiyo, ndiyo maana katika utekelezaji wa sera za Serikali na zile za Chama cha Mapinduzi, nadhani Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Makazi wamekuwa wakisisitiza kuhusu ujenzi wa nyumba siyo kwa sababu ya matatizo ya matetemeko ila kwa sababu ya mfumo wa maisha tu ya kawaida ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tu kwamba katika hali hii *preparedness* ya matetemeko ya ardhi inakuwa ngumu kidogo kwa sababu hata hao walio na teknolojia hiyo wanashindwa kubaini tetemeko la ardhi litatokea lini. Ni tofauti na vimbunga ambapo unakuwa unaiona kabisa kupitia vitu vinavyoitwa *early warning systems*. Lakini katika hili ni maafa tu yanatokea kwa sababu ile miamba chini inakuwa haijakaa sawasawa.

Nilikuwa ninapata maelezo pia kwa Prof. Maghembe hapo kwamba miamba ile inapotikisika kidogo kwa sababu kunakuwa na uwazi mkubwa, ndiyo unakuta sisi huku juu tunaathirika kwa sababu matetemeko haya yanatokea kilomita kadhaa huko chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika hali kama hiyo naomba niseme tu kwamba haya ni mambo ambayo yanatokea lakini kwa bahati nzuri sisi kama kanda yetu matetemeko si makubwa isipokuwa Serikali imelisikia hilo na sera ya sasa hivi ya makazi inaelekeza ujenzi wa nyumba bora kwa Watanzania wote *irrespective* ya kwamba kuna matetemeko au hapa.(*Makofi*)

**MHE. RISHED M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, hivi karibuni kumeanza

kutokea mitetemeko chini ya Bahari, na mfano ambao umeathiri sana watu ni tetemeko linalojulikana kama Tsunami.

Je, Serikali imejiandaa vipi kuweka mitambo katika mwambao wetu au angalau Afrika Mashariki ambayo itaweza kutoa ishara mapema ili kuweza kuwahami wananchi wasipate madhara makubwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kujibu kwa kifupi tu maana yake hapa hatuko madarasani.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rished M. Abdallah, Mbunge wa Pangani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani tukisema hivi karibuni matetemeko yameanza kutokea chini ya Bahari si kweli, hii *concept* ya Tsunami wenyewe wanasema imekuwepo *for many years.*

Miaka mingi imekuwa *tsunami* hizi zinatokea, isipokuwa hili lililopiga juzi Indonesia na maeneo ya Thailand ilikuwa ni kubwa kiasi ambacho *after shocks* zake ndiyo zile tunasema kuna *foreshocks, main shock* na *after shock* katikati ya ile *tsunami* imetokea kule, lakini kwa sababu ya ukubwa wa tetemeko lenyewe ndiyo yale mawimbi ya bahari yakaja mpaka yakapiga na huku kwetu Pangani na mimi pia kwangu yamenipiga kidogo pale maeneo ya Kisiju na Kuruti na Chungubweni kule.

Kwa hiyo yamefika mpaka kanda ya Afrika Mashariki. Kwa sababu tuna huu mfumo wa Kimataifa ambao unashirikiana kusema kweli kama AP *Centre* ikiwa mbali tutapata na sisi kama ilivyopiga Peru juzi imepiga katikati ya bahari lakini wakawa na taarifa siku mbili, siku moja na nusu kabla ya kujiandaa. Sasa kama ile *AP Centre* ikiwa karibu sana labda kuna vitu vichache ambavyo tunaweza kufanya.

Lakini kama *AP Centre* ikiwa mbali na likiwa tetemeko ambalo linakuja kuathiri mwambao wa Afrika Mashariki nadhani kwa ushirikiano wa hizi taasisi za Kimataifa *GST* na wengine tutakuwa tunapata taarifa kabla na tutajiandaa ipasavyo.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya kisayansi ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba swali langu la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Wilaya ya Ziwa Nyasa ambayo imepatikana sasa na tunamshukuru Mhesimiwa Rais ni miongoni mwa hizo ambazo zinakabiliwa na hayo matetemeko na

matetemeko haya yanaambatana na radi zinazosababisha vifo na wakati mwingine kufikiria masuala ya uchawi.

Je, kwa kuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinao wataalamu wa kuweza kusaidia kutega radi hizo Waziri atakubaliana nami ni wakati muafaka kuisaidia Wilaya hiyo ili kuwezesha wawekezaji watakapokuja kufanya kazi zao bila hofu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani radi sio *phenomenal* ya Wilaya ya Ziwa Nyasa tu, lakini nimepokea maombi yako tutayafikisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Lakini pia tutapeleka hapa kwenye *Geological Survey* ya Tanzania na Mamlaka ya Hali ya Hewa na vyombo vingine wafanyie tathmini namna ambavyo wataalamu wanaweza kutusaidia kuondoa hofu hii ili hizi radi zisionekane kama ni sehemu ya uchawi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hata mimi kwangu radi ni kibao.

Na. 109

**Ahadi ya Kupeleka Umeme Vijiji vya Korogwe**

**MHE. LAUS O. MHINA** aliuliza:-

Kwa muda mrefu kumekuwa na ahadi ya kusambaza umeme katika maeneo ya vijiji vya Dindira, Mkalamo katika Kituo cha Afya cha Rozimin, Kibaoni/Lusanga, Makumba, Kijango, Kwemazandu na Kijingu Moto:-

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa hasa ikizingatiwa kuwa njia kuu za umeme zimepita katikati/karibu na vijiji hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Laus Omar Mhina, Mbunge wa Korogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANESCO* imefanya tathmini ya gharama za ujenzi wa miundombinu ya umeme kwenye maeneo ya Dindira, Mkalamo, Kibaoni/Lusanga, Makumba, Kijango, Kwemazandu na Kijingu Moto na makadirio ya gharama za ujenzi katika maeneo haya inakadiriwa kufikia shilingi 729,684,327.29. Mradi utahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa *kV 11* yenye urefu wa kilomita 37 na ufungaji wa *transfoma* 6 ambazo 4 ni za kV 50 na 2 za *kVa 100.*

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme wa Dindira utatokea Dindira *Tea Factory*, Kiwanda cha Chai pale Dindira utakwenda Lusanga utatokea Kerenge Makaburini, Kwemazandu utatokea Gombero, Kijangwa utatokea Magoma Hali ya Hewa, Makumba utatokea Kijangwa na Kijungu Moto utatokea Mashewa njia ya umeme ya *VODACOM.* Makadirio ya ujenzi wa miundombinu ya mradi huo yanatarajiwa kuwasilishwa kwa Wakala wa Nishati Vijijini kwa ajili ya kuangalia uwezekano wa kuingizwa katika Bajeti ya mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya wananchi wa Korogwe amewahi kutufikishia suala hili na naomba kumpongeza kwa hilo na kwa hivyo, naomba kumhakikishia ushirikiano wa Wizara yangu katika kuyapatia umeme maeneo haya yote. *(Makofi)*

**MHE. LAUS O. MHINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nashukuru pia kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nataka anieleweshe tu kidogo katika majibu yake ya msingi amesema Makadirio ya ujenzi wa miundombinu ya mradi huu yanatarajiwa kuwasilishwa. Sasa anaweza akarekebisha akasema kwamba yamekwishawasilishwa hasa ukizingatia kwamba Bajeti ya Wizara hii itasomwa tarehe 5 Julai, 2010?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya mradi huu ya shilingi milioni 729.7 yamewasilishwa *REA* na maelezo ya mradi huu utakavyokuwa na kulingana na upatikanaji wa fedha utatolewa wakati wa Makadirio ya Bajeti ya Wizara yetu tarehe 5 Julai, 2010.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru ningependa kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa katika bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini ya mwaka jana ilitolewa ahadi kwamba Wilaya ya Kongwa itapata mradi wa *MCC* kwa miradi midogo 4 ya Kongwa, Ibwaga, Sagala, Pandambili, Yembayemba, Nako, Mkoka, Zoisa, Iyanda, Mangweta, Mseta hadi Tubugwe. Kwa kuwa sasa tumeshamaliza mwaka tunaingia bajeti nyingine na wananchi wana matumaini makubwa sana mradi huo ulioahidiwa katika Bajeti iliyopita. Je, Wizara inasema nini kuhusu mradi huo utekelezaji wake?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri jibu ingawa ni swali jipya.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri hii miradi ya MCC tuliijibu humu ndani kama wiki mbili zilizopita wakati tukielezea utekelezaji wa miradi ya *MCC* kwenye Wilaya ya Geita kwa maana ya pale Misungwi, Nyangw'ale na Busanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii miradi ya *MCC* inaangukia kwenye makundi yale ya usambazaji ambayo ni katika makundi matatu ya miradi ya umeme ndani ya *MCC.* Tulisema kwamba tarehe 9 Julai kazi ya kumpata mkandarasi ambaye sasa atakwenda kwenye maeneo na tunatarajia atakuwa anaanza hiyo kazi kati ya mwezi Agosti, mwishoni au Septemba katikati inakamilika tarehe 9 Julai na kwa maana kwamba miradi

hii ya mkoa wa Dodoma kama ilivyo kwa Morogoro, Mwanza, Mbeya, Iringa yote itapatiwa utekelezaji baada ya kusaini mikataba na wakandarasi tarehe 9 Julai.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa sasa hivi mkoani Kigoma hasa Manispaa ya Kigoma Ujiji sasa hivi tumepatiwa majenereta matano (5) ambayo yanaweza yaka-*supply* mji mzima na umeme mwingine ukabakia. Na kwa kuwa kijiji cha Msimba sasa hivi na chenyewe kina umeme, na kwa kuwa kijiji cha Mahembe sasa hivi kuna nguzo za umeme zimetandazwa pale. Na kwa kuwa sasa hivi yale majenereta ni makubwa. Je, kijiji cha Mahembe hawawezi wakapata umeme?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa sababu umebobea sana ndiyo wanakuuliza maswali yoyote yale, haya wajibu tu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kwamba naomba nipokee pongezi na shukrani walizotoa kwa upatikanaji wa umeme ambao kusema kweli mahitaji ya Kigoma ni megawati kama 5 hivi na sasa wanapata kama megawati 9 au 10. Kwa hiyo, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba mimi naamini kabisa kwamba haya maeneo ya Lusinda, Mahembe na maeneo mengine ya Kigoma Ujiji na kadhalika sasa hivi baada ya kumaliza tatizo la uzalishaji tatizo litakuwa ni hilo la usambazaji ambalo nadhani tumepokea maombi haya uliyoyaleta kwa niaba ya wananchi wa hapo maeneo ya Mahembe na tutaangalia huu utaratibu kwa sababu sio nguzo tu bado kuna nyaya, transfoma na kadhalika, lakini niseme tumelipokea na tutalifanyia kazi.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mimi ningependa tu kupata tamko la Serikali kumekuwa na ahadi nyingi sana za umeme katika jimbo la Busega na ahadi hizi zimekuwa katika kila kikao cha Bunge zinaahidiwa. Sasa sijajua kwamba hii miradi kweli inatekelezwa au haitatekelezwa?

**NAIBU SPIKA:** Jamani, Mheshimiwa Waziri na wewe unataka kujibu maana wewe unakaa karibu pale pale. Mko majirani.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninafahamu Mheshimiwa Mbunge anachokiulizia ni ule mradi unaofadhiliwa na mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB).* Wanufaika katika mradi huo ni pamoja na Wilaya ya Bukombe baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Magu, Bariadi pamoja na mkoa wa Arusha.

Tumekuwa tukitoa taarifa lakini ukweli ni kwamba kulikuwa na mambo ambayo yalikuwa yametuchelewesha lakini sasa yamekamilishwa kati ya Wizara ya Fedha, watoaji mkopo na sasa tuko kwenye hatua za maandalizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakusudia kati ya kesho na wiki ijayo kutoa taarifa rasmi hapa Bungeni kuelezea maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo, miradi ya *MCC* pamoja na miradi inayotekelezwa kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *REA* katika ile mikoa 16 na miradi inayozidi 40.

Kwa hivyo, naomba Mheshimiwa Mbunge atuvumilie kati ya kesho na wiki ijayo tutoe taarifa yenye maelezo ya kina kuhusu hatua za utekelezaji kuhusu miradi hiyo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Anategemea atavuta subira.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba tarehe 9 Julai imeletwa tenda watafungua kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya *MCC*. Je, baada ya kufungua hizo tenda mchakato wa kuanza utekelezaji wa mradi huu hautachukua muda mrefu kwa sababu hii ahadi imekuwa mara kwa mara?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye majibu tulisema kwamba tarehe 9 Julai tunakamilisha hatua na mkandarasi. Lakini hili linafanywa baina ya sisi lakini mtekelezaji mkuu ni *MCC*. Mara ya mwisho nilisema kwamba *MCC* wametupa kijitabu chenye taarifa ya mtiririko wote wa utekelezaji wa miradi.

Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa George Malima Lubeleje kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini afanye subira kidogo ili tutoe taarifa ya miradi yote inayofanywa chini ya Wizara lakini pia kama akipenda anaweza kuja kwetu na sisi tukamwonyesha kijitabu cha *MCC account* linalotoa taratibu za utekelezaji wa mradi huo wa kwake na mingineyo ambayo iko kwenye maeneo ya mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Na. 110

### Mradi wa Umeme Vijijini

**MHE. TATU M. NTIMIZI** aliuliza:-

Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 iliweka mkazo juu ya kupeleka umeme vijijini:-

Je, Serikali inasema nini juu ya mradi huu wa umeme katika vijiji vya Igalula ambapo hakuna kilichofanyika mpaka sasa, licha ya wataalam kuzunguka vijiji vya Jimbo hilo na kutambua sehemu za kupitishia umeme tangu mwaka 2006/2007?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tatu Musa Ntimizi, Mbunge wa Igalula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa umeme wa jimbo la Igalula umekwishafanyiwa upembuzi yakinifu na utahusisha ujenzi wa njia ya umeme yenye urefu wa kilomita 95 ya msongo wa KV 33 kuanzia Tabora katika kituo cha kupozea umeme cha *TANESCO* kilichopo Kiloleni kwenda Kigwe, Igalula hadi Goweko kando kando ya barabara kuu ya Tabora hadi Manyoni kupitia Kilimatinde.

Vijiji vya njiani ambavyo vimepangwa kupatiwa umeme chini ya mradi huo ni Inala, Kinamaji, Kigwa A, Kigwa B, Igalula, Imalaseko na Goweko. Gharama za mradi huo ni shilingi bilioni 1.6 *TANESCO* inaandaa maombi ya fedha za utekelezaji wa mradi kutoka Wakala wa Nishati Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufikishaji wa huduma ya umeme unakusudiwa uunge mkono shughuli za uchumi za wananchi kwenye maeneo husika ili kuboresha jitihada za maendeleo na maisha bora. Katika jimbo la Igalula shughuli kuu za uchumi katika maeneo hayo ni kilimo na ufugaji, hasa kilimo cha mpunga, ufuta, tumbaku, mahindi na karanga.

Ufugaji mkubwa katika maeneo haya ni ufugaji wa nyuki kwa ajili ya asali na ufugaji wa ng’ombe. Serikali kwa kutambua hili ndio maana imechukua hatua nilizotaja za tathmini ya awali ili kuunga mkono jitihada hizi za wananchi. Naomba nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake wa karibu, na ninamhakikishia ushirikiano wa Wizara yangu katika kuhakikisha utekelezaji wa mradi huu. *(Makofi)*

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa jibu zuri la matumaini katika jimbo langu. Naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Wagombea wanaopita katika jimbo langu la Uchaguzi wanasema kwamba wamekutana na Waziri Ngeleja kuhusu Mpango wa Umeme katika jimbo langu la Uchaguzi na yeye ndiye ambaye anafanikisha mradi huu. Je, ni kweli ni yeye na Ngeleja au ni Serikali yenye mpango huu? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Achana na wanaopitapita hao. Mheshimiwa Ngeleja jibu swali.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulivyosema siku ya mjadala nadhani ilikuwa ni siku ya kwanza kwamba mazingira ya Bunge hili yapo mengi yatasemwa. Lakini pia hekaheka zinazoendelea kwenye majimbo huko pia inaweza kuwa ni fursa kwa watu kusema chochote ambacho wanadhani kwamba kinaweza kuwasaidia.

Lakini ukweli ni kwamba sisi Serikali tulikuwa tunafanya kwa niaba ya wananchi na kwa utaratibu wa kawaida wawakilishi wa wananchi ni hawa Waheshimiwa Wabunge walioko hapa Bungeni. Kwa hivi sisi ni wa kutekeleza miradi hii kwa kupitia wawakilishi ambao tumekuwa tukiwasiliana nao mara kwa mara. Lakini pia haimzuii mtu yoyote mwenye maslahi katika eneo ambalo miradi inatekelezwa kutuulizia. Lakini kusema hivyo haimaanishi kwamba tunaondoa ile fursa ya mawasiliano ya karibu, ushirikiano ambao tumekuwa nao kupitia Waheshimiwa wawakilishi kwenye majimbo husika. *(Makofi)*

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Miradi ya kupeleka umeme vijijini na pamoja na miradi ya *ABD* inayotarajiwa kupeleka umeme katika kijiji cha Hungumarwa, Mamashimba .................

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, naona sijui hatukusikii vizuri, sijui hiyo mashine ikoje.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, unanisikia sasa?

**NAIBU SPIKA:** Bado kidogo hatukusikii vizuri. Jaribu kisemea chombo kingine.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya kupeleka umeme vijijini ni pamoja na miradi ya umeme inayotarajiwa kupelekwa katika kijiji cha Hungumarwa, Ilola, Mwamashimba na Shirima katika Tarafa ya Mwamashimba katika Wilaya ya Kwimba ambayo inafadhiliwa na *ADB.* Lakini Mheshimiwa Waziri aliposimama hakuweza kuitambua. Je, miradi hiyo ambayo bado hatujasikia ipo au haipo?

**NAIBU SPIKA:** Miradi Wilaya ya Jimbo la Kwimba. **NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu anaosema wa Ngungumala ni kweli tumeutaja mara kwa mara hapa Bungeni, lakini nao upo kwenye ule utaratatibu wa miradi chini ya ADB, ambao Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini amemaliza kuusema sasa hivi kwamba ulikuwa umechelewa kwa mazingira hayo ya majadiliano baina ya ADB, Wizara ya Fedha na vitengo vingine vya Serikali. Kama alivyosema, utekelezaji huu kwa sababu majadiliano haya yamekamilika, tunatarajia kupata *schedule of implementation* ambayo itabaini utekelezaji utaanza lini na sisi kama

tulivyosema, tutawafikishia Waheshimiwa Wabunge ili wote wenye miradi ya umeme wawe na taarifa ya utekelezaji wa miradi yao.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, muuliza swali amesema katika Jimbo la Igalula Wataalam wa Umeme wameanza kuzungukia tangu mwaka 2006/2007. Naibu Waziri amejibu kwamba tayari ameshajua kiasi gani cha pesa ambacho kimetengwa kwa kazi hiyo; lakini hakujibu ni lini Jimbo la Igalula litapata huo umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hakika nadhani Mheshimiwa Selelii alitaka kuulizia suala la umeme kule kwake Ndala na Puge lakini amenichomekea. Nilichosema ni kwamba na ni utaratibu wa kawaida katika utekelezaji wa miradi hii. Lazima ufanye tathmini ya awali ili ujue kwa wakati huu wa sasa mradi huu utagharimu shilingi ngapi. Tumesema gharama za vijiji vyote hivyo ni kama bilioni 1.6. Sasa hayo maombi ya fedha nimesema TANESCO inaandaa maombi ya fedha na utekelezaji wa mradi huu kutoka Wakala wa Nishati Vijijini. Kwa hiyo, naomba nirudie kwamba, tutayaweka haya kwa miradi yote ya nchi nzima halafu tutapata *schedule of implementation* kwamba kulingana na pesa zitakazopatikana mradi huu tutautekeleza lini na kwa wakati gani.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Moja kati ya ahadi zilizotolewa na Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete mwaka 2005 ni kuanzisha Mfuko Maalum ambao utatumika kwa ajili ya kusambaza umeme vijijini. Sasa kwa kuwa miaka mitano hiyo ndiyo inamalizika; nilitaka Mheshimiwa Naibu Waziri anisaidie kama huo Mfuko Maalum umeshaanzishwa na kama umeanzishwa umesambaza katika maeneo mangapi ya vijijini?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoongelea habari ya Wakala wa Nishati Vijijini, tunaongelea pia mfuko ambao unahusika na hizo fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi. Kwa hiyo, nilidhani Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba, Mfuko ule umeshaanzishwa sambamba na uimarishwaji wa Wakala huo na fedha tayari zimeshaanza kutumika kama ambavyo tumekuwa tukitoa taarifa hapa Bungeni. Vilevile hata kwenye matamko mbalimbali fedha tayari zimeshaanza kutumika kama ambavyo tumekuwa tukitoa taarifa hapa Bungeni kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali. Hata hii miradi ambayo Waheshimiwa Wabunge wanaulizia sasa, fedha inayotekelezwa kupitia Wakala wa Nishati Vijijini, kimsingi, inatekelezwa kupitia huo Mfuko wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Fund).* Kuhusu miradi ambayo imetekelezwa, kama unavyofahamu ni suala la takwimu tuna miradi mingi sana, tunamkaribisha Mheshimiwa Mbunge aje Ofisini tumpe makabrasha yanayohusu miradi iliyotekelezwa.

**NAIBU SPIKA:** Sote tuliuanzisha Mfuko huu hapa na tukaweka fedha kutokana na bajeti hii. Tulianza na bilioni kumi wakati ule.

Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na ninawashukuru Mawaziri waliojibu maswali leo, kwa sababu kwa kukosa maswali kwa Waziri Mkuu na sisi

tulipanga maswali matano baada ya Waziri Mkuu, ndiyo maana wamepata maswali mengi sana ya nyongeza, kwa sababu tulikuwa tunatumia muda vizuri. Nawashukuru kwa kujibu kwa ufasaha sana.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya wageni. Kwanza kabisa, nina wageni wa Mheshimiwa John Magufuli, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ambao ni Katibu Mkuu wa Wizara yake, Dr. Charles Nyamrunda; Mwenyekiti wa Bodi ya Nyama Ndugu David Mpiri; Mwenyekiti wa Bodi ya TAFIRI, Prof. Lusato Kulwijira; Mwenyekiti wa Bodi ya VCT, Prof. Dominic Kambarage; Mwenyekiti wa Bodi ya NARCO, Ndugu Salum Shamte; Wakuu wa Vitengo na Wakurugenzi wa Idara mbalimbali; naomba waliko kokote kule wasimame. Ahsanteni sana tunawakaribisheni na leo kazi ipo hapa kwetu.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, ambao ni Mke wake Bi Sarah Wanyancha, yuko na watoto wake Marwa Wanyancha na Mwita Wanancha. Pia yupo Baba Mkwe wake, Kanali Mstaafu Mzee Joseph Kuzilwa. Nafikiri mnamfahamu, ahsanteni sana. Naona familia imekuja kuwaunga mkono, lakini pia alisahau kuleta jina la Ndugu Ibrahim Rajab, yeye ni mfanyabiashara kutoka Musoma Mjini.

Tuna wageni 12 wa Mheshimiwa Ramadhani Maneno kutoka Jimbo la Chalinze kutoka jamii ya wafugaji wakiongozwa na Ndugu Mbambile Kisanjo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Chamakweza. Karibuni sana, tumefurahi kuwaoneni na leo ndiyo Wizara yenu kwa hiyo mambo sawa.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Haroub Said Masoud, hawa ni Kocha wa Amani Fresh, Ndugu Salum Maghrum na Ndugu Rogers Albato. Nawashukuru sana na leo Mheshimiwa Waziri ameeleza kwa kirefu sana kuhusu habari za michezo.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Mwadini Jecha na Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, ambao ni Ndugu Jafar Ally Zaidy, yeye anasoma Digrii ya Kwanza Chuo cha Ualimu Mtwara; yupo Nasra Ibrahim naye anasoma *form one* Baobao Bagamoyo, hawajasema ni akina nani labda ni watoto wao.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka ambao ni Ndugu Lucas Kasmir Ole Mukusi, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Manyara; ahsante Mwenyekiti. Kuna Ndugu Daniel Melau, Mwenyekiti wa Kijiji cha Kimotorok. Kuna Wajumbe watatu wa Halmashauri ya Kijiji cha Kimotorok; wale pale karibuni sana. Tumefurahi kuwaona maana leo ni Wizara yenu, kwa hiyo ni vizuri mkasikiliza Serikali inasema nini.

Tuna wanafunzi 40 kutoka Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini Dodoma, nadhani wamekosa nafasi. Wanafunzi 33 na Walimu 16 kutoka Shule ya Msingi Mkapa; iko wapi hii? Karibuni walimu na wanafunzi wote. Tuna wanafunzi kutoka TAG Mpwapwa Centre. Pia tuna wanafunzi 60 na walimu wanane kutoka Shule ya Msingi Amani kutoka Dar es Salaam; karibuni sana. Tunawatakia masomo mema.

Napenda kutangaza shughuli za Kamati. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Omar Kwaangw', anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba mchana kutakuwa na Mkutano Ukumbi Namba 231.

Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, Mheshimiwa William Shellukindo, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba mchana kutakuwa na mkutano katika Ukumbi wa Msekwa B.

Mkurugenzi wa Huduma za Wabunge, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote ambao ni Wanachama wa NSSF kwamba, wakachukue kadi zao mpya zinaitwa *Smart Cards* kutoka kwa Maafisa wa NSSF ambao wapo mapokezi kwenye Jengo la Utawala kuanzia hii leo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnaokwenda kugombea mkirudi mnakuja kujiunga na NSSF.

Halafu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dr. John Magufuli, anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa, kuna bidhaa za maziwa na ngozi katika Viwanja vya Bunge. Nadhani kule kwenye maonesho, kwa hiyo, wanaohitaji wanakaribishwa huko. Tumemaliza shughuli za matangazo; Katibu.

## KAULI ZA MAWAZIRI

### Kauli ya Serikali Kuhusu Kusitishwa kwa Muda Matumizi ya Mizani aina ya *Steel Yard*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, Kanuni Namba 49, naomba kutoa Kauli ya Serikali kuhusu kusitishwa kwa muda matumizi ya mizani aina ya *Steel Yard* kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kupitia Tangazo lake Namba 233 la tarehe 3 Julai, 2009, ilipiga marufuku matumizi ya *Steel Yard* katika ununuzi wa zao la pamba. Hatua hii ilichukuliwa baada ya Serikali kuridhika na uhakiki uliofanywa kupitia Wakala wa Vipimo ambao ulibaini kuwa, mizani ya aina hii ni rahisi kuchezewa na hivyo kuwapunja wakulima wanapouza pamba yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkutano wa Wadau wa Zao la Pamba uliofanyika Jijini Mwanza mnamo tarehe 12 Mei, 2010, ilibainika kuwa maandalizi ya kuwezesha matumizi ya mizani ya aina nyingine hayajakamilika na zitahitajika takriban shilingi bilioni nne kununua mizani iliyopendekezwa na Wakala wa Vipimo. Wizara pia kwa nyakati tofauti, imefanya mikutano na Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo, Taasisi ya Sekta ya Pamba, kwa kiingereza ni *Tanzania Cotton Association* na *Tanzania Cotton Growers Association* na wadau hao waliomba kuongezewa muda wa maandalizi kabla ya kutekeleza Sheria inayokataza matumizi ya mizani aina ya *Steel Yard*. Kutokana na changamoto zilizojitokeza katika majadiliano na kwa kuzingatia kuwa sekta ya zao la pamba ni moja ya sekta zilizoathirika na mdororo wa uchumi duniani,

Serikali imetafakari upya utekelezaji wa Kanuni inayopiga marufuku matumizi ya mizani aina ya *Steel Yard.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto zilizojitokeza na maombi ya wadau wa sekta ya pamba kutokana na msimu utakaoanza hivi karibuni tarehe 28 Juni, 2010, Serikali inasitisha kwa muda utekelezaji wa kanuni ya kufuta matumizi ya mizani ya *Steel Yard* inayotumika katika ununuzi wa zao la pamba kwa kipindi cha mwaka mmoja. Hivyo, Wakala wa Vipimo waendelee na kama hawajaanza waanze mara moja ukaguzi wa mizani aina ya *Steel Yard* ili zitumike msimu huu wa 2010/2011. Mabadiliko haya ni kwa msimu huu wa 2010/2011 pekee ili kuruhusu maandalizi ya kutosha ya kusitisha matumizi ya mizani aina ya *Steel Yard* ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wadau wote, kuimarisha mfumo wa usimamizi wa matumizi ya mizani na kununua mizani zilizopendekezwa na kuthibitishwa na Wakala wa Vipimo. Aidha, pamoja na maandalizi hayo yote kufanywa mapema, wadau wataelimishwa na kuhamasishwa kuanza kutumia mizani ya *digital* badala ya ile ya *analogy* kwani si rahisi mizani ya *digital* kuchezewa kwa nia ya kufanya udanganyifu ili kuwaibia wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatumia fursa hii kukumbusha na kusisitiza kuwa, mnunuzi yeyote atakayebainika kuwa amechezea mizani za kununulia mazao kwa lengo la kufanya udanganyifu katika ununuzi wa pamba na mazao mengine, atachukuliwa hatua kali za kisheria, ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa leseni ya kufanya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2010/2011 - Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutuwezesha kukutana hapa leo ikiwa ni Bunge la Bajeti la Tano kwa Serikali ya Awamu ya Nne. Aidha, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji inayohusu Wizara, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii, kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya waliojiunga na Bunge lako Tukufu katika kipindi cha mwaka 2009/2010, kufuatia kuteuliwa kwao na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ambao ni Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene kutoka Chama cha Mapinduzi na Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu kutoka Chama cha Wananchi - CUF.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha Mheshimiwa Mbunge mwenzetu; Hayati Mheshimiwa Sigfrid Selemani Ng'itu, aliyekuwa Mbunge wa Ruangwa. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya marehemu, ndugu na Wananchi wa Jimbo la Ruangwa. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina. Aidha, naomba pia, nitumie fursa hii kuwapa pole Wananchi wa Kilosa, Same na sehemu nyinginezo nchini, kutokana na athari za mafuriko na maporomoko yaliyosababisha kupoteza maisha ya wananchi wenzetu, uharibifu na upotevu wa mali na makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mwaka wa uchaguzi mkuu ambapo Watanzania watapata fursa ya kumchagua Rais atakayeongoza nchi yetu kwa miaka mitano ijayo. Napenda kuchukua fursa hii kwa dhati kabisa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Makamu ya Rais na Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda (Mb), Waziri Mkuu kwa kazi zao nzuri katika kuongoza nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchaguzi mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba mwaka huu, pia utawachagua Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili Tukufu. Napenda kukupongeza wewe Mheshimiwa Naibu Spika, Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa busara na hekima zenu zilizowezesha kuongoza na kusimamia kwa utulivu shughuli za Bunge kwa kipindi chote. Aidha, nachukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kazi kubwa ambayo wameifanya ya kusukuma na kusimamia maendeleo ya Wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, Mbunge wa Ileje, kwa ushauri, maoni na ushirikiano mkubwa waliotupatia katika maandalizi ya bajeti hii na kipindi chote ambacho Kamati imesimamia sekta hizi. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara itaendelea kuzingatia na kutekeleza maoni, ushauri na mapendekezo yatakayotolewa na Kamati pamoja na Bunge lako Tukufu wakati wa kujadili bajeti ya Wizara yangu.

Ninachukua fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki kwa hotuba yake nzuri ambayo kwa ufasaha imetoa malengo ya Serikali na mwelekeo wa utendaji wa Sekta mbalimbali pamoja na kazi zitakazotekelezwa na Serikali katika mwaka 2010/2011. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maelekezo yake mahususi ya kuboresha sekta za mifugo na uvuvi hususan kupitia mikutano ya kisekta aliyoiongoza yeye binafsi hapa Dodoma, Mwanza na Dar es Salaam. Maelekezo hayo yamekuwa ni dira katika kuandaa bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii pia kumpongeza Waziri wa Fedha na Uchumi Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, Mbunge wa Kilosa kwa hotuba yake kuhusu hali ya uchumi wa nchi yetu na bajeti ya Serikali kwa ujumla kwa mwaka

2010/2011. Aidha, nawapongeza Mawaziri wote waliotangulia kwa hotuba zao nzuri ambazo zimeainisha maeneo mbalimbali tunayoshirikiana kwa karibu katika kutoa huduma za kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi nchini. Pia, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia masuala ya maendeleo ya sekta za mifugo na uvuvi kupitia hotuba zilizotangulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango na Bajeti kwa mwaka 2010/2011 umezingatia vipaumbele vya kitaifa, ikiwa ni pamoja na kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, MKUKUTA II, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala, Sera za Taifa za Mifugo na Uvuvi pamoja na Azma ya Kilimo Kwanza. Vilevile, mpango na bajeti umezingatia Maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa Wizara, alipokutana na Uongozi wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Ikulu mwezi Machi, 2009 na maazimio ya mikutano miwili ya wadau wa sekta za mifugo na uvuvi mwaka 2009 chini ya Uenyekiti wa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maeneo ya Kipaumbele kwa mwaka 2010/2011 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Sekta ya Mifugo: Kuimarisha huduma za ugani na utafiti wa mifugo; Kuendelea kutoa ruzuku ya madawa ya kuogeshea mifugo na chanjo; kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya mifugo; kuboresha miundombinu muhimu ya mifugo kama minada, masoko, majosho na malambo; na kuimarisha upatikanaji wa huduma za uhimilishaji mifugo.

Katika Sekta ya Uvuvi: Kudhibiti uvuvi na biashara haramu na kuhifadhi mazingira; kuimarisha miundombinu ya kupokelea, kuhifadhi, kusafirisha samaki na mazao ya uvuvi; kuimarisha utoaji wa huduma za ufugaji wa samaki na ukuzaji wa viumbe wengine kwenye maji *(Fish Farming);* kuimarisha huduma za ugani na utafiti wa uvuvi; kuimarisha usimamizi wa sekta ya uvuvi na ukusanyaji wa takwimu; na kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya mifugo ina umuhimu mkubwa katika kumwondolea umaskini mwananchi, hususan katika maeneo ya vijijini. Katika mwaka 2009/2010, idadi ya mifugo inakadiriwa kufikia ng’ombe milioni 19.2, mbuzi milioni 13.7, kondoo milioni 3.6, nguruwe milioni 1.9 na kuku milioni 58. Kati ya ng’ombe hao, 680,000 ni ng’ombe wa maziwa. Vilevile, kati ya kuku hao, milioni 35 ni kuku wa asili na milioni 23 ni kuku wa kisasa ambapo milioni 7 ni kuku wa mayai na milioni 16 ni kuku wa nyama. Wastani wa ulaji mazao ya mifugo kwa mtu kwa mwaka 2009/2010 ni kilo 12 za nyama, lita 43 za maziwa na mayai 75. Ulaji huu ni mdogo ikilinganishwa na viwango vya FAO vya kilo 50 za nyama, lita 200 za maziwa na mayai 300 kwa mtu kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nchi yetu imebahatika kuwa na maeneo mengi ya uvuvi, ikiwa ni pamoja na kilometa za mraba 64,000 za ukanda wa bahari, kilometa za mraba 223,000 za Bahari Kuu, Maziwa Makuu ya Victoria (kilometa za mraba 35,088), Tanganyika (kilometa za mraba 13,489) na Nyasa (kilometa za mraba 5,700). Pia, yapo maziwa ya kati na madogo 29, mabwawa 14,746 na mito. Sekta ya uvuvi huchangia

katika kuondoa umaskini nchini kwa kuwapatia wananchi lishe bora, ajira na kipato. Hata hivyo, ulaji wa mazao ya uvuvi kwa mtu kwa mwaka bado ni mdogo, ambao katika mwaka 2009/2010 ulifikia kilo 8.0 ikilinganishwa na kilo 10.7 zinazopendekezwa na FAO.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta za mifugo na uvuvi kwa kipindi cha mwaka 2009/2010 zimeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kuainisha, kupima, kumilikisha na kuendeleza maeneo ya ufugaji endelevu ili kudhibiti kuhamahama, kupunguza migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, kupunguza uharibifu wa mazingira na kuzuia kuenea kwa magonjwa ya mifugo;

(ii) Kuongeza uwekezaji katika sekta za mifugo na uvuvi ili kuongeza uzalishaji, tija na thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi;

(iii) Kudhibiti magonjwa mbalimbali ya mifugo, hususan ya milipuko;

(iv) Kupatikana kwa mikopo yenye masharti nafuu kwa ufugaji na uvuvi;

(v) Kupatikana kwa pembejeo na zana za gharama nafuu kwa ajili ya ufugaji na uvuvi;

(vi) Kupatikana kwa soko la uhakika la mazao ya mifugo na uvuvi;

(vii) Kudhibiti uvuvi na biashara haramu ya samaki na mazao ya uvuvi; na

(viii) Upatikanaji wa elimu na teknolojia pamoja na matumizi ya teknolojia za kisasa kwa wafugaji na wavuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 inatambua mchango mkubwa unaoweza kutolewa na sekta za mifugo na uvuvi katika kuwapunguzia wananchi umaskini na kuongeza pato katika uchumi wa Taifa. Hivyo, utekelezaji wa maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa sekta za mifugo na uvuvi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Mifugo Kujenga Mazingira ya Kuvutia Uwekezaji katika Viwanda vya Kuongezea Thamani Mazao ya Mifugo kama vile Ukataji Nyama, Usindikaji wa Maziwa na Utengenezaji wa Bidhaa za Ngozi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kujenga mazingira ya kuvutia uwekezaji kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Tunaendelea kuboresha Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006;

(ii) Kupitia upya Sheria ya Nyama Na. 10 ya Mwaka 2006, Sheria ya Biashara ya Ngozi Na. 18 ya mwaka 2008, Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya Mwaka

2008. Aidha, katika kikao cha 19, Bunge lako Tukufu lilipitisha Miswada ya Sheria za Nyanda za Malisho na Vyakula vya Mifugo na Sheria ya Usajili, Utambuzi na Ufuatiliaji wa Mifugo ya Mwaka 2010;

(iii) Kuandaa Kanuni 29 chini ya Sheria ya Veterinari (3), Sheria ya Magonjwa ya Mifugo (6), Sheria ya Maziwa (6), Sheria ya Ngozi (6), Sheria ya Nyama (4) na Sheria ya Ustawi wa Wanyama (4); na

(iv) Kuziwezesha Bodi za Maziwa na Nyama ili kusimamia ubora wa maziwa na nyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuwepo kwa mazingira mazuri ya uwekezaji, kumevutia uwekezaji katika viwanda vya kusindika nyama, maziwa na ngozi ili kuongeza thamani ya mazao hayo ambapo:-

(i) Serikali kupitia Kampuni ya Ranchi za Taifa – NARCO imeingia mkataba na Kampuni ya Ujenzi ya SUMA – JKT kujenga machinjio ya kisasa katika Ranchi ya Ruvu kwa gharama ya shilingi bilioni 10.7. Machinjio hayo yatakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 800 na mbuzi/kondoo 400 kwa siku;

(ii) Serikali imeuza asilimia 51 ya thamani ya mali za machinjio ya Dodoma kwa Kampuni ya *National Investment Company Limited* (*NICOL)* na kubakiza asilimia 49 chini ya Kampuni ya Ranchi za Taifa - *NARCO*. Aidha, kampuni ijulikanayo kama *Tanzania Meat Company* imeanzishwa kwa ajili ya kuendesha machinjio hayo, ambapo ng'ombe 100 wanachinjwa kila siku na faida imeanza kupatikana;

(iii) Kiwanda cha kusindika nyama cha *Manyara Ranch* chenye uwezo wa kuchinja na kusindika jumla ya ng'ombe 50 na mbuzi/kondoo 100 kwa siku kimekamilika;

(iv) Viwanda vya kusindika maziwa vimeongezeka kutoka 22 mwaka 2005/2006 na kufikia 46 mwaka 2009/2010. Pia, uwezo wa usindikaji wa maziwa kwa siku umeongezeka kutoka lita 56,580 mwaka 2006/2007 hadi lita 105,380 mwaka 2009/2010. Kuongezeka kwa usindikaji kumetokana na kuimarika kwa shughuli za usindikaji katika viwanda vikubwa na vya kati vya Tanga Fresh, *Mara Milk*, *Tan Dairies* na *Musoma Dairy*. Vilevile, ongezeko hilo limetokana na kuanzishwa kwa viwanda vidogo vya kusindika maziwa vikwemo viwanda vya Same, Longido na Simanjiro (Orkesumet, Naberera na Terrat). Viwanda hivi vina uwezo wa kusindika lita 500 za maziwa kwa siku kila kimoja;

(v) Usindikaji wa ngozi uliongezeka kutoka kilo milioni 1.6 zenye thamani ya shilingi bilioni 1.6 mwaka 2005/2006 hadi kufikia kilo milioni 3.5 zenye thamani ya shilingi bilioni 7.3 mwaka 2009/2010; na

(vi) Ili kukuza uwekezaji wa ndani, Serikali imeweka kodi ya ongezeko la thamani VAT ya asilimia 18 ya maziwa kutoka nje; imeweka ushuru wa asilimia 40 ya mauzo ya ngozi ghafi nje ya nchi na imeondoa kodi ya vifungashio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwashawishi Watanzania wale nyama na mayai na kunywa maziwa kwa wingi zaidi kwa ajili ya kujenga afya zao na kukuza soko la ndani la bidhaa hizo: Wizara imeendelea kuhamasisha wananchi kutumia mazao yatokanayo na mifugo kwa kushirikiana na wadau wengine kuandaa promosheni mbalimbali, ikiwemo Wiki ya Unywaji Maziwa ambayo huadhimishwa Kitaifa mwanzoni mwa mwezi Juni ya kila mwaka. Katika kipindi cha miaka 5 iliyopita, maadhimisho hayo yamefanyika katika Mikoa ya Morogoro, Mbeya, Rukwa, Dodoma na Lindi. Kutokana na uhamasishaji huo, unywaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita 39 mwaka 2005/2006 hadi lita 43 mwaka 2009/2010 kwa mtu kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Mpango wa Majaribio wa Unywaji Maziwa Shuleni *(School Milk Pilot Scheme*) uliozinduliwa mwaka 2004, umeendelea kutekelezwa katika shule 81 ambapo wanafunzi 57,350 katika Wilaya za Mbeya, Hai, Moshi Vijijini, Tanga na Njombe walinufaika. Mpango huo unafadhiliwa na wazazi, wasindikaji wadogo, makampuni ya *Fukeni Dairy Company Ltd, Peach Software Company Ltd, Tanga Fresh* na Shirika la Maendeleo la *Italia - CEFA*. Pia, uhamasishaji wa ulaji wa nyama na mayai umeendelea ambapo ulaji wa mayai umeongezeka kutoka mayai 53 mwaka 2005/2006 hadi 75 mwaka 2009/2010 wakati ulaji wa nyama umeongezeka kutoka kilo 10 hadi kilo 12 kwa mtu kwa mwaka katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kushirikiana na Halmashauri kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*), Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji (*PADEP*), Mradi wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo Wilayani (*DASIP)* na Mfuko wa Jamii Tanzania (*TASAF)* kuchangia ujenzi wa malambo 638, visima virefu 29 na mabwawa makubwa 2 katika Halmashauri mbalimbali nchini katika kipindi cha kuanzia mwaka 2005/2006 hadi 2009/2010. Aidha, nakala 357 za Mwongozo wa Ujenzi Bora wa Vyanzo vya Maji kwa Mifugo na Miundombinu ya Mifugo umesambazwa kwa Halmashauri zote nchini. Pia, kupitia Mipango ya *DADPs* na sekta binafsi, jumla ya majosho 816 yamekarabatiwa na 264 kujengwa na kufanya idadi ya majosho yaliyo katika hali nzuri ya kufanya kazi kuwa 1,556 kati ya majosho 2,314 yaliyopo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji elimu ya ufugaji kwa njia ya shamba darasa ulianza mwaka 2006/2007 ambapo jumla ya wataalam 118 wa ugani kutoka katika Halmashauri 26 walipata mafunzo ya mbinu shirikishi ya uanzishaji wa mashamba darasa ya mifugo. Jumla ya mashamba darasa 2,164 kuhusu ufugaji bora na umuhimu wa kuvuna mifugo yameanzishwa katika Halmashauri 119, ambapo wafugaji 93,495 wameelimishwa. Kutekelezwa kwa mpango huu kumewezesha kupanua wigo wa soko kwa wafugaji wadogo ambapo jumla ya ng'ombe 74,400 walinenepeshwa ili kuzalisha nyama bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuhimiza wafugaji kufuga kisasa na kibiashara kama ilivyoelekezwa katika Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006. Jumla ya nakala 2,000 za Mwongozo wa Kanuni za Ufugaji Bora wa Mifugo zimechapishwa na kusambazwa kwa wafugaji. Aidha, Wizara kupitia Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) imemilikisha *(sub-lease)* jumla ya hekta 227,414 kwa wawekezaji kwa lengo la kuanzisha na kuendesha ufugaji wa kibiashara katika ranchi ambapo vitalu 114 vimemilikishwa kwa wawekezaji wazalendo kati ya vitalu 134 vyenye eneo la hekta 289,069.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhifadhi mazingira kwa kuzingatia ufugaji endelevu usioharibu mazingira, rasilimali muhimu kama ardhi na vyanzo vya maji kote nchini: Muswada wa Sheria ya Maeneo ya Malisho na Vyakula vya Mifugo itakayosimamia ufugaji kulingana na uwezo wa ardhi ilipitishwa na Bunge lako Tukufu katika kikao cha 19. Aidha, wataalam 70 kutoka wilaya 31 za Mikoa ya Arusha, Dodoma, Kilimanjaro, Manyara, Morogoro, Pwani, Singida na Tanga walijengewa uwezo kuhusu madhara ya mabadiliko ya tabianchi na ufugaji unaozingatia uhifadhi wa mazingira, ikiwa ni pamoja na kuhifadhi na kuboresha malisho kwa kutumia njia za asili kama vile Ngitiri katika Mikoa ya Shinyanga na Tabora na Olelii katika Mikoa ya Arusha na Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuimarisha miundombinu ya masoko ya mifugo ili kuboresha biashara ya mifugo na mazao yake kwa kujenga jumla ya minada 6 ya upili na mpakani ya Nyamatara (Misungwi), Buzirayombo (Chato), Lumecha (Ruvuma), Buhigwe (Kigoma) na Kasesya (Rukwa); na kukarabati minada 9 ya upili. Aidha, jumla ya minada 73 imejengwa na kukarabatiwa katika Halmashauri ili kuboresha biashara ya mifugo. Vilevile, mfumo wa utoaji wa taarifa za masoko ya mifugo (*LINKS*) unatumika katika minada 53 ambayo hutoa taarifa za bei na aina ya mifugo iliyouzwa kwa madaraja kwa kutumia ujumbe wa simu. Pia, taarifa za LINKS zinapatikana kwenye tovuti ya Wizara *http://www.lmistz.net* na *http://www.mifugo.go.tz.* Serikali kupitia NARCO inajenga machinjio kubwa na ya kisasa Ruvu ili kuongeza soko la mifugo. Vilevile machinjio ndogo 26 zimejengwa katika Halmashauri 26.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendeleza mikakati ya kukuza Sekta ya Mifugo kupitia ugani, tiba, kinga, usambazaji wa maji na uboreshaji wa malisho elimu kuhusu ufugaji bora ilitolewa kwa wadau kupitia vipindi 286 vya redio na 60 vya luninga. Vilevile, mabango 90,130, vipeperushi 282,110 na vijitabu 312,000 kuhusu ufugaji bora, kinga na tiba ya mifugo, uvunaji wa maji ya mvua na uboreshaji wa malisho vilitayarishwa na kusambazwa kwa wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kuimarisha vyuo vya mafunzo ya mifugo vya Tengeru, Madaba, Morogoro, Mpwapwa, Buhuri (Tanga) na Temeke kwa kuvikarabati na kuvipatia vitendea kazi. Aidha, wanafunzi 1,580 waliohitimu katika vyuo hivyo wameajiriwa katika Halmashauri ili kutoa huduma za ugani. Wataalam wa ugani 118 kutoka Halmashauri 26 walipatiwa mafunzo ya ukufunzi kuhusu upangaji wa mipango shirikishi ya ugani na mbinu shirikishi ya shamba darasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati ya kudhibiti magonjwa mbalimbali ya mifugo imeandaliwa na kutekelezwa kama ifuatavyo:-

(i) Ugonjwa wa Sotoka umedhibitiwa na nchi yetu imetambuliwa na kupewa cheti na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani cha kutokuwa na virusi vya ugonjwa huo tangu mwaka 2007;

(ii) Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa (*RVF*) umeendelea kudhibitiwa kwa kusambaza jumla ya dozi milioni 5.5 za chanjo ambapo jumla ya mifugo milioni 4.9 ilichanjwa katika Halmashauri 52, mashamba ya ng'ombe wa maziwa, utafiti na Ranchi za Taifa;

(iii) Udhibiti wa Mafua Makali ya Ndege uliendelea kwa kujenga uwezo wa kutambua na kufuatilia ugonjwa huo kwa kuchunguza jumla ya sampuli 22,300 za kuku na ndege pori. Elimu kwa umma ilitolewa kupitia vipindi vya luninga, vipeperushi 1,020,000 na mabango 1,010,000. Nakala 500 za Mpango Mkakati na kalenda 500 zilichapishwa na kusambazwa kwa wadau. Pia, vijitabu 2,000 vya kufundisha wataalam na nakala 5,000 za vijarida kwa ajili ya wanafunzi zilisambazwa. Vilevile, wataalam 1,630 wa mifugo, afya na maliasili walipatiwa mafunzo. Hadi sasa ugonjwa huo haujaingia nchini;

(iv) Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (*CBPP*) umeendelea kudhibitiwa ambapo ng'ombe milioni 11.134 wamechanjwa katika mikoa yote nchini;

(v) Mpango wa kitaifa wa kudhibiti Ugonjwa wa Miguu na Midomo (*FMD)* umeanza kutekelezwa na ufuatiliaji wa ugonjwa huo ulifanyika katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambapo iligundulika *FMD virus type O* katika Mikoa ya Mbeya na Iringa;

(vi) Wizara imeendelea kudhibiti Ugonjwa wa Mdondo kwa kusambaza dozi milioni 140 za chanjo inayostahimili joto (*I-2*). Tathmini inaonesha kupungua kwa vifo kutoka asilimia 95 hadi 4 katika maeneo yaliyozingatia taratibu za uchanjaji;

(vii) Wizara imeendelea kudhibiti ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa kwa kusambaza jumla ya dozi 472,000 za chanjo ambapo jumla ya mbwa 433,687 walichanjwa na uchanjaji unaendelea. Pia, Serikali inatekeleza Mradi wa Kudhibiti Kichaa cha Mbwa katika Mikoa ya Morogoro, Pwani, Dar es Salaam, Lindi na Mtwara, ambapo mbwa wapatao 400,000 watachanjwa kila mwaka; na

(viii) Serikali imetoa ruzuku ya jumla ya shilingi bilioni 13.5 kwa ajili ya kununua lita 882,616 za dawa za kuogesha mifugo kwa mikoa yote kuanzia mwaka 2006/2007 hadi 2009/2010 ili kudhibiti magonjwa yaenezwayo na kupe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uimarishaji wa vituo vya uzalishaji wa mbegu bora za ng'ombe na mifugo mingine na kuongeza ufanisi katika usambazaji wa mbegu hizo: Kituo cha Uhimilishaji cha Taifa cha NAIC Usa River kiliendelea kuimarishwa

kwa kufanya ukarabati wa majengo pamoja na kuendeleza shamba la malisho na uzio. Pia, Wizara ilinunua madume bora 12 na kufikisha idadi ya madume bora 34 yenye uwezo wa kuzalisha dozi 340,000 za mbegu kwa mwaka. Kituo cha NAIC kilizalisha jumla ya dozi 339,815 za mbegu ambapo jumla ya ng'ombe 296,106 walihimilishwa. Vilevile, jumla ya wataalamu 877 wa uhimilishaji walipata mafunzo. Pia, vituo vitano vya uhimilishaji vimeanzishwa katika Kanda za Kati (Dodoma), Mashariki (Kibaha), Ziwa (Mwanza), Nyanda za Juu Kusini (Mbeya) na Kusini (Lindi).

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuimarisha mashamba ya uzalishaji wa mitamba bora, jumla ya mitamba 636 aina ya Boran ilinunuliwa na kusambazwa kwenye mashamba ya Mabuki (Misungwi), Nangaramo (Masasi), Ngerengere (Morogoro Vijijini) na Sao Hill (Mafinga). Mashamba hayo yameendelea kuimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi, kukarabati miundombinu na watumishi kupatiwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu. Katika kipindi hicho, jumla ya mitamba 3,714 yenye thamani ya shilingi bilioni 1.48 ilizalishwa katika mashamba ya Wizara na kuuzwa kwa wafugaji. Aidha, sekta binafsi ilizalisha na kusambaza kwa wafugaji jumla ya mitamba 30,155.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupunguza migogoro kati ya wakulima na wafugaji, Serikali imetenga hekta 1,423,201.28 kwa shughuli za ufugaji katika vijiji 266 vya Wilaya 33 katika mikoa 15 ya Dodoma, Iringa, Kagera, Kigoma, Lindi, Mara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Singida, Tabora na Tanga. Aidha, mkakati wa kuelimisha wafugaji wa asili kuhusu matumizi bora ya ardhi na utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa watumiaji mbalimbali unaendelea kutekelezwa kwa kushirikiana na asasi zisizo za kiserikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea na juhudi za kuhimiza uundwaji wa vikundi, vyama na mitandao ya wafugaji kwa lengo la kuharakisha maendeleo ambapo jumla ya vikundi 1,820 vya wafugaji vimeanzishwa nchini. Aidha, mitandao 40 ya wafugaji wadogo wa ng'ombe wa maziwa imeanzishwa katika Mikoa ya Kagera (25) na Tanga (15). Pia, mitandao 2 imeanzishwa ya wazalishaji wa mbuzi wa maziwa aina ya *Norwegian* katika Kata ya Mgeta (Morogoro) na *Torgenburg* Wilaya ya Babati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uvuvi kuwasaidia wavuvi kutumia maarifa ya kisasa ya uvuvi ili kuongeza ufanisi na mapato yao: katika kuwaongezea wavuvi mapato kutokana na uvuvi endelevu, Wizara yangu imetekeleza yafuatayo:-

(i) Kujenga uwezo kwa kuwapatia mafunzo ya uhifadhi bora wa bahari na maeneo ya Pwani kwa wananchi 12,000 na uhifadhi na uchakataji wa mazao ya uvuvi kwa wavuvi 1,830 na wafanyabiashara 430 kutoka Wilaya za Rufiji, Kilwa, Mafia na Tanga. Aidha, mafunzo hayo yametolewa kwa wamiliki na wafanyakazi wa viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi 291 katika Ukanda wa Ziwa Victoria na kuhusu uvuvi wa ndoano za kulambaza kwenye maji ya kina kirefu kwa vikundi 32 vya wavuvi katika ukanda wa Ziwa Nyasa;

(ii) Kuboresha mialo 25 ya kupokelea samaki katika Ukanda wa Ziwa Victoria kupitia Mradi wa Usimamizi wa Uvuvi katika Ukanda wa Ziwa Victoria (*IFMP*); na

(iii) Kuandaa na kusambaza vipeperushi 38,500 na kurusha hewani vipindi 75 vya redio na 20 vya luninga kwa ajili ya kuuelimisha umma kuhusu uvuvi endelevu na uhifadhi wa mazao ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Mradi wa *MACEMP*, Wizara imewezesha jumla ya wananchi 6,887 (wanaume 4,279 na wanawake 2,608) wa jamii za Pwani kuibua, kutekeleza na kusimamia miradi midogo 403 yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 5.7 inayolenga kuboresha maisha yao. Pia, jamii za wavuvi zimewezeshwa kuanzisha jumla ya *VICOBA (Village Community Bank)* 63 katika Wilaya za Rufiji (16), Kilwa (24) na Mafia (23) kupitia Mradi wa *MACEMP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepunguza kodi ya malighafi za uvuvi hadi asilimia tano na kuondoa kodi ya zana za uvuvi zikiwemo boti, nyavu na injini ili kuwezesha wavuvi kumudu gharama za zana za uvuvi. Aidha, Wizara imehamasisha uanzishwaji wa miradi midogo ya uvuvi 212 katika maeneo ya Ukanda wa Pwani ili kuwasaidia wavuvi kumudu kupata zana za uvuvi. Pia, kupitia mpango wa ubadilishanaji wa zana haribifu kwa zana bora, jumla ya wananchi 654 wamefaidika na mpango huo kwa kupewa mashine za kupachika 13, masanduku 4 ya barafu, maboti 11 na nyavu za jarife 1,214.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya wananchi 850 waishio ndani ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu waliwezeshwa kufanya kazi mbadala za kiuchumi ili kupunguza utegemezi katika uvuvi. Aidha, vikundi vitatu vya wanajamii katika maeneo tengefu ya Bongoyo, Mbudya na Sinda katika Mkoa wa Dar es Salaam, vimeanzishwa na kupatiwa boti 10 za doria kwa ajili ya kudhibiti uvuvi haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji kwa kutekeleza yafuatayo ili kuwavutia wawekezaji katika kuanzisha viwanda vya kusindika samaki, hasa katika Ukanda wa Mwambao wa Bahari ya Hindi na Visiwa vya Unguja, Pemba na Mafia:-

(i) Imekamilisha kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Uvuvi na Mikakati yake ya mwaka 1997 ili iendane na mabadiliko ya sasa ya kiuchumi na kijamii;

(ii) Imefanya mapitio ya Kanuni za Uvuvi za mwaka 2005 na kuandaa Kanuni mpya za mwaka 2009. Aidha, Kanuni za Uvuvi katika Bahari Kuu za mwaka 2009 zimeandaliwa;

(iii) Kufanya mapitio ya Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Na. 29 ya Mwaka 1994;

(iv) Kukamilisha ujenzi wa Maabara ya Taifa ya Udhibiti wa Ubora wa Samaki, Nyegezi (Mwanza) ambayo inatambuliwa kimataifa; na

(v) Ili kuvutia wawekezaji wa ndani kuwekeza katika sekta ya uvuvi, Serikali inatoza ushuru wa samaki wanaoingizwa kutoka nchi za nje kwa Dola za Kimarekani 0.25 kwa kilo. Kiasi cha shilingi 578,868,082.50 zimekusanywa hadi Aprili 2010 kutokana na ushuru huu. Vilevile, imeongeza ushuru kwenye mazao ya pweza na ngisi wanaouzwa nje ya nchi kutoka Dola ya Kimarekani 0.025 hadi 0.25 kwa kilo ambao umeongeza mapato kwa kiasi cha shilingi 904,005,575.40 kwa kipindi cha Julai 2009 hadi Aprili 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mazingira mazuri ya uwekezaji nchini, sekta binafsi imewekeza katika viwanda vya kutengeneza zana za uvuvi, ambapo kiwanda cha *FANAKA* katika ukanda wa Ziwa Victoria na *IMARA FISH NET* katika Ukanda wa Pwani vimeanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Wizara imeendelea kuzishirikisha jamii za wavuvi katika usimamizi wa rasilimali ya uvuvi ambapo jumla ya vikundi 637 vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi (*BMUs*) vimeanzishwa katika Ukanda wa Ziwa Victoria (438), Bwawa la Mtera (29), Bwawa la Nyumba ya Mungu (20), Mto Ruhuhu (11) na Ukanda wa Pwani (144) ili kuhimiza serikali za vijiji na mitaa kuelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kupambana na uvuvi haramu. Vilevile, viongozi 2,655 wa Halmashauri za Vijiji na Jamii za wavuvi kwenye Halmashauri za Wilaya katika Ukanda wa Pwani walielimishwa kuhusu kusimamia uanzishwaji wa *BMUs* kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kutoa mafunzo kuhusu athari za uvuvi haramu nchini ambapo jumla ya wadau 96 kutoka Wilaya za Mafia (39), Rufiji (52), Wataalam wa Idara ya Uvuvi (2) na wa WWF/RUMAKI (3) walishiriki. Pia, mafunzo ya ulinzi shirikishi wa rasilimali ya pwani yalitolewa kwa waraghabishi 48 kutoka Wilaya za Mafia na Rufiji na wataalam wa ugani 68 kutoka Halmashauri za Ukanda wa Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Uendelezaji wa Ukuzaji Viumbe Kwenye Maji kwa kuimarisha vituo vya ukuzaji viumbe kwenye maji vya Kingolwira (Morogoro), Ruhila (Ruvuma), Mtama (Lindi), Karanga (Kilimanjaro), Musoma, Mwanza, Bukoba na Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi, imepandikiza jumla ya vifaranga milioni 3.3 vya perege na 11,406 vya kambale katika mikoa 15 ya Pwani, Morogoro, Dodoma, Iringa, Kilimanjaro, Tanga, Rukwa, Shinyanga, Mbeya, Ruvuma, Tabora, Ruvuma, Kagera, Mwanza na Mara. Pia, mabwawa 63 kwa ajili ya ufugaji wa Mwatiko *(Milkfish)* yamechimbwa katika maeneo ya mwambao wa Bahari ya Hindi. Aidha, ufugaji wa Kambamiti kibiashara *(Prawn Farming*) umeendelea kufanyika katika mabwawa 30 Wilayani Mafia na Kampuni ya *Alphakrust* ambapo jumla

ya tani 310 zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 2.9 zilizalishwa na kati ya hizo, tani 160 zimeuzwa katika soko la Jumuiya ya Nchi za Ulaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya utafiti ya kuzalisha vifaranga vya kambale inaendelea katika Kituo cha Ufugaji Samaki cha Kingolwira Morogoro na kwa kushirikiana na Sekta Binafsi (Mwanza Fish Farm) jumla ya vifaranga 310,150 vimezalishwa na kusambazwa kwa wakulima. Samaki hawa wameonekana wanafaa kwa kufugwa. Uzalishaji wa Kambamiti umefanyika katika Chuo cha Maendeleo ya Uvuvi Mbegani kwa kushirikiana na Kampuni ya PRAWNTO ambapo wamezalisha vifaranga 75,000 na kuvisambaza kwa wafugaji katika Mkoa wa Tanga. Majaribio ya ukuzaji wa lulu *(pearls)* yanaendelea kwa kushirikiana na WWF, ambapo jumla ya vipande 750 vimepandikizwa katika Wilaya za Mafia (400), Mtwara Vijijini (150) na Mbegani-Bagamoyo (200).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliandaa mpango mahususi wa kuzalisha na kusambaza mbegu bora za samaki ambapo jumla ya vifaranga milioni 2.6 aina ya sato na 10,000 aina ya kambale vimezalishwa na kusambazwa katika mabwawa mbalimbali nchini. Wizara imeshirikisha sekta binafsi katika kutekeleza dhana ya "Kilimo Kwanza" ambapo *Mwanza Fish Farm* wamezalisha jumla ya vifaranga 58,550 aina ya sato na 300,150 aina ya kambale na kusambazwa kwa wakulima. Kwa upande wa maji bahari, Kampuni ya *Prawnto* kwa kushirikiana na Chuo cha Maendeleo ya Uvuvi Mbegani, imezalisha vifaranga 75,000 vya kambamiti na kusambazwa kwa wakulima katika maeneo ya Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha mwani kinaendeshwa katika maeneo mbalimbali ya Pwani kwa kuhusisha takriban wakulima 3,000 ambapo jumla ya tani 1,467 za mwani mkavu zimezalishwa na kati ya hizo tani 459.5 zenye thamani ya Dola za Kimarekani 195,287.5 zimeuzwa nje ya nchi. Vilevile, mafunzo ya ujasiriamali na uboreshaji wa kilimo cha mwani yametolewa kwa wakulima 1,784 wa Ukanda wa Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, kumekuwepo na matukio muhimu yaliyogusa Sekta za Mifugo na Uvuvi. Matukio hayo muhimu ni pamoja na:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ilikumbwa na ukame, hususan maeneo ya kaskazini mwa nchi na kusababisha ukosefu mkubwa wa malisho na maji. Hali hii ilisababisha vifo vingi vya mifugo pamoja na kushuka kwa bei ya mifugo katika maeneo ya wafugaji na kupanda kwa mazao ya mifugo katika maeneo ya walaji hasa ya mijini. Ng'ombe 159,139, mbuzi 21,783, kondoo 7,300 na punda 1,178 walikufa katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na hali iliyojitokeza, Serikali kupitia Halmashauri zake ilitoa maelekezo kwa wananchi, hususan wafugaji na wafanyabiashara ya mifugo juu ya hatua za kuchukua kukabiliana na janga la ukame. Hatua hizo ni pamoja na kuwaelekeza wafugaji kuvuna mifugo kabla ya kudhoofu ili kupata bei nzuri; na kutoa utaratibu wa kuhamishia mifugo kwenye maeneo mengine ili kuepuka migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapa pole wananchi wote walioathirika na hali hiyo ya ukame na kwamba hali hii iwe changamoto kwa wafugaji kuchukua hatua za tahadhari mapema. Serikali itaendelea kuelimisha wafugaji kufuga kwa kuzingatia uwezo wa eneo la malisho, kuvuna ziada; kulima na kuhifadhi malisho; kuchimba na kukarabati malambo na vyanzo vingine vya maji katika maeneo ya wafugaji kwa kushirikiana na Halmashauri na wadau wengine. Aidha, serikali itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika viwanda vya kusindika nyama ili kuongeza wigo wa soko la mifugo hasa ukame unapotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkutano wa Waziri Mkuu na Wadau wa Sekta ya Mifugo Nchini uliofanyika Dodoma, tarehe 28 hadi 30 Septemba, 2009 chini ya Uenyekiti wa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb), ulilenga kuhamasisha ufugaji bora nchini. Mkutano huo ulishirikisha wadau mbalimbali wapatao 586 wakiwemo Mawaziri, Wabunge, Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Viongozi wa Chama Tawala, Wenyeviti wa Halmashauri, Watendaji Wakuu wa Serikali na Wataalam, Wafugaji, Wasindikaji wa bidhaa za mifugo; Asasi za Kijamii, watoa huduma za mifugo, wauzaji wa pembejeo na vyombo vya habari. Mkutano huo ulipitisha maazimio yanayolenga kuboresha Sekta ya Mifugo katika kutekeleza azma ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkutano wa Waziri Mkuu na Wadau wa Sekta ya Uvuvi Nchini ulifanyika Mwanza, tarehe 16 hadi 18 Desemba, 2009 chini ya Uenyekiti wa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb). Mkutano huo ulilenga kuhamasisha usimamizi endelevu wa rasilimali ya uvuvi pamoja na kuendeleza ufugaji wa viumbe kwenye maji chini ya kaulimbiu ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkutano huo uliwashirikisha wadau mbalimbali wapatao 542 wakiwemo Mawaziri na Wabunge, Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Viongozi wa Chama Tawala, Wenyeviti wa Halmashauri, Watendaji Wakuu wa Serikali na Wataalam, Wavuvi, Wafugaji na Wakulima wa mazao ya uvuvi, wachakataji wa mazao ya uvuvi, sekta binafsi na Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Mkutano huo uliazimia kutokomeza uvuvi na biashara haramu ya samaki na mazao yake nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkutano wa Waziri Mkuu na Watafiti wa Sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi Nchini ulifanyika tarehe 18 na 19 Machi, 2010 katika Ukumbi wa Hoteli ya Kunduchi Beach, Dar es Salaam. Mkutano huo uliratibiwa na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia na kushirikisha Wizara za Kilimo, Chakula na Ushirika; Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Viwanda, Biashara na Masoko pamoja na taasisi mbalimbali za utafiti. Madhumuni ya mkutano yalikuwa ni kujadili na kuainisha mambo muhimu ya utafiti na matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi ili mchango wa utafiti uweze kuongeza tija kwenye sekta husika kulingana na azma ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Mkuu kwa kuitisha na kuendesha mikutano hiyo. Ni matumaini yangu kuwa, utekelezaji wa maazimio ya mikutano hii utasaidia kutoa msukumo wa kipekee katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi sanjari na dhana ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Wizara yangu ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi 11,267,731,000. Kati ya hizo, shilingi 2,393,166,000 ni kutoka sekta ya mifugo na shilingi 8,874,565,000 ni kutoka sekta ya uvuvi. Hadi kufikia tarehe 15 Juni, 2010, jumla ya shilingi 8,356,357,543.55 zilikusanywa ikiwa ni asilimia 74.2 ya lengo la makusanyo. Katika mwaka 2010/2011, Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 10,643,950,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara ilitengewa jumla ya shilingi 67,334,294,900. Kati ya hizo; Shilingi 9,271,422,000 kwa ajili ya mishahara ya watumishi (PE); Shilingi 27,982,032,000 kwa ajili ya matumizi mengine (OC); na Shilingi 30,080,841,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya hizo, shilingi 9,723,810,000 zilikuwa fedha za ndani na shilingi 20,357,031,000 fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi mwezi Juni, 2010 jumla ya shilingi 30,081,705,035.00 zimetolewa, sawa na asilimia 80.7 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya hizo, shilingi 11,902,781,946.00 ni kwa ajili ya Mishahara na shilingi 18,178,923,089.00 ni kwa ajili ya Matumizi Mengine (OC). Kati ya fedha hizo, jumla ya shilingi 25,484,284,000.00 (asilimia 84.7) zimetumika. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya shilingi 21,364,205,989.57 fedha za maendeleo zimetolewa (asilimia 71). Kati ya hizo, shilingi 8,175,000,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 13,189,205,989.57 ni za nje *(ASDP Busket Fund, PRSP II, UNICEF* na *MACEMP)*. Kati ya fedha hizo, jumla ya shilingi 19,509,481,510.00 (asilimia 91.3) zimetumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Taifa ya Mifugo (2006); katika mwaka 2009/2010, Wizara imeendelea kusambaza na kutoa elimu kwa wadau kuhusu Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006 ambapo nakala 5,000 za sera zimesambazwa kwa wadau. Pia, Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu Sera hiyo kupitia matukio mbalimbali ya kitaifa yakiwemo, Sikukuu ya Wakulima Nanenane; Wiki ya Uhamasishaji Unywaji wa Maziwa; Wiki ya Utumishi wa Umma pamoja na mikutano mbalimbali ya kitaaluma na wadau. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa Mkakati wa kutekeleza Sera ya Taifa ya Mifugo. Katika mwaka 2010/2011, Wizara itaandaa mpango wa kutekeleza mkakati huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara imekamilisha kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Uvuvi (1997) na Mikakati yake ya Mwaka 1997 ambapo rasimu ya Sera ya Taifa ya Uvuvi, 2010 imeandaliwa ili iendane na mabadiliko ya sasa ya kiuchumi na kijamii. Katika mwaka 2010/2011, Wizara itakamilisha maandalizi ya Mkakati wa kutekeleza Sera hiyo na kuandaa Mpango wa utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na wadau, imeendelea kuandaa na kutoa mapendekezo ya marekebisho ya sheria za sekta za mifugo na uvuvi ambazo ziko katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Maandalizi ya Miswada ya kutungwa Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo *(The Grazingland and Animal Feed Resources Act, 2010)* na Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo *(The Livestock Identification, Registration and Traceability Act, 2010)* yamekamilika na Miswada hiyo imepitishwa katika kikao cha 19 cha Bunge la mwezi Aprili 2010;

(ii) Mapendekezo ya kutunga Sheria ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo *(National Livestock Research Institute Act);* Sheria ya Maabara Kuu ya Mifugo (*Central Veterinary Laboratory Act)* na Sheria ya Uzalishaji wa Mbari Bora ya Wanyama *(Animal Breeding Act)* yamekamilika na utaratibu unaendelea wa kuyawasilisha serikalini kwa hatua zaidi; na

(iii) Mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu *(The Marine Parks and Reserves Authority Act No. 29, 1994)* na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi *(The Tanzania Fisheries Research Institute Act No. 6, 1980)* yamekamilika na hatua inayofuata ni kuyawasilisha serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara imeandaa kanuni mbalimbali za kutekeleza sheria za mifugo na uvuvi kama ifuatavyo:-

(i) Kanuni za Uvuvi *(Fisheries Regulation),* 2009 zilikamilishwa na kuanza kutumika kwa kupewa GN. 308 ya 2009;

(ii) Kanuni 6 za Sheria ya Ngozi Na. 18 ya Mwaka 2008 zimeandaliwa na kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(iii) Kanuni 4 za Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya Mwaka 2008 zimeandaliwa na kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(iv) Kanuni za Utotoaji wa Vifaranga *(Hatcheries Regulations, 2010)* imeandaliwa chini ya Sheria ya Magonjwa ya Mifugo Na. 17 ya Mwaka 2003 na kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na

(v) Rasimu ya Kanuni 4 chini ya Sheria ya Nyama Na. 10 ya Mwaka 2006 zimeandaliwa na kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

Katika mwaka 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na wadau itakamilisha Sheria na Kanuni zilizoainishwa hapo juu. Pia, Wizara itatafsiri Kanuni za Uvuvi za mwaka, 2009 kwa Lugha ya Kiswahili na kuzisambaza kwa wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) imeendelea na jukumu lake la kuzalisha, kunenepesha na kuuza mifugo kwa ajili ya nyama. Aidha, Kampuni hiyo imeendelea kutoa huduma za ushauri kwa wafugaji wanaozunguka ranchi zake 10 za Kikulula, Mabale, Kagoma na Misenyi (Kagera), Kongwa (Dodoma), Mzeri

(Tanga), Ruvu (Pwani), Mkata (Morogoro), Kalambo (Rukwa) na West Kilimanjaro (Kilimanjaro). Ranchi hizo kwa pamoja zina jumla ya hekta 230,384 zenye uwezo wa kuweka ng'ombe kati ya 80,000 - 90,000. Kwa sasa, Kampuni ina jumla ya ng'ombe 33,515. Pamoja na ng'ombe hao, kampuni hufuga aina nyingine za wanyama wakiwemo kondoo 1,536, mbuzi 1,034, farasi 41, nguruwe 91 na punda 55.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, NARCO imetekeleza yafuatayo:-

(i) Kuzalisha ndama 6,823 kutokana na ng'ombe wazazi 12,811, sawa na asilimia 53.3 ya malengo ya uzalishaji ikilinganishwa na ndama 9,265 kati ya ng'ombe wazazi 12,834 sawa na asilimia 72 mwaka 2008/2009;

(ii) Kuuza ng'ombe 7,597 wenye thamani ya shilingi 2,361,890,000;

(iii) Kununua ng'ombe 4,062 kutoka kwa wafugaji wanaozunguka maeneo ya ranchi kwa ajili ya programu ya unenepeshaji;

(iv) Kuendelea na ujenzi wa machinjio ya kisasa katika Ranchi ya Ruvu ambao umefikia asilimia 50 ya ujenzi; na

(v) Kusimamia na kutoa ushauri wa ufugaji bora katika ranchi ndogo ndogo zilizomilikishwa kwa wawekezaji wazalendo, ambapo ranchi hizo zimewekeza ng'ombe 50,227, mbuzi 3,419 na kondoo 827.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, NARCO itatelekeza kazi zifuatazo: Kuendelea na ujenzi wa machinjio katika ranchi ya Ruvu; kusimamia na kushauri ufugaji bora katika ranchi ndogo zilizomilikishwa kwa wawekezaji wazalendo; kukamilisha utoaji wa hati miliki ndogo 20; na kuendelea kutafuta wawekezaji ili waingie ubia na NARCO katika masuala ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Nyama Tanzania ina jukumu la kusimamia maendeleo ya sekta ndogo ya nyama, kwa mujibu wa Sheria ya Nyama Na. 10 ya Mwaka 2006. Katika mwaka 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Nyama imeandaa nyaraka muhimu zitakazoiwezesha Bodi ya Nyama kuajiri Sekretarieti. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na vyama vya wadau vya Wafugaji Kanda ya Kati (UWAKAMA) na Wafanyabiashara ya Mifugo na Nyama (TALIMETA) imehamasisha wafugaji 392 wa Kilosa na Kilindi na wafanyabiashara 88 wa Morogoro, Temeke na Dodoma kujiunga na vyama hivyo na kuingia katika ufugaji wa kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Bodi ya Nyama itaendelea kutekeleza yafuatayo: Kuajiri sekretarieti ya Bodi ya Nyama; kuhamasisha wadau kuhusu sheria na kanuni za nyama na kujiunga na vyama vya wadau wa nyama kitaifa; kushirikiana na vyama vya wadau kuhamasisha uendelezaji wa tasnia ya nyama; na

kushirikiana na mashirika ya viwango (TBS na TFDA) kuhuisha viwango vya ubora wa nyama na kuweka utaratibu wa kudhibiti ubora wa nyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Maziwa Tanzania ina jukumu la kusimamia sekta ndogo ya maziwa kupitia Sheria ya Maziwa Na. 8 ya Mwaka 2004. Katika mwaka 2009/2010 Bodi kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) imefanya mapitio ya viwango 17 vya bidhaa zitokanazo na maziwa. Aidha, Bodi imeendelea kusimamia na kuratibu Programu ya Unywaji wa Maziwa Shuleni inayofanyika kwenye shule 81 na kunufaisha jumla ya wanafunzi 57,350 ikilinganishwa na wanafunzi 53,742 katika shule 73 mwaka 2008/09 (Jedwali Na. 2). Kazi nyingine zilizotekelezwa na Bodi ya Maziwa ni pamoja na:-

(i) Kuandaa na kuchapisha vitabu vya mwongozo wa kufundishia wazalishaji, wahudumu wa vituo vya kukusanyia maziwa, wauzaji na wasafirishaji kwa kushirikiana na Mashirika ya *ASARECA* na *Policy Analysis and Advocacy Project* (*PAAP)*;

(ii) Kusajili wadau 150 na kutoa mafunzo kwa wataalam wakufunzi 20 kutoka Mikoa ya Mwanza (12) na Arusha (8) watakaotoa mafunzo kwa wadau ili kuwawezesha kusajiliwa na Bodi;

(iii) Kutoa mafunzo kwa wachuuzi 200 katika Mikoa ya Mwanza (100) na Arusha (100) kuhusu Kanuni za ubora wa maziwa na kuwasajili ili kuwawezesha kufanya biashara rasmi;

(iv) Kuratibu maadhimisho ya Wiki ya Kuhamasisha Unywaji Maziwa yaliyofanyika Kitaifa Mkoani Lindi; na

(v) Kuajiri watumishi 7 wa Sekretarieti ya Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Bodi ya Maziwa inatarajia kusajili wadau wa maziwa 1,000. Aidha, Bodi ya Maziwa itaendelea kusimamia Programu ya Unywaji wa Maziwa Shuleni na kuanzisha programu hiyo katika Mikoa ya Mara na Morogoro. Kazi nyingine zitakazotekelezwa na Bodi ni pamoja na:-

(i) Kuandaa maadhimisho ya Wiki ya Uhamasishaji Unywaji Maziwa nchini yatakayofanyika Dar es Salaam Mei/Juni 2011 na Maadhimisho ya Siku ya Unywaji wa Maziwa Shuleni Duniani mwezi Septemba 2010;

(ii) Kurasimisha wachuuzi wa maziwa 300 na kuendesha mafunzo kwa wadau 200 katika Mikoa ya Mbeya, Kagera, Iringa na Tanga juu ya utekelezaji wa Sheria ya Maziwa Na. 8 ya Mwaka 2004; na

(iii) Kufuatilia utekelezaji wa msamaha uliotangazwa na Serikali katika Bunge la Bajeti mwaka 2010/2011 wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mashine na vifaa vya kukusanya, kusafirisha na kusindika maziwa kwa ajili ya kuhamasisha uwekezaji

katika sekta ndogo ya maziwa na kuboresha kipato kwa wananchi. Mashine na vifaa vitakavyohusika ni kama ifuatavyo: Vifaa maalum vya kubebea maziwa (milk cans), pampu maalum za kusukuma maziwa (milk pumps), bomba maalum la kupitisha maziwa kwenye viwanda vya kusindika (milk hoses), kompresa maalum zinazotumika kwenye vifaa vya kupoza maziwa, matanki ya kuhifadhia maziwa, gari maalum lenye kifaa cha kupoza na kusafirisha maziwa, mtambo maalum wa kuchemsha maziwa, kifaa maalum cha kuchekecha maziwa ili kutoa siagi, vifaa maalum vya kupoza na kutengeneza baridi na kifaa maalum cha kukandamiza mabonge ya maziwa na kukamua maji ili kuzalisha jibini.

Mheshimwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara imeendelea kutenga maeneo ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu *(Marine Parks and Reserves Unit - MPRU)* ambapo eneo la Kigombe katika mwambao wa Mkoa wa Tanga limetangazwa kuwa Hifadhi ya Bahari ya Silikanti kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 28 Agosti, 2009 kwa GN. Na. 307. Aidha, taarifa za hali ya rasilimali hai na uchumi jamii zitakazowezesha uandaaji wa mipango ya jumla ya usimamizi wa hifadhi hiyo zimekusanywa. Pia, Visiwa vya Ulenge, Kwale, Mwewe na Kirui vilivyoko katika Wilaya ya Mkinga, Mkoa wa Tanga, vipo kwenye mchakato wa kutangazwa kuwa maeneo tengefu. Aidha, kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kufanya doria ya siku-kazi 115 ili kudhibiti uvuvi haramu katika maeneo ya hifadhi ambapo baruti 15, *spear guns* 3, makokoro 23, kamba za kokoro meta 19, mitumbwi 7, kambakochi kilo 18.5, gunia 65 za mwani mbichi wa asili, maboya 23 na madema 30 vilikamatwa;

(ii) Kusimamia na kuendeleza shughuli mbadala zikiwemo ufugaji nyuki, samaki na kaa, ukulima wa mwani na mboga mboga, utalii rafiki na mazingira, utengenezaji wa batiki na ususi kwa wananchi 850;

(iii) Kutekeleza Mpango wa Kuhifadhi na Kusimamia Matumbawe katika maeneo ya Mafia, Mtwara, Tanga na Dar es Salaam;

(iv) Kutoa mafunzo ya uhifadhi bora wa bahari na maeneo ya pwani kwa watumishi 36 na wananchi 147 waishio ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa;

(v) Kuandaa na kusambaza kwa wadau majarida na vipeperushi 7,500 kuhusu hifadhi ya bahari na maeneo tengefu; na

(vi) Kuimarisha taasisi kwa kuajiri watumishi wanane (8) na hivyo kufanya taasisi kuwa na jumla ya watumishi 66.

Katika mwaka 2010/2011, Wizara kupitia *MPRU* itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kuandaa na kukamilisha Mpango wa Jumla wa Usimamizi *(General Management Plan)* kwa ajili ya Hifadhi mpya ya Bahari ya Silikanti-Tanga;

(ii) Kuendelea kulinda na kuhifadhi rasilimali za bahari katika maeneo yote ya hifadhi kwa kuimarisha doria ili kudhibiti uvuvi haramu kwa kufanya siku-kazi za doria 338;

(iii) Kuendelea kuhamasisha ulinzi shirikishi katika maeneo yote ya hifadhi kwa ajili ya kulinda rasilimali za bahari na uvunaji endelevu wa rasilimali hizo;

(iv) Kujenga uwezo wa taasisi kwa kuajiri watumishi wapya 31 na kununua magari matatu (3) kwa ajili ya Hifadhi za Bahari za Kigombe - Tanga na Mnazi Bay - Mtwara na uratibu (Makao Makuu ya taasisi);

(v) Kuendelea kutangaza vivutio vya utalii vilivyomo katika maeneo yote ya hifadhi na taratibu za uwekezaji zinazozingatia mazingira rafiki (*ecotourism*);

(vi) Kuzijengea uwezo jamii zilizopo katika maeneo ya hifadhi za bahari na maeneo tengefu kwa kuendeleza na kuanzisha miradi ya shughuli mbadala; na

(vii) Kuimarisha na kuboresha mazingira ya kazi ya watumishi wa taasisi kwa kuwapa vitendea kazi na mafunzo ya muda mfupi na mrefu na motisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (TAFIRI) imeendelea kufanya tafiti mbalimbali ili kubaini wingi, mtawanyiko na aina ya rasilimali zinazopatikana katika maji ya asili. Utafiti uliofanyika katika Ziwa Victoria umeonesha kuwa, sangara wameongezeka kutoka tani 307,539 mwaka 2009 hadi tani 367,819 mwaka 2010, dagaa kutoka tani 786,653 mwaka 2009 hadi tani 1,176,372 mwaka 2010. Aidha, furu na samaki aina nyingine wameongezeka kutoka tani 489,220 mwaka 2009 hadi 528,169 mwaka 2010. Pia, utafiti wa kubaini wingi na mtawanyiko wa kambamiti umefanyika Sadani (Bagamoyo), Rufiji, Kisiju (Mkuranga) na Jaja (Kilwa) na kuonesha kuwa kambamiti wameongezeka kutoka tani 202 mwaka 2007 na kufikia tani 358 mwaka 2009.

Kazi nyingine zilizotekelezwa na Wizara kupitia *TAFIRI* ni pamoja na:-

(i) Utafiti unaolenga kutatua matatizo ya ufugaji samaki unaendelea, ambapo kazi hii inatekelezwa katika Kituo cha Utafiti cha Dar-es-Salaam;

(ii) Utafiti wa hali ya uvuvi katika Maziwa ya Rukwa, Eyasi, Manyara na Bwawa la Mtera na Mto Kilombero unaendelea; na

(iii) Ujenzi wa ofisi na maabara ya Kituo cha Utafiti cha Dar-es-Salaam.

Katika mwaka 2010/2011, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kuendelea na utafiti kuhusu teknolojia sahihi ya kuzalisha vifaranga na vyakula bora vya samaki;

(ii) Kufanya uchunguzi wa kuanzisha utalii wa samaki aina ya Pomboo, Papa Nyangumi, Jodari na Kasa;

(iii) Kuanzisha mabwawa ya mfano ya ufugaji samaki katika vituo vya utafiti vya Dar es Salaam, Kigoma, Kyela, Mwanza na Sota (Rorya);

(iv) Kufanya savei ya mashamba ya samaki ili kutambua mbinu za kudhibiti madhara ya wadudu na magonjwa ya samaki;

(v) Kufanya utafiti wa hali ya uvuvi katika Ziwa Rukwa na Mto Ruvuma na Mto Mara;

(vi) Kufanya utafiti wa soko la samaki na mazao ya uvuvi katika maeneo ya Kyela na Kigoma;

(vii) Kufanya utafiti wa kiwango cha upotevu unaotokana na uchakataji wa samaki;

(viii) Kukarabati meli ya utafiti (MV Kiboko);

(ix) Kukamilisha ujenzi wa maabara ya Kituo cha Utafiti cha Dar es Salaam na maabara za Kyela, Mwanza, Sota na Kigoma; na

(x) Kuimarisha vituo vya utafiti vya Kyela, Mwanza, Sota na Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo - Mpwapwa pamoja na vituo sita vya Kongwa, Mabuki, Naliendele, Tanga, Uyole na West Kilimanjaro vilivyo chini ya Taasisi hiyo, vimeendelea na utafiti wa mifugo kwa lengo la kuongeza tija na uzalishaji wa mifugo nchini. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na:-

Kutathmini na Kusambaza Mifugo Bora Vijijini: Tathmini inaendelea, ambapo jumla ya ndama 200 walizalishwa katika Kituo cha Mpwapwa na kati ya hao, 95 ni aina ya Mpwapwa na 105 ni chotara wa Mpwapwa na Boran. Vilevile, ndama 20 chotara wa *Jersey/Friesian* na Ng'ombe wa Asili wamezaliwa katika kituo cha Tanga. Pia, ndama 12 wa ng'ombe wa Ufipa na ndama 10 wa ng'ombe aina ya *Friesian* wamezaliwa katika kituo cha Uyole na katika kituo cha Mabuki wamezaliwa ndama 3 aina ya Ankole. Aidha, mbuzi 160 aina ya Malya wamezaliwa katika vituo vya Mpwapwa (82) na Kongwa (78) na mbuzi 13 chotara wa Gogo na Malya wamezaliwa katika kituo cha Kongwa. Taasisi imeendelea kuzalisha nguruwe bora kwa ajili ya kusambaza kwa wafugaji vijijini ili kuboresha ufugaji wa nguruwe, ambapo 44 wamezaliwa kati yao 28 wamesambazwa kwa wafugaji vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, jumla ya madume bora 109 ya ng'ombe aina ya Mpwapwa yamepelekwa kwa wafugaji vijijini katika Wilaya za Manyoni (50), Bahi (30), Kongwa (8), Monduli (8), Shinyanga (7), Mpwapwa (2), Chamwino (2) na Mbeya vijijini (2) kwa ajili ya kuboresha mifugo ya asili. Aidha, madume 12 aina ya *Friesian* wamesambazwa katika Wilaya za Mbeya Mjini (3), Mbeya Vijijini (3), Mbarali (2), Mbozi (2), Sumbawanga (1) na Rungwe (1). Vilevile, jumla ya

majike 23 aina ya Mpwapwa yamesambazwa katika Wilaya za Chamwino (10), Singida Mjini (10), Dodoma Mjini (2) na Dar es Salaam (1). Pia mbuzi wa asili, mbuzi bora 61 wamesambazwa katika Wilaya za Kinondoni, Ilala, Temeke, Maswa, Shinyanga, Ngorongoro, Mpwapwa, Mtwara, Dodoma Mjini, Bahi, Kongwa na Chamwino. Tathmini ya uzalishaji wa mifugo iliyosambazwa inaendelea katika mazingira ya wafugaji vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka 2010/2011, ndama 250 aina ya Mpwapwa watazalishwa na madume 150 yatasambazwa katika vijiji mbalimbali kwa ajili ya kuboresha ng’ombe wa asili. Pia, ndama 30 wa ng’ombe wa maziwa aina ya *Friesian* watazaliwa na 12 (madume), watasambazwa. Aidha, mbuzi bora 200 aina ya Malya watazaliwa na madume 100 watasambazwa vijijini. Kazi zingine zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea kukusanya takwimu muhimu kuhusu ukuaji na uwezo wa kuzalisha mbuzi bora na utafiti shirikishi vijijini. Vilevile, utafiti utaendelea ili kubaini teknolojia zinazoongeza uzalishaji wa nguruwe vituoni na vijijini ambapo jumla ya nguruwe 200 watazaliwa na 180 watasambazwa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, jumla ya ng’ombe 55 aina ya Ufipa, 23 aina ya Ankole, 20 aina ya *Singida white* waliendelea kufanyiwa tathmini ya uwezo wa kuzalisha na mwonekano wa nje katika vituo vya Uyole, Mabuki na Mpwapwa. Tathmini ya awali kwa ng’ombe aina ya Ufipa inaonesha kuwa wastani wa uzito wa kuzaliwa ni kilo 18.4 (madume) na 17.3 (majike). Katika mwaka 2010/2011, Taasisi itaendelea kufanya tathmini ya ng’ombe wa asili ili kubaini uwezo wa kuzalisha na mwonekano wa nje. Aidha, Taasisi itanunua ng’ombe 20 aina ya *Iringa red* kwa ajili ya kuwafanyia tathmini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010 Taasisi imeendelea kutathmini aina mbalimbali za kuku wa asili vituoni. Kosaafu tano za kuku wa kienyeji aina ya *Njachama, Kuza, Msumbiji, Sukuma na Kishingo* zilikusanywa katika mikoa ya Mtwara na Lindi kwa ajili ya utafiti. Tathmini inaonesha kuwa, wastani wa uzito wa mayai ni kati ya gramu 30 na 45 na uzito wa kuku ni kati ya gramu 800 na 1,200. Pia, Kosaafu sita za kuku wa kienyeji aina ya *Kuchi, Kishingo, Sasamala, Bukini, King’weng’we (Fude)* na *Nteva* walikusanywa kutoka katika mikoa ya Dodoma na Singida na kuwahifadhi na kazi ya kuwatathmini inaendelea kituoni Mpwapwa. Aidha, katika kituo cha Uyole, kuku 54 wa asili aina ya *Kachewa* na *Kuchi* walikusanywa kutoka wilaya za Songea Vijijini, Namtumbo, Iringa Vijijini, Mufindi, Chunya, Mpanda, Nkasi na Sumbawanga vijijini kwa ajili ya kuwatathmini na kuwahifadhi.

Katika mwaka 2010/2011, Taasisi itaendelea kufanya yafuatayo:-

(i) Kuainisha kuku wenye sifa za kutaga mayai mengi na ukuaji kutoka katika aina za kuku waliokwisha kusanywa;

(ii) Kufanya utafiti utakaowezesha kuku wa asili kuongeza utagaji kwa asilimia 10, uzito wa yai kwa asilimia 10 na ukuaji kwa asilimia 15; na

(iii) Kuhifadhi aina za kuku wa asili ambao wako hatarini kutoweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, tathmini ya mbuzi aina ya *Gogo white*, *Upare white, Sonjo red*, Newala na kondoo aina ya *Red Maasai, Black Head Persian* na Gogo iliendelea kufanyika katika vituo vya Mpwapwa, West Kilimanjaro na Naliendele. Matokeo ya awali ya ukuaji yanaonesha kuwa wastani wa uzito wa kuzaliwa kwa madume ni kilo 2.3 na majike ni kilo 1.9 kwa mbuzi aina ya *Sonjo Red*; na kilo 2.0 kwa madume na kilo 1.9 kwa majike aina ya *Upare White*. Aidha, wastani wa uzito katika umri wa kuachishwa kunyonya wanapofikia miezi mitatu ni kilo 7.8 kwa madume na kilo 6.5 kwa majike wa mbuzi aina ya *Sonjo Red*; na kilo 5.3 kwa madume na kilo 4.5 kwa majike wa mbuzi aina ya *Upare White*. Vilevile, tathmini ya awali inaonesha kuwa wastani wa uzito wa kuzaliwa kwa kondoo aina ya *Red Maasai* ni kilo 2.5 kwa madume na majike; na kilo 2.4 kwa madume na majike wa kondoo aina ya *Black Head Persian (BHP)*. Wastani wa uzito wanapofikia umri wa miezi mitatu ni kilo 9.7 kwa madume na kilo 9.4 kwa majike wa kondoo aina ya *Red Maasai*; na kilo 9.9 kwa madume na kilo 8.8 kwa majike wa aina ya *BHP*. Katika mwaka 2010/2011 tathmini hii itaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Taasisi iliendelea kukusanya, kutathmini na kutunza aina mbalimbali za malisho kwenye Benki ya Vinasaba. Jumla ya vinasaba 152 viliendelea kufanyiwa tathmini katika vituo vya utafiti vya Mpwapwa (80) na Uyole (72). Katika mwaka 2010/2011 aina nyingine 50 za malisho kutoka nje na ndani ya nchi zitakusanywa, kustawishwa, kutathminiwa na kuhifadhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, jumla ya kilo 3,549 za mbegu za nyasi aina za *Chloris gayana* na *Cenchrus ciliaris* na kilo 875 za mikunde zilizalishwa katika vituo vya Mpwapwa, Tanga, Uyole na Mabuki. Kati ya hizo, kilo 688 za mbegu za *Chloris gayana* ziliuzwa kwa ajili ya kuendeleza malisho katika Chuo cha Mafunzo ya Mifugo Mpwapwa (kilo 200) na katika Wilaya za Nkasi (kilo 250), Mbarali (kilo 84), Rungwe (kilo 50), Mbeya Vijijini (kilo 50), Kiteto (kilo 30) na Mufindi (kilo 24). Pia, kilo 26 za mbegu za malisho jamii ya mikunde zilisambazwa katika Chuo cha Mafunzo ya Mifugo Mpwapwa (kilo 10), Wilaya za Songea (kilo 6) na Nkasi (kilo 10). Vilevile, usambazaji wa miche ya miti malisho aina ya *Leucaena pallida* miche 18,000 na *Gliricidia sepium* miche 12,000 umefanyika katika Wilaya za Kongwa na Singida Vijijini kwa lengo la kuboresha malisho hasa wakati wa kiangazi. Aidha, vinasaba vya mbegu za malisho aina tatu za mikunde *(Centrosema, Clitoria na Siratro)* na aina mbili za nyasi (*Chloris gayana* na *Cenchrus ciliaris*) zimesambazwa katika Wilaya za Nyamagana, Ilemela na Ukerewe. Pia, marobota 15,340 ya majani makavu yalivunwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Taasisi itazalisha kilo 3,000 za mbegu za nyasi, kilo 600 za mbegu za mikunde ya malisho, kusambaza vinasaba vya malisho na miti malisho vinavyoonekana kuzalisha malisho mengi kwa wafugaji na kuongeza uvunaji wa malisho kufikia marobota 40,000 ya majani makavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea kuimarisha vituo vya utafiti wa mifugo kwa kuvipatia vitendea kazi muhimu, vikiwemo trekta tatu na zana zake, mashine za kuangulia vifaranga tatu, pikipiki 11 na kompyuta saba. Aidha, ukarabati wa nyumba 41 za watumishi na ofisi nne umefanyika katika vituo

vya utafiti. Katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kuimarisha vituo vya utafiti kwa kuvipatia vitendea kazi muhimu, kujenga na kukarabati miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maabara Kuu ya Taifa ya Mifugo – Temeke inalo jukumu la kufanya uchunguzi, utambuzi na utafiti wa magonjwa mbalimbali ya mifugo. Aidha, inafanya majaribio ya dawa mpya na chanjo za mifugo; kutengeneza chanjo mbalimbali za kuzuia magonjwa ya mifugo na kuchunguza ubora wa bidhaa zitokanazo na mifugo. Pia, maabara hufanya uchunguzi wa nguvu za dawa za majosho, ubora wa vyakula vya mifugo na kutoa mafunzo ya Ufundi Sanifu Maabara na Stashahada ya Afya ya Wanyama.

Katika mwaka 2009/2010, Maabara Kuu ya Mifugo imetekeleza yafuatayo:-

(i) Kufanya uchunguzi na utambuzi wa magonjwa mbalimbali ya mifugo kutokana na sampuli 18,770. Baadhi ya magonjwa muhimu yaliyotambuliwa ni Homa ya Nguruwe, Ndigana Kali, Mkojo Mwekundu, Ndigana Baridi, Nagana, Ugonjwa wa Miguu na Midomo, Homa ya Matumbo ya Ndege, Mdondo, *Mareks Disease, Gumboro* na Sotoka ya Mbuzi na Kondoo;

(ii) Kuzalisha na kusambaza chanjo dozi milioni 82.2 za ugonjwa wa Mdondo; 313,950 za Kimeta; 271,400 za Chambavu; na 25,000 za Ugonjwa wa Kutupa Mimba. Aidha, utengenezaji wa chanjo ya Homa ya Bonde la Ufa (*RVF*) umeanza na chanjo hiyo ipo katika majaribio ya awali;

(iii) Kufanya uchunguzi na kuhakiki ubora wa vyakula vya mifugo, ambapo sampuli 3,899 zilihakikiwa na kuonesha kuwa zaidi ya asilimia 80 ya sampuli hizo zilikuwa na upungufu wa viinilishe na ushauri kutolewa;

(iv) Kuendelea na ujenzi wa kituo cha kuzalisha chanjo Kibaha ambapo nyumba mbili za wafanyakazi zimekamilika;

(v) Kuendelea na ukarabati wa Maabara Kuu ya Mifugo na kuimarisha Taasisi ya Utafiti wa Mbung'o na Ndorobo Tanga na Kituo cha Udhibiti wa Mbung'o na Ndorobo Kigoma;

(vi) Kuendelea na ufugaji wa mbung'o katika kituo cha TTRI Tanga kwa ajili ya utafiti wa kudhibiti mbung'o, ugonjwa wa nagana na malale. Aina na idadi ya mbung'o waliohasiwa katika kituo hicho ni *Glossina pallidipes* (987 na mabuu 151), *G. austeni* (25,928) na mabuu 5,114), *G. brevipalpis* (45 na mabuu 5) na *G. morsitans centralis* (6,720 na mabuu 1,513);

(vii) Kufanya tathimini ya chanjo ya kuzuia mdondo inayostahimili joto (*I-2*) katika mikoa ya Iringa, Mbeya, Morogoro, Singida na Tanga;

(viii) Kufanya uchunguzi wa ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa (RVF) katika mikoa ya Iringa na Morogoro;

(ix) Kufanya uchunguzi kuhusu sotoka ya mbuzi na kondoo katika mikoa ya Iringa na Mbeya;

(x) Kufanya uchunguzi wa Ugonjwa wa Miguu na Midomo katika mikoa ya Iringa, Lindi, Mbeya, Morogoro na Mtwara;

(xi) Kufanya uchunguzi wa Homa ya Nguruwe katika mikoa ya Morogoro na Pwani; na

(xii) Kufanya uchunguzi wa Mafua Makali ya Ndege katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Manyara, Mara, Mbeya Morogoro, Mwanza na Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Maabara Kuu itazalisha na kusambaza katika Halmashauri chanjo za kuzuia magonjwa mbalimbali zikiwa ni pamoja na dozi milioni 100 za Mdondo, 500,000 za Kimeta, 400,000 za Chambavu 25,000 za Ugonjwa wa Kutupa Mimba na milioni 5 za Homa ya Bonde la Ufa (*RVF)*. Pia, Maabara itafanya kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea kufanya uchunguzi, utambuzi na utafiti wa magonjwa mbalimbali ya mifugo;
(ii) Kuendeleza ufugaji wa aina mbalimbali za mbung'o kwa ajili ya tafiti za kudhibiti nagana na malale;

(iii) Kuendelea kufanya uchunguzi na uhakiki wa ubora wa vyakula vya mifugo pamoja na malisho katika maeneo mbalimbali;

(iv) Kuendelea na uchunguzi na uhakiki wa ubora wa mazao ya mifugo yakiwemo maziwa, nyama na mayai;

(v) Kuchunguza nguvu za dawa za kuogesha mifugo;

(vi) Kuendelea na tafiti mbalimbali za kutathimini na kuanzisha teknolojia mpya za kudhibiti magonjwa ya mifugo; na

(vii) Kuimarisha Maabara Kuu ya Mifugo na vituo vyake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuimarisha Maabara ya Taifa ya Udhibiti wa Ubora wa Samaki – Nyegezi kwa kukarabati miundombinu na kutoa vitendea kazi. Jumla ya sampuli 1,354 za minofu ya samaki, maji na tope zilipokelewa na kufanyiwa uchunguzi ili kubaini vimelea, masalia ya viuatilifu, mabaki ya sumu na madini tembo. Kati ya sampuli zilizopokelewa, 849 zilichunguzwa katika maabara ya Nyegezi na 505 zilichunguzwa katika maabara za Shirika la Viwango Tanzania, SABS (Afrika Kusini) na Chemipher (Uganda). Pia, ukaguzi umefanyika mara 1,114 kwa samaki na mazao yake wakati wa kusafirishwa nje ya nchi. Vilevile, kaguzi 84

zimefanyika katika viwanda vya kuchakata samaki vilivyoko katika ukanda wa Ziwa Victoria. Pia, wakaguzi watatu walipatiwa mafunzo nchini Afrika Kusini.

Katika mwaka 2010/2011, Maabara itaendelea kuimarishwa ili kuendeleza udhibiti wa ubora wa samaki na mazao ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Veterinari lina jukumu la kusimamia viwango vya huduma zinazotolewa na wataalamu wa afya ya mifugo nchini. Katika mwaka 2009/2010, Baraza limeimarisha ukaguzi katika ngazi za Kanda, Mikoa na Halmashauri kwa kuteua wakaguzi wapya 25 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Aidha, Baraza lilitekeleza yafuatayo:-

(i) Kufuatilia ukaguzi wa maadili katika Halmashauri 123 za mikoa ya Dar-es-Salaam, Dodoma, Iringa, Kagera, Lindi, Mara, Mbeya, Morogoro, Mtwara Mwanza, Pwani na Ruvuma. Kutokana na ukaguzi huo, wataalam 6 walipata maonyo makali na 2 wameshtakiwa kwa kutoa huduma bila kusajiliwa;

(ii) Kuteua wasajili wasaidizi 101 katika Halmashauri na wakaguzi 173 katika Halmashauri, Mikoa na Kanda. Aidha, wakaguzi 130 walipatiwa mafunzo kuhusu kanuni na taratibu za ukaguzi wa huduma za mifugo;

(iii) Kusajili madaktari 22 wakiwemo 4 wa kigeni na kufanya idadi ya madaktari waliosajiliwa nchini kuwa 615. Aidha, vituo 5 vya kutolea huduma vimesajiliwa na kufanya jumla ya vituo kuwa 309;

(iv) Kuandikisha na kuorodheshwa wataalamu wasaidizi 110 wenye stashahada na astashahada na kufanya idadi yao kuwa 1,026;

(v) Kuchapisha na kusambaza kwa wadau nakala 1,100 za orodha za wataalam waliosajiliwa na kanuni za ukaguzi chini ya Sheria ya Veterinari Na. 16, 2003;

(vi) Kuhamasisha Halmashauri 60 za mikoa ya Dar-es-Salaam, Dodoma, Iringa, Kagera, Lindi, Mara Mbeya, Morogoro, Mwanza, Mtwara, Pwani, Ruvuma, Shinyanga, Singida na Tanga kushirikisha sekta binafsi katika kutoa huduma za mifugo;

(vii) Kuandaa na kusambaza miongozo 3 juu ya viwango vya zahanati za mifugo, vifaatiba na dawa kwa watoa huduma;

(viii) Kujenga zahanati mbili za mifugo za mfano katika vyuo vya mifugo vya Morogoro na Mpwapwa;

(ix) Rasimu ya Mpango wa kuendesha Baraza umeandaliwa na watumishi 3 wamepata mafunzo kuhusu kuendesha baraza kwa ufanisi; na

(x) Kuboresha mfumo wa ukusanyaji na utunzaji wa kumbukumbu za Baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011 Baraza la Veterinari litaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Veterinari Na. 16 ya Mwaka 2003 kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kusajili madaktari wa mifugo 30 na vituo vya huduma za mifugo 24 na kuvifanyia ukaguzi vituo 90;

(ii) Kuorodhesha na kuandikisha wataalam wasaidizi wasiopungua 80;

(iii) Kushirikiana na Halmashauri 132 kufanya ukaguzi wa maadili nchini na kutoa mafunzo kwa wakaguzi 130 wa maadili;

(iv) Kufanya ukaguzi wa taaluma katika vyuo vitoavyo astashahada, stashahada na shahada ya mifugo; na

(v) Kushirikiana na Halmashauri 80 kuhamasisha sekta binafsi kutoa huduma za mifugo kupitia vituo vya afya ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuimarisha usimamizi wa Sheria ya Veterinari Na. 16 ya Mwaka 2003, natoa wito kwa kila Halmashauri ya Wilaya, Mji, Manispaa na Jiji kuhakikisha inaajiri madaktari wa mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuainisha maeneo ya kipaumbele ya utafiti wa mifugo katika mwaka 2009/2010, Wizara iliandaa rasimu 12 za programu za utafiti. Programu hizo zinahusu utafiti wa ng’ombe wa maziwa; ng’ombe wa nyama; mbuzi na kondoo; kuku; nguruwe; lishe na malisho; kosaafu za mifugo; magonjwa ya milipuko; magonjwa yanayoenezwa na kupe na mbung’o; utambuzi wa magonjwa; uzalishaji wa chanjo za mifugo; na magonjwa ya mifugo yanayoambukiza binadamu. Katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuratibu, kufuatilia na kutathmini utafiti na utoaji huduma za utafiti na maendeleo ya mifugo na uvuvi kulingana na programu zilizotayarishwa;

(ii) Kuimarisha mfumo wa utunzaji kumbukumbu za utafiti wa mifugo na uvuvi nchini;

(iii) Kushirikiana nchi za Kenya, Uganda na Ethiopia katika kuainisha teknolojia za uzalishaji wa maziwa, kuzitathmini na kuzisambaza kwa wafugaji;

(iv) Kuwezesha taasisi za utafiti wa mifugo na uvuvi nchini; na

(v) Kuandaa programu 3 za ufugaji samaki na udhibiti wa mazingira yake;

(vi) Kuandaa agenda ya utafiti wa mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara imeendelea kuimarisha na kuiwezesha Mifuko ya Utafiti na Maendeleo ya Kanda 7 za utafiti *(Zonal Agricultural Research Development and Extension Fund – ZARDEF*) kwa kuipatia jumla ya shilingi milioni 600 iliyowezesha kugharamia miradi 43 ya utafiti kulingana na vipaumbele vya Kanda husika. Aidha, Vitengo vya mawasiliano ya utafiti vya kanda vimeimarishwa. Pia, kanda zote zilikamilisha awamu ya kwanza ya mafunzo kuhusu Utafiti Shirikishi wa Kilimo na Mifugo kulingana na mahitaji ya wadau *(Client Oriented Research and Development Management Approach – CORDEMA)* kwa wataalamu 349. Katika mwaka 2010/2011, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kuwezesha Mifuko ya *ZARDEF* kuendeleza kufanya utafiti kulingana na vipaumbele vya kanda na mahitaji ya wadau chini ya Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo – *ASDP;*

(ii) Kushirikiana na Taasisi za kitaifa na kimataifa kuratibu utafiti shirikishi wa mifugo;

(iii) Kuratibu utoaji wa mafunzo ya utafiti shirikishi katika awamu ya pili;

(iv) Kuratibu mafunzo ya muda mfupi kwa watafiti na wataalamu wengine 30 na ya muda mrefu kwa watafiti na wataalamu wengine 19;

(v) Kutoa ushauri wa kitaalam kwa watafiti juu ya uandishi wa mapendekezo ya utafiti; na

(vi) Kuratibu kazi za utafiti za vituo 5 vya Utafiti wa Uvuvi na Vyuo vya Mbegani na Nyegezi na kupitia na kuboresha ajenda ya Utafiti wa Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea na jukumu la kuandaa na kuratibu mafunzo kwa wataalam wa Sekta za Mifugo na Uvuvi, ikiwa ni pamoja na kukuza na kuendeleza mitaala.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara imeendelea kuwawezesha watafiti na watumishi wa kada nyingine kwa kuwapatia mafunzo katika fani mbalimbali. Jumla ya watumishi 28 wamepatiwa mafunzo, kati ya hao, 5 Shahada ya Uzamivu, 19 Shahada ya Uzamili na 4 Shahada ya kwanza. Pia, mafunzo ya muda mfupi yalitolewa kwa watumishi 50. Vilevile, wanachuo 1,221 wakiwemo 742 wa stashahada na 479 wa astashahada wameendelea na mafunzo katika vyuo 6 vya mifugo vya Buhuri, Madaba, Morogoro, Mpwapwa, Temeke na Tengeru. Kati ya hao wanaume ni 842 na wanawake ni 379. Wanachuo 546 wamemaliza mafunzo yao mwezi Juni, 2010 katika Stashahada za Afya ya Mifugo (211), Uzalishaji wa Mifugo (146) na Astashahada ya Afya ya Mifugo na Uzalishaji (189) na kupangiwa vituo vya kazi katika Halmashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na wafadhili mbalimbali wakiwemo *Heifer International Tanzania, World Vision*,

KKKT na MVIWATA, ilitoa mafunzo ya muda mfupi kwa wafugaji 1,120 wakiwemo wanawake 463 na wanaume 657. Mafunzo hayo yalihusu ufugaji wa ng'ombe na mbuzi wa maziwa, kuku, uendelezaji wa malisho, uboreshaji wa zao la ngozi, usindikaji wa maziwa na afya ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilikarabati ofisi 5, madarasa 10, mabweni 20, nyumba za watumishi 20, mabwalo 5, hosteli 7, maabara 4, bwawa moja, kisima kimoja na kuvipatia vitendea kazi ili kuviwezesha kudahili wanafunzi 2,500 kwa mwaka. Aidha, Wizara iliwasilisha kwa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE)* mihtasari ya Stashahada ya Afya ya Mifugo, Stashahada ya Uzalishaji wa Mifugo, Stashahada ya Mafundi Sanifu Maabara ya Mifugo na Astashahada ya Afya na Uzalishaji kwa ajili ya uhakiki na kupatiwa ithibati. Pia, Wizara ilichapisha na kusambaza nakala 300 za vitabu vya rejea kuhusu mbari za mifugo, uhimilishaji na mazao ya mifugo kwenye Maktaba za Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo na nakala 100 zimesambazwa kwa wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kuboresha mazingira ya vyuo kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuongeza uwezo wa vyuo vya mifugo kuweza kuchukua wanafunzi 2,000 kwa mwaka, ambapo kwa mwaka 2010/2011 mafunzo yatatolewa kwa wanafunzi 1,500;

(ii) Kuweka kwenye moduli na kuiwasilisha *NACTE* mihtasari ya Stashahada ya Utunzaji wa Nyanda za Malisho na Udhibiti wa Ndorobo pamoja na wa Stashahada ya Afya na Uzalishaji wa Mifugo;

(iii) Kuhamasisha sekta binafsi kugharamia mafunzo na kuanzisha vyuo binafsi;

(iv) Kuendesha tathmini za mafunzo ili kubaini mahitaji mapya ya mafunzo katika soko la ajira;

(v) Kuimarisha usimamizi na ukaguzi wa vyuo, kuhakiki utekelezaji wa mitaala na kuratibu shughuli za mitihani;

(vi) Kuwezesha mafunzo kwa wakufunzi 12 katika ngazi ya uzamili na 3 katika ngazi ya uzamivu. Pia, kuwezesha mafunzo ya muda mfupi kwa wakufunzi 20 kuhusu mbinu za ufundishaji;

(vii) Kuanzisha Wakala wa Mafunzo ya Mifugo ili kuongeza ufanisi katika kutoa elimu ya ufugaji; na

(viii) Kuimarisha uwezo wa watumishi, ambapo wataalam 21 watapatiwa mafunzo ya muda mrefu na 32 muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya uvuvi kwa wanafunzi 294 katika vyuo vya Mbegani (210) na Nyegezi (84) katika ngazi za Astashahada na Stashahada. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni:-

(i) Kuimarisha vyuo kwa kukarabati majengo na miundombinu muhimu na kuvipatia vitendea kazi;

(ii) Kuvipatia vyuo vya Nyegezi na Mbegani vifaa vya kufundishia;

(iii) Kuanza mchakato wa kuanzisha Wakala wa Mafunzo ya Uvuvi ambapo vyuo vya Nyegezi na Mbegani vitakuwa chini yake; na

(iv) Kugharamia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ya taaluma za uvuvi kwa watumishi 36, wakiwemo 5 katika Shahada ya Uzamivu, 10 Shahada ya Uzamili, 5 Shahada ya Kwanza, 5 Stashahada, 2 Astashahada na 9 mafunzo ya muda mfupi kupitia mradi wa *MACEMP* na wafadhili wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kuboresha mazingira ya vyuo vya mafunzo ya uvuvi kwa kuvikarabati na kuvipatia vifaa vya kufundishia. Aidha, Wizara itapanua uwezo wa vyuo hivyo ili kuviwezesha kutoa mafunzo kwa wanachuo 500 katika ngazi ya Astashahada na Stashahada, ambapo katika mwaka 2010/2011, mafunzo yatatolewa kwa wanafunzi 300. Pia, Wizara itagharamia mafunzo kwa watumishi 37 wakiwemo 4 wa shahada ya uzamivu, 16 shahada ya uzamili, shahada ya kwanza 5 na 12 wa muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, uzalishaji wa maziwa uliongezeka kutoka lita bilioni 1.60 mwaka 2008/2009 hadi lita bilioni 1.65, sawa na ongezeko la asilimia 2.8. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa ukusanyaji wa maziwa na idadi ya ng'ombe wa maziwa 75,000. Kati ya kiasi hicho lita milioni 653 zilitokana na ng'ombe wa kisasa na lita milioni 997 kwa ng'ombe wa asili. Pamoja na ongezeko hili, uzalishaji wa maziwa kutoka mifugo ya asili ulipungua kutokana na uhaba wa malisho uliosababishwa na ukame ulioyakumba maeneo mbalimbali nchini hasa maeneo ya kaskazini na kati ambako wafugaji wengi wa asili huendesha shughuli zao. Aidha, unywaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita 42 kwa mwaka 2008/2009 hadi lita 43 kwa mtu kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kukarabati mashamba ya kuzalisha mitamba, kupima mashamba na kuyapatia vitendea kazi ili yaweze kuzalisha kwa ufanisi. Katika mwaka 2009/2010, Wizara ilitekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kukarabati mfumo wa maji katika shamba la Kitulo na nyumba 3 za watumishi katika mashamba ya Kitulo na Nangaramo;

(ii) Kupima maeneo ya mashamba ya Sao Hill, Nangaramo na Ngerengere ili kuyapatia hati miliki;

(iii) Kununua matrekta 2 na vifaa vyake kwa ajili ya mashamba ya Kitulo na Sao *Hill,* pikipiki 2 kwa ajili ya Mabuki na Kitulo, *bailer* moja kwa ajili ya kituo cha Mabuki; na

(iv) Kununua ng'ombe wazazi 100 kwa ajili ya mashamba ya Nangaramo na Ngerengere, madume ya mbuzi aina ya *boer* 12 na madume 10 ya *boran* ili kuimarisha kundi la ng'ombe wazazi (*stud herd*) katika Shamba la Ngerengere.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, jumla ya mitamba 624 ilizalishwa na Mashamba ya Serikali na kusambazwa kwa wafugaji wadogo katika mikoa ya mbalimbali ya Tanzania Bara. Aidha, Wizara kwa kushirikiana Kampuni ya Ranchi za Taifa na Mashirika yasiyo ya Kiserikali ilisambaza jumla ya mitamba 5,427 kwa wafugaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2010/2011, Wizara itaendelea kuimarisha mashamba ya kuzalisha mifugo kwa kuyanunulia ng'ombe wazazi 100, vifaa na vitendea kazi ili kuongeza uzalishaji wa mitamba katika mashamba hayo, pamoja na kuendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wake. Aidha, Wizara itakamilisha mchakato wa upatikanaji wa hati miliki kwa mashamba yake yote 5 ya Kitulo, Mabuki, Nangaramo, Ngerengere na Sao Hill. Aidha, Wizara itaanza mchakato wa kutafuta maeneo ya kuanzisha mashamba mengine ya mifugo katika mikoa mitano ya Kigoma, Lindi, Manyara, Rukwa na Tabora, pamoja na kuyatafutia mitaji kutoka katika vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, usindikaji wa maziwa umeendelea kuongezeka kutokana na juhudi za Wizara kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika viwanda vya kusindika maziwa pamoja na kupata ushindani wa bidhaa zitokanazo na maziwa kutoka nje. Katika mwaka wa 2009/2010, kiasi cha maziwa kinachosindikwa kwa siku *(operating capacity)* kimeongezeka kutoka lita 88,940 mwaka 2008/2009 hadi lita 105,380 mwaka 2009/2010 sawa na ongezeko la asilimia 18.9. Ongezeko hilo limetokana na kuimarika kwa shughuli za usindikaji katika viwanda vikubwa na vya kati vya Tanga Fresh, Mara Milk, Tan *Dairies* na Musoma *Dairy* na kuanzishwa kwa viwanda vidogo vikiwemo viwanda vya Engiteng (Longido, Orkesumet, Naberera, Same na Terrat).

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika juhudi za kuhamasisha usindikaji wa maziwa nchini Wizara imefanya uchunguzi wa upatikanaji wa maziwa kwa ajili ya ukusanyaji na usindikaji katika Kanda ya Mashariki. Aidha, uchunguzi kama huo umefanywa katika Kanda ya Kati na Shirika lisilo la Kiserikali la *Rural Livelihood Development Company – RLDC*. Chunguzi hizo zimebaini kuwepo kwa maeneo yenye maziwa ya ziada hasa kwenye kipindi cha malisho mengi na wadau wamehamasishwa kuwekeza katika maeneo hayo. Pia, Wizara imeandaa Andiko la Programu ya Unywaji wa Maziwa Shuleni na kuliwasilisha Serikalini kwa lengo la kuombea fedha ili lianze kutekelezwa sambamba na Programu ya Majaribio ya Unywaji wa Maziwa Shuleni inayoratibiwa na Bodi ya Maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea na chunguzi hizo katika Kanda ya Ziwa na Nyanda za Juu Kusini ili kubaini maeneo yenye maziwa ya ziada na kuendelea kuwahamasisha wadau wa maziwa kuwekeza katika

biashara na usindikaji wa maziwa. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuimarisha ukusanyaji wa maziwa ili kuongeza usindikaji wa maziwa kufikia lita 110,000 kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhimilishaji ni teknolojia mojawapo inayotumika kuongeza ubora wa mifugo. Wizara imeendelea kuratibu na kuhamasisha matumizi ya teknolojia hiyo kwa kuimarisha na kuongeza Vituo vya Kanda vya Uhimilishaji. Katika mwaka 2009/2010, Wizara ilifanya yafuatayo:-

(i) Kuanzisha Kituo cha Kanda ya Kusini (Lindi) na kuimarisha Kituo cha Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya) kwa kukipatia mitambo ya kutengeneza hewa baridi ya naitrojeni;

(ii) Kununua vifaa vya uhimilishaji kwa ajili ya vituo 5 vya Kanda vya Kanda ya Ziwa (Mwanza), Kati (Dodoma), Mashariki (Kibaha), Kusini (Lindi) na Nyanda za Juu Kusini (Mbeya);

(iii) Kuimarisha Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji – *NAIC* – Usa River kwa kukinunulia vifaa vya maabara na vya uhimilishaji;

(iv) Kuzalisha dozi 86,800 za mbegu za uhimilishaji ikiwa ni ongezeko la asilimia 15 ikilinganishwa na mwaka 2008/2009;

(v) Kuhimilisha ng’ombe 73,900 ikiwa ni ongezeko la asilimia 7 ikilinganishwa na mwaka 2008/2009;

(vi) Kuzalisha lita 24,600 ya hewa baridi ya naitrojeni katika kituo cha *NAIC*;

(vii) Kufundisha wataalamu wa uhimilishaji 402 ikiwa ni ongezeko la asilimia 24 ikilinganishwa na mwaka 2008/2009; na

(viii) Kuandaa Kanuni ya Uhimilishaji chini ya Sheria ya Magonjwa ya Mifugo Na. 17 ya Mwaka 2003.

Katika mwaka wa 2010/2011, Wizara itaendeleza uhimilishaji kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuanzisha kituo cha Kanda ya Magharibi (Tabora) na Mkoa wa Tanga kwa kuvipatia mtambo wa kutengeneza hewa baridi ya naitrojeni;

(ii) Kuimarisha vituo vyote vitano vya kanda vya uhimilishaji kwa kuvipatia vitendea kazi;

(iii) Kununua madume bora 10 kwa ajili ya mbegu za uhimilishaji; na

(iv) Kuzalisha dozi 100,000 za mbegu za uhimilishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kushirikiana na wadau wa nyama kuendeleza sekta ndogo ya nyama ambayo inahusisha ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe na kuku. Katika mwaka 2009/2010, uzalishaji wa nyama uliongezeka kwa asilimia 6.1 kutoka tani 422,230 mwaka 2008/2009 hadi tani 449,673 mwaka 2009/2010. Kati ya hizo, nyama ya ng'ombe ni tani 243,943, mbuzi na kondoo tani 82,884, nguruwe tani 38,180 na kuku tani 80,916. Ongezeko hilo limetokana na wafugaji kuuza mifugo yao kama tahadhari ya kuepuka hasara kutokana na ukame ulioyakumba maeneo mengi nchini mwaka 2009. Aidha, kupungua kwa bei ya mifugo wakati huo wa ukame kulihamasisha wafanyabiashara kununua mifugo kwa ajili ya kuchinja. Ongezeko hilo pia lilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya nyama na mazao yake na kupanuka kwa wigo wa masoko, ambapo masoko maalum kama vile maduka makubwa, migodi na hoteli zimeongeza ununuzi wa nyama inayozalishwa hapa nchini na kupunguza uagizaji kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za kuongeza ubora wa nyama, Wizara imeendelea kuhamasisha mfumo wa unenepeshaji wa mifugo kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya. Mfumo huu wa unenepeshaji umeendelea kupokelewa na wafanyabiashara wa mifugo hasa wa Mikoa ya Kanda ya Ziwa na ya Kati na jumla ya ng'ombe 74,400 walinenepeshwa mwaka 2009/2010 likiwa ni ongezeko la asilimia 20 ikilinganishwa na ng'ombe 62,000 walionenepeshwa mwaka 2008/2009. Katika mwaka wa 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa nyama itaendelea kuhamasisha wafugaji na wafanyabiashara ya mifugo kuwekeza kwenye ufugaji wa kisasa ukiwemo wa ranchi na unenepeshaji ili kunenepesha ng'ombe 85,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa kuku na mayai nchini umeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2009/2010, jumla ya vifaranga milioni 35.6 vya kuku wa kisasa vilizalishwa nchini na vifaranga 251,503 vya kuku wazazi viliagizwa kutoka nje. Vilevile, mayai milioni 6.03 ya kutotoa vifaranga yaliagizwa kutoka nje. Kutokana na wafugaji kuhamasika kufuga kuku uzalishaji wa mayai uliongezeka kutoka bilioni 2.81 mwaka 2008/2009 hadi mayai bilioni 2.9 mwaka 2009/2010. Idadi ya kuku wa asili imeongezeka kutoka milioni 34 mwaka 2008/2009 na kufikia milioni 35 mwaka 2009/2010. Katika juhudi za kuhamasisha ufugaji wa kuku wa asili, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo *(FAO)* na Halmashauri zimehamasisha matumizi ya kasha maalumu linalohifadhi joto la kutunzia vifaranga ambalo linaweza kutumika kwenye maeneo ya vijijini kwani halitumii nishati yoyote. Teknolojia hiyo ya asili imesambazwa katika mikoa ya Dodoma, Singida, Pwani, Mbeya, Iringa, Dar es Salaam na Morogoro.

Mheshimiwa Nabu Spika, katika mwaka wa 2010/2011, Wizara itaendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia sahihi za ufugaji wa kuku ikiwemo ya utumiaji wa kasha la kutunzia vifaranga katika mikoa mikoa kumi. Aidha, Wizara itahamasisha uzalishaji wa mayai kufikia bilioni 3.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa nyama ya nguruwe umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na kuongezeka kwa mahitaji. Katika mwaka

2009/2010 uzalishaji wa nyama ya nguruwe umeongezeka kutoka tani 36,000 mwaka 2008/2009 hadi tani 38,180. Katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kuliimarisha Shamba la Ngerengere na kulipatia nguruwe bora kwa ajili ya mbegu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kuzihamasisha Halmashauri kutenga maeneo ya ufugaji na kuhakikisha wafugaji wanamilikishwa na kuyaendeleza ili kuwa na mipango ya ufugaji wa kisasa na endelevu kama inavyoelekeza Sheria ya Vijiji Na. 5 ya Mwaka 1999. Katika mwaka 2009/2010, jumla ya hekta 32,094.87 zimepimwa katika vijiji 26 katika Halmashauri za Kilombero, Kilosa, Kilwa, Mkuranga, Mpanda, Musoma, Rufiji na Ulanga. Hadi sasa jumla ya hekta 1,423,201.28 zimepimwa katika vijiji 266.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa mbegu bora za malisho ni muhimu katika kuendeleza ufugaji nchini. Ili kuongeza upatikanaji wa mbegu bora za malisho na kukidhi mahitaji ya wafugaji na wadau wengine, Wizara imeendelea kuimarisha mashamba ya mbegu za malisho ya Vikuge (Pwani) na Langwira (Mbeya) kwa kukarabati ofisi na nyumba za kuishi wataalam, kununua trekta na vifaa vya ofisi na kuweka umeme kwenye ofisi. Katika mwaka 2009/2010, mashamba ya taasisi za umma yamezalisha jumla ya tani 45 za mbegu bora za malisho na marobota 303,000 ya hei. Aidha, sekta binafsi imezalisha marobota 418,831.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuimarisha mashamba 8 ya serikali ya uzalishaji wa mbegu bora za malisho ili kuzalisha tani 50 za mbegu na marobota 450,000 ya hei;

(ii) Kuzijengea uwezo Halmashauri za Wilaya 40 kuhusu uzalishaji, utumiaji na uhifadhi wa malisho na Halmashauri za Wilaya 30 kuhusu uendelezaji wa nyanda za malisho;

(iii) Kuwezesha Wiki ya Ufugaji wa asili kwa wadau;

(iv) Kuandaa mpango kabambe wa kuendeleza nyanda za malisho;

(v) Kutoa mafunzo kwa wataalam 45 katika Halmashauri za wilaya 45 kuhusu matumizi ya *Geographical Information System-GIS*; na

(vi) Kuhamasisha matumizi endelevu ya rasilimali ardhi ili kupunguza migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa rasilimali ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2009/2010 ukame mkubwa uliikumba nchi na kusababisha madhara makubwa hususan kwa binadamu na mifugo kwa kukosekana malisho na maji katika Kanda ya kaskazini hasa mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro. Takwimu zinaonyesha kuwa ng'ombe wapatao 159,139 wenye thamani ya shilingi bilioni 47.7, mbuzi 21,783 wenye thamani ya shilingi milioni 871.3, kondoo

7,300 wenye thamani ya shilingi milioni 292.0 na punda 1,178 wenye thamani ya shilingi bilioni 1.2 walikufa katika Wilaya za Monduli, Longido, Ngorongoro, Kiteto na Simanjiro kati ya ng'ombe 1,304,384, mbuzi 497,498 kondoo 559,350 na punda 6,500 waliokuwepo kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweza kutoa tahadhari kwa wafugaji juu ya majanga katika muda muafaka Wizara inaimarisha Mfumo wa Kutoa Tahadhari ya Majanga ihusuyo mifugo nchini (*Livestock Early Warning System)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kuimarisha vituo vya kukusanya takwimu za majanga katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Mwanza, Shinyanga na Tabora na kuanzisha mfumo huo katika Kanda ya Kati. Aidha, Wizara itaimarisha mfumo huu katika Kanda ya Kusini kwa madhumuni ya kupanua matumizi ya mfumo huu nchi nzima. Pia, Wizara kwa kutumia taarifa za mfumo huu itashirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu Kitengo cha Maafa kuandaa mpango wa tahadhari wa kukabiliana na ukame na majanga mengine kwa upande wa mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyakula vilivyosindikwa ni muhimu katika kuongeza uzalishaji na tija kwa mifugo. Katika mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea kuratibu usindikaji na kusimamia ubora wa vyakula vya mifugo vinavyozalishwa na sekta binafsi. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara ilitoa mafunzo kwa wakaguzi wa chakula 20 kutoka katika Mikoa ya Mara, (Tarime, Rorya, Serengeti, Bunda na Musoma), Mwanza (Ilemela, Nyamagana, Magu, Misungwi, Sengerema, Geita na Kwimba) na Shinyanga (Kahama, Shinyanga, Kishapu, Maswa, Bariadi na Meatu) ili kuwajengea uwezo wa kudhibiti ubora wa vyakula vya mifugo. Aidha, tani 720,711 za aina mbalimbali ya vyakula vya mifugo zilizalishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011 kazi zifuatazo zitatekelezwa:-

(i) Kuwajengea uwezo wakaguzi 45 wa vyakula vya mifugo kutoka Halmashauri za Wilaya 45; na

(ii) Kuhamasisha sekta binafsi kuendelea kuwekeza katika usindikaji wa vyakula vya mifugo ili kuongeza uzalishaji wa vyakula vya mifugo nchini kufikia tani 830,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*) na Mradi wa Uwekezaji wa Wilaya katika Sekta ya Kilimo (*DASIP*) katika mwaka 2009/2010 iliwezesha kuchimba malambo 55 na kukarabati malambo 30 na kuchimba visima 8. Kazi zingine zilizotekelezwa na Wizara ni pamoja na:-

(i) Kuhamasisha na kutoa miongozo ya kujenga miundombinu ya maji ya mifugo kwa kusambaza nakala 357 kwa wadau mbalimbali wa ufugaji; na

(ii) Kukagua miundombinu ya maji katika Mikoa ya Manyara (7), Singida (7) na Lindi (6) na kubaini miundombinu mingi imeharibika. Hivyo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeshauriwa kukarabati miundombinu hiyo kupitia *DADPs.*

Katika mwaka 2010/2011 Wizara itaendelea kushirikiana na wadau wengine kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kufuatilia ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji kwa ajili ya mifugo;

(ii) Kuandaa mwongozo wa ujenzi wa malambo madogo kwa wafugaji; na

(iii) Kutambua vyanzo vya maji kwa ajili ya mifugo vilivyoendelezwa katika mikoa (6) ya Arusha, Manyara, Mara, Mwanza, Tabora na Singida na kuingiza kwenye *data base* na mfumo wa *Geographical Information System.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kudhibiti kuenea kwa magonjwa ya mifugo hasa yale ya mlipuko yenye kuleta madhara na hasara kwa wafugaji na uchumi wa Taifa kwa ujumla. Katika mwaka 2009/2010, Wizara imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kudhibiti magonjwa ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkakati wa Kudhibiti Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe *(CBPP)* unaendelea kutekelezwa ambapo chanjo dozi milioni 3.0 zilinunuliwa ili kupambana na ugonjwa huo katika Mikoa ya Kanda ya Magharibi na ya Kati. Jumla ya ng'ombe milioni 2.6 wamechanjwa na tathmini inaonesha kupungua kwa matukio ya ugonjwa huo nchini. Katika mwaka 2010/2011, Wizara itawezesha na kuendelea kuratibu uchanjaji wa ng'ombe milioni 3 katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa chini ya Mpango wa *"Roll Back Vaccination Plan."*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeanza kutekeleza Mkakati wa kudhibiti Ugonjwa wa Miguu na Midomo chini ya Mradi wa *SADC- TADs* wa kuimarisha maabara na vituo vya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo. Mradi huo unatekelezwa katika nchi za Tanzania, Angola, Malawi, Msumbiji na Zambia baada ya Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) kutoa fedha mapema mwaka 2009. Katika mwaka 2009/2010, Wizara imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kutoa mafunzo mbalimbali kwa watumishi 86.

(ii) Kuandaa taratibu za kudhibiti Ugonjwa wa Miguu na Midomo na kuhamasisha wadau kuhusu udhibiti wa Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe nchini kwa kuwahusisha wataalam wa mifugo kutoka Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Halmashauri, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (*SUA*), Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (*TAWIRI*) na Makao Makuu ya Wizara;

(iii) Kufanya uchunguzi wa Ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (*PPR*) katika Kanda za Kaskazini, Kusini na Ziwa kwa kuchunguza sampuli 4,000 kutoka kwenye mbuzi na kondoo;

(iv) Kununua vifaa mbalimbali vya kazi zikiwemo kompyuta 16 na seti 1 ya vifaa vya uchunguzi wa ugonjwa wa Sotoka *(Rinderpest test kits);* na

(v) Kununua pikipiki kumi na magari tisa kwa ajili ya ukaguzi wa mifugo na mazao yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika 2009/2010 Wizara kwa kupitia Shirika la Kilimo na Chakula Duniani imenunua dozi milioni 3.5 za chanjo ya Sotoka ya Mbuzi na Kondoo ambayo imetumika katika Halmashauri za mikoa ya Arusha, Manyara, Mara, Kilimanjaro, na Tanga ambazo zimechanja jumla ya mbuzi na kondoo 3,320,780.

Katika mwaka 2010/2011, Wizara itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kununua dozi milioni 5 za chanjo kwa ajili ya Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya ng'ombe na kuratibu uchanjaji na udhibiti wa ugonjwa;

(ii) Kununua vifaa kwa ajili ya Maabara Kuu ya Taifa ya Mifugo na Vituo vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo;

(iii) Kufanya uchunguzi wa aina ya virusi vya Ugonjwa wa Miguu na Midomo kwa wanyama wafugwao na wanyama pori; na

(iv) Kufanya tathmini ya ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF)* imeendelea kutekeleza Mkakati wa kudhibiti Mafua Makali ya Ndege *(Avian Influenza)* kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kutoa elimu na kuhamasisha umma kuhusu njia na tahadhari za kukabiliana na ugonjwa huo kwa kutayarisha na kusambaza vipeperushi na vijarida 10,000, mabango 15,000, na kupitia vyombo vya habari vikiwemo magazeti, radio na televisheni;

(ii) Kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii kufanya utafiti na kufuatilia ugonjwa huo kwenye njia kuu za mapitio ya ndege pori na katika makundi ya kuku na bata wafugwao ambapo jumla ya sampuli 2,500 za ndege pori, kuku na bata zilichunguzwa na kuthibitishwa kutokuwepo kwa ugonjwa nchini;

(iii) Kudhibiti uingizaji wa ndege au ndege pori, kuku na mazao yake kutoka nchi zilizoathirika;

(iv) Kuzijengea uwezo wa kuchunguza na kutambua virusi vya ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege Maabara Kuu ya Taifa ya Mifugo -Temeke;

(v) Kuchapisha na kusambaza vitabu 1,000 kwa ajili ya wataalam wa mifugo katika wilaya zilizoko katika hatari ya kuambukizwa ili kuvitumia kuelimisha jamii; na

(vi) Kutoa mafunzo kwa wataalam 170 na wadau 98 wakiwemo Madiwani, Waandishi wa Habari na Mashirika yasiyo ya Kiserikali kutoka Mikoa ya Arusha, Kigoma, Kilimanjaro, Manyara, Mwanza, Tabora na Tanga;

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011 Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Afya na Ustawi wa Jamii, Maliasili na Utalii na wadau wengine, itarejea na kuandaa Mpango Mkakati wa Tahadhari dhidi ya Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Taifa wa Mafua Makali ya Ndege kupitia Mradi wa *SPINAP (AU–IBAR)* unaofadhiliwa na Umoja wa Nchi Huru za Afrika. Pia, Wizara itaendelea kujenga uwezo wake wa kudhibiti Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege kupitia Mradi wa Kudhibiti Mafua Makali ya Ndege unaotekelezwa na nchi za Kenya, Tanzania, Uganda, Sudan na Ethiopia. Vilevile, Wizara itaendelea kutekeleza Mradi wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki wa Kudhibiti Magonjwa ya Mlipuko wenye lengo la kuzijengea uwezo nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki katika kukabiliana na Mafua Makali ya Ndege na magonjwa ya milipuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara imeendelea kudhibiti ugonjwa wa Mdondo kwa kutumia chanjo inayostahimili joto (*I-2*) ili kupunguza vifo vya kuku, hususan vijijini. Katika mwaka 2009/2010, jumla ya dozi 21,610,000 za chanjo zilisambazwa katika Halmashauri mbalimbali nchini kupitia Vituo vya Kanda vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo.

Katika mwaka 2010/2011, Wizara itafanya mapitio na kukamilisha Mpango Mkakati wa Kudhibiti Ugonjwa wa Mdondo. Aidha, dozi 50,000,000 zitasambazwa kwenye Halmashauri kupitia Vituo vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Magonjwa yaenezwayo na kupe, hususan Ndigana Kali, Ndigana Baridi, Maji Moyo na Mkojo Mwekundu husababisha takriban asilimia 70 ya vifo vya ng’ombe nchini. Katika mwaka 2009/2010, Serikali kupitia mipango ya *DADPs* ilikarabati majosho 50 na kujenga mapya 50. Aidha, jumla ya lita 650,000 za dawa za kuogesha mifugo zenye thamani ya shilingi bilioni 10 zilinunuliwa na kusambazwa katika Halmashauri zote nchini. Wafugaji waliendelea kununua dawa hizo kwa asilimia 60 na asilimia 40 inayobaki kulipwa na Serikali kama ruzuku. Pia, jumla ya dozi 92,609 za chanjo ya ndigana kali zimenunuliwa na sekta binafsi. Matumizi ya chanjo hiyo yamepunguza vifo vya ndama kutoka asilimia 85 hadi asilimia 5.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri na wadau wengine itaendelea kuratibu, kukarabati na kujenga majosho

kulingana na mahitaji ya wafugaji. Aidha, Wizara itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ruzuku ya dawa na chanjo dhidi ya Ndigana Kali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kudhibi Mbung'o na Ndorobo pamoja na kutekeleza mpango wa kutokomeza mbung'o katika Bara la Afrika *(Pan African Tsetse and Trypanosomosis Eradicationa Campaign* – PATTEC) kwa kushirikiana na Halmashauri. Katika mwaka 2009/2010, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kuainisha na kuchunguza mtawanyiko wa mbung'o na kuchora ramani mpya kwa Mkoa wa Kigoma na Tabora. Matokeo ya uchunguzi yameonesha kupungua kwa mbung'o ambao kwa sasa wamebakia katika baadhi ya misitu ya miyombo iliyo na wanyamapori;

(ii) Kununua viuatilifu aina ya *Glossinex* na *Decatix* lita 45 kwa ajili ya kudhibiti mbung'o katika miradi shirikishi ya jamii;

(iii) Kuainisha vijiji katika Kata 6 za wilaya ya Rufiji kwa ajili ya uhamasishaji na uanzishaji wa miradi shirikishi ya jamii ya kudhibiti mbung'o na ndorobo;

(iv) Kuhamasisha na kutoa elimu kwa wafugaji 538 wa mkoa wa Rukwa kuhusu udhibiti shirikishi wa mbung'o na ndorobo; na

(v) Kuanzisha mtandao (*Network for Mapping African Trypanosomosis in Tanzania- Net MATT*) wa kuimarisha ukusanyaji wa takwimu na kuandaa ramani ya mtawanyiko wa Nagana na Malale kwa kushirikisha wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kuhamasisha Halmashauri za Mikoa ya Pwani, Tabora na Kigoma kuhusu matumizi ya teknolojia shirikishi ya kudhibiti mbung'o na ndorobo. Aidha, Wizara itanunua vifaa vya kudhibiti mbung'o na ndorobo vikiwemo vyambo, mitego na viuatilifu na kufanya uchunguzi na tathmini ya mtawanyiko wa mbung'o ili kuchora ramani mpya katika mkoa wa Rukwa na Singida. Vilevile, Mpango wa Kutokomeza Mbung'o na Ndorobo Barani Afrika *(PATTEC – Pan African Tsetse and Trypanosomosis Eradication Campaign*) utaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Magonjwa ya Mifugo Yanayoambukiza Binadamu: katika mwaka 2009/2010, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa kudhibiti Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa kupitia Mradi unaofadhiliwa na Taasisi ya *Bill na Melinda Gates* katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Lindi na Mtwara kwa Tanzania Bara na Pemba kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Jumla ya dozi 100,000 za chanjo ya Kichaa cha Mbwa zimenunuliwa na kusambazwa katika Halmashauri 24 za mikoa mitano ya Dar es Salaam, Morogoro, Mtwara, Lindi na Pwani. Pia, mafunzo kuhusu udhibiti wa ugonjwa huo yalitolewa kwa wataalam 61. Vilevile, majokofu 20 ya kuhifadhia chanjo na magari 5 yalinunuliwa kwa ajili ya mikoa inayotekeleza mradi. Aidha, dozi 150,000 za chanjo zilinunuliwa na kusambazwa katika Halmashauri 61 na

uchanjaji umeanza. Pia, Siku ya Kichaa cha Mbwa Duniani iliadhimishwa tarehe 29 Septemba, 2009 ambapo elimu ilitolewa kwa umma kuhusu ugonjwa huo pamoja na kuchanja mbwa 9,576 katika wilaya za mikoa ya Dar-es-Salaam na Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kudhibiti Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa kwa kununua dozi 150,000 za chanjo na kuzisambaza katika Halmashauri. Pia, Mradi unaofadhiliwa na Taasisi ya Bill na Melinda Gates utaendelea kutekelezwa ikiwa ni pamoja na kununua pikipiki 24 kwa ajili ya wilaya zinazotekeleza mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea kutekeleza Mkakati wa kudhibiti Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa, ambapo jumla ya dozi 500,000 za chanjo zimenunuliwa na kusambazwa katika Halmashauri 50. Pia, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na wadau wengine kwa ufadhili wa UN iliandaa Mpango wa Kitaifa wa Kujihami dhidi ya ugonjwa huo *(National RVF Contingency Plan*). Katika mwaka 2010/2011 Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kudhibiti Ugonjwa wa Bonde la Ufa *(RVF)* kwa kununua dozi milioni moja na kuzisambaza katika Halmashauri pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu ugonjwa huo na hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, jumla ya ng’ombe 1,028 na mbuzi 240 walichunguzwa dhidi ya Ugonjwa wa Kutupa Mimba, ambapo ng’ombe 104 waligundulika kuwa na ugonjwa na hakuna mbuzi waliogundulika kuwa na ugonjwa. Aidha, ushauri ulitolewa kwa wafugaji kuchinja ng’ombe waliogundulika kuwa na ugonjwa ili kuepuka kuenea kwa ugonjwa huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, jumla ya ng’ombe 5,000, mbuzi 1,440 na kondoo 840 watachunguzwa dhidi ya Ugonjwa wa Kutupa Mimba katika mashamba ya kuzalisha mitamba, ranchi za Taifa pamoja na mashamba ya taasisi za umma na ya sekta binafsi. Pia, Wizara itapima kiwango cha maambukizi ya ugonjwa huo kwenye mifugo ya asili na kuzalisha chanjo ya *S19* kwa ajili ya kudhibiti ugonjwa huo katika Maabara Kuu ya Taifa ya Mifugo - Temeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara iliendeelea kufuatilia maambukizi ya ugonjwa wa Kifua Kikuu cha ng’ombe kwenye mashamba ya mifugo ambapo ng’ombe 147 walichunguzwa katika Chuo cha Kilimo cha Uyole na 10 waligundulika kuwa na ugonjwa. Ushauri ulitolewa kwa Chuo kuchinja ng’ombe wote waliobainika kuwa na ugonjwa. Katika mwaka 2010/2011, jumla ya ng’ombe 5,000 watachunguzwa dhidi ya ugonjwa wa Kifua Kikuu cha ng’ombe katika mashamba ya kuzalisha mitamba, ranchi za Taifa pamoja na mashamba ya taasisi za umma na ya sekta binafsi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ugonjwa wa Mafua ya Nguruwe unaosababishwa na virusi vya aina ya *Influenza A-H1N1* ulitokea hapa nchini kwa mara ya kwanza mwaka 2009. Kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya mwaka 2009/2010, ugonjwa huo ni wa binadamu na hautokani na nguruwe kama ilivyohisiwa hapo awali. Jumla ya sampuli 160

zimechunguzwa na hadi sasa hakuna uthibitisho kuhusu nguruwe waliougua au kufa kwa ugonjwa huo nchini. Katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kuchukua hatua za tahadhari kukabiliana na ugonjwa huo zikiwa ni pamoja na:-

(i) Kufuatilia mwenendo wa magonjwa ya nguruwe nchini;

(ii) Kudhibiti usafirishaji wa nguruwe na mazao yake hasa kutoka maeneo yanayosadikiwa kuwa na matukio ya ugonjwa kwa binadamu;

(iii) Kutoa elimu kwa jamii kuhusu ugonjwa na hatua za kuchukua kuepuka maambukizi; na

(iv) Kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na wadau wengine katika ufuatiliaji, utambuzi na udhibiti wa ugonjwa huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ufuatiliaji wa Magonjwa na Ukaguzi wa Mifugo na Mazao yatokanayo na Mifugo: Katika kudhibiti kuenea kwa magonjwa ya mifugo, Wizara imeendelea kufanya ukaguzi wa mifugo na mazao yake pamoja na kutoa vibali vya kusafirisha mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2009/2010, jumla ya mifugo 870 iliyoingia na iliyotoka nchini ilikaguliwa. Aidha, jumla ya vibali 31 vilitolewa 668 kwa ajili ya kuingiza na kusafirisha mifugo nje ya nchi. Vituo 12 vya ukaguzi vya Holili, Horohoro, Isongole, Mtukula, Tunduma, Sirari, Dar-es-Salaam, KIA, Namanga, Kibaha, Kigoma na Mwanza vimeimarishwa kwa kukarabatiwa na kupatiwa vitendea kazi. Katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea na ukarabati wa vituo vya ukaguzi wa mifugo 15 na kuvipatia vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea kusimamia usalama na ubora wa vyakula vitokanavyo na mifugo. Katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kuhamasisha jamii kuhusu kuzingatia kanuni za ufugaji bora ili kuzalisha chakula salama na bora ambapo wafugaji 200 watapatiwa elimu. Aidha, viwango vya ubora wa nyama na maziwa vitapitiwa na kuboreshwa kwa kuzingatia maendeleo ya sayansi na teknolojia. Pia, sampuli 100 za vyakula mbalimbali vitokanavyo na mazao ya mifugo zitachunguzwa ili kubaini mabaki ya dawa za mifugo. Vilevile, Wizara itaandaa vijitabu vya kuelimisha jamii baada ya kupata matokeo ya uchunguzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Udhibiti wa Usalama na Ubora wa Pembejeo za Mifugo: Wizara imeendelea kusimamia ubora wa dawa na chanjo za mifugo zinazoingizwa nchini kwa ajili ya tiba na kinga za magonjwa ya mifugo kwa kushirikiana na Mamlaka ya Chakula na Dawa. Aidha, Wizara imepitia na kuboresha orodha ya dawa na vifaa tiba vya mifugo ili itumike na Mamlaka ya Chakula na Dawa pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania katika kudhibiti usajili na uingizaji wa dawa za mifugo nchini. Vilevile, Wizara imeendelea kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu nchini *(TPRI*) ili kuhakikisha kuwa viuatilifu vinavyoingia nchini ni bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana *TFDA* na *TBS* na wadau wengine itaendelea kuhakikisha kuwa wafugaji nchini wanapata

pembejeo bora na salama za mifugo kwa kuandaa viwango, kusimamia ubora, matumizi na hifadhi sahihi ya pembejeo hizo. Pia, itatoa elimu kwa wakaguzi 20 kutoka katika vituo 6 vya ukaguzi. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na itaendelea Pia, ukaguzi wa maduka ya pembejeo za mifugo utafanyika katika mikoa ya Kanda za Kati, Kusini, Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Udhibiti wa Usafi wa Machinjio na Ukaguzi wa Nyama na Ngozi: Wizara iliendelea na jitihada ya kusimamia usafi wa machinjio ili kuwahakikishia walaji nyama safi na salama. Ukaguzi ulifanyika kwa machinjio za mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Mwanza, Dodoma, Singida, Tabora, Arusha, Kilimanjaro na Tanga. Asilimia 42 ya machinjio zilizokaguliwa zilikuwa hazikidhi viwango vya usafi hivyo Halmashauri husika zilishauriwa kufanya ukarabati kwa lengo la kuziboresha. Pia, Halmashauri hizo zilishauriwa kuingiza miradi ya ujenzi na ukarabati wa machinjio katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs*). Aidha, Machinjio ya Halmashauri ya Igunga imejengwa na kukamilika na inatumika. Pia, machinjio za Halmashauri za wilaya ya Nzega, Urambo na Kilwa zimefikia asilimia 80 ya ujenzi. Machinjio za Halmashauri za Wilaya za Mpwapwa na Kondoa zimefanyiwa ukarabati na zinatumika. Jumla ya wanyama 1,218,193 (ng'ombe 605,389, mbuzi 358,474, Kondoo 146,993 na nguruwe 107,337) walichinjwa na kukaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi wa maghala ya wafanyabiashara wa ngozi ulifanyika kwa makampuni manane ya Dar es Salaam, Arusha mawili na Kilimanjaro matatu. Wamiliki wa makampuni hayo walishauriwa kuboresha usafi wa maghala yao. Aidha, makampuni 14 yalipewa leseni za kuuza ngozi nje ya nchi ambapo vipande 650,000 vya ngozi za ng'ombe, mbuzi vipande 980,000 na kondoo vipande 320,000 viliuzwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, udhibiti na ukaguzi utaimarishwa kwa kutoa mafunzo kwa wakaguzi wa nyama na ngozi 120, na wakaguzi 30 wa mazao ya mifugo kwenye Halmashauri. Aidha, ukaguzi wa kuthibiti ubora wa mazao yatokanayo na mifugo ya nyama, mayai, maziwa na mazao yake na utoaji wa elimu kwa jamii kuhusu viwango na usalama wa vyakula vitokanavyo na mifugo utafanyika katika kanda ya Kusini na Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara ya mifugo na mazao yatokanayo na mifugo imeendelea kuongezeka ndani na nje ya nchi. Aidha, Wizara imeshirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kuratibu biashara hiyo. Idadi ya mifugo iliyouzwa minadani imeongezeka kutoka ng'ombe 781,230, mbuzi 623,732 na kondoo 114,564 wenye thamani ya shilingi bilioni 319.2 mwaka 2008/2009 hadi kufikia ng'ombe 857,208 mbuzi 682,992 na kondoo 122,035 wenye thamani ya shilingi bilioni 382.4 mwaka 2009/2010. Ongezeko hilo la idadi ya mifugo iliyouzwa linatokana na kuimarishwa kwa huduma za minada na wafugaji kuongeza mauzo ya mifugo yao kama tahadhari ya kuepuka hasara kutokana na ukame uliokumba maeneo mengi nchini mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, jumla ya ng'ombe 2,970 na mbuzi 302 wenye thamani ya shilingi bilioni 2.8 wameuzwa katika nchi za Comoro, Burundi na Kenya. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya tani 36.9 za nyama ya ng'ombe, tani 122 za nyama ya mbuzi na tani 34.6 za nyama ya kondoo ziliuzwa nje katika nchi za Oman, Kuwait, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Muscat, Malawi na Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo. Vilevile tani 11.1 za *ice cream* za maziwa ziliuzwa nje katika nchi ya Zambia. Mauzo ya mifugo hai na nyama nje ya nchi yameshuka ikilinganishwa na mauzo katika mwaka 2008/2009 ambapo ng'ombe 3,264 na mbuzi na kondoo 1,834 wenye thamani ya shilingi bilioni 2.1 waliouzwa katika nchi za Comoro, Kenya, Burundi na Malawi na tani 139.8 za nyama ya ng'ombe zenye thamani ya shilingi 416,947,750, tani 35.4 za nyama ya kondoo zenye thamani ya shilingi 120,204,477 na tani 46.7 za nyama ya mbuzi zenye thamani ya shilingi 117,330,455 zilizouzwa katika nchi za Kuwait, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Misri na Oman.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kuhamasisha, kufuatilia na kuratibu uuzaji wa mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi katika mwaka 2010/2011 ili kurejesha na kuongeza mauzo nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuratibu ukusanyaji na uuzaji wa ngozi za mifugo nje ya nchi. Jumla ya vipande milioni 1.5 vya ngozi za ng'ombe, milioni 2.4 vya mbuzi na milioni 0.65 vya kondoo vyenye thamani ya shilingi bilioni 8.5 vilikusanywa. Kati ya hivyo, vipande vya ngozi za ng'ombe 739,315, mbuzi milioni 1.9, na kondoo 176,400 viliuzwa nje ya nchi kwa thamani ya shilingi bilioni 8.19. Mapato kutokana na mauzo ya ngozi yameshuka kwa asilimia 36 ikilinganishwa na mapato ya shilingi bilioni 12.8 mwaka 2008/2009 kutokana na kushuka kwa bei ya ngozi katika soko la kimataifa kulikosababishwa na mtikisiko wa uchumi uliojitokeza kuanzia katikati ya mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya vipande vya ngozi iliyosindikwa imepungua kutoka vipande milioni 2.3 vyenye thamani ya shilingi bilioni 7.3 mwaka 2008/2009 hadi kufikia vipande milioni 1.96 vyenye thamani ya shilingi bilioni 6.57 mwaka 2009/2010. Kupungua kwa idadi ya ngozi zilizosindikwa imetokana na mtikisiko wa uchumi wa dunia ambao uliathiri soko la ngozi na hivyo kupungua kwa ukusanyaji na usindikaji wa ngozi. Hata hivyo, uwiano wa ngozi iliyosindikwa na kuuzwa nje ya nchi umeongezeka kutoka asilimia 57 mwaka 2008/09 hadi kufikia asilimia 69 mwaka 2009/10 ya ngozi zote ziliouzwa nje ya nchi. Ongezeko la usindikaji linatokana na kuhamasika kwa wafanyabiashara kuuza ngozi zilizosindikwa ili kupata bei nzuri kwenye masoko ya nje kuliko kuuza ngozi ghafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi umeendelea kutekelezwa kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda Biashara na Masoko, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Halmashauri 55 na Chama cha Wadau wa Sekta ya Ngozi. Katika mwaka 2009/2010 Wizara kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo *(Livestock Development Fund*) imeimarisha huduma za ugani kwa kununua pikipiki 19 na kuzisambaza katika Halmashauri za Arusha, Bariadi, Chunya, Geita, Igunga, Kahama, Kinondoni, Manyoni, Mbinga, Misungwi, Mpwapwa, Ngorongoro, Njombe, Rorya, Same na Sengerema. Vilevile, visu 13,750, vinoleo 3,250 na vifaa vya

kunyanyulia nyama 130 vimesambazwa katika Halmashauri zinazotekeleza mkakati huu. Aidha, jumla ya wafugaji 2,144, wachinjaji na wachunaji 742, wawambaji 410, maafisa ugani 591, wafanyabiashara wa ngozi 356, wasindikaji 104 na watendaji wa Serikali 605 katika Halmashauri 55 zinazotekeleza mkakati wamepata mafunzo kuhusu uboreshaji wa zao la ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/10 Halmashauri za Bagamoyo, Kibaha, Morogoro, Kilosa, Mvomero, Chato, Karagwe, Misenyi, Mpanda na Sumbawanga zimeingizwa katika Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi na kufanya jumla ya Halmashauri zinazotekeleza Mkakati kuwa 65. Aidha, Wizara imechapisha nakala 1,800 za Mkakati wa Kufufua na kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi nchini na kusambazwa kwa wadau mbalimbali nchini.

Katika mwaka wa 2010/2011, Wizara itaendelea kutekeleza mkakati wa kufufua zao la ngozi kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kujenga vituo katika Halmashauri 30 kwa ajili ya kutoa mafunzo ya uendelezaji wa zao la ngozi; na

(ii) Kuwezesha uanzishwaji na uendeshaji wa Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuimarisha miundombinu ya masoko ya mifugo ili kuboresha biashara ya mifugo na mazao yake. Katika mwaka 2009/2010, Wizara imekamilisha ujenzi wa mnada wa mifugo wa Buzirayombo na wa mbuzi Kizota. Aidha, minada ya mifugo ya Kizota, Mhunze, Pugu na Lumecha imekarabatiwa. Pia, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine imeendelea kukusanya, kuchambua, kuhifadhi na kusambaza taarifa za masoko ya mifugo kutoka minada 53. Ili kuongeza ukusanyaji wa mapato yanayotokana na mauzo ya mifugo minadani, Wizara imehamasisha ukusanyaji wa maduhuli katika Halmashauri za mikoa ya Kanda za Ziwa, Magharibi, Kati, Kaskazini na ya Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kukusanya na kutoa taarifa kutoka minada 53 iliyounganishwa na Mtandao wa mawasiliano *LINKS*. Pia, Wizara itaweka mizani kwenye minada 10 ya Igunga, Ipuli, Kizota, Korogwe, Meserani, Mhunze, Nyamatara, Pugu, Themi na Weruweru. Vilevile, Wizara itatoa mafunzo kuhusu ukusanyaji wa takwimu kwa wataalam 50 wanaosimamia minada.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Wizara itaendelea kuwezesha wakusanya maduhuli kwenye minada ili kuongeza mapato ya serikali kutoka shilingi bilioni 2.5 mwaka 2009/2010 hadi kufikia shilingi bilioni 6.

Mheshimiwa Naibu Spika, utambuzi, usajili na ufuatiliaji mifugo na mazao yake: Mfumo wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji mifugo na mazao yake uliendelea kuimarishwa ambapo katika mwaka 2009/2010 Wizara ilitengeneza chapa 5,000 na kusambaza

madaftari 2,243 ya usajili kwa majaribio katika Halmashauri za wilaya 33 za Mikoa ya Arusha (283), Dodoma (86), Iringa (126), Kagera (709), Mara (481), Mbeya (147), Morogoro (213), Rukwa (178) na Shinyanga (20). Aidha, wataalam 197 wamepata mafunzo kuhusu mfumo wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuwajengea uwezo wakaguzi 65 wa Halmashauri kuhusu usimamizi wa Sheria ya Ustawi wa Wanyama;

(ii) Kutoa mafunzo kwa wataalam 154 wa mifugo katika usimamizi na uendeshaji mfumo wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji mifugo na mazao yake; na

(iii)Kuanzisha na kutekeleza mfumo wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji mifugo katika mifumo ya uzalishaji ya asili na biashara kwa kusajili wafugaji 200,000 na kutambua ng'ombe 500,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Ugani Sekta ya Mifugo: utoaji wa huduma za ushauri kwa wafugaji ni njia moja wapo ya kuwapatia wafugaji teknolojia sahihi na mbinu za ufugaji bora. Katika mwaka 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri iliendelea kutoa ushauri wa kitaalamu, miongozo na kanuni za ufugaji bora na wa kibiashara. Jumla ya nakala 52,000 za vipeperushi, 30,000 za mabango na 13,000 za vijitabu kuhusu ufugaji bora zilichapishwa na kusambaza kwa wadau. Pia, vipindi 78 vya redio na 12 vya luninga kuhusu ufugaji bora viliandaliwa na kurushwa hewani.

Kupitia miradi ya *DADPs* na wafadhili wengine, wafugaji 10,215 katika mikoa ya Dar-es-Salaam, Dodoma, Iringa, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Manyara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Singida, Tabora na Tanga walipatiwa mafunzo juu ya ufugaji wa kibiashara. Vilevile, Wizara ilitoa mafunzo kwa wataalam 63 kutoka wilaya 20 za Nyanda za Juu Kusini na 11 za Kanda ya Ziwa kuhusu Upangaji wa Mipango Shirikishi ya Ugani. Aidha, Wizara iliendesha mafunzo kwa Mashirika yasiyo ya Kiserikali na watoa huduma binafsi 61 katika Kanda za Kati na Ziwa kwa lengo la kushirikisha sekta binafsi katika kutoa huduma za ugani kwa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kutayarisha, kuchapisha na kusambaza nakala 58,000 za vipeperushi, 20,000 za mabango na 10,000 za vijitabu kuhusu ufugaji bora;

(ii) Kuandaa filamu moja ya ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa;

(iii) Kuandaa na kurusha hewani vipindi 52 vya redio na 12 vya runinga kuhusu ufugaji bora;

(iv) Kushirikiana na Halmashauri kutoa mafunzo kwa wafugaji 8,000 kuhusu ufugaji bora na wa kibiashara;

(v) Kukarabati vituo vya mafunzo kwa wafugaji vya Mabuki (Mwanza) na Kikulula (Kagera) ili viweze kutoa mafunzo kwa wafugaji wengi zaidi;

(vi) Kutoa mafunzo kwa wataalamu 20 wa mifugo katika Halmashauri kuhusu Upangaji wa Mipango Shirikishi ya Ugani na jinsi ya kuendesha Mashamba Darasa;

(vii) Kuandaa na kusambaza kwa wadau aina 3 za Mipango Shirikishi ya Ugani; na

(viii) Kusambaza teknolojia zilizoibuliwa na watafiti kuhusu ufugaji wa kisasa na wa kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Ugani Sekta ya Uvuvi: Wizara, imeendelea kuelimisha umma ambapo wavuvi 500 walipewa mafunzo ya athari za uvuvi haramu, matumizi bora ya rasilimali za uvuvi, utunzaji wa mazingira na mbinu shirikishi za usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Aidha, elimu ya ufugaji bora wa samaki ilitolewa kwa wafugaji 121 wa Halmashauri za Mbinga, Namtumbo na Songea. Pia, mafunzo ya uchakataji, uhifadhi na usafirishaji wa samaki na mazao ya uvuvi kwa wamiliki na wafanyakazi katika viwanda vya uchakataji samaki yalitolewa kwa washiriki 124 katika Ukanda wa Ziwa Victoria na Wafanyabiashara 430 katika Wilaya za Rufiji, Mafia na Kilwa. Vilevile, Wizara iliendelea kutoa elimu kuhusu mbinu bora za ufugaji wa samaki na hifadhi ya mazao ya uvuvi kupitia vipindi 50 vya redio na 20 vya runinga, nakala 1,000 za mabango, 6,000 za vijarida na 3,000 za vipeperushi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kuandaa na kurusha hewani vipindi 52 vya redio na 12 vya runinga vinavyohusu uvuvi endelevu;

(ii) Kutoa mafunzo rejea ya ufugaji bora wa samaki kwa Maofisa Ugani 133 kutoka kwenye Halmashauri na kuwezesha ufugaji wa samaki katika Halmashauri 10;

(iii) Kuandaa na kusambaza teknolojia 3 za ukuzaji wa viumbe kwenye maji kwa kutumia vizimba, chelezo na ukuzaji wa lulu; na

(iv) Kushirikisha vikundi 144 vya usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi katika halmashauri 16 za Ukanda wa Pwani katika kudhibiti uvuvi haramu, kuendeleza mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali za bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenendo wa Uvunaji wa Samaki na Uuzaji wa Mazao ya Uvuvi: mwaka 2009/2010, Wizara imeendelea kuratibu shughuli za uvuvi nchini ambapo jumla tani 335,674.26 za mazao ya uvuvi yenye thamani ya shilingi bilioni 401.42 zilivunwa. Pia, nguvu ya uvuvi imeongezeka kutoka wavuvi 170,038 waliotumia vyombo vya uvuvi 52,327 mwaka 2008 hadi wavuvi 172,090 wanaotumia vyombo vya uvuvi 52,898 mwaka 2009. Aidha, mauzo ya samaki na mazao yake katika soko la nje mwaka 2009 yalikuwa tani 41,148.26 na samaki hai wa mapambo 53,188 ambapo jumla ya shilingi bilioni 207.45 zilipatikana kutokana na mauzo hayo. Kutokana na mauzo hayo, Serikali ilipata ushuru wa shilingi bilioni 6.41.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine, itaendelea kusimamia uvunaji endelevu wa rasilimali ya uvuvi katika maji yote. Aidha, ili kuendeleza sekta ya uvuvi, Wizara itaendelea kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za Serikali za kudhibiti uvuvi haramu na utoroshaji wa samaki na mazao ya uvuvi mipakani. Katika mwaka 2009/2010 vituo 18 vya doria vilivyopo Dar es Salaam, Mwanza, Musoma, Bukoba, Tanga, Mtwara, Mafia, Kilwa, Horohoro, Kipili, Kasanga, Sota, Sirari, Kasumulo, Rusumo, Kanyigo, Kigoma na Tunduma vimeimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi. Aidha, boti 12 zimenunuliwa na kugawiwa kwenye vituo vya doria vya Kipili (1), Kanyigo (1), Kasumulo (1), Sota (1); Dar es Salaam (2), Tanga (2), Mtwara (2), Mafia (1) na Kilwa (1). Vilevile, injini mbili zimenunuliwa kwa ajili ya vituo vya Kigoma na Bukoba. Pia, boti nyepesi *(rubber dinghies)* nne zimenunuliwa na kusambazwa kwenye vituo vya Dar es Salaam (1), Mafia (1) Mtwara (1) na Tanga (1).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine imeendelea kufanya doria za nchi kavu, majini, angani na maeneo ya mipakani ili kudhibiti uvuvi na biashara haramu ya samaki. Katika mwaka 2009/2010, jumla ya siku-kazi za doria 6,096 zilifanyika nchi nzima ambazo ziliwezesha kukamatwa kwa makokoro 3,602, kamba za kokoro mita 235,745, nyavu za utali *(monofilament)* 1,186, nyavu zenye macho madogo 12,412, nyavu za dagaa zenye macho madogo 110, katuli 18, mikuki 17, baruti 25, vifaa vya kuzamia jozi 14, mitumbwi 686, injini za boti 7, baiskeli 35, pikipiki 26, na magari 12. Pia, doria hizo ziliwezeshwa kukamatwa kwa samaki wachanga wabichi kilo 107,806, samaki wabichi kilo 2,182, samaki wakavu kilo 23,111, samaki waliovuliwa kwa baruti kilo 158, samaki waliovuliwa kwa sumu kilo 438, majongoo bahari kilo 300 na dagaa kilo 14,000. Jumla ya watuhumiwa 672 walikamatwa na kesi 117 ziko mahakamani kwa makosa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakaguzi wa Wizara wa samaki na zana za uvuvi walifanya ukaguzi wa kustukiza kwenye kiwanda cha kutengeneza nyavu cha *IMARA FISHNET* kilichopo Dar-es-Salaam ambapo jumla ya nyavu zenye macho madogo 101,290 zilikamatwa na kufikishwa katika vyombo vya dola, na kesi mbili dhidi ya mwenye kiwanda zinaendelea mahakama. Aidha, kutokana na ukaguzi huo nyavu zenye macho madogo 4,066 zilisalimishwa kwa hiari na wafanyabiashara katika mkoa wa Dar-es-Salaam. Kutokana na kukithiri kwa uvuvi haramu nchini, mnamo tarehe 18 Januari,

2010 Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb) alitoa tamko la Serikali la kuwataka wavuvi nchini kusalimisha kwa hiari zana haramu za uvuvi kwenye vyombo vya usalama ndani ya siku 14. Kutokana na tamko hilo hadi kufikia tarehe 18 Machi 2010 zana haramu 7,217 zilisalimishwa. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa tamko lake ambalo limeleta mafanikio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na nchi za Kenya na Uganda, imeendelea kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika Ziwa Victoria kupitia Taasisi ya "*Lake Victoria Fisheries Organisation.*" Kwa kuimarisha uvuvi endelevu Serikali imechangia Taasisi hiyo jumla ya dola za kimarekani 600,000 kwa mwaka 2009/2010 kwa ajili ya doria maalum itakayojumuisha nchi za Kenya, Uganda na Tanzania. Katika mwaka 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kupambana na uvuvi haramu na utoroshaji wa samaki na mazao ya uvuvi kwa kufanya siku-kazi za doria 12,000. Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kuwezesha ujenzi wa Ofisi ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi katika Ukanda wa Bahari Kuu;

(ii) Kutoa mafunzo kwa Waangalizi (*Sea Observers*) 20, Wataalam wa kutumia "*Vessel Monitoring System*" 10 kuhusu kulinda, kudhibiti na kuzuia uvuvi haramu;

(iii) Kuanzisha vituo viwili vya doria vya Kabanga na Mbinga;
(iv) Kununua boti tatu kwa ajili ya vituo vya doria vilivyopo kwenye Halmashauri za Mbinga, Sumbawanga na Musoma; na

(v) Kukarabati vituo vya doria vya Kigoma, Bukoba na Musoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na *World Wide Fund for Nature (WWF),* imeandaa Mwongozo wa kuanzisha maeneo ya usimamizi wa pamoja ya uvuvi ambapo maeneo matatu yameanzishwa katika Wilaya za Mafia, Rufiji na Kilwa. Pia, vikundi 512 vya Usimamizi wa Rasilimali ya Uvuvi vimeimarishwa, ambapo vikundi 438 viko katika Ziwa Victoria 29 Bwawa la Mtera, 20 Bwawa la Nyumba ya Mungu, 11 Mto Ruhuhu 6 Mafia na 8 Rufiji. Aidha, kazi ya kuvijengea uwezo vikundi 14 vya Rufiji na Mafia imefanyika kwa kuvitengenezea mipango ya usimamizi wa uvuvi endelevu. Pia, Wizara imeanzisha vikundi vipya 130 katika Ukanda wa Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwa kufanya tathmini ya hali ya uvuvi katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Katika mwaka 2009/2010, maeneo ya Bwawa la Nyumba ya Mungu (Kilimanjaro), Ziwa Babati (Manyara), Kindai, Singidani na Kitangiri (Singida) yalifanyiwa tathmini. Tathmini hizo zimebaini kuwepo kwa uharibifu wa mazingira kutokana na shughuli za kilimo kufanyika kandokando ya maziwa, mito, na mabwawa na utupaji wa taka zisizooza, matokeo ya uharibifu huo wa mazingira ni kupungua kwa kina

cha maji na hivyo kuathiri upatikanaji wa samaki. Changamoto iliyopo ni ukusanyaji na utunzaji wa takwimu sahihi za uvuvi katika ngazi za Halmashauri.

Katika mwaka 2010/2011, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kuratibu na kutathmini utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya uvuvi nchini pamoja na kuendeleza programu sahihi ya kupeana taarifa kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali ya uvuvi;

(ii) Kuimarisha Vikundi vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi na kuhamasisha uanzishwaji wa vikundi 54 katika Halmashauri 13 za ukanda wa Pwani zinazotekeleza Mradi wa MACEMP;

(iii) Kuendelea kuvijengea uwezo wa kutengeneza mipango ya usimamizi wa uvuvi endelevu vikundi vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi vilivyopo katika Halmashauri 16 za ukanda wa Pwani zinazotekeleza Mradi wa MACEMP;

(iv) Kuanzisha mtandao wa vikundi vya usimamizi wa rasilimali za uvuvi;

(v) Kukarabati majengo ya iliyokuwa *TAFICO* eneo la Rasi Mkwavi (Kigamboni) kwa ajili ya kutumiwa na vitengo vya doria, nyumba 3 za watumishi katika kituo cha doria cha Kigoma (1) na Kipili (2); na

(vi) Kukarabati karakana za kutengenezea boti za Kigoma, Mtwara na Mwanza ili zitumike kwa ajili ya kutolea mafunzo ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha usalama na ubora wa mazao ya uvuvi kwa ajili ya soko la ndani na nje, Wizara imetoa mafunzo ya muda mfupi juu ya uhifadhi bora wa samaki, ukaguzi wa ndani wa viwanda na viwango kwa wataalam 25. Aidha, vituo 7 vya ukaguzi wa ubora na usalama wa mazao ya uvuvi vya Bukoba, Kigoma, Kilwa, Mafia, Musoma, Mwanza na Tanga vimeimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi na wataalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010 jumla ya sampuli 638 zilichunguzwa ili kuhakiki ubora na usalama wa mazao ya uvuvi. Kati ya sampuli hizo, 566 ni kwa ajili ya vimelea haribifu, 46 ni kwa ajili ya mabaki ya sumu na madawa na 26 kwa ajili ya uchunguzi wa madini tembo. Uchunguzi huo ulifanyika katika Maabara ya Taifa ya Uthibiti wa Ubora wa Samaki Nyegezi – Mwanza, Shirika la Viwango Tanzania, Chemiphar-Uganda na SABS-Afrika Kusini ambapo sampuli zote zilionekana kuwa salama. Aidha, ukaguzi wa kuhakiki ubora na usalama wa samaki na mazao yake kabla ya kusafirishwa nje ya nchi ulifanyika ambapo jumla ya kilo 19,128,653 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo 18,151 walikaguliwa. Pia, kilo 1,193,130 za mazao ya uvuvi zilizoingizwa nchini zilikaguliwa na kuhakikiwa. Vilevile, ukaguzi ulifanyika kwenye viwanda 29 vya kuchakata na kuhifadhi mazao ya uvuvi vilivyopo kanda ya Ziwa Victoria na Pwani na kuonekana kuwa vimekidhi viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Mradi wa Utekelezaji wa Mpango wa Usimamizi wa Uvuvi katika Ziwa Victoria imeboresha mialo 19. Pia, ujenzi wa mialo 6 katika Halmashauri za Bukoba (1), Chato (1), Magu (1), Musoma (1), Rorya (1) na Sengerema (1) unaendelea. Aidha, kupitia Mradi wa MACEMP usanifu wa ujenzi wa mialo 3 katika Halmashauri za Kilwa (1), Mafia (1) na Rufiji (1), zilizoko ukanda wa Pwani umekamilika.

Katika mwaka 2010/2011 Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kukarabati na kununua vifaa vya Maabara ya Samaki, Nyegezi;

(ii) Kufanya uchunguzi wa kimaabara kwa sampuli 800 za minofu ya samaki, maji taka, masalia ya madawa ya mimea, viuatilifu na madini tembo;

(iii) Kufanya ukaguzi wa kuhakiki ubora wa samaki na mazao yake kabla ya kusafirishwa nje ya nchi;

(iv) Kufanya ukaguzi kwenye viwanda vya kuchakata na kuhifadhi samaki na mazao ya uvuvi; na

(v) Kutoa mafunzo kuhusu uhifadhi wa samaki kwa wakaguzi 40 wa samaki, mafundi wa maabara 20 na wadau wa wavuvi 500 wanaoshughulikia ubora na usalama wa samaki na mazao yake.

**Mheshimiwa Naibu Spika, Kuimarisha Ukusanyaji wa Takwimu za Sekta ya Uvuvi ili kuwa na uvuvi endelevu ni muhimu kuimarisha upatikanaji wa takwimu sahihi. Kwa kulitambua hilo, katika mwaka 2009/20010, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO) imetoa mafunzo kuhusu ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu kwa wataalam wa sekta ya uvuvi wa Halmashauri za Babati, Bagamoyo, Geita, Iramba, Kigoma Vijijini, Kyela, Lindi Vijijini, Ludewa, Mbinga, Mpwapwa, Muleba, Mwanga, Mkinga, Mtwara Vijijini, Nkasi, Rorya, Sengerema, Simanjiro na Sumbawanga Vijijini. Aidha, Wizara imefanya sensa ya uvuvi katika mikoa ya Kilimanjaro, Manyara na Singida ambayo matokeo yake yameonyesha kuwa Ziwa Jipe kuna mialo 4, wavuvi 78, vyombo vya uvuvi 50 na zana za uvuvi 1,152; Ziwa Kitangiri lina mialo 3, wavuvi 457, vyombo 224 na zana za uvuvi 8,553; na Ziwa Babati mialo 11, wavuvi 202, vyombo 91 na zana za uvuvi 512. Vilevile, sensa ilifanyika kwenye wilaya 16 za mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Pwani na Tanga katika Ukanda wa Bahari ya Hindi chini ya Mradi wa MACEMP na kubaini kuwepo kwa mialo 257, vyombo vya uvuvi 7,664, wavuvi 36,321, wakulima wa mwani 5,579 na zana za uvuvi 55,335.**

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kusimamia na kuboresha ukusanyaji wa takwimu ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa sahihi za uvuvi. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine itafanya sensa ya uvuvi katika maeneo ya Ziwa Victoria, Tanganyika, Nyasa, mabwawa ya Mtera na

Nyumba ya Mungu. Pia, Wizara itatoa mafunzo ya ukusanyaji takwimu za uvuvi kwa vikundi 48 vya ulinzi shirikishi wa rasilimali za uvuvi (BMUs) katika ukanda wa pwani.

Wizara imeendelea kuhimiza ukuzaji wa viumbe kwenye maji kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa samaki na mazao mengine ya kwenye maji. Makadirio ya uzalishaji wa samaki jamii ya perege katika mabwawa 15,133 ulikuwa tani 11.3, Kambamiti kwenye mabwawa 30 (Mafia) ulikuwa tani 60 na zao la mwani mkavu ulikuwa tani 527. Katika mwaka 2009/2010, Wizara imeainisha maeneo yanayofaa kwa ukuzaji na ufugaji wa viumbe kwenye maji bahari katika vijiji 39 vya mikoa ya Mtwara (8), Lindi (9), Pwani (19) na Tanga (3). Aidha, Wizara kwa kushirikiana na *World Wildlife Fund (WWF*) na Chuo cha Maendeleo ya Uvuvi Mbegani, imeendelea kufanya majaribio ya ukuzaji wa lulu kwa kutumia chaza ambapo jumla ya vipande vya lulu 750 vimepandikizwa katika maeneo ya Mafia (400), Mtwara Vijijini (150) na Mbegani (200).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Kampuni ya *PRAWNTO* imeanzisha kituo cha kuzalisha vifaranga vya samaki katika Chuo cha Maendeleo ya Uvuvi Mbegani ambapo jumla ya vifaranga 75,000 vya kambamiti vimezalishwa na kusambazwa kwa wafugaji katika Mkoa wa Tanga. Aidha, maeneo mengine mawili kwa ajili ya kuanzisha vituo vya kuzalishia vifaranga vya samaki wa maji bahari yameainishwa katika vijiji vya Chihiko (Mtwara) na Kizingani (Mkinga).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha vituo 8 vya ufugaji wa samaki wa maji baridi, Wizara imekarabati mabwawa 34, imejenga matanki 19 ya kutunzia vifaranga na kuchimba mabwawa mapya 4 kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa vifaranga vya samaki. Aidha, kisima kirefu kimechimbwa katika Kituo cha Uzalishaji Vifaranga vya Samaki cha Kingolwira ili kuwa chanzo cha uhakika wa maji kwa ajili ya uzalishaji endelevu. Pia, vituo 8 viliimarishwa kwa kununuliwa samani za ofisi na vitendea kazi. Vilevile, nyumba moja imekarabatiwa katika kituo cha Luhira (Songea) kwa lengo la kuwa darasa la kufundishia wagani-kazi watakaosaidia kueneza elimu ya ufugaji samaki katika maeneo yao.

Kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kutoa huduma za ugani juu ya ukuzaji viumbe kwenye maji kwa wafugaji wa samaki 1,021 katika maeneo ya Dar-es-Salaam (28), Kagera (3), Kilimanjaro (20), Lindi (14), Morogoro (9), Mtwara (10), Pwani (797), Ruvuma (60), Tabora (4) na Tanga (76);

(ii) Kushirikiana na sekta binafsi kuzalisha na kusambaza vifaranga 967,551 vya samaki wa maji baridi aina ya perege kwenye mabwawa na malambo katika mikoa 15 ya Dar-es-Salaam, Dodoma, Iringa, Kagera, Kilimanjaro, Lindi, Mara, Morogoro, Mwanza, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Tabora na Tanga;

(iii) Kuzalisha na kusambaza kwa wafugaji vifaranga 10,000 vya kambale kutoka kituo cha Kingolwira;

(iv) Kutambua mabwawa 66 yanayofaa kupandikizwa samaki kati ya 85 yaliyofanyiwa tathmini katika ranchi za mifugo za Dakawa (4), Kagoma (8), Kalambo (3), Kongwa (5), Kikulula (8), Mabale (10), Misenyi (8), Mzeri (15), Ruvu (15), Usangu (6) na Uvinza (3); na

(v) Kupandikiza vifaranga vya samaki aina ya perege 130,000 kwenye mabwawa 8 katika ranchi za Mzeri na Ruvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na taasisi zisizo za kiserikali za SEMMA na Kampuni ya Nyamwese kupitia mradi wa *MACEMP* imeendelea kuboresha kilimo cha zao la Mwani katika maeneo ya ukanda wa pwani ya bahari ya Hindi. Kupitia taasisi hizo, Wizara imewezesha kuundwa kwa vikundi vya ushirika wa wakulima wa mwani vya Maliwazano (Mkinga) na Jibondo (Mafia). Kikundi cha Maliwazo kimewezeshwa kwa kupatiwa mbegu za mwani, vitendea kazi, mafunzo ya kilimo bora cha mwani na usimamizi wa ushirika, kujengewa ghala la kuhifadhia mwani na kupatiwa boti ndogo 10 za kubebea mwani. Vilevile, wanakikundi 32 wa kikundi cha Jibondo wamepatiwa mafunzo ya kilimo bora cha mwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia ufugaji na uendelezaji wa mazao yatokanayo na ukuzaji wa viumbe kwenye maji kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuimarisha vituo vinane vya ufugaji wa samaki na kuzalisha na kusambaza vifaranga bora vya samaki milioni tatu;

(ii) Kuimarisha vituo vitatu vya uzalishaji wa mbegu za viumbe wakuzwao kwenye maji bahari vilivyoko Bagamoyo, Tanga na Mtwara;

(iii) Kuhamasisha shughuli za ufugaji samaki, unenepeshaji wa kaa na ukuzaji wa lulu; na

(iv) Kutoa mafunzo ya muda mfupi ya ukusanyaji wa takwimu, teknolojia za kisasa za utengenezaji wa vyakula vya samaki, uzalishaji wa vifaranga bora vya samaki na mifumo ya kisasa ya Ukuzaji Viumbe kwenye Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Sekta za Mifugo na Uvuvi: Wizara inatekeleza Mradi wa *MACEMP* kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, pamoja na Halmashauri 16 za mwambao wa Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010 wananchi 4,486, wakiwemo wanawake 1,806 na wanaume 2,680 wamewezeshwa kutekeleza miradi midogo ya kiuchumi 252 katika Halmashauri za Wilaya za Rufiji (2), Mafia (13), Bagamoyo (42), Muheza (10), Mkinga (28), Pangani (24), Mkuranga (16), Lindi Vijijini (20), Lindi Mjini (9), Mtwara Vijijini (15), Manispaa za Mtwara-Mikindani (20), Kinondoni (10), Temeke (5) na Ilala (7) na Jiji la Tanga (31) yenye thamani ya shilingi bilioni 3.9. Aidha, vikundi 31 vya kijamii vinavyojihusisha na miradi ya utunzaji na hifadhi ya mazingira ya bahari

na Ukanda wa Pwani katika Halmashauri za Wilaya za Pangani (10) na Muheza (3), Manispaa za Kinondoni (6), Temeke (5) na Ilala (1), na Jiji la Tanga (6) vimewezeshwa kwa kupatiwa fedha kiasi cha shilingi milioni 154.6 ili kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011 Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri 16 na wadau wengine itaendelea kutekeleza Mradi wa *MACEMP* katika kusimamia mazingira ya bahari na ukanda wa pwani kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuwezesha Halmashauri 16 za mwambao na Taasisi za Serikali kutekeleza majukumu ya mradi;

(ii) Kukamilisha mipango ya matumizi bora ya ardhi;
(iii) Kukamilisha mipango ya matumizi ya uwiano ya matumizi ya raslimali za bahari na ukanda wa pwani;

(iv) Kukamilisha ujenzi wa Jengo la Ofisi la Mvuvi na Ofisi za Mamlaka ya Usimamizi wa Bahari Kuu;

(v) Kuendelea kuzijengea uwezo jamii za wavuvi wa Ukanda wa Pwani kwa kuendeleza miradi midogo ili kuinua kipato;

(vi) Kuwezesha doria za kudhibiti uvuvi haramu na matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali za bahari na ukanda wa Pwani;

(vii) Kukamilisha mchakato wa uanzishwaji wa mfuko wa kukabiliana na athari za mazingira ya bahari na ukanda wa pwani ujulikanao kama *(Marine Legacy Fund);*

(viii) Kuwahamasisha wananchi wa mwambao wa bahari kuimarisha na kuanzisha *SACCOS* pamoja na Benki ya Wananchi wa Mwambao wa Pwani; na

(ix) Kuendelea na usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika Bahari Kuu (EZZ), ikiwa ni pamoja na kuimarisha doria na ukusanyaji wa mapato, kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Uvuvi katika Bahari Kuu *(Deep Sea Fishing Authority).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Utekelezaji wa Mpango wa Usimamizi wa Uvuvi katika Ziwa Victoria ni mradi unaotekelezwa na nchi za Kenya, Tanzania na Uganda. Mradi unasimamiwa na Taasisi ya Uvuvi ya Jumuia ya Afrika Mashariki katika Ziwa Victoria - *Lake Victoria Fisheries Organization (LVFO).*

Katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia Mradi huo imetekeleza yafuatayo:-

(i) Kuboresha mialo sita ya Bwai (Musoma), Sota (Rorya), Kigangama (Magu), Kahunda (Sengerema), Kikumba Itare (Chato) na Marehe (Bukoba) kwa gharama ya shilingi bilioni 3.3;

(ii) Kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali ya uvuvi kwa kugharamia doria zilizowezesha kukamatwa kwa wahalifu 55, makokoro 113, nyavu za timba 773 na nyavu za makila 10,737;

(iii) Kutoa ushauri kwa jamii za wavuvi kupitia Vikundi vya Usimamizi wa Rasilimali ya Uvuvi (BMUs) ambapo mitandao 212 ya BMUs imeundwa katika ngazi ya Kijiji (68), Kata (120), Wilaya (12) na Mkoa (3);

(iv) Kutoa mafunzo kwa viongozi 576 wa mtandao ngazi ya Kata (516), Wilaya (48) na Mkoa (12); na

(v) Kuwezesha ujenzi wa huduma za jamii katika mialo na vijiji vinavyopakana na Ziwa Victoria ambapo jumla ya shilingi milioni 165 zilitumika katika ujenzi wa zahanati 2, moja Muleba na nyingine Sengerema; madarasa 9, Chato (2), Sengerema (4) na Rorya (3); ofisi za walimu Chato (1) na Sengerema(1) na nyumba moja ya walimu (Muleba).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara kupitia Mradi wa Utekelezaji wa Mpango wa Usimamizi wa Uvuvi katika Ziwa Victoria, itaendelea kutoa mafunzo kwa BMUs na kufanya doria katika Ziwa Victoria ili kupambana na uvuvi haramu na kuhakikisha rasilimali ya uvuvi katika Ziwa Victoria inakuwa endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa Kuimarisha Uwezo wa Kudhibiti Magonjwa ya Mlipuko ya Mifugo (*SADC–TADs Project)*, ambao unahusisha nchi tano za Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika za Angola, Malawi, Msumbiji, Tanzania na Zambia. Mradi unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ambapo Tanzania imetengewa jumla ya dola za Kimarekani 5,888,189. Madhumuni ya mradi huo ni kuimarisha maabara na vituo vya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia Mradi huo imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuandaa taratibu za kudhibiti ugonjwa wa Miguu na Midomo pamoja na kuhamasisha wadau kuhusu udhibiti wa ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng’ombe nchini kwa kushirikiana na wadau;

(ii) Kufanya uchunguzi wa Ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo *(Pestes des Petits Ruminants*) katika Kanda za Kaskazini, Kusini na Ziwa ambapo sampuli 4,000 kutoka kwenye mbuzi na kondoo zilichunguzwa;

(iii) Kufanya uchunguzi wa ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng’ombe katika kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambapo uchunguzi umeonyesha kupungua kwa matukio ya ugonjwa;

(iv) Kununua vitendea kazi vya maabara na vifaa mbalimbali vya uchunguzi wa ugonjwa wa Sotoka *(Rinderpest test kit*);

(v) Kununua pikipiki 10 kwa ajili ya Vituo vya ukaguzi wa mifugo na mazao yake vya Bandari ya Dar es Salaam, Uwanja wa ndege Dar es Salaam, Tunduma (Mbeya), Sirari (Mara), Bandari ya Kigoma, Mutukula (Kagera), Horohoro (Tanga), Holili (Kilimanjaro), Isongole (Mbeya) na Bandari ya Mwanza na magari 9 kwa ajili ya Maabara Kuu ya Temeke na Vituo vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo vya Kanda vya Arusha, Iringa, Mpwapwa, Mtwara, Mwanza, Tabora na Temeke; na

(vi) Kutoa mafunzo mbalimbali kwa watumishi 86.

Katika mwaka 2010/2011, Wizara itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kununua vifaa kwa ajili ya Maabara Kuu ya Taifa ya Mifugo – Temeke na Vituo vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo vya Kanda;

(ii) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wataalam 20 na ya muda mrefu katika shahada ya uzamili kwa wataalam 4; na

(iii) Kufanya uchunguzi wa ugonjwa wa Miguu na Midomo kwa mifugo na wanyama pori pamoja na ugonjwa wa Homa ya Mapafu katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ina jumla ya watumishi 1,920 kati ya hao 900 ni wataalam wa mifugo, 340 ni wataaam wa uvuvi na 680 ni wa kada nyingine. Mahitaji halisi ni watumishi 2,530. Katika mwaka 2009/2010, Wizara imeajiri watumishi 40, kupandisha vyeo watumishi 97 na kuthibitisha kazini watumishi 38. Aidha, jumla ya wastaafu 46 wamelipwa mafao yao na kuwezesha maziko kwa watumishi 9 waliofariki dunia. Vilevile, kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kutoa mafunzo ya mfumo wa Wazi wa Upimaji na Tathmini ya Utendaji Kazi (OPRAS) ndani ya Wizara kwa watumishi 200;-

(ii) Kuwezesha mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 38 na ya muda mfupi kwa watumishi 11;

(iii) Kununua vitendea kazi vya kuhifadhia nyaraka ili kuboresha utunzaji wa nyaraka na kumbukumbu za Serikali;

(iv) Kusambaza kwa wadau nakala 350 za Mkataba wa Huduma kwa Mteja;

(v) Kuwezesha watumishi 52 kushiriki katika michezo ya SHIMIWI iliyofanyika katika Manispaa ya Morogoro mwezi Oktoba, 2009;

(vi) Kuwezesha vikao 4 vya TUGHE na 2 vya Baraza la Wafanyakazi;

(vii) Kuandaa Programu ya Mafunzo ya Watumishi wa Wizara; na

(viii) Kushirikisha Sekta binafsi katika utoaji huduma za ulinzi na usafi katika Makao Makuu ya Wizara na baadhi ya Taasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara itaajiri jumla ya wataalam 72, kati ya hao, 36 ni wa mifugo, 22 ni wa uvuvi na 14 wa fani nyingine. Aidha, watumishi 380 watapandishwa vyeo na 80 kuthibitishwa kazini. Pia, watumishi 200 wa kada mbalimbali watapatiwa mafunzo, kati ya hao 50 ya muda mrefu na 150 ya muda mfupi. Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kuelimisha wadau kuhusu Mkataba wa Huduma kwa Mteja na kufanya tathmini ya ubora wa huduma kwa wateja;

(ii) Kukamilisha Benki ya takwimu (*DataBank*) za watumishi kwa ajili ya kutunza kumbukumbu;

(iii) Kushirikiana na vyama vya wafanyakazi na Baraza la Wafanyakazi ili kuwezesha watumishi kuboresha utendaji kazi na kujenga uhusiano mzuri kati ya watumishi na mwajiri;

(iv) Kuhamasisha wafanyakazi kushiriki katika michezo ili kuboresha afya zao na kuimarisha uelewano miongoni mwao;

(v) Kuboresha utoaji wa huduma kwa Wadau kwa kuzingatia Mkataba wa Huduma kwa Mteja; na

(vi) Kuimarisha mfumo wa wazi wa kupima utendaji kazi (OPRAS) ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea na jukumu la kuuelimisha umma kwa kutumia njia mbalimbali za mawasiliano. Katika mwaka 2009/2010, jumla ya nakala 4,000 za kalenda ya mwaka 2010, nakala 2,000 za Jarida la Mifugo na Uvuvi na nakala 1,000 za mabango kuhusu Sekta za Mifugo na Uvuvi zimechapishwa na kusambazwa. Aidha, vipindi 12 vya televisheni na 20 vya radio vinavyohusu Wizara viliandaliwa na kurushwa hewani. Pia, Mkakati wa Mawasiliano wa Wizara umeandaliwa. Katika mwaka 2010/2011 Wizara itaendelea kutayarisha na kusambaza taarifa za matukio mbalimbali kuhusu Maendeleo ya Sekta za Mifugo na Uvuvi pamoja na kutayarisha na kusambaza nakala 1,000 za majarida na 1,000 za kalenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rushwa, Jinsia na UKIMWI: katika mwaka 2009/2010, Wizara imeendelea kuzingatia sheria na miongozo ya ajira katika utumishi wa umma, manunuzi na ugavi ili kuleta uwazi katika utoaji huduma na hivyo kuzuia mianya ya rushwa kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa. Aidha, Wizara imeendelea kutoa elimu ya jinsia na kujumuisha masuala ya jinsia katika

mipango, mikakati na programu mbalimbali za kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi. Pia, Kamati ya Jinsia imeendelea kuimarishwa kwa kupatiwa mafunzo ya muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011 Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kuzuia na Kuziba Mianya ya Rushwa wa Wizara. Pia, itafanya tathmini ya jinsia ili kuweza kubaini mbinu za kuleta usawa wa jinsia ndani ya Wizara. Aidha, Wizara itaendelea kutoa mafunzo zaidi kwa mratibu wa dawati la jinsia na watumishi wengine kuhusu masuala ya jinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara imeendelea kufanya tathmini ya hali ya UKIMWI pamoja na kuhamasisha watumishi kupima kwa hiari afya zao. Kutokana na uhamasishaji huo, idadi ya watumishi waliojitokeza kupatiwa huduma ya posho ya chakula cha lishe kwa mujibu wa Waraka Na. 2 wa Mwaka 2006 imeongezeka kutoka 3 mwaka 2008/2009 hadi 7 mwaka 2009/2010. Aidha, Kamati ya UKIMWI ya Wizara imeimarishwa na masuala ya UKIMWI yamefanywa Ajenda muhimu katika mikutano na makongamano yanayoandaliwa na Wizara na Vyama vya Kitaaluma vya Sekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kuhamasisha watumishi kupima kwa hiari afya zao, kuwahudumia walioathirika na kukamilisha Mpango Mkakati wa Wizara wa Kuzuia maambukizi mapya ya UKIMWI kufuatia kukamilika kwa tathmini ya hali ya UKIMWI katika Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi: Katika mwaka 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeanza kupitia Sera, Sheria na Kanuni za Sekta za Mifugo na Uvuvi kuhusu mazingira. Aidha, Wizara imeendelea kutoa elimu ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira katika jamii za wafugaji wa asili na wavuvi ili kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za mifugo na uvuvi. Wizara ilitoa mafunzo kuhusu namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na matumizi endelevu ya nyanda za malisho kwa wataalam 48 kutoka katika Halmashauri za Arumeru, Babati, Bahi, Chamwino, Hanang, Handeni, Iramba, Kilindi, Kilosa, Kilombero, Kisarawe, Kiteto, Kongwa, Korogwe, Kondoa, Longido, Manyoni, Meatu, Monduli, Morogoro-Manispaa, Morogoro-Vijijini, Mvomero, Mpwapwa, Mwanga, Ngorongoro, Simanjiro, Same, Siha, Singida na Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea na mchakato wa kuanzisha mfumo wa tahadhari ya majanga ya mifugo nchini kwa kutoa mafunzo juu ya ukukusanyaji na uchambuzi wa takwimu kwa wataalam 37 kutoka katika Halmashauri 7 za Lindi Mjini, Lindi vijijni, Kilwa, Liwale, Nachingwea, Ruangwa na Rufiji na kuhusisha Kituo cha Utafiti cha Naliendele kutoka mikoa ya Kanda ya Kusini. Katika mwaka 2010/2011, Wizara etaendelea kutoa mafunzo kuhusu ukukusanyaji na uchambuzi wa takwimu kwa wataalam 50 kutoka mikoa ya Kanda za Kaskazini-Mashariki, Kati na Ziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika,  katika mwaka 2009/2010, Wizara iliratibu na kushiriki katika mikutano na maadhimisho mbalimbali ya Sekta za Mifugo na Uvuvi kama ifuatavyo:-

(i) Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Nane Nane yaliyofanyika katika Manispaa ya Dodoma kuanzia tarehe 1 hadi 8 Agosti, 2009 yakiwa na Kaulimbiu "Kilimo Kwanza-Mapinduzi ya Kijani, Uhakika wa Chakula na Kipato". Nawapongeza wafugaji, wavuvi na wananchi wote walioshiriki katika kufanikisha maonesho hayo;

(ii) Wiki ya Unywaji Maziwa iliyofanyika Kitaifa Mjini Lindi tarehe 26 Mei hadi 1 Juni, 2010 ikiwa na Kaulimbiu "Je, umekunywa maziwa leo? Fuga ng'ombe wa maziwa"; na

(iii) Siku ya Chakula Duniani iliyofanyika tarehe 16 Oktoba, 2009 katika Manispaa ya Musoma ikiwa na Kaulimbiu "Tuimarishe Uhakika wa Chakula Kukabiliana na Majanga."

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, napenda kutoa shukrani za dhati kwa wale wote walioshirikiana nasi kwa njia moja au nyingine katika kutimiza majukumu yetu. Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. James Mnanka Wanyancha, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Mbunge wa Jimbo la Serengeti kwa kazi nzuri na ushirikiano mkubwa alioutoa, Katibu Mkuu Dkt. Charles Nyamrunda, Wakuu wa Idara na Wenyeviti wa Taasisi za Wizara, Wafanyakazi na Wadau wote kwa mshikamano wao katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi. Napenda kutoa shukrani za pekee kwa washiriki wetu wa maendeleo pamoja na wahisani wanaotuunga mkono katika kutekeleza miradi mbalimbali ya Sekta za Mifugo na Uvuvi; misaada yao tunaiheshimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuzitambua na kuzishukuru Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Umoja wa Nchi za Ulaya (EU), Serikali za Australia, Austria, Denmark, Japan, Jamhuri ya Afrika ya Kusini, Jamhuri ya Watu wa China, Ireland, Marekani, Misri, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Uswisi na Italia kwa kuchangia katika maendeleo ya sekta za mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kutoa shukrani kwa Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya FAO, IAEA, UNICEF, UNDP na WHO, Mifuko ya Kimataifa ya GEF na IFAD.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, napenda kutambua na kuzishukuru taasisi za kimataifa ambazo ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika; Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Japani (JICA), Shirika la Misaada la Ireland (Irish Aid), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DfID), Taasisi ya Rasilimali za Wanyama ya Umoja wa Afrika (AU/IBAR), Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE), Shirika la Maendeleo la Uswisi (SDC), Shirika la Ushirikiano la Ujerumani (GTZ), Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Denmark

(DANIDA), Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden (SIDA) na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Norway (NORAD).

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuyashukuru Mashirika na Taasisi za hiari za *Bill and Melinda Gates Foundation*, *Association for Agricultural Research in East and Central Africa (ASARECA), International Livestock Research Institute (ILRI)*, *World Wide Fund for Nature (WWF), Heifer Project Tanzania (HPT)*, *Overseas Fisheries Co-operation Foundation of Japan (OFCF), Vetaid, Care International*, *OXFAM, Wellcome Trust*, *Austro-Project, World Vision, FARM Africa, Land 'O' Lakes, Bangladesh Rural Advancement Committee (BRAC), World Society for Protection of Animals (WSPA), Global Alliance for Livestock and Veterinary Medicine (GALVmed), Institute of Security Studies (ISS),* Mashirika na Taasisi mbalimbali za humu nchini zinazojihusisha na uendelezaji wa sekta za mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupitia kwako nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati wote hao pamoja na wafugaji, wavuvi na wadau wengine na kuwaomba waendelee kushirikiana nasi katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 18 Mwezi wa Sita 2010, wakati Waziri Mkuu akisoma hotuba ya kuthibitisha Hotuba ya Makadirio na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2010/2011, alilijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali itaanzisha Mkoa mpya wa Geita. Kutokana na hatua hii nzuri ya Serikali, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuanzisha Mkoa mpya wa Geita. Kwa niaba ya Wananchi wa Wilaya ya Chato, tunamshukuru sana. Nina hakika Wananchi wa Mkoa huu mpya wa Geita sasa watajipanga ili baada ya Serikali kutoa Tangazo la Serikali la kuanzisha rasmi Mkoa huu, waamue ni wapi Makao Makuu ya Mkoa yatakuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mandhari nzuri ya Mji wa Chato, sitashangaa Wananhi wa Mkoa huu kuufanya Mji wa Chato kuwa Makao Makuu ya Mkoa mpya wa Geita. Hii ni kuzingatia hali halisi, kwa sababu Makao Makuu ya Mkoa wa Kagera yapo Bukoba, Makao Makuu ya Mkoa wa Mwanza yapo Mwanza, Makao Makuu ya Mkoa wa Mara yapo Mara, Makao Makuu ya Mtwara yapo Mtwara, Makao Makuu ya Tanga yapo Tanga.

**NAIBU SPIKA**: Na Makao Makuu ya Njombe yapo Njombe. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Makao Makuu ya Chato yawe ni Chato kwa sababu yapo Bandarini, lakini najua hili litazungumziwa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, nawashukuru sana Wananchi wa Kata ya Buziku na Chato kwa kumchangia Mheshimiwa Rais Shilingi laki tatu kwa ajili ya kuchukulia fomu. Ninapenda kuwajulisha kwamba, michango yao nilimkabidhi Waziri Mkuu na yeye alimkabidhi Mheshimiwa Rais siku aliyochukua fomu hapa Dodoma. Najua Wananchi wengi wa Wilaya ya Chato katika Kata zote 22 ikiwemo

Mnganza, Buziku, Nyamirembe, Buseresere na kadhalika, wamejiandaa kama wenzao wa Kata hizi kumchangia Mheshimiwa Rais na Mbunge wao kuchukua fomu. Ninataka kuwahakikishia michango yao nitakwenda kuipokea mara baada ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Chato, napenda kumhakikishia Rais kuwa, Wananchi wa Wilaya hii wanatambua kazi nzuri zinazofanywa na Serikali yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, napenda kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Biharamulo Mashariki (Chato), kwa ushirikiano wao mkubwa walionipa katika kipindi chote ambacho nimekuwa Mbunge wao. Kwa kuwa katika kipindi cha miaka kumi wamenipitisha bila kupingwa mfululizo; ni natumaini watatumia kura zao vizuri katika uchaguzi ujao kumchagua Mbunge atakayeweza kuwaletea maendeleo wanayoyatarajia katika Mkoa mpya wa Chato na Taifa kwa ujumla. Waswahili wanasema "Zimwi likujualo halikuli likakwisha" Wanachato wanalijua hili na katika Uchaguzi Mkuu ujao ninaamini watakichagua vizuri Chama cha Mapinduzi ili tuendeleze Ari zaidi, kwa Nguvu zaidi na kwa Kasi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Wizara inaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ya jumla ya shilingi 68,452,205,700.00 kama ifuatavyo**:-**

(a) Shilingi 10,010,795,000.00 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi (PE);

(b) Shilingi 24,030,445,000.00 ni kwa ajili ya matumizi mengine (OC); na

(c) Shilingi 34,410,965,700.00 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya hizo, shilingi 8,717,387,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 25,693,278,700.00 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe shukurani zangu za dhati kwako kwa nafasi uliyonipa na ninajua wananchi wa eneo lako watakupitisha tu; kwa nini wakunyime wewe! Naomba nitoe shukrani zangu nyingi kwa Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hotuba hii, nimeambatanisha Randama ya Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** baada ya kusema haya, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** *The Comedy* wamesema hawakuwezi kabisa kwenye *statistics*. Tunaendelea na hatua inayofuata, sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji. *(Kicheko)*

**MHE. KAIKA S. TELELE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha wa 2009/2010 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, ilikutana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi katika Ofisi Ndogo ya Bunge ya Dar es Salaam tarehe 31 Mei, 2010. Katika kikao hicho, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi alitoa maelezo kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010, changamoto za utekelezaji kwa kipindi cha mwaka 2009/2010, malengo na maeneo ya kipaumbele pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2009/2010: Wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2009/2010, Kamati ilitoa maoni na ushauri wa kuzingatiwa. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kiasi kikubwa Wizara imeyafanyia kazi maoni na ushauri wa Kamati. Baadhi ya maeneo yaliyofanyiwa kazi ni pamoja na:-

(i) Kuongeza vyanzo vya mapato kwa kutoza ushuru wa samaki wanaoingizwa kutoka nchi za nje kwa dola za kimarekani 0.25 kwa kilo. Aidha, ushuru wa ngozi ghafi zinazosafirishwa kwenda nje umeongezwa kutoka asilimia 20 hadi 40.

(ii) Bajeti ya utafiti kuchukua asilimia 22.7 ya Bajeti yote ya Wizara.

(iii) Maabara Kuu ya Mifugo ya Temeke imeboreshwa kwa kuajiri wataalam, kukarabati majengo na kupatiwa vifaa vya kisasa na vitendea kazi muhimu pamoja na kutoa mafunzo kwa wataalam.

(iv) Kituo cha Uhimilishaji kimeboreshwa kwa kuongezewa uwezo wa kuzalisha mbegu za madume bora kutoka dozi 100,000 hadi kufikia dozi 340,000 kwa mwaka.

(v) Katika kuhakikisha viwanda vya maziwa vinaondolewa kodi za mitambo na vifungashio, Wizara tayari imewasiliana na Wizara ya Fedha na inayafanyia kazi. Aidha, kodi ya ushuru wa forodha na kodi ya ongezeko la thamani zimeondolewa kwenye vyombo vya kuhifadhia na kupoozea maziwa.

(vi) Katika kutengeneza mazingira mazuri yatakayowezesha upatikanaji wa zana za kisasa za uvuvi, Serikali imepunguza kodi ya malighafi kutoka asilimia 20 hadi asilimia 5 ya kodi halisi na kuondoa kodi ya zana za uvuvi zikiwemo boti, nyavu na injini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Wizara pia imekumbana na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2009/2010. Changamoto hizo ni pamoja na:-

(i) Kuchelewa kutolewa kwa fedha za miradi ya maendeleo.

(ii) Kutopatikana kwa mikopo yenye masharti nafuu kwa wafugaji na wavuvi.

(iii) Kutopatikana kwa pembejeo na zana za gharama nafuu kwa ajili ya ufugaji na uvuvi.

(iv) Uhaba wa soko la uhakika la mazao ya mifugo na uvuvi.

(v) Elimu na teknolojia za kisasa kutokuwafikia wafugaji na wavuvi.

(vi) Uwekezaji mdogo katika sekta za mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi yenye Fungu 99, inaomba jumla ya shilingi 58,792,621,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 34,041,240,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 24,751,381,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya fedha za matumizi ya kawaida, shilingi 10, 010,975,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 24,030,445,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, kati ya fedha za maendeleo, shilingi 8,717,387,000 ni fedha za ndani na shilingi 16,033,994,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi hayo ya fedha yatawezesha Wizara kutekeleza kazi mbalimbali ilizojipangia. Baadhi ya kazi hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Katika Sekta ya Mifugo: Kuimarisha huduma za ugani na utafiti wa mifugo; kuendelea kutoa ruzuku ya madawa ya kuogesha mifugo na chanjo; kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya mifugo; kuboresha miundombinu muhimu ya mifugo kama minada, masoko, majosho na malambo; na kuimarisha upatikanaji wa huduma za uhimilishaji mifugo.

(ii) Katika Sekta ya Uvuvi: Kudhibiti uvuvi haramu na biashara ya samaki inayotokana na uvuvi huo na kuhifadhi mazingira; kuimarisha miundombinu ya kupokea, kuhifadhi na kusafirisha samaki na mazao mengine ya uvuvi; kuimarisha utoaji wa huduma za ufugaji wa samaki na ukuzaji wa viumbe wengine kwenye maji (*Fish*

*Farming*); kuimarisha usimamizi wa Sekta ya Uvuvi na ukusanyaji wa takwimu; na kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza kazi zilizopangwa kutekelezwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2010/2011, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni ya Jumla: Bajeti ya Wizara bado ni ndogo na tegemezi kwa asilimia 74.6 kwa wahisani kutoka nje. Hali hii inatia mashaka hasa kama wahisani wakichelewa kutoa fedha zao, miradi mingi ya maendeleo itakwama. Kamati inasisitiza Serikali iendelee kujenga uwezo wa kuwa na mapato yake ya ndani kwa miradi ya maendeleo na hii itawezekana endapo tutaamua kuanzisha vyanzo mbalimbali vya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaamini dhana ya Kilimo Kwanza imekuja kwa nia ya kuleta Mapinduzi ya Kijani na kukifanya kilimo chetu kuwa cha kisasa na cha kibiashara. Hata hivyo, wakati wa kupitia Bajeti ya Wizara, Kamati imeona kwamba hakuna viashiria vya kuwapo Mikakati ya dhati kutekeleza dhana hiyo. Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Wizara zote zinazohusika na Sekta ya Kilimo, zipewe fungu la kutosha kutekeleza azma ya Kilimo Kwanza katika nguzo zake kuu ili zianze utekelezaji huo mapema iwezekanavyo na ziwajibike ipasavyo kwa matumizi bora ya fungu hilo. Serikali ioneshe waziwazi na kwa vitendo ni namna gani itatekeleza dhana ya Kilimo Kwanza.

(ii) Serikali haina budi kuhusisha Sekta Binafsi katika utekelezaji wa Kilimo Kwanza kwa kuhakikisha inawawekea vivutio muafaka kwani ikumbukwe Sekta Binafsi inachangia kwa asilimia kubwa katika kukua kwa uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uhaba wa Wataalam umekuwa ni tatizo katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi na hivyo kuathiri mchango wa sekta hii katika Pato la Taifa. Inakadiriwa kuwa kuna upungufu wa Maafisa Ugani wa Mifugo 13,469 na 15,839 wa Sekta ya Uvuvi nchini ikilinganishwa na mahitaji ya 16,500 na 16,000 sawia.

Kamati inaamini uwepo wa wataalam wa kutosha na wenye kuwezeshwa kwa kupatiwa vitendea kazi na kuboreshewa maslahi yao ni mojawapo ya njia itakayowezesha sekta hizi muhimu kukua kwa kasi inayotakiwa kwani watafikisha huduma inayostahili kwa wafugaji na wavuvi. Kamati inashauri Serikali iongeze wataalam hao ili waweze kuwafikia wananchi wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi za Utafiti ni muhimu sana katika kuongeza tija katika uzalishaji na utoaji huduma ndani ya jamii. Pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuongeza bajeti ya taasisi hizi, bado hazijafikia kiwango kinachotakiwa. Kamati inaishauri Serikali iendelee kuongeza bajeti inayotengwa kwa taasisi hizi. Aidha,

Wizara itengewe fungu kutokana na bilioni 30 zilizotengwa kwa ajili ya taasisi mbalimbali za utafiti nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi mingi ya ufugaji na uvuvi ipo kwenye Halmashauri ambazo ndizo mamlaka za utekelezaji, lakini Halmashauri hizo hazina wataalam wa kutosha. Kamati bado inashauri Serikali Kuu iendelee kuratibu na kusimamia Miradi yote nchini na wala isiziachie Halmashauri pekee ili miradi hiyo iweze kuleta matokeo mazuri. Aidha, ihakikishe wataalam zaidi wanapelekwa katika Halmshauri hizo ili kuweza kusimamia vyema miradi hiyo na hatimaye kuleta tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Mifugo: Unywaji wa maziwa kwa nchi yetu bado upo chini na hii inatokana na sababu mbalimbali zikiwemo; bei kubwa ya maziwa, uhaba wa viwanda kwa ajili ya kusindika maziwa na gharama ya vifungashio pamoja na miundombinu mibovu ya kufikisha maziwa katika soko.

Kutokana na matatizo yanayoonekana kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kufanya zao hili kutotumiwa ipasavyo, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

(i) Uhamasishaji ufanyike kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kunywa maziwa. Aidha, programu ya unywaji maziwa katika shule iendelezwe katika maeneo yote nchini.

(ii) Kamati inaipongeza Serikali kwa kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mashine na vifaa vya kukusanya, kusafirisha na kusindika maziwa ili kuhamasisha uwekezaji katika sekta hii na kuboresha kipato kwa wananchi. Hata hivyo, Kamati bado inashauri Serikali kuruhusu vifungashio vya maziwa vyenye ubora unaotakiwa kuingizwa nchini na kuondolewa kodi ya ongezeko la thamani ili kuendelea kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya maziwa.

(iii) Uhaba wa Viwanda vya kusindika maziwa umesababisha maeneo ambayo wanazalisha maziwa mengi kumwaga maziwa hayo kutokana na ukosefu wa soko. Kamati inashauri Serikali iweke vivutio kwa wawekezaji binafsi na pia ihamasishe wafugaji kuunda vyama vya ushirika vya wafugaji na wasindikaji wa maziwa ili kurahisisha upatikanaji wa soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ngozi ni zao ambalo likitumiwa vizuri linaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Taifa. Ngozi za mifugo bado hazichangii ipasavyo katika Pato la Taifa ikilinganishwa na idadi ya mifugo tuliyonayo na hii inatokana na ngozi ya mifugo yetu kutokuwa na ubora unaotakiwa katika soko. Kamati inasisitiza yafuatayo:-

(i) Elimu zaidi iendelee kutolewa kwa wafugaji kuhusu umuhimu wa kutunza mifugo yao.

(ii) Sheria ya Ngozi isimamiwe ipasavyo ili kuleta manufaa yaliyokusudiwa kwa wafugaji na wafanyabiashara ya ngozi.

(iii) Viwanda vingi vya kusindika ngozi vianzishwe nchini na Serikali ivipe motisha. Aidha, kwa viwanda vilivyopo, Serikali iweke mkakati utakaowezesha viwanda hivyo kuingia ubia na Makampuni mbalimbali kama ya magari ili kuwa na uhakika wa soko kama ilivyo kwa nchi nyingine za Ethiopia na Eritrea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Machinjio na Viwanda vya Nyama: Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada zinazoendelea za ujenzi wa machinjio ya kisasa ya Ruvu. Nchi yetu imebarikiwa kuwa na mifugo mingi, wakiwemo ng'ombe takribani milioni 19.1 na mbuzi milioni 13.6 inasikitisha kuona hatuna machinjio ya kutosha na viwanda kwa ajili ya kusindika nyama.

Kamati inashauri yafuatayo: Serikali ijenge machinjio ya kutosha katika maeneo mbalimbali nchini; na viwanda vyote vya nyama ambavyo walipewa wawekezaji na kushindwa kuviendeleza virudishwe kwa Serikali ili watafutwe wawekezaji watakaoweza kuviendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu kwa muda mrefu sasa imekuwa na migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi kutokana na kutokuwepo mpango madhubuti wa matumizi ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini. Kutokana na hali hii, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali iweke utaratibu utakaowezesha wafugaji wote nchini kutengewa maeneo kwa ajili ya mifugo yao ili kuepuka migogoro inayotokea baina yao na watumiaji wengine wa ardhi kama Wakulima na Wawekezaji.

(ii) Ranchi ambazo wamepewa Wawekezaji na kushindwa kuziendeleza zigawiwe kwa wafugaji watakaondeleza maeneo hayo.

(iii) Serikali iendelee kutoa elimu juu ya ufugaji wa kisasa wa kuwa na mifugo michache na kuinenepesha itolewe kwa wafugaji ili kuongeza thamani ya mifugo yao kabla ya kwenda sokoni na hivyo kujiongezea kipato chao wenyewe na Pato la Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha kwa ajili ya udhibiti wa milipuko ya magonjwa ya mifugo, kwa takriban asilimia 86.4 inategemea wafadhili kutoka nje. Kamati inapata wasiwasi endapo ikatokea milipuko ya magonjwa na fedha za wafadhili zikachelewa, basi kwa hakika nchi itaathirika sana.

Kamati inashauri Serikali ijipange vizuri, kupambana na kwa kutumia fedha zake za ndani, endapo milipuko ya magonjwa itatokea. Aidha, katika bajeti zijazo ni vyema kujihakikishia uwepo wa fedha za ndani kukabili milipuko ya magonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo iliyopo nchini ni mingi sana ikilinganishwa na uwezo wa miundombinu ya kuihudumia kama malambo na majosho. Kamati inashauri Serikali ijitahidi kujenga malambo madogo madogo kwa ajili ya kuipatia mifugo maji na majosho ya kuogesha mifugo ili kudhibiti kuenea kwa magonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uvuvi ni Sekta muhimu katika nchi hii kutokana na mchango wake mkubwa katika kuwapatia wananchi ajira, lishe, kipato na kuingizia nchini fedha za kigeni.

Pamoja na umuhimu wake, bado Sekta hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo Kamati inashauri lazima kuwepo na mikakati maalum ya kukabiliana na changamoto hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uvuvi haramu. Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudi inazochukua ili kupambana na uvuvi haramu katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Pamoja na juhudi hizo uvuvi haramu bado unaendelea kwa baadhi ya maeneo. Kamati inashauri mamlaka husika kusimamia sheria zilizopo na ikibidi katika maeneo ya vijijini zitungwe sheria ndogo ili kudhibiti uvuvi huo. Aidha, elimu zaidi iendelee kutolewa kwa wavuvi juu ya umuhimu wa kutumia zana bora za uvuvi na hii iende sambamba na kuwapatia mikopo ya kuweza kununua zana bora za uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuandaa mazingira ya kufugia vifaranga vya samaki, ili tuweze kuwa na samaki wengi na kupunguza uharibifu unaofanyika katika sehemu chache zenye samaki, Kamati inaishauri Wizara kuandaa mazingira mazuri kwa ajili ya ufugaji wa vifaranga vya samaki. Aidha, Kamati inaona ipo haja ya kufufua maeneo yaliyokuwa yanafugwa samaki (*aquaculture*) ambayo kwa sasa hayatumiki ili kuendeleza sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uboreshaji wa biashara ya samaki wa michezo na wa mapambo. Biashara ya samaki wa michezo (*sports fish)* imekuwa ikiziingizia nchi nyingi fedha za kigeni. Nchi yetu imebahatika kuwa na samaki wa michezo kama *trouts* na *common carp* lakini inashindwa kufanya biashara hiyo. Kamati inashauri kama ilivyokuwa zamani ziundwe kambi kwa ajili ya shughuli hiyo ili kuwavutia watalii na kuliingizia Taifa pato. Aidha, biashara ya samaki wa mapambo *(Aquarium fish)* nayo iendelezwe kwani itasaidia kutoa ajira kwa vijana wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi wa Usimamizi wa Mazingira katika Ukanda wa Pwani (*MACEMP*), Kamati inapongeza jitihada zinazofanywa na Mradi wa Usimamizi wa Mazingira katika Ukanda wa Pwani (*MACEMP*) ili kuboresha maisha ya

wananchi wa maeneo ya Ukanda wa Pwani. Pamoja na pongezi hizo, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Kuwepo na maandalizi ya kutosha ili Mradi huo utakapokwisha Serikali iweze kutenga fedha za kuuendeleza.

(ii) Vianzishwe vikundi vidogo vidogo na vipatiwe elimu ya usindikaji.

(iii) Wavuvi wapewe nafasi ya kwenda nchi nyingine kama vile Ghana kujifunza namna ya kusindika samaki ili kuwaongezea utaalam na ubora na kuongeza thamani ya samaki wanaovuliwa nchini.

(iv) Ili kuwapatia wananchi shughuli za nyongeza ni vyema *MACEMP* ishirikiane na *SIDO* katika kuwafundisha wananchi kazi nyingine za mikono kama usindikaji wa vyakula na ufugaji wa nyuki.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la mwani linalimwa sana katika Ukanda wa Pwani na hivyo kuwa tegemeo hasa kwa wanawake. Pamoja na kuwa ndio tegemeo kubwa kwa wanawake katika kujiongezea kipato, lakini bei ya zao hili bado ni ndogo sana ikilinganishwa na mazingira magumu ya uvunaji wake. Kamati inaendelea kusisitiza yafuatayo:-

(i) Bei ya mwani iendane na gharama za uvunaji.

(ii) Viwanda vya kusindika mwani vijengwe ili kuongeza thamani yake.

(iii) Vifaa kwa ajili ya kuingilia baharini kuvuna mwani *(Protective gear)* vitolewe kwa wakulima.

(iv) Taarifa juu ya masoko ziwafikie wakulima

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wawekezaji katika sekta ya uvuvi. Kamati inatambua kuwa ili Sekta ya uvuvi ikue kwa kiwango cha kuridhisha na kuchangia kukua kwa uchumi ni lazima kuwepo na uwekezaji wa kutosha, uwekezaji katika sekta hii bado ni mdogo sana ikilinganishwa na rasilimali zilizopo za uvuvi. Kamati inashauri Serikali iweke mazingira mazuri ya kuwavutia wawekezaji wakubwa watakaofanya uvuvi wa kibiashara *(Large Scale Fishing)* ili kuweza kuchangia katika kukua kwa sekta hii na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ili kuwasilisha Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Napenda kuwatambua wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mwenyekiti; Mheshimiwa Kidawa H. Saleh, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Kheri K. Ameir, Mjumbe; Mheshimiwa Teddy L.

Kasella – Bantu, Mjumbe; Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mjumbe; Mheshimiwa Salim H. Khamis, Mjumbe; Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mjumbe; Mheshimiwa Joyce N. Machimu, Mjumbe; Mheshimiwa Janet Mbene, Mjumbe; Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mjumbe; Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mjumbe; Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mjumbe; Mheshimiwa Juma S. Omary, Mjumbe; Mheshimiwa Mwanakhamis K. Said, Mjumbe; Mheshimiwa Salum K. Salum, Mjumbe; Mheshimiwa Abdulkarim E. Shah, Mjumbe; Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mjumbe; anayewasilisha taarifa hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati napenda kuwapongeza Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dr. John P. Magufuli na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha, kwa ushirikiano wao mzuri waliyoipa Kamati katika kipindi chote hiki. Aidha, nampongeza Katibu Mkuu, Dr. Charles Nyamrunda pamoja na wataalam wote wa Wizara kwa ushirikiano wao wakati wa kujadili na kuchambua bajeti ya Wizara kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dr. Thomas Kashililillah, Makatibu wa Kamati Ndugu Pamela Pallangyo na Ndugu Pili Omari kwa kuiwezesha Kamati kufanikisha shughuli zake na kuratibu taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, napenda pia nichukue nafasi hii kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Ngorongoro kwa kunichagua na kunivumilia miaka yote mitano na naomba tena kwa mara nyingine wanikumbuke katika ufalme wao katika siku za usoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, nashauri Bunge lako Tukufu likubali na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Fungu 99 kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 yenye jumla ya Sh. 58,792,621,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana watakukumbuka tu kwa yale mema uliyotenda kwao. (*Makofi*)

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI :** Mheshimiwa Naibu Spika, tunakabiliwa na Uchaguzi Mkuu mwezi Oktoba. Hotuba yetu ya leo itakuwa tofauti sana na zile ambazo zimetangulia. Hotuba hii tutajielekeza zaidi katika kile ambacho Kambi ya Upinzani inatarajia kutekeleza pale wananchi watakapotupa ridhaa ya kuongoza nchi hii baada ya uchaguzi Mkuu Oktoba 2010. Kwa maana nyingine nawasilisha hotuba mbadala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu, Mwenye hekima. ambaye ametuumba kutokana na

nafsi moja tu. Naye ni Mweza wa kuteremsha muujiza. Kwa hakika sifa njema zote ni zake yeye Mola Mlezi wa walimwengu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2010/2011, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 99(3) na (7) toleo la 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hali halisi ya ufugaji nchini. Pamoja na kwamba nchi yetu ni ya pili katika Bara la Afrika kwa wingi wa mifugo, tukiwa na ng'ombe milioni 19, mbuzi milioni 11.7, kondoo milioni 3.9, nguruwe milioni 1.7 na kuku zaidi ya milioni 33, lakini bado mchango wa mifugo katika pato la Taifa ni mdogo mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba juhudi kadhaa zimechukuliwa na Wizara husika kuimarisha Sekta ya Mifugo lakini sekta hii bado inakabiliwa na matatizo kadhaa yanayojikita katika Sera yenyewe na mfumo mzima wa ufugaji hapa nchini. Maendeleo endelevu katika Sekta ya Mifugo bado hayajawekewa mpango mkakati mahususi utakaohusisha mahusiano katika matakwa ya kijamii, kiuchumi na kimazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limekuwa linawaathiri sana wafugaji hapa nchini, ni ile hatua ya Serikali kuanzisha na kuendelea kupanua Mbuga za Wanyama na Mapori ya Hifadhi katika maeneo ambayo wafugaji huyatumia kuchungia mifugo yao, jambo ambalo linazidi kuathiri fursa katika matumizi ya ardhi kwa wafugaji na hatima yake ni kuwatenga kabisa na ardhi yao ya asili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera za Serikali za kupanua kilimo kutoka mashamba madogo kwenda kwenye mashamba makubwa ukulima wa umwagiliaji wa mashamba makubwa na uchimbaji wa madini shughuli hizi zimechukua ardhi kubwa sana iliyokuwa inatumiwa na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kwamba ukaribishwaji wa wawekezaji wakubwa katika sekta za kilimo, maliasili na madini kumepelekea kuwasukumiza pembeni wafugaji kutoka katika maeneo yao ya asili, hivyo kusababisha migongano na mifarakano kwenye matumizi ya rasilimali ardhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukame wa mara kwa mara unaotokezea nchini umekuwa unaathiri sana maendeleo ya mifugo kutokana na kushuka uzalishaji, kudhoofika kwa mifugo kunakosababisha kushuka kwa bei na vifo vya mifugo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Kambi ya Upinzani tutakapopata ridhaa ya wananchi kuiongoza nchi hii, katika Uchaguzi ujao, tutachukua hatua za makusudi kuandaa Sera, Mikakati na Mipango kuihuisha Sekta ya Mifugo kwa kuoanisha masuala ya kijamii, uchumi na mazingira na kwa kuangalia matakwa ya jamii yenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tutajitahidi kuielewa hali halisi ya mazingira ilivyo, mabadiliko yake, namna inavyoathiri mfumo mzima wa ufugaji. Mikakati mizuri hatimaye itaandaliwa na kuweka mfumo madhubuti wa kushirikisha jamii za wafugaji katika kuiendeleza Sekta hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya juhudi kubwa za kuhakikisha inatoka katika dhana ya uchungaji na kuingia katika dhana ya ufugaji. Katika kuhakikisha hilo linatimizwa, imejitahidi kuanzisha mashamba ya uzalishaji mitamba bora na mashamba ya malisho bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaelewa kuwa Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Arusha ndio mikoa inayojulikana kuwa ni Mikoa ya wafugaji. Hivyo basi kitendo cha Serikali kushindwa kufungua vituo hivyo karibu na wachungaji walipo tunaliona suala hii ni kutokuwa na mipango endelevu ya kupunguza matumizi kwa wafugaji na kwa Serikali yenyewe. Tunaitaka Serikali iliangalie upya suala hili kutimiza malengo ya uanzishwaji kwake ili kuwasogezea karibu wafugaji huduma hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo ni ujenzi wa machinjio ya kisasa kwenye maeneo ambayo uzalishaji wa ng'ombe si mkubwa. Hali hii inaathiri sana ile dhana ya kuwataka wafugaji kuvuna mifugo yao. Kutokana na matatizo ya ardhi yanayowakabili wafugaji hapa nchini, Kambi ya Upinzani tunakusudia kuchukua hatua zifuatazo kukabiliana na tatizo hilo.

Tutaendesha sensa ya mifugo nchi nzima kujua idadi halisi ya mifugo tuliyonayo nchini hasa ukizingatia ni zaidi ya miaka 20 sasa sensa kama hiyo haijafanyika na kwamba tumepoteza idadi kubwa ya mifugo kutokana na matokeo ya mara kwa mara ya ukame. (*Makofi*)

Serikali yetu kuanzia ngazi ya vijiji hadi Serikali Kuu itahakikisha kwamba ardhi ya kutosha na iliyo nzuri itatengwa kwa ajili ya matumizi ya ufugaji. Sambamba na hilo, tutaanzisha maeneo kadhaa ya hifadhi ya malisho ambayo yatatumika iwapo maeneo ya kawaida ya malisho yameathiriwa na ukame. (*Makofi*)

Tutaandaa miundombinu ya kutosha kama vile malambo, majosho, malisho na zahanati za mifugo katika maeneo yale ambayo wafugaji walihama kutokana na ukosefu wa miundombinu hiyo, ili iwe ni kichocheo kwa wafugaji hao kurejea katika maeneo yao ya asili. (*Makofi*)

Kadhalika miundombinu kama hiyo tutaijenga ya kutosha katika maeneo mapya yaliyoteuliwa kuhamishia wafugaji ili kunusuru uharibifu wa mazingira na kupoteza mifugo mingi kutokana na vifo. (*Makofi*)

Wafugaji wataendelea kuelimishwa umuhimu na namna ya kuvuna mifugo yao kwa ajili ya kujiletea maendeleo ya kijamii ikiwa ni pamoja na makazi ya kudumu, elimu, afya na kadhalika. (*Makofi*)

Wafugaji watapatiwa mikopo yenye masharti nafuu kwa ajili ya kuendeleza ufugaji wa kisasa na kuanzisha kilimo cha mazao chakula na biashara.

Tutaimarisha minada na masoko ya mifugo pamoja na viwanda vya kusindika mazao ya mifugo katika maeneo ambayo ina mifugo mingi, ili kuongeza thamani ya mifugo na hatimaye kuongeza tija. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uzalishaji wa mazao ya mifugo, mwitikio wa uwekezaji katika mashamba makubwa ya mifugo na viwanda vya kusindika mazao ya mifugo umekuwa ni mdogo sana. Hii ni kutokana na sababu kwamba hakuna vivutio vya kutosha vya kuweza kuwavutia wawekezaji kuwekeza katika Sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la msingi sasa kwa Serikali kuiwezesha Sekta za Mifugo na Uvuvi kuandaa mazingira mazuri yanayoweza kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeelezwa hapa kwamba uzalishaji maziwa nchini umeongezeka kufikia lita 1.6 milioni. Lakini ni la kusikitisha kwamba usindikaji wa maziwa bado ni mdogo mno. Kwa mfano, ndugu zetu wa Kenya wanasindika maziwa lita milioni 1.2 kwa siku ukilinganisha na uzalishaji wa lita milioni 10 kwa siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kupungua huku kwa usindikaji wa maziwa unatokana kufungwa kwa viwanda vingi kutokana na usimamizi mbaya wa viwanda hivyo uliopelekea kuzalisha bidhaa hafifu na hivyo kukosa soko. Sababu nyingine ni pamoja na ukosefu wa mikopo ya benki na masoko ya uhakika. (*Makofi*)

Mheshiwa Spika, viwanda vya kusindika nyama navyo ni vichache, hali inayopelekea kutoitumia vyema fursa ya biashara ya nyama na bidhaa zitokanazo na nyama nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zifutazo tunazotarajia kuzichukuwa iwapo tutaingia madarakani badala ya Uchaguzi Mkuu ujao ni zifuatazo:-

Tutaimarisha huduma za ugani vijijini ikiwa ni pamoja na kuwapatia Maafisa Ugani makazi na usafiri.

Tutaimarisha uzalishaji katika Sekta hii ya Mifugo kwa kuhakikisha Serikali, taasisi za kifedha na *NGOs* tunawekeza ipasavyo katika uzalishaji na usindikaji wa bidhaa za mifugo. Ikiwa ni pamoja na kupanua masoko ya bidhaa hizo nje ya nchi.

Tutaendeleza na kuimarisha huduma za uhamilishaji ili kupata mifugo bora kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa nyama na maziwa.

Tutahakikisha maeneo yote ambayo ina mifugo mingi nchini tunajenga viwanda vya kisasa vya kusindika maziwa na nyama na kuimarisha minada ya mifugo ili kuongeza pato kwa mfugaji. Lengo ni kuhakikisha kwamba minada ya mifugo na viwanda vya usindikaji vinamfuata mfugaji na si vyinginevyo. (*Makofi*)

Tutapiga marufuku uingizaji wa nyama na maziwa kutoka nje ya nchi ili kuimarisha soko la ndani. (*Makofi*)

Katika kipindi kifupi kijacho, baada ya soko la ndani kujitosheleza, tutaimarisha soko la nje la bidhaa za mifugo hasa katika masoko ya nchi za Afrika Mashariki na Uarabuni.

Tutawaunganisha wazalishaji wote wa maziwa kama ilivyo *KCC* na *Brookside* kule Kenya na wale wazalishaji wa nyama ili wawe na nguvu ya kujisimamia wenyewe katika kuendeleza ufugaji nchini.

Tutalisimamia vyema soko la ngozi kwa kuimarisha viwanda vya usindikaji pamoja na kutengeneza bidhaa zitokanazo na ngozi ili kuongeza thamani yake.

Tutaimarisha Maabara Kuu ya Mifugo pamoja na maabara nyinginezo ili pamoja na mambo mengine tuweze kuzalisha chanjo za mifugo sisi wenyewe ili kupunguza gharama za uagizaji chanjo kutoka nje ya nchi. (*Makofi*)

Tutajitahidi kuzalisha zaidi ng’ombe za Mpwapwa ambao sasa hawaongezeki kwani aina hii ya ng’ombe ni ukombozi katika uzalishaji mfugaji. (*Makofi*)

Tutaimarisha huduma za kinga na tiba ya mifugo ili kupunguza vifo vya mifugo na kupungua kwa uzalishaji.

Tutaboresha mishahara na maslahi ya watalaam na watendaji wengine. Suala hili litasaidia sana kupunguza watalaam wa mifugo ambao wanaihama fani hii na kuhamia fani nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali halisi ya uvuvi nchini. Sekta ya Uvuvi nchini ni miongoni mwa sekta muhimu katika kukuza uchumi wa kaya na wa Taifa kwa ujumla. Sekta hii imechangia takriban 1.6% ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi katika Bahari Kuu ni moja ya maeneo ambayo Serikali yetu itaiangalia kwa makini na hatimaye kuchukua maamuzi ambayo yatapelekea kuongeza mapato ya Serikali kutokana na kusimamia vyema shughuli za uvuvi huo ikiwa ni kusimamia kodi zinazolipwa na meli za uvuvi kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani imeshangaa sana kuona kuwa kitabu cha mapato *(Revenue Book)* katika mapato yatokanayo na leseni za uvuvi, bahari ya ukanda wa pwani na leseni za meli zinazovua bahari kuu inaonyesha mapato ni shs.1000 tu.

Mheshimiwa Waziri, Dr. Magufuli amefanya jitihada binafsi kubwa sana katika kuhakikisha Sekta ya uvuvi inaingiza kipato cha kutosha katika pato la Taifa, hivyo kushindwa kuonyeshwa hata ada ya leseni kwenye vitabu vya mapato, tafsiri yake ni kuhujumu jitihada binafsi za Mheshimiwa Waziri. Kambi ya Upinzani inahitaji maelezo ya kina katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio haya, Sekta ya Uvuvi inakabiliwa na changamoto kadhaa zinazorejesha nyuma maendeleo ya uvuvi hapa nchini. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na:-

- Uendeshaji wa uvuvi haramu na uharamia katika Maziwa na Bahari Kuu.
- Kuendelea kuwepo uvunaji na matumizi ya rasilimali ya uvuvi isiyo endelevu.
- Ukosefu wa upatikanaji wa mitaji na mikopo kwa ajili ya kuwekeza kwenye shughuli za uvuvi.
- Magendo ya samaki kutoka nchi moja kwenda nyingine.
- Wamiliki wa viwanda vya kusindika samaki kuendelea kuvuna samaki wachanga.
- Vikundi vya ulinzi wa rasilimali za uvuvi havina zana za kutosha na za kisasa za kukabiliana na uharamia pamoja na uvuvi haramu unaoendeshwa katika maziwa.
- Shughuli za kilimo na ufugaji pamoja na uchafuzi wa taka za viwandani.
- Kilimo cha mwani bado hakijapewa umuhimu unaostahiki hasa ukizingatia kwamba kilimo hiki kinatoa ajira nyingi kwa akina mama kinachopelekea kupunguza umasikini wa kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi watakapotupa ridhaa ya kuendesha nchi hii, tumejipanga kuchukua hatua mchanganyiko zifuatazo ili kuiendeleza sekta hii ya uvuvi, ikiwa ni pamoja na kukabiliana na uharamia na uvuvi haramu hapa nchini:-

- Tutaendesha tafiti za kutosha zitazopelekea kujua ni kiasi gani cha rasilimali ya samaki iliyopo, ili kuweza kupanga mipango na mikakati endelevu ya uvunaji, utumiaji na uhifadhi wa rasilimali hiyo.
- Tutaanzisha, tutaimarisha na kusimamia taasisi za kifedha ambazo zitawapatia wavuvi mikopo yenye masharti na riba nafuu kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uvuvi.
- Tutaendelea kuanzisha na kuendeleza viwanda vya kusindika samaki, hatua ambayo itapelekea wavuvi kuvuna samaki maalum kwa ajili ya soko na hivyo kupata bei nzuri.
- Sambamba na hilo, tuendeleze ufugaji wa samaki wa aina na kabila tofauti ili kukidhi mahitaji ya soko.

- Tutapunguza ukubwa na wingi wa kodi wanazotozwa wavuvi wadogo ili kupata unafuu wa gharama katika kuendeleza shughuli za uvuvi.

- Tutaimarisha doria kwa kutoa vyombo vya kutosha na vya kisasa kukabiliana na uharamia na wavuvi haramu.

- Tutasimamia sheria na kanuni zilizopo na ikibidi kutunga mpya kusimamia suala la uvuvi ili uwe endelevu.
- Tutatoa motisha kwa wavuvi wadogo ili waweze kuachana na uvuvi haramu, kwa kuwapa fursa ya kubadilisha zana haramu wanazotumia na badala yake kupewa zana mahususi bila malipo yoyote.

- Tutaanzisha na kuendeleza viwanda vya kuzalisha zana na vifaa vya kuvulia hususan ukanda wa bahari ambako viwanda ni vichache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha Mwani Serikali yetu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa mwani kwa pamoja tutaendelea kuhamasisha kilimo cha mwani kwa lengo la kuongeza tija na kipato. Ni dhahiri kwamba kina mama wengi wamejiajiri katika kilimo cha mwani, ajira hii ni nzuri kwa hivyo itatupasa kuisimamia ipasavyo, hususan suala la soko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Wete kwa kuniunga mkono na kunipa ushirikiano mkubwa katika kipindi chote cha Ubunge wangu. Naamini nimewatumikia vyema kwa kadri Mwenyezi Mungu alivyonijaalia.

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani kwa umahiri mkubwa waliouonyesha katika kutuongoza, kutusimamia na kutuelekeza vyema katika shughuli zetu za siku hadi siku.

Kadhalika natoa shukrani zangu kwa Waheshimiwa Wabunge wote na hususan Wabunge wa Kambi ya Upinzani kwa mashirikiano makubwa niliyoyapata yaliyonipelekea kujiona kama ni mtu tuliozaliwa familia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii adhimu kutoa shukurani za dhati kwa familia yangu, wakiwemo wake zangu Bi. Asha na Bi Mkiwa, watoto na familia yangu kwa ujumla, kwa kunipa moyo na kuniunga mkono kwa muda wote nikifanya shughuli zangu za kuwakilisha wananchi katika Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuliendesha vyema Bunge hili la spidi na

viwango. Sote tumejionea namna Bunge hili la tisa linavyoendesha shughuli zake kwa ufanisi mkubwa. Namwomba Mwenyezi Mungu kwa Utukufu na Rehema Zake atujaalie sote tuliomo ndani ya ukumbi huu *Inshallah* tukutane tena katika Bunge lijalo la kumi, Novemba 2010. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Amenikumbusha kulikuwa na Kiongozi mmoja wa Dini akawa amefariki Muumini wake, basi wakasema huko mbinguni kuna hiki na hiki yote yalikuwa mazuri. Lakini akaishia kulia mwenyewe. Sasa kama mbinguni kuna mazuri kwa nini mnalia? Tunashukuru sana kwa hotuba hiyo. Tunao wachangiaji idadi yao siyo kubwa sana lakini wanatosha. Yuko Mheshimiwa Job Ndugai halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Laizer na Mheshimiwa Yono Kevela ajiandae.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kwanza niweze kuchangia katika Hotuba ya Mheshimiwa Dr. John Magufuli na Mheshimiwa Dr. Wanyancha rafiki yangu, nawapongeza sana kwa kazi nzuri Wizarani pamoja na wasaidizi wao wote. Nawashukuru sana wananchi wa Kongwa kwa heshima waliyonipa kwa vipindi viwili kuwa mwakilishi wao hapa Bungeni. Nitasema kidogo hapo mwisho kuhusu ndugu zangu wa Kongwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ningependa kulipeleka zaidi Serikalini kwa sababu ni mwakilishi wa Bunge hili kwenye Chuo Kikuu cha Dodoma kwenye Baraza la Chuo Kikuu, ni vyema nisimame na niishukuru sana Serikali ya Awamu ya Nne kwa vile kwa niaba ya Bunge hili nimeshiriki sana katika vikao kule, kwa kweli tumejenga Chuo na tunaendelea kujenga Chuo cha heshima, kikubwa na ujenzi wa Chuo kama ule sio jambo dogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke, unapojenga Chuo, unajenga madarasa, inabidi ujenge *seminar rooms*, inabidi ujenge *lecture theaters*, inabidi ujenge *cafeterias*, lazima uwe na *laboratories*, lazima uwe na majengo ya utawala, uwe na *auditoriums*, kuna *auditoriums* ambazo zinajengwa pale kumbi ya kuchukua wanafunzi elfu 1300 kumbi moja anafundisha Professor mmoja kwa wakati mmoja. Ni kumbi kubwa, lazima uwe na Misikiti na Makanisa katika eneo la Chuo Kikuu, lazima uwe na maeneo ya michezo, lazima uwe na hosteli za wanafunzi, lazima uwe na *sewage system* ambayo inaweza kubeba maelfu kama tunayoyategemea pale Chuo Kikuu cha Dodoma, lazima uwe na vituo vya tiba, lazima uwe na fenicha za kutosha, mambo ni mengi, lazima uwe na maeneo ya Benki na Posta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli shughuli iliyofanyika pale ni kubwa, ni shughuli ya kujivunia. Waliposimama baadhi ya rafiki zetu upande wa pili kujaribu kuponda jambo hili, niliwashangaa sana. Kwa kifupi sisi wananchi wa Mkoa

tunamshukuru sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wetu kwa *goodwill* ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Chuo cha Tiba ambacho kinajengwa hapo, *phase one* imekamilika, Muhimbili wanataka kufanya *extension* hapa Kibaha, karibu miaka kumi hawajaweza, sisi ndani ya muda wa mwaka mmoja tumeshajenga *phase one, phase two* mwakani inaendelea na tunategemea kujenga hospitali ya rufaa hapo kwa ajili ya kuwa *teaching hospital*. Ni mambo makubwa sana yanayoendelea hapo Chuo Kikuu cha Dodoma. Naiomba Serikali mambo mawili tu kuhusu Chuo Kikuu cha Dodoma:-

Moja, *title deed* bado, tumelisemea sana hili, tunaomba Serikali iliangalie. Lakini pili, inatakiwa *rent* kwa sababu eneo ni kubwa saba itabidi Chuo Kikuu cha Dodoma kiwe kinalipa shilingi milioni 700 kwa mwaka kwa ajili ya ardhi tu pekee yake wakati ardhi ile ni ya umma na kitu hicho kukipata katika bajeti ya Chuo sio jambo rahisi. Tunaomba Serikali i-*waive* hiyo *rent* na *title deed* ipatikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri moja kwa moja nikianza na ukurasa wa 12 (d), ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri anasema habari ya kuwaelimisha wafugaji umuhimu wa kuuza sehemu ya mifugo yao ili wajipatie mapato. Ninachozungumzia hapa umuhimu wa kuuza, hili neno kuuza mifugo, lina matatizo na tumelisemea sana Bungeni halikubaliki kwa wafugaji. Kwa nini wauze mifugo?

Mheshimiwa Naibu Spika, lugha inayotakiwa hapa ni kuvuna mifugo, ukimwambia mfugaji kuvuna mifugo anakuelewa, lakini hii habari ya kusema kila siku wafugaji wauze mifugo ina maswali mengi, tunaulizwa sana vijijini, mbona mambo yenu mengine nyie hamuuzi? Wenye nyumba tatu tatu mbona hamuuzi mmbakie na moja? Wenye magari manne manne mbona hamuuzi mmbakie na moja? Wenye wake watatu mbona hawabakii na mmoja na kadhalika, maswali ni mengi sana. Kwa hiyo, hii ya kuuza mifugo Wizara ebu badilikeni, twende kwenye kuvuna mifugo. Ukizungumza habari ya kuvuna mnaelewana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye ukurasa wa 19(j) wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri kutenga maeneo ya mifugo, kwamba zimetengwa katika nchi yetu hekta milioni 1,400 vijijini. Nataka kumwambia Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla kwamba jamani hili jambo la kutenga maeneo ya mifugo, kweli baadhi ya maeneo yametengwa katika baadhi ya vijiji, lakini yale maeneo hayajatengwa na kupewa hadhi ya matumizi ya ardhi kwa maana ya matumizi ya mifugo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jinsi hiyo, yanazidi kupungua mwaka hadi mwaka, tutabakia na hekta hizi vitabuni lakini ukienda vijijini kule ebu nionesheni maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya mifugo ambayo yanaheshimika kwa ajili ya matumizi ya mifugo, utayakuta ni machache sana. Kwa hiyo, tujitahidi tuwe na maeneo kama zilivyo Hifadhi za Taifa, kama zilivyo *game reserves* ambayo yametengwa na yamepimwa, *title deed* zimetoka ni kwa ajili ya ufugaji pekee yake. Huo ndio ukombozi, sasa tatizo maeneo yetu mengi tumeyaachia vijiji, kuyapata katika maeneo makubwa

namna hiyo tuwe na ufugaji kama wa Botswana ni jambo gumu lakini ndio *challenge* ambayo ningeomba Wizara iitazame kipekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kulizungumzia hapa ni kwamba tuna hifadhi za habari na maeneo tengefu, *marine parks* na *reserves* za *authority*. Hizi *marine parks* ziko chini ya Wizara ya Mifugo, naona jambo hili halijakaa vizuri. Katika kuendeleza uhifadhi katika nchi yetu, uwe ni *terrestrial* kwa maana ya bara au *marine* au maji baridi. Ningeshauri tuwe na taasisi ambazo zinachukua maeneo yote hayo kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano wenzetu Kenya, Kenya *Wildlife Service* inashughulikia *parks* zote bara na inashughulikia *marine reserves* na *marine parks* zilizoko Mombasa, Watamu na Malindi, zote ziko chini ya Kenya *Wildlife Service*. Sisi maeneo haya mawili yako tofauti kwa nini? *Marine parks, marine reserves* ziwe chini ya Tanzania *National Parks*, imekwisha mipango yake inakuwa ni mizuri, inakuwa ni *consented*, inakuwa ni ya pamoja, utalii wake unapangika vizuri kuliko hawa wako huku, hawa wako huku, haikai vizuri kidogo. Nashauri sana hili liende *National Parks*. Sasa naona kengele imelia niende kwa haraka sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, muhimu kuliko yote, ukurasa wa 36 fungu 58(4), kuendelea kutafuta wawekezaji ili waingie ubia na *NARCO* katika masuala ya mifugo. Kuhusu *ranch* ya Kongwa, tunazo taarifa kwamba *ranch* ile iko katika utaratibu huu. Nataka kuiambia Bodi ya *NARCO*, Wizara na Serikali kwa ujumla, ardhi ile ilichukuliwa miaka ya arobaini kutoka kwa wananchi wale kwa lazima, ikafanywa shamba la karanga, baadaye ikafanywa shamba la mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi *ranches* zina *capacity* ya ng’ombe 90,000 lakini wako ng’ombe 30,000, moja ya tatu, eneo kubwa halitumiki na Kongwa *Ranch* ni mojawapo kati ya maeneo ambayo yako katika utaratibu huu, tunaomba sana wananchi wa Kongwa ni wafugaji, wana uwezo wa kufuga kisasa, wana uwezo wa kuingia katika utaratibu huu, tutashangaa sana na hatukubaliana hata kidogo kama eneo la Kongwa litagawiwa kwa watu wengine, sisi tukasahauliwa. Jambo hili naliomba sana, naomba sana tusije tukasahauliwa, tutakosa maelezo ya kuwaambia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa. Nawaambia wananchi wa Kongwa kuwa mimi Mbunge wao nimekuwa nikiwatetea hapa na bado nina nguvu ya kutosha, ninayo nia na uwezo wa kutosha kabisa wa kuendelea kuwatumikia, hamnioni nikizungukazunguka na kuzurura huko kwa sababu niko hapa nikifanya kazi ambayo wao wenyewe wamenituma. Naomba kuwahakikishia kwamba niko imara, narudi tena kwenye ulingo, naamini kabisa watanipa ushirikiano wao ili sasa niweze kuutumia uzoefu nilioupata katika vipindi hivi viwili katika kusaidiana nao kuhakikisha kwamba Kongwa inaendelea kwa kila nyanja ya uchumi na maisha ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ahsante na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante na sisi tunakutakia heri. Nitamuita Mheshimiwa Michael Laizer, atafuatiwa na Yono Kevela ambaye pia atafuatiwa na Mheshimiwa Shoka Khamis Juma.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Kwanza napenda tu niikumbushe Serikali kilio cha wafugaji. Wafugaji katika nchi hii wamekuwa ni watu wa kulia, malalamiko kila siku lakini wamekuwa kama watoto yatima ambao hawasikilizwi. Lakini naomba Serikali mwaka huu katika bajeti hii hebu wakae na kuangalia matatizo haya ya wafugaji, hivi kwa nini wanalia? Kwa nini wanalalamika? Kama mkulima ana mtoto mfugaji, huku humsikilizi mtoto wangu mfugaji kwa nini analalamika kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba muwasikilize kwa sababu kilio chao kimekuwa kikubwa, wananyang'anywa ardhi, nashangaa Mheshimiwa Waziri kusema kwamba vijiji kadhaa maeneo ya malisho yamepimwa na hakuna eneo hata moja lenye hati. Huo ni uongo kabisa. Kama wamepimiwa maeneo yawe na hati, itambulike kama ni eneo la wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine ambayo ni kero kwa wafugaji, ni maeneo ya madawa ya mifugo. Kuna ugonjwa wa *east cost fever*, ndio ugonjwa unaomaliza mifugo, Serikali haiwezi ikasimama kwamba wamepeleka madawa kwa ajili ya ugonjwa huo kwa wafugaji. Kwa hiyo, umaskini unazidi kuwa mkubwa kutokana na madawa kukosekana. Kama unavyopeleka mbolea, unapeleka pembejeo kwa wakulima, upeleke kwa pembejeo madawa kwa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni soko, viwanda vinavyotamkwa kila siku. Mimi nina miaka kumi na tano hapa Bungeni, nilikuta hotuba iko vile vile miaka kumi na tano ni hotuba ile ile inasomwa kila siku, tuko kwenye maandalizi, tunawatafuta wawekezaji mpaka lini hawa wawekezaji watapatikana? Kwa ajili ya masoko. Unapeleka kiwanda kilomita 1000, hivi unaweza ukajenga soko la korosho Longido na shamba liko Mtwara? Au unaweza ukajenga soko la samaki Longido na samaki wanavuliwa Lake Victoria? Inawezekana? Mnatuambia viwanda vya nyama viko sehemu fulani, sehemu Fulani, tutapeleka lini kutoka huko kaskazini? Kiwanda cha Mzindakaya kilichoko Rukwa, yaani mifugo kutoka Longido iende Rukwa? Au mifugo kutoka Longido waende Pwani? Kwa nini wasijengewe kule Kaskazini, kwa nini Manyara na Arusha tusiwe na kiwanda kule?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni upimaji wa mifugo, *life weight*. Nyama inaenda kupimwa kwa kilo lakini huyu mfugaji ng'ombe wake hapimwi, anayepata hasara ni mfugaji, yule anayekwenda kupima kwa kilo hana hasara. Lakini pamba ikipungua bei inazungumzwa hapa Bungeni mpaka Serikali inafidia upungufu ule, mpaka wafanyabiashara wa pamba wanapewa fedha waende kununua pamba iliyoshindikana kununulika kwa wakulima lakini mfugaji anatazamwa tu. Serikali haimtambui mfugaji kana kwamba sio Mtanzania, tunahitaji mifugi ipimwe kwenye

minada, kilo iwepo. Nimekwenda pale Ruvu kuna kilo imekufa sijui miaka kumi iliyopita lakini ng'ombe wanauzwa kila siku, mizani.

**NAIBU SPIKA:** Nilikuwa nashangaa kilo ndio nini kumbe mizani.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, mizani, samahani. Nikizungumza matatizo ya wafugaji wakati mwingine napata *pressure* kidogo, mori inapanda kwa sababu ya matatizo. Kwa hiyo inapimwa kwa mizani. Kwenye minada yote iwekwe mizani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 28, Waziri alisema kwamba Waziri Mkuu alikutana na wadau ambao ni Wabunge, Wakuu wa Mikoa, Viongozi wa Chama, Wenyeviti wa Halmashauri na Watendaji wa Serikali. Hawa sio wafugaji wenye kero, tunataka Serikali ikae na hawa wafugaji wenye kero, hawa watumishi hawawezi kumwambia Waziri Mkuu kwamba tuna kero hii, hii na hii, ni bosi wao. Tunataka wakutane na wenye kero, walionyanganywa mifugo. Mnakwenda kutafuta majambazi wengine huku waliowapora wafugaji wanakaa, hakuna la kuwaambia. Nilitegemea kwamba Serikali ingetoa tamko kwamba mifugo ya wafugaji walionyanganywa, Serikali ingewarudishia. Kuna masikini ambao hawana mifugo tena lakini Serikali inakaa kimya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo ya wafugaji hakuna maji, yanatajwa malambo, lakini wafugaji wanahama kila siku kwa ajili ya matatizo ya maji. Naomba Serikali kama inataka kuimarisha ufugaji nchi hii ni lazima itambue matatizo, itambue kwamba hapa panahitajika maji, hapa panahitajika majosho. Majosho yaliyopo sasa nchini hayatumiki. Ni lazima kwanza majosho yaliyopo yaimarishwe sio kujenga mengine, imarisheni kwanza yaliyopo ndio tuendelee kujenga mengine. Hakuna sababu ya kujenga majosho mengine huku yalioko hayatumiki. Wayaimarishe kwa kupeleka madawa vijijini ili wananchi, wafugaji waweze kutumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nizungumzie tatizo la Jimbo langu kwamba mifugo imekufa kipindi kilichopita, wananchi wamekuwa maskini mno. Nilitegemea ndugu yangu Dr. Magufuli angesema jambo la kuwasaidia wafugaji wa Longido ambao wamekuwa maskini kwa ajili ya ukame uliopita, hakutaja kabisa na nilikuwa na imani na yeye tangu Rais alipomteua nilikuwa na imani kwa sababu yeye ni mfugaji, lakini bahati mbaya ni mfugaji mvuvi. Ame-*base* upande wa samaki akasahau kwamba kuna ng'ombe. Kila siku nikimsikia katika hotuba yake ni samaki, samaki, nyavu, nyavu, humsikii akizungumzia mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue nafasi ya kipekee kukushukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia hoja ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Lakini kabla sijaingia kwenye kuchangia ni vizuri nitoe shukurani za dhati, kwanza kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Njombe kwa kupewa Mkoa wa Njombe na hatimaye kile kilio changu cha kuomba Wilaya ya Wanging'ombe katika

Jimbo la Njombe Magharibi kusikilizwa halafu na kutekelezwa. Lakini nichukue nafasi ya kipekee vile vile kuishukuru Serikali kwa vile hili suala lilikuwa linanisumbua miaka mingi kuhusu upatikanaji wa Wilaya ya Wanging'ombe hususani kule Njombe Magaribi. Kwa kweli nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa Busara na uelewa mkubwa wa ombi langu la kuhusu suala la Wanging'ombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuhusu suala la jina kuitwa Njoluma, naungana na Mheshimiwa Rais kwamba Njoluma haikubaliki kwamba watu wanataka uitwe Mkoa wa Njombe. Kwa sababu ukisema kwamba Njoluma, mimi wa Wilaya ya Wanging'ombe utakuwa umenitenga. Kwa hiyo wananchi wanasema kwamba jina la Mkoa liitwe Njombe kama ulivyopendekeza na yeye kama wananchi wanavyopenda liwepo na jina la Njoluma sifa yake siyo nzuri kwani Chama cha Ushirika na nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge wa Makete na Wabunge wengine kwa kutoa kauli moja kwamba wanataka uitwe Mkoa wa Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije kwenye hoja yenyewe kuhusu suala la mifugo. Suala la mifugo ni suala la muhimu sana na nikupongeze Mheshimiwa Dr. Maguli na wenzake pamoja na Mheshimiwa Dr. Wanyancha toka waingie kuna uhai mkubwa sana kwenye sekta ya Mifugo na Uvuvi. Sizungumzii hili kwa sababu nampalilia yuko hapa. Kwa kweli yeye ni mchapa kazi sana na huyo mwenzake pamoja na watumishi wote kwa ujumla. Kuna mambo mengi huko nyuma hayakuwepo sasa hivi yamekuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hili tulikuwa tunaomba kwa niaba ya wananchi wa sasa hivi Wilaya ya Njombe wamenituma kuhusu chanjo. Chanjo ipo juu sana. Hivi karibuni mmetangaza kwamba chanjo ya mifugo iwe shilingi 9,000/=. Pale Wanging'ombe walikuwa wanalalamika sana, wanasema angalau hiyo chanjo ipunguzwe iwe inaendana na mazingira ya hali halisi, iwe bei ya chini ili wananchi wa kawaida waweze kuchanja ng'ombe kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nichukue nafasi ya kipekee kwamba katika Wilaya ya Njombe, Mkoa wa Njombe sasa hivi na kule Wilayani kwangu kule Wanging'ombe kuna uboreshaji sana wa majosho, kuna uboreshaji sana wa malambo na mabirika ya kunyweshea mifugo. Kuna vijiji ambavyo vilikuwa havina mabirika, vimepata mabirika na majosho. Kwa mfano, Kijiji cha Kanamalenga, Mpululu, Usuka, Mambegu, Kijombe, Saja na Wanging'ombe yenyewe. Kwa kweli watu wanakushukuru sana. Wanawashukuru Wizara, wanawapongezeni sana kwa sababu vitu hivyo huko nyuma vilikuwa havipo, lakini sasa vipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka nitoe ushauri kuhusu suala la mikopo. Tunaelewa wakulima wanapata mikopo, lakini hawa wafugaji naona mikopo kidogo inakuwa kwao ni tatizo kidogo. Kwa hiyo, ningeshauri Wizara yako ijaribu kushirikiana na mabenki, wale wafugaji wapewe mikopo, wawe na ushirika wapewe mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili sizungumzii kwa upande mmoja tu, nazungumza kwa Tanzania nzima, kwa mfano, wenzetu wa Manyara, wa Lilondo kule na wananchi wa Wilaya ya Wanging'ombe wangefurahi sana kupata mikopo ya mifugo. Labda lingine ambalo nataka nichangie ni kuhusu la hawa kuku wa kienyeji. Kwa haraka haraka kuku wa kienyeji inaonekana kama hawana umuhimu. Lakini nashukuru kwenye picha, kwenye hotuba yake Mheshimiwa Waziri kazungumza vizuri kuhusu suala la kuku wa kienyeji wanaofugwa kisasa. Sasa nilikuwa nafikiria kwamba hilo lingekuwa wazo la msingi sana kuliko kuwa limbukeni na kuku hawa wa kisasa ambayo yanatuletea madhara makubwa sana, lakini tukiimarisha ufugaji wa kuku wa kienyeji huyu mkulima wa kawaida, huyu mfugaji wa kawaida anaweza akafaidika sana na suala la hawa kuku wa kienyeji.

Mheshimiwa Naibu Spika, iwe ni pamoja na masoko. Tuhakikishe kwamba hawa wafugaji wa kuku wa kienyeji wanakuwa na soko la uhakika la kuku wa kienyeji. Sisi wengi wetu tumesomea hawa kuku wa kienyeji na ndiyo vipato vyetu kwenye maeneo yetu. Kwa hiyo, nashauri kwamba ni vizuri tuimarishe sana kuhusu kuku wa kienyeji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais alipokuja Ikulu Ndogo pale Njombe, sasa hivi Mkoa wa Njombe alilisita sana kuhusu ufugaji. Si bado naendelea?

**NAIBU SPIKA:** Dakika chache.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Sawa. Kwa hiyo alisisitiza sana kuhusu ufugaji wa kuku wa kienyeji. Kwa hiyo kuku wa kienyeji bado ni kitu ambacho ni cha muhimu sana. Itakuwa ni mkombozi sana wa maeneo yetu huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda lingine ambalo nataka kuchangia ni kuhusu suala la minada. Kule kwangu kwenye Wilaya ya Wanging'ombe tuna minada mingi sana. Kuna minada ya Saja, Lyamuluki kule na Wanging'ombe yenyewe. Sasa hii minada inatakiwa tuiimarishe vizuri yaani itangazwe kwa kiasi kikubwa. Kwa sababu isipotangazwa wanaokuja pale kununua wanakuwa wachache sana. Kwa hiyo, naomba hii minada iboreshwe kwa kutangazwa kwa bidii na Wizara kama Wizara ionyeshe msisitizo kwenye minada hii wala hata mwakilishi wako Wizarani pale aje kuangalia ni kitu gani ambacho tunaweza tukarekebisha. Pamoja na kwamba sasa hivi mambo yanakwenda vizuri kupitia Halmashauri lakini tulitegemea Watalaam mngekuja pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukipata wale ng'ombe wanaouzwa pale kwenye minada maana yake inakuwa rahisi hata kupata nyama nzuri hapa nchini kwa sababu ile nyama ingeweza kusafirishwa nje na halafu na huku ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nimpongeze kuhusu uanzishwaji wa viwanda, kwani viwanda bado ni tatizo nchini. Nazungumza hivyo kwa sababu niko Kamati ya Viwanda, Biashara na Masoko. Suala la viwanda vya ngozi na viwanda vya nyama yaani

kwa maana ya machinjio bado ni tatizo. Kwa hiyo nafikiria kwamba, tungeboresha ili angalau tuwe na viwanda endelevu, machinjio endelevu ili yaweze kusaidia sana watu wetu hasa walaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nataka nizungumzie kuhusu machinjio yaliyopo pale Ilembula. Yale machinjio ni ya kisasa na yamegharimu hela nyingi sana. Naomba niliandikia hata kwenye uchangiaji wa maandishi, katika yale machinjio kuwe na maji na umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya naona muda umekwisha. Nakushukuru sana kwa nafasi hii. (*Makofi)*

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa maoni yangu katika hotuba hii ya Waziri wa Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kunipa nguvu ya kuweza kusimama hapa na kuweza kutoa maoni yangu. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nakushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyofahamu hapa kila Mbunge huwa anatetea maeneo yake. Wako wanaozungumzia habari ya kilimo tu, wapo wengine wanazungumzia mifugo tu. Wanachukua dakika zao zote kuzungumzia mifugo. Sasa na sisi tupo tunaoshughulikia mambo ya uvuvi. Kwa hivyo, nashukuru kupata nafasi hii ili niweze kutoa maoni yangu kuhusiana na suala la uvuvi hususan wavuvi wetu walioko kwenye ukanda wa bahari kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lililopita la mwaka 2008, kwenye kikao kama hiki cha bajeti, ulitolewa Waraka na Mkurugenzi wa Uvuvi ambao ulipiga marufuku baadhi ya zana za wavuvi. Sasa baada ya kuzungumza sana humu Bungeni, Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii alikuja na Waraka wa Serikali akapoza baadhi ya mambo. Sasa katika kupoza kwake Mheshimiwa Waziri aliwaahidi au alituahidi wavuvi pamoja na sisi wadau wa uvuvi yaani tulio karibu na wavuvi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu kidogo nisome kwenye sehemu ya huo Waraka wa Mheshimiwa Waziri alivyowaahidi wavuvi na naomba anipe maoni yake. Mheshimiwa Waziri, nanukuu alisema hivi. “Mheshimiwa Spika, Serikali hivi sasa inaandaa mkutano maalum utakaowashirika Waheshimiwa Wabunge wote wa maeneo ya uvuvi, Wakuu wa Wilaya wote, Wakurugenzi, Watendaji wa Halmashauri zote. Lengo la Mkutano huo ni kuendelea kutoa elimu kuhusu zana haramu za uvuvi kwa kupitia viongozi hawa tutahakikisha, tuna hakika watafikisha elimu kwa wavuvi wa maeneo hayo. Tarehe na mahala utakapofanyika mkutano tutatangaza kwenye vyombo vya habari na kisha kuwatumia wahusika barua rasmi za mwaliko.

Aidha, nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge na wadau mbalimbali wa sekta ya uvuvi kwa ushauri wao ambao umetusaidia sana. Anaendelea anasema Wizara

itaendelea kutoa ufafanuzi kila itakapohitajika kufanya hivyo. Kauli hii ya Serikali itasambazwa kwa Wakuu wa Mikoa wote, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri na Waheshimiwa Wabunge ili isaidie kutoa ufafanuzi kwa maeneo yanayohusika." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli hii imetoka muda mrefu sana. Lakini mpaka leo mimi kama Mbunge ambaye natoka kwenye sehemu za wavuvi sijawahi kuitwa na wala hawa wadau wanaohusika hawa sijawahi kuona wameitwa kuja kupewa taarifa ili hawa wavuvi tuwape elimu, waweze kufahamu majukumu yao. Lakini Mheshimiwa Waziri anaendelea, anasema, Wizara itaendelea kutoa ufafanuzi kila itakapohitajika. Sasa Mheshimiwa Waziri huu ufafanuzi utawapa akina nani. Au utakuwa wa kuwapa viongozi. Kama alivyosema Mheshimiwa Lekule Laizer sasa hivi hapa, amezungumzia kwamba hii elimu wanayotakiwa kupewa ni wafugaji wenyewe. Sasa na hii wapewe wavuvi wenyewe. Sasa ukitoa elimu kwa viongozi itamalizikia huko huko tu haifiki kwa wavuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa ushauri wa bure kwa Mheshimiwa Waziri ili wasiendelee kuwaonea wavuvi, awaite wavuvi wenyewe wakae awaeleze uvuvi huu ni haramu, uvuvi huu hauruhusiwi, hivi awaeleze. Kwa nini sehemu nyingine zinafanyiwa semina, lakini wavuvi hawawekewi semina. Je, kwa nini wasiwekewe semina, wakati kuna watu wanatoka sehemu mbalimbali, wengine wanatoka mikoa ya Mwanza, Shinyanga wanakuja Dar es Salaam kufanyiwa semina? Lakini wavuvi wanaotoka kwenye bahari wanaotoka Tanga, wanatoka Kilwa, wanatoka Mafia na wapi inaonekana ni mbali, *hawaitwi* wakapewa semina. Lakini wakati wa kufuatilia mambo yao wanafuatiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi siyo kwamba sipendi mazingira. Napenda mazingira sawasawa na wenzangu. Lakini hawa, hawa na wao wanaofanya shughuli hizi ni binadamu. Lazima tuwafundishe na halafu tunapowazuia kufanya jambo hili tuwape mbadala wake. Sasa unachukua nyavu zao unazichoma, lakini ukishazichoma huwapi nyavu nyingine wala huwaambii kwamba nyie nyavu hizi hazifai lakini chukueni nyavu hizi. Miradi ipo mingi, kwa nini hatuwasaidii hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni kuna Waraka mwingine umetoka, kama alivyosema yeye kuwa umesaidia sana kurekebisha mazingira, nakubaliana naye. Lakini ameendelea kusema kwamba hili ni tangazo ambalo lilikuwa limetolewa tarehe 18 mwezi Machi,2010. Linasema hivi naomba uniruhusu tena nilinukuu: anasema "Ilani/Tangazo la usalimishaji wa zana haramu za uvuvi. Kwa mujibu wa ilani/ tangazo hili wavuvi wote wanaomiliki na kutumia zana haramu za uvuvi wanatakiwa kuzisalimisha kwenye Ofisi ya Uvuvi, Polisi, Serikali za Mitaa au kwenye Vijiji. Zana haramu za uvuvi zinazotakiwa kusalimishwa ni pamoja na: anasema pale (a) nyavu zenye macho madogo, chini ya nchi moja na nusu na makokoro ya aina zote. Baruti, milipuko, milipuko ya viwandani na ya kienyeji, mitungi ya gesi ya *Oxygen*, viatu vya kuogelea na miwani ya kuzamia, mikuki, sumu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana naye Mheshimiwa Waziri. Lakini hapa pana vitu vingine haviharibu mazingira. Kwa mfano, mitungi ya gesi. Sasa hii mitungi ya gesi inaharibu vipi mazingira. Jambo lingine viatu vya kuogelea pamoja na miwani ya kuzamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Waraka wake Mheshimiwa Waziri aliouleta aliviruhusu vitu hivi japo kavianzisha kwa *condition,* lakini kaviruhusu. Sasa unazuia, unawaambia watu walete mitungi ya gesi. Sasa mitungi ya gesi inaharibu vipi mazingira, au viatu vya kuogelea au miwani ya kuzamia. Miwani ya kuzamia kazi yake ni kukuruhusu wewe unapozama kwenye maji uone. Sasa unazungumzia mtu asione kwenye maji atafanya vipi kazi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii haina *logic*. Naomba Mheshimiwa Waziri arudi kwenye Waraka wake aliotupa hapa na naomba vile vile nimweleze Mheshimiwa Waziri amezungumza vizuri hasa kwenye suala hili. Amezungumza hapa Mheshimiwa Waziri anasema, matumizi ya gesi ya *Oxygen* miwani na viatu vya kuogelea. Yeye mwenyewe Waraka wake unasema: “Waraka wa Mkurugenzi ulipiga marufuku matumizi ya gesi, *Oxygen,* miwani na viatu. Hata hivyo, kwa mamlaka niliyopewa kupitia Kanuni ya 101 ya Kanuni za Uvuvi za mwaka 2005 nimeamua ifuatavyo: Wavuvi wenye leseni za kuvua samaki hai na wa mapambo nimewaruhusu kutumia vifaa hivi”.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri mwenyewe amewaruhusu hawa watu watumie vifaa hivi, wanaovua samaki hai. Lakini kule wanaambiwa wavipeleke kwenye Ofisi. Sasa sijui hata tumwelewe vipi Mheshimiwa Waziri kuwa yeye amekubali au amekataa au tuufuate huu Waraka au twende tukafuate kule. Hatujui tufuate wapi. Halafu unaendelea unasema: “Wavuvi wanapovitumia vifaa hivi kwa ajili ya ama usalama wao, kutoa nyavu zinapojizonga kwenye *propeller* za injini za maboti au nyavu zinaponasa kwenye magogo. Wanaruhusiwa pia kutumia mitungi ya gesi, *oxygen*, miwani na viatu vya kuogelea. Umewaruhusu Mheshimiwa mwenyewe humu. Sasa nashangaa kule wanaambiwa wapeleke kule. Sasa Serikali ni hii moja, Mheshimiwa Waziri ametupa hii taarifa, ametupa humu humu Bungeni halafu wanatokea wengine wanasema zana zile wazirejeshe kwenye Ofisi zipi au wazipeleke Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa katika ukursa wa 97, Mheshimiwa Waziri hapa anasema, amekamata vifaa vya kuzamia jozi 14. Mitumbwi 686…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mheshimiwa Mbunge)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa. Kengele yako ya pili.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Ahsante sana.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Niruhusu nianze kuwashukuru wapiga kura wangu wa Kiteto kwa imani kubwa

walionayo kwangu na kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kusukuma harakati za maendeleo katika nyanja za elimu, afya, maji, kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Mifugo daima imekuwa ni ndogo. Hii imekuwa ikijirudia mwaka hadi mwaka lakini kwa hicho kidogo kinachopatikana, naomba nimpongeze Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na Watalaam kwa jinsi walivyojaribu kupangia vizuri hicho kidogo kilichopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni faraja kuona kwamba Wizara imejipanga na kujikita vizuri katika suala zima la kutenga maeneo ili maeneo ya mifugo yabaki kuwa ni ya mifugo na yale ya kilimo yabaki kuwa ni ya kilimo, ili kupunguza mgongano na mgogoro unaokuwepo na ambao unazidi kukua kati ya wakulima na wafugaji. Lakini pia utaratibu huu unatoa fursa ya pekee ya kuweza kuendeleza mifugo kama zao la kutuendeleza kama nchi kiuchumi na kiutamaduni. Utaratibu huu ni mzuri na ni vema uzingatiwe na Mikoa karibu yote ambayo migogoro imekuwepo, Pwani, Morogoro, Manyara na baadhi ya maeneo ya Arusha, Rukwa, Tabora na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ninaomba na kusisitiza sana kwamba Wizara inapojipanga kufanya hivyo, pia wajaribu kutazama mambo mengine yanayohitajika ili maeneo haya yaliyotengwa yaweze kutumika vizuri maana kuna rasilimali za muhimu ili maeneo haya yaweze kutumika vizuri kwa mifugo. Ni wazi kwamba maji ni kitu cha lazima, malisho ni kitu cha lazima, maeneo yanayohitajika ya chumvichumvi pia ni ya lazima, kwa hiyo, ni vizuri Wizara kwa kuwatumia wataalamu wake, wanapotenga haya maeneo, wajaribu kuhakikisha kwamba kuna hizi rasilimali zinazokamilisha mahitaji yao na isiruhusiwe baadhi ya watumiaji wengine kunyofoanyofoa baadhi ya rasilimali zitakazofanya maeneo haya kutotumika vizuri yanapokuwa yameshachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wameongelea suala zima la kuhakikisha kwamba kunakuwa na hati zinazolinda maeneo haya ili yabaki kuwa ya mifugo. Jambo hili ni muhimu kwa sababu bado kumeendelea kuwepo na taratibu za kujaribu kupanua hifadhi, iwe ni ya misitu, hifadhi za wanyama, kumega kila mara maeneo ya mifugo. Mfano mmoja ni ule ambao kwa sasa ni tatizo kubwa kwa wapiga kura wangu, hasa katika maeneo ya kijiji kimoja kinachoitwa Irkiushiibor, lakini pia kwa upande wa Simanjiro, hawa wameathiriwa kijiji cha Kimotorok na mpango wa kupanua msitu wa Mkungunero, ambao uliendelezwa kama mpango ndani ya Wilaya ya Kondoa. Lakini baada ya taratibu hizi kuwa zimekamilika, wanaanza kutupa jicho kidogo na kuonea kijicho uzuri uliopo katika maeneo ya Irkiushiibor pamoja na Kimotoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada zimekuwepo za kujaribu kuchukua kwa kupora hekta zaidi ya 5000 kutoka Kiteto na pia zaidi ya 5000 kutoka Simanjiro ili kuongezea katika hifadhi hii ya pori la Mkungunero. Ninamuomba Mheshimiwa Waziri, ahakikishe kwamba utaratibu wa Mkungunero unaishia kwenye mipaka ya kiutawala kati ya Mikoa hiyo ya Dodoma na Manyara, usivuke mpaka kwa sababu haukuwa utaratibu. Baya zaidi katika kijiji cha Irkushiibor, wanataka kuchukua eneo ambalo ndio pekee lenye maji yanayotegemewa na wakazi wa eneo hilo, eneo wanaloita la Lombenek. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la magonjwa ya mifugo ni kubwa. Lakini inasikitisha kuona kwamba kwa magonjwa ya milipuko, 86.4% inategemea pesa za wahisani. Wahisani hawa wasipotoa fedha hizi, kitaifa tutafanya nini? Ninaomba Wizara ilitazame hili ili angalau magonjwa haya ambayo ni matatizo makubwa kwa wafugaji, yaweze kutengewa fedha kutoka katika bajeti yetu na kile kinachotoka kwa wahisani, kiweze kujazia nguvu zetu zaidi kuliko kutegemea hisani ya wahisani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapoongelea hili la magonjwa, niipongeze Wizara kwa kuendelea kutenga fedha za kutosha kwa chanjo ya ugonjwa wa Ndigana au *ICF*, kitu ambacho kwa kweli ndio tatizo linalouwa mifugo katika maeneo yetu. Lakini kutenga tu hizi fedha haitoshi, ni vema kuwa na utaratibu mzuri unaoeleweka chanjo inapofanyika kwa sababu, ni eneo ambalo bado lina *monopoly*. Ukienda katika Mkoa wa Manyara na Arusha, ni mtu mmoja tu ndiye anayeruhusiwa kusimamia chanjo katika eneo hili. Ninadhani ni eneo ambalo linahitaji milango kufunguliwa zaidi, watu wenye utaalamu waweze kupatikana na hii huduma muhimu ikaweza kupatikana kwa wafugaji wengi zaidi kuliko ikibaki mikononi mwa mtu mmoja ama wawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri tena kuongelea suala zima la ugani. Inatisha kuona kwamba kati ya wataalamu 16,500 wanaotakiwa, kuna upungufu wa wataalam 13,469, waliopo ni chini ya 3,000. Kwa kweli kama tutazingatia mifugo kama zao na tunahitaji kunufaika na zao hilo, ni kwa vipi tutanufaika endapo hakuna uwekezaji wa kutosha hasa katika suala zima la wataalamu? Ninaiomba Wizara ijaribu kutoa kipaumbele katika suala zima la wataalamu ili huduma hizo ziweze kupatikana, lakini pia uwekezaji uwe mkubwa kidogo katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoongelea mifugo kama zao, kuna sekta ndogo ndogo, sekta ndogo ya nyama, sekta ndogo ya ngozi, sekta ndogo ya maziwa, nadhani kama Wizara, ningeshauri wajaribu kufanya tafiti zinazoweza kubainisha jinsi ya kuongeza thamani kwa mazao haya. Tutaongezaje thamani ya mazao ya maziwa, ngozi na nyama, kwa sababu kwa njia hii wafugaji wanaweza wakashauriwa, wakaelekezwa vizuri zaidi jinsi ya kunufaika na mazao haya ya mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho nije kwenye tatizo ambalo limekuwa linajirudiarudia kati ya wafugaji, suala zima la ukame. Ukame umeathiri hasa Wilaya za Kaskazini, Wilaya ya Longido, Wilaya ya Ngorongoro, Monduli, Simanjiro na Kiteto pia. Kuna wafugaji waliopoteza zaidi ya 60% hadi 70% ya mifugo yao. MKUKUTA kwa watu kama hawa kama mpango wetu wa kitaifa, utakuwa na maana gani endapo hatutajipanga kama Serikali kuwa na utaratibu wa kuwarejesha watu hawa katika taaluma na katika uchumi wao huo waliouzoea? Ninaomba Wizara ichukue hatua za makusudi na ihakikishe kwamba kutakuwepo na utaratibu angalau wa kuwa na fedha kiasi kidogo kwa mfano, kama chakula cha njaa kinavyotolewa na mwishoni watu wakapewa mbegu ili waweze kujitegemea. Pia tutafute namna ya kutoa mbegu ya mifugo kwa wafugaji waliopoteza mifugo mingi ili mwishoni na wao waweze kuondokana na umasikini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapa na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. TEDDY L. KASELLA – BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Awali ya yote, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii. Kwa kweli, ninafurahi sana kutumia Bunge lako Tukufu, kuwapigia debe wapiga kura wao wawarudishe ili waweze kurudi katika Wizara hii na waendeleze malengo yao walipoyafikisha ili tuweze kuondokana na umasikini kwa kutumia mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niende kwenye hoja kamili. Tunapozungumzia Kilimo Kwanza maana yake tunazungumzia kilimo ambacho ni pamoja na mifugo. Tunapozungumzia kilimo na mifugo, maana yake ni hivi vyote vinatakiwa viende katika staili ya kisasa ambapo kwa mifugo ni lazima twende katika staili ya kupunguza mifugo ili tuweze kuilinda mifugo yetu michache lakini iliyo bora katika utaalamu na ituletee faida, tunapouza tuweze kupata faida zaidi na hivyo kuondokana na umaskini kwa kutumia mifugo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza kabisa ambalo mimi ninaliona litatusaidia kwa wafugaji wa Tanzania nzima na hasa wafugaji wa Jimbo langu la Bukene, ni ile Sheria Namba 5, tuliyoipitisha hapa Bungeni ya mwaka 1999, Sheria ya Ardhi Vijijini. Kama wafugaji na wakulima wakipewa ardhi yao na ikagawanywa kwamba hii ni ya wakulima na hii ni ya wafugaji, naamini kabisa migogoro katika nchi hii kati ya wafugaji na wakulima itakwisha. Kwa hiyo, ninachoiomba Serikali, ni kuongeza fedha zaidi kwenye Wizara ya Ardhi, ili itekeleze sheria hii, iwagawie wananchi, wakulima wapate ardhi yao na wafugaji wapate ardhi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sheria hii, mkulima au mfugaji mmoja mmoja anaweza kupata ardhi yake au wafugaji wengi kwa kikundi wanaweza kupata ardhi yao. Mimi ninaamini hawa wafugaji wakipata ardhi yao na wataalamu wetu wakienda kule wakawafundisha wafugaji wetu kugawa ardhi kwa manufaa ya ufugaji bora, maana yake wagawe ardhi yao kwamba hapa ni pa kufugia, hapa ni pa malisho na hapa wanalima, katika makundi tofauti,ninaamini kabisa hapatakuwa na malalamiko yoyote ya mfugaji kwenda kulisha ng’ombe wake kwenye shamba la mkulima. Kwa hiyo, ninasisitiza hili Serikali ihakikishe inatekeleza Sheria tuliyopitisha ili kila mtu apate hati yake na wale wataalamu sasa wafanye kazi ya kutekeleza utaalamu wao wa kuwafundisha wafugaji. Mimi ninaamini kabisa wafugaji hawana ubishi, wakifundishwa jinsi ya kulima malisho, jinsi ya kuangalia ng’ombe wao wachache, ninaamini kabisa watafuata na sisi wote hatuna sababu ya kuwa maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado nakwenda kwenye ng’ombe hao hao. Ukimuangalia ng’ombe au mbuzi, ana vitu vingi sana vya faida; ngozi yake ina thamani, ile ngozi kama wataalamu wakienda kumueleza, ile Sheria tuliyopitisha juzi, kwamba hatakiwi kuweka alama hovyo kwenye ngozi maana ngozi nayo ni pesa, aweke alama kwenye masikio au kwenye kwato zake, kwa kweli tutapata bei nzuri kwenye ngozi

ambayo tunaweza kuiuza ndani ya nchi na nje ya nchi, tukapata viatu vya kutosha. Kama wakati mmoja kaka yangu Mheshimiwa Waziri Magufuli, alivyosema, tukisema viatu vyote vya ngozi inayotengenezwa Tanzania vinunuliwe na shule zote, maana yake tumemnyanyua mfugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata zile kwato ni pesa, kwa maana kwato hizo zikiwekwa vizuri zinaweza kutengeneza mapambo ya akina mama, tukavaa mabangili, shanga na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, vyote katika staili ya ng'ombe au mnyama yoyote ni pesa. Ninaomba wataalamu wetu waende wakawafundishe na sheria hii itekelezwe na mimi ninaamini tutakuwa tumemaliza umaskini kwa mfugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kidogo tena katika mabwawa. Hapa tulipokuwa tunazungumza jana maji na umwagiliaji, tulizungumzia kwamba kuna mabwawa madogo madogo yatatengenezwa. Mimi ninaamini mabwawa haya madogo ya maji na umwagiliaji vile vile yawekwe kwa ajili ya mifugo, tupate majosho na malambo ya kutosha karibu na wafugaji na hapo tutakuwa tumetekeleza ile dhana ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie wataalamu wetu na mishahara yao jinsi ilivyo midogo. Kwa mfano, Chuo cha Mbegani, wataalamu wale wanafundisha wanafunzi kutoka nchi zote, hata kule *South Africa* wanakuja kusoma pale lakini wale wanachuo wakitoka pale wanakwenda kufanya kazi kwenye mashirika, wanapata mshahara mkubwa zaidi kuliko yule Mwalimu Mkufunzi. Kwa hiyo, ninaomba Serikali iwaangalie wataalamu wetu, wasifanye kazi wakiwa na kinyongo na wenyewe wapewe maslahi kulingana na kazi zao. Kama mwanafunzi akitoka pale anapata mshahara zaidi ya yule Mkufunzi, ninaomba Serikali iwafikirie hawa wataalamu wetu na wenyewe wapate mshahara wa kutosha ili wafikirie zaidi kufundisha na kuangalia kwamba meza yao ndio hiyo, wafanye kazi hapo na maisha yao yatoke pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale pale Mbegani, tulikuta boti moja ambayo ni mbovu. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali itengeneze ile boti ili waitumie kufundishia na vilevile iwazalishie ili watu wa Mbegani wajitegemee, wasiende kuombaomba kama wanavyofikiria. Wao peke yao waweze kuwa na taasisi, kama ile boti itakuwa nzima wakiongezewa na nyingine, zikafanya kazi ya kuzalisha samaki, wataendelea kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niingie kwenye uvuvi kabisa, mimi zamani nilikuwa nafikiri kwamba uvuvi, ni kwa watu wenye bahari na maziwa na mito lakini kwa sababu niko kwenye Kamati hii, nimeona uvuvi sio lazima uwe na ziwa au mto, uvuvi unaweza kuvua ukaweka samaki wako sehemu, kama kule kwetu tunaita majaluba tunayolimia mpunga, kwa hiyo, kwa urahisi zaidi kwa Jimbo langu na lugha ninayoilewa ni kwamba ni majaluba, basi wataalamu wetu waende kwenye sehemu zetu, wawafundishe wananchi wetu na mimi ninawakaribisha katika Jimbo la Bukene, jinsi ya kuweka samaki katika majaluba, ili wananchi wapate biashara. Samaki ni biashara na samaki ni lishe, ni protini, kwa hiyo, vijana na akina mama waweze kufanya biashara zao ndogo ndogo na hivyo wajikwamue katika umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Bukene kuna bwawa moja ambalo lilikuwa ni la historia na kila mara huwa ninalisema ni la mahali ambapo alikwenda kuwinda marehemu Dokta Mwaisela na ndio ile wodi ya pale Muhimbili Dar-es-Salaam imetokana na huyo Daktari, ni Madaktari wa kwanza Waafrika katika nchi hii. Hili bwawa liko Itobo, mimi naomba Wizara hii ilitumie bwawa hilo kutuwekea samaki, wataalamu waende pale, watuwekee samaki, tuweze kuvuna na vile vile kupata biashara kwa vijana na akina mama na hapo wote tuweze kuondokana na umasikini kutokana na kilimo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sisi tulikwenda Vietnam, kila kijiji kina bwawa la samaki wengi, wala hauvui, unaenda kuchukua tu. Ukitaka kupika, unaenda kuchukua unapika na wanaendelea. Nimeona kabisa Vietnam nchi nzima kuna mabwawa ya namna hiyo. *(Makofi)*

**MHE. DR. IBRAHIM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Waziri wa Mifugo, hoja ya mtoto wangu, naiunga mkono na pili nampa hongera Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nataka kuchangia hapa, alitokea mtani wangu mmoja akashangaa kwamba mimi nataka kuchangia hoja hii, akaniambia nyie watu wa Pwani mnafuga ninyi? Mimi nataka nimhakikishie kwamba watu wa Pwani tunafuga na hususani Kibaha tunafuga. Kibaha Vijijini tunafuga kuku na tunafuga ng'ombe wengi, Wasukuma hawa hawa wanaotoka huko, wanaokimbia kuuwawa wakiwa wazee wanakuja kule kwetu sisi tunawakaribisha. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie matatizo ya wafugaji hususan wa ng'ombe na kuku. Nikianza na ng'ombe, nazungumzia hapa wananchi wa kata za Magindu, Kwala, Ruvu, Mlandizi na Soga na hususani kwenye upande wa ng'ombe nazungumzia wafugaji wa Gwata, Vinyeze, Kigoda, Muyombo, Mziguni B, Kwala, Ruvu, Nandizi na Soga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji hawa wana matatizo makubwa yafuatayo, kwanza, upande wa mabwawa, kwa upande mmoja, napenda nitoe shukrani nyingi sana kwa Serikali kwamba ilijitahidi ikajenga mabwawa mengi na hususan katika Kata ya Magindu ambapo kuna ukame uliokisiri, wakati wa kiangazi walijenga mabwawa mengi. Lakini neema nayo huleta matatizo, tulipata neema ya mvua lakini neema hii ikaleta matatizo, mabwawa mengi haya yamepasuka yanahitaji ukarabati mkubwa na Halmashauri imeomba wapatiwe walau kama shilingi milioni 150 ili yaweze kukarabatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana wakati nachangia hoja ya Waziri wa Maji, niliishukuru Serikali kwa mradi wa maji wa Wami Chalinze ambao utakuja mpaka kwenye Kata ya Magindu. Mradi huu utakapokuwa umeanza, utaondoa tatizo moja la maji ya matumizi ya binadamu, lakini bado tutakuwa na shida ya maji kwa ajili ya mifugo. Kwa hiyo, ndiyo maana nasema suala la ukarabati wa mabwawa, ni suala muhimu kwa wananchi wa maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kama walivyozungumza Waheshimiwa Wabunge wengine, ni suala majosho, majosho kwa kweli hayatoshi, kwa sababu ukitazama katika Kata zote hizi, Magindu ina josho moja tu sehemu ya Masaki, Kwala nzima ina josho moja tu la Madutumi na Ruvu ndiyo linajengwa hivi sasa. Najua jitihada kubwa zinafanywa, lakini nadhani kama walivyozungumza Waheshimiwa Wabunge waliopita, ni vizuri tukafanya kazi kwa ari zaidi, kasi zaidi na nguvu zaidi ili tuweze kuhakikisha kwamba tunapata majosho ya kutosha katika maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nikimaliza na suala la ng'ombe niingie sasa kwenye wafugaji wa kuku. Kibaha tunafuga kuku sana, wafugaji wa kuku vijijini ni moja ya shughuli ambazo zinawasaidia wananchi wetu katika kupambana na umaskini, lakini ufugaji huu una changamoto nyingi. Kwanza, kuna kuku ambao wanafugwa ambao ni wa kienyeji na kuna kuku ambao tunawaita wa kisasa. Kwa upande wa kuku wa kisasa wanaototoa mayai, kunakuwa na ukosefu mkubwa wa vifaranga na pale vinapopatikana mara nyingi vinaandamana na ulanguzi, yaani unaweza kwenda kwenye makampuni haya ambayo yanazalisha vifaranga na wao mara nyingi wanakuambia uende ukanunue kwa ma-*agent* na ma-*agent* nao wanauzia watu wengine na kadhalika na kadhalika, hatimaye unakuta kwamba kifaranga ambacho ungenunua kwa shilingi 1500 unakuja kukinunua kwa zaidi ya shilingi 2000.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili suala la bora wa vifaranga vyenyewe nyakati nyingine wafugaji hawa wanakumbana na matatizo ya vifaranga wanavyonunua kutokuwa bora. Si ubora tu wa vifaranga, dawa za kuku zimekuwa bei kubwa na chakula cha kuku kimekuwa bei kubwa. Kwa hiyo, ninaomba Serikali itizame kwa karibu masuala ambayo yataweza kusaidia pengine kwa kutoa ruzuku kwenye sekta hii ili watengenezaji wa chakula waweze kutengeneza chakula katika bei ambayo wanunuaji au watumiaji wa chakula hiki ambao ni wafugaji wanaweza kumudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchangia, napenda na mimi nitumie nafasi hii, kuwashukuru sana wananchi wa Kigoda katika Kata ya Magindu, nilipowaona hivi karibuni si tu kwamba walinitaka nisimame kugombea tena Ubunge lakini wao walikwenda mbele zaidi wakanichangia shilingi 200,000 nikalipie fomu, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliona niseme haya machache ili kumkumbusha Mheshimiwa Waziri na timu yake ambayo tunajua wanafanya kazi nzuri waweze kuyatizama kwa karibu na kutukumbuka na sisi kwenye maeneo haya kwamba na sisi tunafuga pia si Wasukuma na Wanyamwezi peke yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia katika hoja ya Wizara...

**NAIBU SPIKA:** *Microphone* yako ina tatizo.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** *Hallow*, imekaa vizuri, nasikia kama mwangwi umepungua kidogo.

**NAIBU SPIKA**: Inayo kelele hiyo.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasikia kama mwangwi umeisha, nashukuru sana kwa kunipa nafasi katika muda huu na mimi nichangie katika hoja ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naipongeza sana Wizara hii, kwa jinsi ambavyo imejikita katika kuibadilisha Wizara na kuhakikisha kwamba sekta hizi mbili zinafanya kazi vizuri, sekta ya uvuvi na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado nasikia mwangwi.

**NAIBU SPIKA:** Haisikiki vizuri kwa kweli sijui uondoke mstari huo kabisa, wakati wa mapumziko Mafundi waangalie tatizo la *line* hiyo.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nianze upya kwa sababu kweli nimekuwa *disturbed* sijaweza kujiweka vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya kwanza nataka nimpongeze Waziri, nimpongeze Naibu Waziri, niipongeze Wizara kwa ujumla, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kwa kipindi ambacho wamekuwa katika Wizara hii. Sekta hizi mbili zimekwenda vizuri, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninakusudia niunge mkono hoja. Nitaanza kwa kuongelea eneo la uvuvi. Eneo la uvuvi ni moja ya sekta muhimu katika kuchangia uchumi wetu wa Taifa. Kwa kweli eneo hili limekuwa linafanya vizuri. Lakini ninahisi pengine kasi ya uendelezaji sekta hii haiendani na ule ubora na labda kama ingeboreshwa zaidi ingeweza kuchangia vizuri kwenye pato letu la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa nafuatilia hotuba labda sikufika mpaka mwisho baada ya kufika maeneo ambayo nilikuwa nayahitaji zaidi, lakini nimeona juhudi kubwa sana imefanyika kwa upande wa bahari. Nilipokuwa nasoma hapa kwenye kitabu chao, ukurasa wa 21, nimeona kwenye sekta ya uvuvi kuanzia ukurasa wa 20 kuna kuwaelimisha na kuhamasisha wavuvi wadogo kuimarisha na kuanzisha *SACCOS* ili ziwasaidie kupata mikopo, hii iko kwenye ukanda wa bahari. Ukija kwenye kipengele kinachofuata, kutengeneza mazingira mazuri yatakayosaidia upatikanaji wa zana za

kisasa na uvuvi bila ya vikwazo ziko pia ukanda wa bahari. Haya ni mambo mazuri pengine waliamua kuanza nayo nafikiri ndiyo mpango wao, naupongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninachotaka niombe sasa kwa hizi hatua nzuri ambazo wamezichukua, hatua ya kwanza hii ambayo ni ya kitaifa ambayo Serikali imepunguza kodi ya malighafi za uvuvi mpaka kufikia asilimia tano, hili nina hakika limewasaidia wavuvi wengi au niseme limewasaidia wavuvi wote. Lakini sasa tunapokuja katika hili la pili ambalo ni kuwasaidia, Wizara imehamasisha uanzishaji wa miradi midogo midogo ya uvuvi 212 katika maeneo ya ukanda wa Pwani, hii ililenga zaidi katika ukanda wa Pwani, *okay* mimi nakubaliana nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiendelea kusoma tunaona mambo mazuri ambayo hawa wenzetu wamefaidika nayo, wameweza kufikia hatua ya kuwa wachangiaji wazuri kwanza katika kuitika katika mchango mzima wa kupunguza uharibifu wa mazingira. Wao wenyewe wameweza kusaidiwa, wamepewa mashine za kupachika kumi na tatu, kwa mujibu wa kitabu hiki, wamepewa masanduku ya barafu manne, wamepewa maboti 11 na nyavu za jarifa 1,214. Kwa hiyo, naona hawa wanapoambiwa wabadilike watabadilika kwa sababu wanaondolewa sasa katika ule uharibifu na ufugaji duni kuingizwa katika kuunga mkono harakati za kutunza mazingira na zana nzuri za kisasa. Sasa hili ninalisema hivi kwa maana kwamba ninaomba sana Wizara ibebe hatua hizi, ikazifanye katika wavuvi wa Ziwa Victoria na maziwa mengine, kwa sababu kama itakuwa juhudi ni kuwanyang’anya zana zile za kizamani zinazoharibu mazingira, lakini hakuna juhudi nyingine inayofanyika, lazima tu mnapoondoka hii biashara ya kuharibu mazingira itaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naisema hivyo kwa kweli nikiwa ninaendelea na ukurasa 23, hapa wanaeleza kwamba wameshawishi sekta binafsi kuanzisha zana za uvuvi, nimeipenda hii na kuifuatilia na kuitamka hapa kwani ni moja ya matatizo wanayopambana nayo, wavuvi wetu wanaendelea kununua zana duni kwa maana kwamba viwanda vinaendelea kuachiwa kutengeneza zana duni. Sasa ili zana duni zisiendelee, hapa kiwanda cha Fanaka kilicho ukanda wa Ziwa Victoria ambacho tayari kimeonyesha kinatengeneza zana nzuri ndipo wavuvi waelekezwe kwenda kununua zana zao na wale ambao wanatengeneza zana mbovu waache ili na wao sasa wawe na zana zile zinazofaa kusudi tuweze kumaliza kabisa tatizo la uvuvi haramu. Kama si hivyo, itakuwa inaonekana kama sasa labda kuna watu wanaokusudiwa kuonewa, kwa sababu mvuvi anayekwenda kuvua mara nyingi wanaendelea kuvua sasa hivi kwa zana hizi za makokolo ni wale wenye kipato kidogo, wavuvi wenye uwezo mkubwa wanavua katikati ya Ziwa, kwenye maji marefu  na ambako kuna samaki wazuri na wakubwa. Kwa hiyo, naiomba Serikali iliangalie suala hili ili tuwe *positive* kwa wavuvi ili tuweze kufanikiwa katika zoezi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wengine ambao anasaidiana nao *BMUs, BMUs* katika Ziwa Victoria wanafanya kazi nzuri lakini na wenyewe wanafanya kazi nzuri zaidi kwa vifua kuliko kutumia ile namna ya mawasiliano mazuri. Sasa mapambano yanapokuwepo kati ya watu ambao wana shida na wewe mwenyewe unataka kuwazuia lazima mapambano yatakuwa makubwa. Mimi naomba likifanikiwa hili ambalo

nimeanza nalo, kwa kweli naamini tunaweza tukaenda vizuri na baada ya muda ikaja ikatolewa taarifa nzuri hapa Bungeni kwamba tumeweza kufanikiwa kukomesha uvuvi usiofaa katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze wavuvi, wafugaji wa samaki wa Muleba katika kitabu hiki hawajaandikwa, lakini wako wavuvi wameshachimba mabwawa na wanafuga na wana samaki. Ukienda pale katika Kata yangu ya Ruhanga, wana mabwawa ya samaki, ukienda Kata nyingine iko Muleba Kusini wana samaki. Sasa kama tayari tuna mabwawa zaidi ya kumi ama ishirini katika Wilaya ya Muleba na hii ilikuwa tumeanza kupiga debe tangu mwaka 2001 sasa hivi walau tumeanza hatua ya kufanikiwa na tunayo maeneo mazuri ambayo mimi nina uhakika kwamba wananchi wanaweza wakahamasishwa wakachimba mabwawa na wakafuga samaki. Naomba na Muleba iwemo kwenye orodha na katika hatua zinazofuata hamasa iende ikafanyike zaidi Muleba ili wananchi waweze kuchimba mabwawa na kufuga samaki katika mabwawa kwa sababu watatusaidia kipato, watatusaidia lishe na watatusaidia kwa namna mbalimbali kujikomboa katika hali ya umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninaloomba kuhusu hii sekta ya uvuvi ni utafiti. Sisi tulizoea kula samaki wakati wowote kwa sababu sisi tuko karibu na Ziwa Victoria, sasa hivi hatuna samaki. Nimekwenda tangu tumefunga hili Bunge mpaka nimerudi mimi sijala samaki, tunakula dagaa. Sisi kwetu dagaa ni samaki lakini si yule samaki tunayemheshimu. Hii inatokana na nini? Sasa hivi uvuvi, wanavua mwaka mzima, hakuna wakati mzuri wa kuvua, matokeo yake wanabaki wanavua pasipostahili. Mfano, wavuvi wakubwa wameanzisha tabia ya kwenda kuvua kando kando ya Ziwa, huu ni uharibifu wa mazalia ya samaki. Siamini kama hawa wenzetu wameruhusiwa kuvua maeneo haya, naomba wavuvi wakubwa wabaki kwenye maji marefu, wavue kule lakini kuwe na muda maalum kwamba lini wavue ili uvuvi ufanyike na wananchi wapate kitowewo cha samaki. Sasa hivi kwa kweli samaki hazipatikani kabisa hii ni hatari sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho nalotaka kumaliza nalo ni kuipongeza Serikali kuhusu suala zima la sekta ya ufugaji, kwa kweli nawapongeza sana na katika hili nataka niseme moja tu kwa sababu ya muda wangu uliobaki napenda niwasilishe shukrani za wananchi wa Rutoro, Ngenge na Kishuro ambao wanaishi katika *ranch*, lakini kwa juhudi kubwa za Waziri wa Wizara hii Mheshimiwa Dk. Magufuli, wameendelea kukaa pale kwa barua yake aliyopeleka hata alipotutembelea Rais naye akaja akahimiza na Mkuu wa Mkoa, Ndugu Babu akasimamia vizuri, Mwenyezi Mungu amwezeshe kwa kweli amesaidia sana na sasa kuna amani. Ninachopenda kuomba muendelee kutuvumilia mpaka hili tatizo liweze kumalizika. Tuna haja ya kuona kwamba Watanzania wanaishi kwa amani na tuna haja kuona kwamba kila aliye Mtanzania anafaidika na Taifa hili. Maendeleo ya nchi yetu yasifukuze wengine yakawatoa nje na wengine wachache wakafaidika tu kwa sababu tunapenda pesa, pesa hazijawahi kuwa ni juu ya Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kusema ahsante na naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo hii sehemu ya mwisho ni ya *ranch* kwa maana ya mifugo, sio uvuvi..

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Uvuvi nimemalizia na hii ya mifugo sijui nimesema kwa dakika mbili tu...

**NAIBU SPIKA**: Ulisema uvuvi.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimemaliza, nimesema uvuvi sana halafu nikamalizia mifugo kwa dakika chache na kwa shukrani hizi kwamba zimfikie Waziri kwa eneo linalohusika.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo ni *ranch* ya mifugo.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Naam. Ahsante sana na Mungu awabariki.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye hotuba hii ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Kwanza, napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo, Naibu Waziri wake, pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara hii, kwa utendaji wao mzuri na kusema kweli katika utendaji wao mzuri mimi binafsi sina shaka nao, ni watu ambao wanaijua kazi yao, nawapongezeni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mdau wa pande zote mbili, mimi ni mfugaji lakini vilevile hata na kwenye upande wa uvuvi mimi ni mdau kwa sababu nimelazimika kujifunza mambo mengi haya si kwa sababu tu ya kupata kipato lakini mimi kama mwakilishi wa wale wananchi, wananchi wengi wangependa kupata *consultation* ya mwakilishi wao na hauwezi kuwashauri kwa vitu usivyovifahamu kwa hiyo wakati mwingine nimelazimika kujifunza baadhi ya vitu hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini itoshe tu kusema kwamba kwenye upande wa mifugo kama tunavyofahamu, yako matatizo mengi ambayo yanatusumbua, yapo matatizo ya wananchi wetu kuhamahama, hili ni tatizo kubwa, lakini tuna matatizo ya masoko ya mifugo yenyewe pamoja na masoko ya maziwa. Hali kadhalika yako matatizo ya kuwa na mifugo ambayo isiyokuwa bora, unakuta badala ya wafugaji wetu kuwa wafugaji wa kisasa wanaendelea kuwa wachungaji na katika hali hiyo unakuta mifugo haina hali nzuri na hata wale wafugaji wenyewe au wachungaji nao hawana afya nzuri, kwa kweli si jambo zuri sana. Kwa uzoefu wangu, mimi katika nafasi hii ya ufugaji sioni kama kuna ugumu wa kuweza kuboresha mambo haya, ni jambo ambalo linawezekana pamoja na mambo mengi mazuri ambayo Serikali imefanya lakini iendelea kuongeza mengi mazuri katika kuhakikisha kwamba tunaboresha suala ufugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninachoweza kusema kwenye upande wa kutokuwa na mifugo bora, kwanza inatokana na aina ya mifugo tuliyonayo. Mifugo yetu mingi ni ya aina ya Zebu ambapo Zebu kuja kumfuga mpaka aweze kukupatia fedha za

kutosha au aweze kuwa na uzito wa kutosha lazima umfuge ndani ya miaka isiyopungua nane mpaka kumi. Kwa hiyo, ombi langu katika hilo, kwa kuwa tunazo *ranch* zetu na za kutosha, basi ni vizuri Serikali ijikite zaidi kutoa ruzuku ya mbegu kwa maana ya madume wa kutosha lakini pamoja na mitamba wa kisasa kwa ajili ya maziwa lakini na madume bora hasa hawa Bolani kwa ajili ya nyama, kwa kufanya hivyo, sasa mfugaji ataweza kufuga ndani ya miaka mitatu akauza ng'ombe wake kwa bei nzuri. Kwa hiyo, ninadhani Serikali badala ya kupeleka fedha kwenye uvuvi na ufugaji basi ipeleke fedha hizi kwa wafugaji, maana ya kusema fedha hizi ziende kwa wafugaji ni kwamba ili sasa zinunue madume na mitamba ya kutosha kwa ajili ya kubadili ufugaji uweze kuwa ufugaji wa kisasa. Kwa hiyo, nadhani hiyo ni njia mojawapo inayoweza kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tuna matatizo mengi ya kuhamahama na mifugo yetu. Ukiangalia wafugaji wetu wanahamahama kwa sababu ya kutafuta malisho na sana sana maji. Mimi nasema katika nchi yetu au katika ardhi yetu, maji yapo katika maeneo yote, hebu basi kwa kuwa gharama za kutengeneza mabwawa pale ambapo zinaonekana kuwa kubwa, tuchimbe visima virefu kwa kutumia *solar* na pampu. Kisima kimoja, naamini kwa mifugo yetu kitaweza kunywesha kijiji kizima na itasababisha badala ya watu wengi kuhama au kwenda mwendo mrefu kutafuta maji, basi hilo tatizo linaweza likaisha na mifugo mingi sasa haitakonda kwa sababu ya kuhangaika kutafuta maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tuna tatizo kubwa kama tulivyosema la bei za mifugo, mimi nashangaa, leo Serikali imepiga marufuku ununuzi wa mazao kwa utaratibu wa Lumbesa kwamba mpaka mazao yapimwe, lakini vilevile inapanga bei ya mazao. Mimi nashindwa kuelewa ni kwa nini yule mfugaji sasa anaruhusiwa auze ng'ombe kwa gharama yoyote ile pasipokuwa na kipimo chochote kile? Kwa hiyo, kama tunadhani tunataka kuwasaidia, nyama buchani inauzwa kwa kilo, hebu ile mizani ambayo Serikali ilishainunua isimamie ng'ombe wote wanaouzwa minadani wauzwe kwa mizani lakini vilevile iweke bei ya nyama kwa maana ya ng'ombe anapokuwa na *live weight*, wataalamu wanajua kwamba ng'ombe anatoa kati ya 52% mpaka 60% ya *caucus weight*. Kutokana na hali hiyo, ukipiga hesabu, unaweza kujua kwamba kumbe sasa gharama ya kuuza ng'ombe mnadani kwa kilo ni shilingi kadhaa. Kwa hiyo, tunadhani kwamba kwa kufanya hivyo, itakuwa imesaidia wafugaji wetu ili na wao vilevile waweze kuuza ng'ombe kwa bei nzuri inayoweza kuwapatia tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tunafahamu pamoja na kuwa na *ranch* za kutosha, bado ile *holding capacity* labda *ranch* inaweza kuchukua ng'ombe 100,000 na ng'ombe waliopo pale ni 20,000. Kitu cha kufanya hapa ni kidogo tu kwamba, kwanza, Serikali izisaidie zile *ranch* zetu ziweze kujitosheleza kwa maana ya kuzipatia fedha. Lakini pili turuhusu sasa hizi *ranch* ziweze kuwa *share* na wananchi hawa wafugaji wa kawaida kwa utaratibu rahisi kwamba wale wafugaji wenye ng'ombe wachukue baadhi ya mifugo yao wapeleke kwenye zile *ranch* na hiyo ndiyo iwe sehemu ya *share* yao. Tunadhani kwa kufanya hivyo zile *ranch* tunaweza kuzi-*utilise* kwa maana ya kwamba badala ya kutafuta wawekezaji wengine kutoka nje kumbe tunaweza kupata wawekezaji kutoka miongoni mwetu sisi ambao ni wafugaji. Kwa hiyo, tunadhani kwa namna hiyo tutakuwa tumewasaidia wafugaji wetu nao kuwa na hisa lakini vilevile waweze kufuga kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nigusie kidogo kwenye suala la uvuvi kwani yapo matatizo makubwa. Kule kwenye maeneo yetu, watu wanaoshikwa kila siku, wanashikwa wale ambao tayari wameshanunua samaki ambao ni wadogo, lakini wale wavuvi hasa wanaovua kule, ni wachache wanaoshikwa. Ushauri wangu hapo, mbali na kushika Makokoro, wakati mwingine Serikali inatumia fedha nyingi, tuna vikundi vyetu vya *BMUs*, kazi tunayopaswa kufanya pale ni kuwashirikisha wananchi na Serikali itenge fedha kwamba mwananchi anapotoa taarifa kuna Kokoro sehemu fulani hata kama Waziri angetangaza bingo ya shilingi 100,000/= kila mahali Kokoro zilipo wananchi watatoa taarifa na Makokoro yote yataweza kukamatwa. Kwa hiyo, nadhani kwamba kwa kufanya hivyo tatizo la Makokoro ambayo yanatumalizia samaki pamoja na hawa wavuvi haramu ni rahisi sana wakakamatwa. Lakini kibaya ambacho Serikali inakifanya, unamkuta Mama ameshanunua samaki kutoka Ziwani, huyu mama ndiye anayekamatwa, lakini wale wanaovua kule hawawezi kukamatwa. Kwa hiyo, nadhani kwa kufanya hivyo, Serikali inaweza ikatatua tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante na sasa nitamuita Mheshimiwa Benson M. Mpesya kwa mchana huu ndiye atatuhitimishia.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba nikushukuru wewe, kwa kunipa nafasi hii mchana wa leo na mimi niweze kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa leo kwa sababu kwanza nataka nikumbushie ahadi ya Serikali aliyoitoa Rais wakati anaomba kura za wana-Mbeya juu ya kufufua viwanda Mbeya. Miongoni mwa viwanda ambavyo vilipaswa kufufuliwa, ni Kiwanda cha Nyama cha Mbeya kama tulivyozoea kusema *Tanganyika Packers* na ninaamini kabisa kwamba moja kati ya jukumu la Wizara hii ni pamoja na kutekeleza Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirejea kwenye nguzo ya saba ya Kilimo Kwanza inasema uendelezaji wa viwanda katika kuleta Mapinduzi ya Kilimo, hiyo ndiyo nguzo ya saba. Ninaamini kabisa kama Kiwanda cha Nyama cha Mbeya kitaanza kufanya kazi, Serikali itakuwa imetimiza azma ile ya nguzo ya saba katika Kilimo Kwanza. Lakini kiwanda hiki cha Mbeya kiliwekwa chini ya *PSRC* ili kiweze kutafutiwa wawekezaji na sasa kipo chini ya *Consolidated Holdings*. Nguzo ya sita ya Kilimo Kwanza inasema lazima kuwe na vivutio vya kuchochea uwekezaji katika kilimo. Hatujaona juhudi za *Consolidated Holdings* za kuvutia wawekezaji katika Kiwanda hiki cha Nyama cha Mbeya. Nguzo ya nne inasema kuwe na mabadiliko ya mfumo mkakati katika kilimo, *Consolidated Holdings* hawana jipya la kuweza kukinadi kiwanda hiki kwenda kwa wawekezaji. Kwa hiyo, unaona kabisa kwa kuzingatia nguzo kumi zilizopo katika Kilimo Kwanza, *Consolidated Holdings* hawana sifa za kuendelea kusema sisi ndiyo wenye Kiwanda cha Nyama cha Mbeya, wameshindwa kabisa. Lakini tutatimizaje hii azma

ikiwepo azma ya Rais aliyoahidi kufufua viwanda vya Mbeya, kiwanda cha *Tanganyika Packers* na kiwanda cha nyama cha Mbeya kikiwa miongoni mwa viwanda hivi?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine maamuzi yetu kama Serikali yanatilia shaka, wakati tunajua kabisa kwamba Kiwanda cha Nyama cha Mbeya kuna mitambo na kila kitu na ni mali ya Serikali na ni mali ya wakulima, Serikali inaamua kujenga kiwanda kipya cha nyama Ruvu, hii ni *contradiction* katika maamuzi ya Serikali. Ni sawasawa na mjenzi ambaye hujamaliza nyumba linabaki pagale badala ya kumalizia hilo pagale ameamua kujenga pagale la pili na pagale la tatu itakuwa ni nyumba ya mapagale. Busara zangu zinanituma kwamba Serikali ilipaswa kwanza kukimalizia Kiwanda cha Nyama cha Mbeya ndiyo ianze kufikiria namna ya kujenga viwanda vingine. Lakini hatukufanya hivyo na tunakwenda kinyume kabisa na zile nguzo kumi za Kilimo Kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya mimi naweza kusema hawa wenzetu wa *Consolidated Holdings* wamerithi zile tabia za *PSRC* za kuwa kila jambo linapofanyika lazima wapate 10%. Ninazo taarifa kwamba Wizara imeandika barua kutaka kiwanda kile kirejeshwe Serikalini, sisi tuna imani na utendaji kazi wa Mheshimiwa Dr. John P. Magufuli, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha na tuna imani na utendaji kazi wa Katibu Mkuu, Ndugu Nyamrunda pamoja na Wakurugenzi wote na Idara hii nzima. Wanafanya kazi utafikiri Wizara hii ina miaka kumi au ishirini iliyopita lakini kumbe bado ni wachanga, tuna imani nao sana. Kupitia Bunge lako Tukufu, ninaomba Kiwanda hiki cha Nyama Mbeya kirudishwe mikononi mwa Serikali, apewe Mheshimiwa Dr. John Magufuli na mimi nina imani, sina wasiwasi atarudi na Mheshimiwa Dr. James Wayancha naye watarudi katika Bunge hili. Ni rahisi kumuomba Rais kwamba atuendelezee tena sekta hii aifikishe mahali ambapo tutaona inavyochangia katika pato la Taifa. Lakini kulegalega na maamuzi haya yanachochea rushwa, bila 10% hatukitoi kiwanda hiki, jamani mnatuumiza sisi ambao ni wawakilishi wa watu, mnawaumiza wananchi na hasa sisi tunaotoka kwenye Majimbo ya Mijini kwani mjini hakuna kilimo utapambana na Sheria za Halmashauri ya Jiji, hawa wanategemea ajira na ajira itapatikana kwa kufufua viwanda, nani tena zaidi ya Kikwete? Hakuna. Kikwete atapeta, Magufuli utapeta lakini turudishieni Kiwanda cha Nyama cha Mbeya, vijana wangu mjini waache kupiga nondo wapate ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, linaloendana na hilo ambalo kwa kweli linatutia simanzi, wakati tunachukua eneo hili la *Tanganyika Packers*, mimi nafikiri Mbunge mwenzangu wa Mbeya Vijijini, Mchungaji Luckson Mwanjale linamsumbua sana mpaka leo hii. Wakati tunachukua eneo kwa ajili ya *Tanganyika Packers*, tuliwakuta wananchi wenye mapenzi na nchi hii, waliamua kwa moyo wao kuliacha lile eneo ili kiwanda kijengwe, lakini kiwanda hatujajenga. Maeneo yale hatujawarudishia badala yake viongozi wachache waliopewa kulimiliki eneo lile wanatafuta watu kutoka sehemu nyingine ndiyo wanawakodishia yale mashamba walime na wananchi wanaambiwa watazame tu mikono iko nyuma, ilikuwa ni ardhi ya Babu zao na urithi wao halali, hawayatumii maeneo yale, sasa wajanja ndiyo wanayakodisha kulima. Vitendo hivi vinaleta simanzi sana kwa wananchi, kiwanda hakifanyi kazi, yalikuwa ni maeneo yetu,

mnakodisha watu wengine kutoka nje ya vijiji vile ndiyo wanalima na wao wanabaki ni watu wa kutazama tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nguzo ya tano ya Kilimo Kwanza inasema, upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya Kilimo. Hawa wananchi wa *Tanganyika Packers* kwa nini wasipate ardhi yao? Mheshimiwa Waziri ninakuomba warudishiwe ardhi yao wakati tunaendelea kutafuta wawekezaji badala ya kuwatoa watu kutoka nje kuja kuyalima maeneo yale, wale watu ni wasikivu. Wakati tunamnadi Mchungaji Mwanjale walituambia kabisa mturuhusu tulime mtakapokuwa tayari katika viwanda basi tutawapatia kiwanda chenu. Ninaomba hili Serikali ya Chama cha Mapinduzi ambayo najua ni Serikali sikivu, najua Mheshimiwa Dr. John Pombe Magufuli ni msikivu, Katibu wako Mkuu Nyamrunda ni mfuatiliaji, ninaomba eneo la *Tanganyika Packers* wananchi na wanavijiji wanaozunguka eneo lile wapewe kulima siyo hawa wengine ambao wanakodishiwa kutoka huko mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, zimebaki dakika tano ambazo hazitoshi kwa msemaji mwingine, sasa wafuataо watazungumza baada ya kurejea saa kumi na moja. Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Madgalena H. Sakaya, Mheshimiwa John M. Cheyo na Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko. Hawa wanatosha halafu tutampa nafasi Naibu Waziri na Waziri na tutakuwa na muda wa kutosha kuingia kwenye vifungu.

Baada ya kusema hayo sina tangazo lolote, nasitisha kikao hiki mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunasitisha shughuli za Bunge kipindi cha asubuhi, niliwataja wafuatao kwamba wangekuwa wachangiaji, lakini nilimsahau Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa. Sasa ninamwita, halafu watafuatia Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa John Cheyo na baadaye Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko.

**MHE. DR. CHARLES MLINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba radhi nilichelewa kidogo, nilikuwa najiandaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kwanza kwa niaba ya wananchi wa Shinyanga Mjini, kwa kuunga mkono hoja hii. Baada ya kuunga mkono hoja hii, nianze

kwa kutoa pongezi sana kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yote ya Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya ambayo inajidhihirisha kwenye kitabu cha hotuba aliyoisoma Mheshimiwa Waziri, hususan nitaje kwa mfano tu Sheria mbili tulizopitisha mwezi wa nne, ile ya utambuzi, usajili na ufuatiliaji na ile ya nyanda za malisho na vyakula vya mifugo, ambazo mimi ninaamini zitasaidia katika kuboresha ufugaji nchini. Kazi hii wameifanya wenzetu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pongezi zitokane na tangazo la chanjo ya kichaa cha mbwa kutolewa bure nchini kwa waathirika. Kichaa cha mbwa ni moja kati ya magonjwa ya mifugo ambayo yanaathiri binadamu, na watu wengi huwa hawawezi kumudu zile gharama kwa sababu ni kubwa sana. Kwa hiyo, ninawapongeza sana kwa hilo pamoja na mambo mengine mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie dakika hizi ulizonipa ili niweze kuzungumzia Sekta ndogo zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia niongelee sekta ya maziwa. Kwenye hotuba ya bajeti ya Serikali tuliyosomewa hapa Bungeni, ilikuwa na mambo mengi sana yanayoondoa gharama za vifaa, mashine pamoja na vifungashio vya maziwa. Hii ni katika azma Serikali kuona kuwa sekta ndogo ya maziwa inachukua nafasi yake katika maana ya usindikaji wa maziwa, kwani sehemu kubwa ya lita bilioni 1.6 za maziwa yanayozalishwa nchini hayasindikwi na kwa hiyo, yananywewa hivi hivi tu na ndiyo maana wakati mwingine watu wengine wanaugua magonjwa yanayosababishwa na vijidudu vinavyopatikana kwenye maziwa ambayo hayakuchemshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza sana Serikali, ninafahamu Mheshimiwa Waziri alikuwa mstari wa mbele sana katika kupigania kuona kunakuwa na unafuu katika uwekezaji kwenye sekta hii ndogo ya maziwa ili kusudi maziwa mengi yaweze kusindikwa. Hivyo, ninampongeza sana na ni matarajio yangu kuwa, basi wale wawekezaji katika sekta hiyo waweze kuifanya kazi hii kwa ufanisi zaidi na kwa faida kubwa zaidi kwa jamii na pia katika maana ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye jimbo langu la Shinyanga Mjini kuna kiwanda ambacho kitakuwa cha kwanza cha maziwa katika Mkoa wa Shinyanga. Kiwanda hiki kinamilikiwa na Kanisa Katoliki, na hivi karibuni wamepata pesa kwa ajili ya kununulia mashine za kusindika maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Shinyanga una ng'ombe wengi, lakini kwa muda mrefu hadi sasa hauna kiwanda hata kimoja cha maziwa, na kwenye takwimu za Mheshimiwa Waziri hapa imeonesha kuwa maziwa mengi yanatoka kwenye ng'ombe wa kienyeji, na sehemu inayobaki ni ng'ombe hawa wa kisasa wa maziwa. Kwa hiyo, maziwa yanayotokana na ng'ombe wa kienyeji ambao kwa sehemu kubwa ni aina ya Zebu kutoka Mkoa wa Shinyanga, yamekuwa hayasindikwi na kwa hiyo, linakosekana soko la uhakika la wafugaji kiasi kwamba wanakuwa wanauza kienyeji na kwa hiyo, hata bei zao zinakuwa hazifahamiki vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda hiki cha maziwa kinachotarajiwa kukamilishwa hivi karibuni hapo Shinyanga, kitatoa soko zuri sana kwa ajili ya wafugaji wa ng'ombe wa maziwa wa Shinyanga Mjini, Mkoa wa Shinyanga pamoja na Mikoa jirani kwa sababu lile eneo ambalo maziwa yatakusanywa litajumuisha zaidi ya Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwetu sisi watu wa Shinyanga tumeona ni fursa nzuri sana kwamba, wakati tunaelekea kukamilisha kiwanda cha maziwa tayari Serikali imeingilia kati kuhakikisha kuwa, inaisaidia sekta hii ya maziwa kwa kutoa unafuu katika gharama za uwekezaji ili kusudi uwekezaji huu uwe kwa faida ya wananchi wetu katika maana ya wafugaji, unywaji wa maziwa na katika maana ya uchumi. Mimi ninaamini mwisho wa siku usindikaji wa maziwa katika kiwanda cha maziwa kinachotarajiwa Shinyanga, utawasaidia wafugaji kuweza kujenga uchumi wao na kuondokana na umasikini ambao wengi wao licha ya kuwa na ng'ombe, bado wanaishi katika mazingira ambayo ni duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wananchi wataneemeka na uwekezaji huu na hivyo, ninaishukuru sana Serikali katika kuhakikisha kuwa inaondoa kodi za vifaa vya kubebea maziwa, matenki ya kuhifadhia maziwa, malori ya kubebea maziwa na mengine mengi yatakayowezesha sekta hii ndogo ya maziwa iweze kushamiri, si tu kwa jimbo la Shinyanga Mjini, na Mkoa wa Shinyanga lakini kwa Tanzania nzima, kwani maziwa mengi ya Tanzania kama nilivyosema na kama takwimu zinavyojionesha hayasindikwi kiasi kwamba kwa wale tunaotaka kunywa maziwa yaliyosindikwa, tunalazimika kukimbilia yale ya madukani ambayo mengi yanatoka nchi za nje wakati sisi ni matajiri wa ng'ombe hapa nchini. Hali hii haikubaliki na ninaipongeza Serikali katika hatua hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie sekta ndogo ya nyama. Licha ya kuwa tuna mifugo mingi hapa nchini, lakini nyama tunazokula ni zile ambazo kwa kawaida zinasanangwa kwenye jiwe, au gogo.

**MBUNGE FULANI:** Kusanangwa!

**MHE. DR. CHARLES MLINGWA:** Ndiyo, kusananga ni Kiswahili. Ninyi mnafahamu muuzaji anaweka nyama kwenye gogo na kuanza kukatakata kiasi kuwa nyama ile inakuwa na vifupa vingi tu, hali inayopelekea watu wengine kuugua *appendix* kwa sababu ya kula vipande vipande vingi tu vya vifupa. Ni lazima tuondokane na hali kama hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nimekuwa nikijiuliza, hivi tufanye nini ili tuweze kuwa na mabadiliko katika sekta ndogo ya nyama? Kwa Kiingereza ninaweza nikasema kinachopungua hapa ambacho hatuna ni *complete beef value chain* ambapo unakuwa na mfugaji kama hatua ya kwanza, lakini unakuwa na soko la uhakika na soko hili ni viwanda na machinjio kubwa za kisasa ambazo ndizo zitakazonunua mifugo ya mfugaji. Lakini, pia na utoaji wa bei (*pricing formular)* inakuwa ni sahihi kiasi kuwa yule mfugaji ataona tija kuuza kwenye kiwanda au machinjio ya kisasa, hali ambayo kwa sasa hivi haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, asilimia 25 ya nyama inayoliwa Dar es Salaam ni ya ng'ombe wanaotoka Shinyanga, lakini hawa ng'ombe wanabebwa kwenye malori katika mazingira ya ajabu ajabu tu, sasa pale Shinyanga kuna kiwanda cha nyama kilichokuwa cha *Tanganyika Packers* ambacho mwaka 2007 kilinunuliwa na Kampuni inayoitwa *Triple S. Beef Ltd*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikifuatilia kwa karibu sana, na kampuni hii ilikuja wakati mimi nikiwa Naibu Waziri, tumeshirikiana nao kwa hali ya juu sana, mimi kama Mbunge kuona kuwa hatimaye kiwanda hiki kinafanya kazi. Nimekuja kugundua kuwa kazi ya kufufua kiwanda cha nyama ni kubwa sana, lakini inawezekana na ndiyo maana mtu akisema Serikali ichukue viwanda hivi, jamani tusiharakishe sana, na ni vizuri kuelewa ukubwa wa kazi.

Mimi nimebahatika kushirikishwa kwenye mambo mengi kiasi cha kunifanya nielewe mambo mengi sana hata aina za mashine za kisasa zinazohitajika, maana zile mashine za wakati ule zilikuwa ni za kizamani na teknolojia hiyo sasa haiwezi tena kuendelea kutumika na kwa hiyo, kazi ni kubwa.

Hata hivyo, matumaini ni kuwa ninaamini kwa kazi kubwa ambayo wenzetu wa *Triple 'S'* wameifanya, ndani ya miezi sita ijayo kama dunia inabaki kama ilivyo, kiwanda hiki kitafanya kazi. Ingawa kwa hatua fulani watu wachache sana walijaribu kubeza kazi kubwa ambayo ilikuwa inafanyika pale. Mimi niliwapa moyo *Triple 'S'* nikasema huku kubeza mwone kama ni kuruka kihunzi tu kati ya vihunzi vingi mtakavyoviruka na ndiyo maana sasa hivi wako kwenye hatua nzuri sana ya kuzungumza na mabenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *Triple 'S'* wanazungumza na benki iliyowapa fedha wenzetu wa kiwanda cha maziwa cha Shinyanga ili kuona kama itawapa pesa na hatua iliyofikiwa mpaka sasa hivi ni ya kuridhisha na kwa hiyo, kwa wananchi wangu wa Shinyanga Mjini, huyu atakuwa ni mkombozi kwa wafugaji kwa sababu soko litakuwa mlangoni. Lakini, kwa sababu pia ng'ombe wako wengi katika Kanda ya Ziwa, *Triple 'S'* atakuwa ni mkombozi kwa wananchi wa kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira zitapatikana hapo na kwa kuwa Shinyanga Mjini kuna vijana wengi, wataajiriwa pale kwa sababu mimi ninafahamu muundo wa kampuni ile utakavyokuwa kibiashara na kwamba, kuna fursa nyingi za ajira zitazaliwa pale ambazo zitatoa ajira kwa watu wengi sana. Kwa hiyo, mimi nimekuwa nikijihusisha kwa karibu sana na kazi hii kubwa na ambayo pengine sio rahisi sana kwa mtu kuiingia hivi hivi kwa sababu ni ngumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuzungumza yale ambayo ninayo. Kwanza, kabisa napenda tu na mimi kuchukua nafasi hii kuendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea

kuniimarisha kama nilivyosema hapo awali, na kwamba Mungu ni mwema, Mungu ni mwingi wa fadhila, ananitia nguvu, ninaendelea kuimarika na sasa ninaendelea kuongea na Bunge hili. Mungu, ninasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baada ya kuzungumza hayo, sasa katika hali ya kidunia napenda niseme kama ifuatavyo:- Kanda ya Ziwa kwa kiasi kikubwa sana tunapaswa kumshukuru Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete kwa kutupa Mikoa miwili ambayo kwa kweli ni historia. Mikoa hiyo ni Simiyu na Geita, na hapa Mheshimiwa Cheyo naye naona anashangilia tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwangu Geita ni faraja. Geita kuna wapigakura wangu, lakini kunitoka mimi ni faraja kwa sababu Rais mwenyewe ameona ni kuongeza maendeleo katika Kanda ya Ziwa. Kwa hiyo, niwatakie heri wana Mkoa wa Geita kwa yote yale ambayo yatakuwa yamepangwa katika Mkoa wao na Mungu awe nao, asiwatangulie, maana akiwatangulia anaweza akawaacha, awe nao katika maendeleo ya Mkoa wa Geita, lakini waendelee kunikumbuka mimi nilikuwa mwenzao. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwa Magu, kama Magu ndiyo itabakia Mwanza, basi tuendelee kuwa na amani. Lakini kama itakuwaje, hayo siyajui, lakini eeh, Mungu ninaendelea kuomba Magu yote isije ikaenda. Magu ninaipenda iendelee kuwa na mimi ili niendelee kuishi nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho katika hili ni Ilemela. Tuseme nini wana Ilemela? Kwa sababu sisi tumepewa Manispaa? Ni kama Baba na Mama, basi kijana amepewa jiko kwa maana ya kujitegemea. Sasa wana Ilemela, hebu Ilemela amkeni mjue mtapata wapi mapato, mtapata wapi kuishi, mtapata wapi nini, ili Manispaa yetu iendelee kuwa Manispaa kweli na mbele ya safari itakuwa Jiji siku moja. Lakini tunaamini Ilemela ina uongozi shupavu, yuko Diallo, yuko mama Hewa, uko na uongozi mwingine, tutavuka. Ahsante sana kwa wale waliofikiria kutupa Ilemela Manispaa. Sisi Ilemela tunajiamini, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakwenda katika hali halisi ya kuzungumzia suala zima la kile ambacho kimeninyanyua hapa kuhusu suala la mifugo. Wizara hii ina viongozi shupavu, kwa kweli ni shupavu. Ninaomba tuwapongeze tu, kwa kweli ni shupavu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazungumza hivyo kwa sababu mimi ninaishi Mkoa wa Mwanza na Naibu Waziri anatoka Mkoa wa Mara. Waziri anapita Mwanza ndiyo anakwenda huko kwake Chato. Lakini ni miaka mingi imepita, hizi *ranches* kama Mabuki na kwingine, sasa hivi panawaka umeme. Yaani kwa lugha nyingine Magufuli ameamua kufanya kazi ndani ya maeneo haya. Naomba tumpongeze kijana huyu. *(Makofi)*

Kwa kweli Waziri anafanya kazi ya ziada. Yaani sasa hivi unaona Mabuki panawaka umeme! Ingawa sijaingia mle, mimi ni Afisa Mifugo *by profession,* kwa kweli ni kitu ambacho unafurahi, unasema sasa Wizara hii iko kazini na ni kweli wanastahili

pongezi. Mheshimiwa Magufuli, pamoja na Mheshimiwa Wanyancha ambaye sijui walimchagua kwa sababu anatoka kwenye wafugaji, kwa kweli wanafanya kazi nzuri, unaziona. Ukipita pale Ruvu panapendeza, ukipita maeneo ya *Ranches* mbalimbali unafurahia na unajua kwamba watu hawa wapo kazini, na Rais hakukosea, kwa kweli tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kudodosa mambo mawili au matatu hasa kuhusu nyavu hizi zinazochomwa. Niwaombe na niwasihi, wanapochoma hizi nyavu watu wanaona kwa macho jinsi nyavu zinavyochomwa. Wanamwaga mafuta, wanawasha sijui linini hilo, watu wanaona kwa macho, mbona hawaoni kwa macho hawa mliowataja kwenye taarifa hizi kwamba tuliowakamata ni hawa, wanaouza nyavu haramu ni hawa, wenye viwanda vya kutengeneza nyavu haramu ni hawa na wenyewe tuwaone basi kwa macho ili tulinganishe uchomwaji wa nyavu hizi kwamba zinatoka kwa hawa? Kwamba umembana fulani, anaendelea kuuza nyavu haramu na unambana fulani kiwanda kinauza nyavu haramu, tuone vyote viwili kwa macho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkituonesha watu hao, watu watatulia, watajua kabisa kwamba, kumbe kweli Magufuli na Naibu wake wako kazini. Kwamba tunaoneshwa pande zote! Sasa tunaoneshwa kuchomwa tu, aah, hawa wenye maduka wenyewe na wenye viwanda wako wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie juu ya elimu. Katika hali halisi ya vikundi hivi vya wafugaji na wavuvi ambao katika vikundi hivi huwa kuna viongozi wao. Sasa katika semina, makangomano, warsha na kadhalika hebu hawa ndio wahusishwe ili mbele ya safari waende wakaelimishe hawa wafugaji kuhusu nyavu haramu na ufugaji usio halali. Lakini katika kitabu chako Mheshimiwa Waziri nimeona tu kwamba elimu inatolewa kwa wasomi tu kwenye vituo vya Ukirigulu, Nyegezi na kadhalika. Je, hivi hao ni wachache mno katika kuja kutoa elimu za wafugaji wa kawaida? Hawa wafugaji wa asili naomba mvitumie hivyo vikundi viwe vingi.

Nimeona umesema wanawake kadhaa na wanaume fulani lakini hao hawatoshi. Hebu chukua vikundi vya viongozi ndani ya makundi haya ya wavuvi na makundi haya ndani ya wafugaji hao ndio wapewe semina au makongamano, yaani kila sehemu wanapokutana nyinyi mnapofikiria mafungu haya ya sasa ni ya kutoa elimu wapewe elimu hawa watu badala ya kuwaelimisha wasomi elimisheni, hawa wataelimishana wenyewe. Ikibidi wanaweza hata wakaelimishana kwa kilugha. Inawezekana Wamasai hawa marafiki zangu wasijue hata Kiswahili kwa hiyo hata wakielimishana kwa Kimasai inaweza ikazaa matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Nyama Shinyanga. Mmezungumza humu kwenye kitabu cha bajeti kwamba elimu itolewe, ufugaji bora, mazao yao yaende wapi, watazalisha ngozi kwa wingi, watazalisha maziwa kwa wingi, watazalisha jibini kwa wingi na kadhalika leo tumeambiwa kila kitu, sasa hivi vyote vinakwenda wapi? Viwanda vya Ngozi viko wapi? Kiwanda cha Mwanza kimekufa Magufuli na nina swali tarehe 28, kweli kabisa hizi ngozi zako baadaye iweje mwanangu? Ngozi zako nzuri

zitakwenda wapi? Naomba swali hili leo unijibu zitakwenda wapi ili kusudi upige kelele wafufue na malambo yachimbwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuweza kunipa nafasi niweze kuchangia kidogo hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Awali ya yote, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu wake pamoja na wataalam wote wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba na kutuletea hapa.

Pia kwa namna ya pekee niipongeze sana hotuba ya Mheshimiwa Mwadini Jecha - Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani ilikuwa nzuri na imeainisha nini ambacho hakijafanyika kwenye Wizara hii ambapo kikitumika vizuri wanaweza wakaboresha sana huduma hii ya mifugo na uvuvi kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tukubaliane kwa pamoja kwamba sekta ya kilimo na sekta ya mifugo ndiyo pekee ambazo zinaweza kuwainua Watanzania kwenye umaskini. Kwa sababu ndio sekta ambazo zinalisha nchi nzima na ndiyo sekta ambazo zinaajiri zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania. Kwa hiyo, kwa kuboresha sekta hizi mbili tutaweza kusaidia Watanzania kwa kiasi kikubwa sana na kuweza kupunguza umaskini kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya mifugo. Nilikuwa naangalia jedwali Na. 5 hapa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri nimeona maeneo yaliyotengwa kwa nchi nzima ni hekta 1,400,000 na *point* kidogo. Naona kwanza hizi hekta ni kidogo sana kwa idadi ya mifugo tuliyonayo Watanzania. Nadhani hizi takwimu ziko kwenye vitabu. Ukienda vijijini kule hazijatengwa, pengine ni maagizo yametolewa lakini hazijatengwa. Kwa mfano, tukiangalia Tabora kuna Wilaya nyingi ambazo zina mifugo, lakini ni Wilaya moja tu ya Urambo ambayo wamesema ni vijiji 14, haya maeneo hayajatengwa. Kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali ihakikishe inatuma wataalam, maeneo haya ni muhimu tukayatenga kwa sababu hata hivi ninavyoongelea leo nimepigiwa simu baada ya wananchi kusikia kwamba maeneo yametengwa wanasema: “Haya maeneo yametengwa wapi? Mbona hatujayaona?” Kwa hiyo, bado ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atume wataalam wake maeneo ambayo amesema yametengwa waende wayahakiki na yatambulike kisheria kwa sababu hatuwezi kuondoa migogoro ya mifugo na kilimo kama hatutaweza kuyatambua maeneo haya ya kilimo kisheria. Tusipoyatambua kisheria wakifugia hapa wanaambiwa hapa ni hifadhi, wakifugia hapa wanaambiwa hapa ni kilimo, kwa hiyo, inakuwa ni matatizo. Lakini hapo hapo tunasahau kwamba mifugo tuliyonayo inaweza sana kutusaidia kama tutaweza kuipangia taratibu nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la maeneo ambayo yanatengwa. Tunaomba sana maeneo yaliyotengwa yawe ni maeneo ambayo yatatosha kuweza kupanda vyakula vya mifugo vya akiba. Kwa sababu tumegundua kwamba kwa mfano ukame uliotupata hapa nyuma tumejifunza kwamba wafugaji wengi walikuwa

hawajaweka akiba ya chakula chochote. Kwa hiyo, wafugaji wanategemea majani mabichi yakiwa mashambani, lakini ikitokea ukame wa muda mfupi, majani yakikauka, mifugo imekauka, haina akiba ya chakula chochote.

Kwa hiyo, tunaomba sana yatengwe maeneo ya kutosha, zipandwe *hay* za kutosha, *hay* zitengenezwe za kutosha, wananchi waelimishwe, wataalam waende vijijini wakaelimishe jinsi gani ya kutengeneza *silage* zikatengeneze *hay* na kila mfugaji awe na banda la kutunza chakula cha mifugo. Kwa namna hiyo, tunaweza kusaidia angalau ikitokea ukame kwa muda wa mwezi mzima hivi, tukiwa na akiba wakati huo tunaangalia jinsi gani ya kuweza kupata chakula kingine. Lakini utaratibu wa sasa hivi hausaidii ndiyo maana nasema kwamba maeneo yaliyotengwa hayakidhi haja. Kwa hiyo, ninaomba sana tuwe na mipango endelevu tukijua kwamba mifugo inaongezeka, watu wanaongezeka na mahitaji yanaongezeka. Tusitenge maeneo leo halafu kesho na kesho kutwa maeneo yamekwisha tukasahau kwamba wanaozaliwa watahitaji kufuga na kulima pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni la viwanda vya kusindika vyakula vya mifugo, nyama, maziwa na vitu vingine. Kama alivyosema Mheshimiwa Mama Hewa aliyetoka kuzungumza sasa hivi, viwanda vingi sana hapa nchini vya kusindika mazao ya mifugo ni kwamba vimekufa. Vingi havipo kwa sababu viwanda vya ngozi *almost* vyote vimekwisha, viwanda vya maziwa vipo lakini ni vichache, havikidhi mahitaji ndiyo maana maziwa yanatoka Arusha yanakwenda Nairobi yanakuwa *packed* yanarudi Tanzania tunanunua. Hilo ni tatizo. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali ifufue sasa viwanda vyote kwa sababu kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri tumeona jinsi gani ambapo ushuru umepunguzwa kwenye vifaa vya kusindika maziwa na nyama. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba sasa hivi wananchi watapata moyo na wale wanaotaka kuwekeza kwenye sekta ya kusindika maziwa watapata moyo, lakini sasa watakwenda kuuza wapi au masoko yatapatikana wapi? Tunaomba sana kwamba viwanda hivi vifufuliwe na vihakikishe kwamba vimefanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki kituo kinanishangaza sana. Nchi za wenzetu zinalinda viwanda vyao vya ndani, lakini kwa nchi yetu Serikali imesababisha viwanda vyote vimekufa, kwa mfano Kiwanda cha Ngozi cha Moshi kimekufa, Shinyanga kimekufa na mpaka Kibaha walikuwa wanalalamika juzi kinaelekea kufa, kwa sababu hata bidhaa zinazotengenezwa pale hata zikiwa za viwango hakuna mahali pa kwenda kuuza. Leo tunaagiza kila kitu kutoka nje tukiangalia viatu vyote vya wanafunzi na vya watu wazima vyote kutoka nje, mabegi ya akina mama yanatoka nje, pochi nje, mabegi ya nguo yote yanatoka nje, mikanda ya akina baba inatoka nje, hii mali yetu nani aitumie?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetembea nchi nyingi, nchi zote duniani kwanza wanaangalia soko la ndani, wanaangalia kwanza viwanda vyao vya ndani hawawezi kuruhusu vitu kuingia ndani ya nchi yao bila kuhakikisha kwamba mazao yao yamepata soko. Sasa sisi tumekuwa ni soko huria, kila kitu soko huria matokeo yake sisi tumeshindwa kujiendeleza. Tukiangalia hata hotuba ya Waziri wa Fedha, ukiangalia mauzo ya samaki yaliyouzwa nje ni kidogo kwa sababu vingi vinakuja vinaingia ndani.

Nashukuru sana tangu mwaka jana baada ya wenye viwanda kuleta maziwa hapa na Serikali angalau kupunguza ushuru wa vifungashio maziwa ya Watanzania yameanza kuonekana madukani kwa kiasi kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda dukani, hata Dodoma miaka ya nyuma nilikuwa natafuta maziwa ya Tanzania siyapati. Leo, hata jana nimeyatafuta nikayapata. *Tanga Fresh* ukienda ukiulizia unapata, *Musoma Diary* unapata yameanza kuwepo, tatizo *Super Milk* zinazotoka Zimbabwe na Kenya bado zipo. Kwa hiyo, sasa hivi kitakacholeta tatizo ni soko. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali iingie kwenye mkakati mwingine, ipige *stop* maziwa yanayotoka nje ili maziwa yetu yaweze kupata soko. Vinginevyo, tutazalisha kwa wingi wafugaji watafuga kwa wingi, soko hakuna watamwaga. Kwa sababu hata ninavyoongea sasa hivi kuna maeneo ambayo lita ya maziwa inauzwa Sh. 300/=, Sh. 250/= wakati huo huo lita ya maziwa madukani iliyokuwa *packed* vizuri Sh 1,000/= au Sh.1,500/=. Kwa hiyo, hatupigi hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kidogo kwenye suala la uvuvi. Kati ya sehemu ambayo Serikali haijaweza kusaidia Taifa hili kuweza kuingiza kipato cha kutosha ni sehemu ya uvuvi. Uvuvi au samaki hahitaji gharama yoyote. Yupo pale kwenye maji anajilisha mwenyewe, anajifunika mwenyewe, anachohitaji gharama ni kumvuna na kumpeleka sokoni. Kwa bahati nzuri tumezungukwa na bahari, tumezungukwa na maziwa, tunayo mito. inatushinda nini sekta hii kushindwa kuingiza pato la kutosha kuinua uchumi wa wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumelala sana kwenye sekta hii. Nmwomba Mheshimiwa Waziri ajitahidi. Tukiangalia kitabu cha uchumi cha mwaka 2009, Waziri wa Fedha anasema kwamba "Pato la samaki kwenda nje lilipungua kutoka Dola za Kimarekani milioni 141.6 mpaka 127.6. Sababu ni kwamba soko la ushindani limezidi, Mchina na M-Vietnam anazalisha samaki kwa wingi." Kweli hiyo ni sababu? Sisi tunashindwa nini kufuga samaki? Nimefika China, miji yao yote imepambwa na mabwawa ya samaki. Sisi tuna mito, maziwa, kinatushinda nini? Tuwe na mkakati dhahiri, tuhakikishe kwamba wananchi wanapewa elimu, wanafuga samaki kwa wingi, tutafute masoko mazuri ya uhakika tuwe na *quality product* ili iweze kupata biashara nzuri na iweze kuinua kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii ni muhimu. Samaki baharini wanavuliwa bure, hawalipi chochote, hakuna cha ushuru wala cha samaki hata bandari ya samaki tumepigia kelele hapa Bungeni Upinzani mwaka wa tano sasa, wanakuja hata kujaza mafuta kwenye bandari hakuna, wanajaza kila kitu huko kwao waliko. Kwenye samaki tunaibiwa sana, ulinzi baharini ni dhaifu, ulinzi kwenye maziwa ni mdogo. Tunaomba sana Serikali ifanye juu chini sekta hii iweze kuinua kipato cha Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza na mimi nataka kuungana na wenzangu kwa kuishukuru Wizara hii kwa kujitahidi tangu wameanza kwa hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia kuhusu pamba. Leo asubuhi nimefurahi kuona Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara akisisitiza sana juu ya umahiri wa kuwa na mizani na mimi kama Mbunge ninayetoka sehemu ya pamba ninaiomba Serikali iwe kali sana zaidi kwa kipindi hiki kwa yoyote yule anayechezea mizani. Kwa sababu tumechoka kuibiwa na tunaendelea kuwa masikini kwa sababu ya wezi hawa ambao wanajaribu kukarabati ile mizani kwa njia ambayo wanaona itawafaa wao. Hilo nimeona niliseme kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni juu ya wafugaji. Nataka kusema kwa kipindi ambapo tumekuwa katika Bunge hili pametokea kitu kimoja ambacho nafikiri Mheshimiwa Waziri angekichukulia, Wazungu wanasema *seriously,* yaani kwa umakini mkubwa. Panaonekana kuvunjika kwa mahusiano kati ya Serikali na wafugaji. Hili ni jambo ambalo mngeweza mkalichukulia ovyo ovyo lakini nafikiri kama mtu mzima, pametokea na uvunjifu mkubwa kabisa wa mahusiano kati ya wafugaji na Serikali. Tangu matatizo ya Mbarali ambapo zaidi ya ng'ombe 300,000 zilihamishwa na wafugaji wakaingia hasara, matatizo ambayo yaliyotokea Kilosa, matatizo ambayo yametokea Ngorongoro, matatizo ambayo yametokea na sasa hivi inakuwa kama mtindo, hata kule Mara watu wanaanza kusema kwamba hii ni ng'ombe ya Msukuma iondoe, sasa tukifika mahali ambapo ni chini kiasi hicho ujue kwamba tuko katika hatari ya kutoelewana katika sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mazungumzo yangu hapa nitamkabidhi Mheshimiwa Waziri malalamiko ya baadhi ya wafugaji ambao wanatoka sehemu ya Morogoro, Iringa na sehemu mbalimbali. Nimejaribu kusoma tu kwa haraka aya ya tatu ambayo nitakayokupa wanasema : "Tumepitia Miswada hiyo, tuliyoipitisha kwa kina na kulinganisha na historia ya dhuluma dhidi ya wafugaji, ni dhahiri kuwa mgongano unatokea kwa mfumo wa kigeni wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji na udhibiti wa wahamiaji na mambo mengine". Kwa hiyo, hii inaonyesha wazi kwamba hakuna ushirikiano wa mawasiliano juu ya watu hawa. Mimi ningeshauri tuangalie hili kwa mara moja ili tuhakikishe kwamba hao wafugaji wetu tunawathamini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwambia, leo hawa wakigoma tu kuuza ng'ombe zao hakuna nyama kwa mwezi mmoja, pale Dar es Salaam na sehemu nyingine hapatakalika. Hawa ni watu wenye fedha, wakiamua kuchanga fedha zao kwa ajili ya mambo ambayo ni mabaya nchi yetu itakosa amani. Hawa ni watu ambao kusema kweli hakuna kati yetu leo ukimwamsha ana akiba ya zaidi ya shilingi milioni 25. Lakini kila mfugaji aliye na ng'ombe 100 huyu ni tajiri ana zaidi ya shilingi milioni 25, lakini Serikali yetu inaonekana haiwathamini kwa kiwango ambacho wanategemea.

Kwa hiyo, naona nitumie nafasi hii kukusisitizia kabisa mdogo wangu, hebu jenga mahusiano mazuri na hao watu wasikilize kama unavyowasikiliza wakulima wa pamba, kama unavyowasikiliza wakulima wa mahindi na vitu kama hivyo. Wasikilize na nawaona wako hapo wamekuwa wengi namna hii kwenye Bunge hili, ni kwa sababu wanatafuta mtu wa kuwasikiliza. Uliyepewa dhamana ya kuwasikiliza ni wewe, wasikilize. Kama huu ujumbe tu ukifika nitakuwa nimetosheka kabisa kwamba angalau nimeweza kujenga daraja kati ya wewe na wafugaji ambao hawa sisi wote

tunawategemea. Kazi nyingine ni nzuri, viwanda tunaona unajenga, minada unatupandishia bei tu Sh. 3,000/= hizo naona sijui kwa nini unataka watu wetu walipe Sh. 3,000/= lakini tayari umesema, tutalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, malambo ndiyo hayo ambayo hata Mheshimiwa Mama Hewa ameyazungumzia yote haya, ni katika kuwajali hawa watu. Wajali na ukiwajali mimi nafikiri tutaishi kwa amani katika Taifa hili. Usipowajali, basi tunatayarisha Tanzania ambayo haikaliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** *One message* basi leo!

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwanza nianze kwa kuwapa hongera Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yenu ya wataalam kwa kazi nzuri mnayofanya katika sekta hii ya mifugo na uvuvi. Naomba pia kwa namna ya pekee na wewe Naibu Spika na Spika niwape hongera kwa kuendesha Bunge letu vizuri. Kwa kipindi hiki tunachomaliza Bunge letu umelipa heshima linayoistahili na mimi kwa sababu niliwahi kuwa mfanyakazi katika Ofisi ya Bunge, naona tofauti ya dhahiri kabisa kwamba Bunge sasa ni Bunge la Kisasa zaidi. Hongereni sana wewe na Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mengi, lakini nilitaka tu nikubaliane na hoja iliyotoka Urambo aliyoizungumza Mbunge wa Tabora kwa maana ya Urambo. Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 19 wa hotuba yako unazungumzia juu ya maeneo yaliyotengwa takribani hekta milioni 1.4 kwa ajili ya wafugaji. Katika jedwali lako unazungumzia juu ya maeneo hayo kutengwa katika baadhi ya maeneo ikiwemo Kigoma Kijiji. Sasa mimi nilitaka Mheshimiwa Waziri atufafanulie hayo maeneo yaliyotengwa katika hivyo vijiji 266 ni vijiji gani hivyo katika Mkoa wa Kigoma? Maana nimeona Kigoma Vijijini nikashangaa kwa sababu lipo tatizo la siku zote na makosa yanafanyika. Ardhi yenye rutuba iliyovamiwa, narudia tena iliyovamiwa na wafugaji waliofukuzwa Ihefu, waliofukuzwa Bonde la *Lake Rukwa*, waliofukuzwa huko Tabora, wako Kasulu Mashariki na nataka katika hili nitofautiane na Mheshimiwa Mzee Cheyo. Hoja sio kugombana na wafugaji hawa, hoja ni ku-*balance* haya mambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Kasulu Mashariki ambako mimi ni Mbunge wake, tuna ng’ombe zaidi ya laki nane. Sasa wanatisia hata miundombinu ya umwagiliaji iliyojengwa kwa mamilioni ya fedha. Nadhani hoja hapa sio kuanza vitisho kwamba wafugaji watafanya nini, hapana. Tunataka ku-*balance equation* hapa. Huwezi kuwa na wafugaji wanazurura wanatoka wanakotoka kuja kuharibu maeneo mengine. Mimi nilidhani ile Sheria tuliyoipitisha mwaka huu mngeiharakisha ianze kufanya kazi yake ili tufike mahali tuelewane vizuri. Baadhi ya maeneo yamevamiwa na kwa kweli sisi waliovamia maeneo yetu ni Wasukuma katika vijiji vya Titye, kuna maelfu ya ng’ombe, Kabulwazili, Mvugwe, Bungempya, Kitanga, Ahsante Nyerere mifugo inazagaa kila mahali tena inachungwa na wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunashangaa kabisa na hatuna utamaduni huo sisi. Kwa hiyo, hili suala nafikiri ni muhimu sana na namwomba Mheshimiwa Waziri na timu yake, hizi takwimu zao wazirejee upya tujui *exactly* ni vijiji gani hivi ambavyo vimetengwa na Serikali kwa ajili ya wafugaji ili maeneo mengine kwa kweli tuweze kuweka huu uwiano kati ya kilimo na ufugaji.

Napenda kusema pia kwamba kule kwangu kuna skimu kubwa tatu za umwagiliaji. Skimu kubwa ya Rungwe Mpya ya mabilioni ya fedha, skimu kubwa ya Titye na skimu kubwa ya Msambala ya mabilioni ya fedha na zote ziko kwenye tishio la wafugaji hawa na wengi ni Wasukuma Mzee Cheyo ambao wanazagaa kila pahali. Hili ni jambo ambalo lazima liangaliwe vizuri na ningependa katika utaratibu wa baadaye, Wizara kama itawezekana kwa sasa nipate *exactly* katika Mkoa wa Kigoma ni Vijiji gani hivyo ambavyo vimetengwa eti na Serikali ukurasa wa 16 wa hotuba yake eti vimetengwa kwa ajili ya wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema tena, hatuna tena na wafugaji wa moja kwa moja lakini kuwe na uwiano kati ya maeneo ya kufugia na maeneo ya kilimo. Sisi kule kwetu hawa wafugaji wanaozunguka na mifugo yao tumewapiga marufuku kwenye vyanzo vya maji na kwenye mabonde yetu yote yenye skimu lakini hawa watu hawasikii na wanahatarisha maslahi ya wakulima ambao ndiyo wengi zaidi. Lakini pia niseme kwamba Mheshimiwa Waziri atusaidie. Sisi kule kwetu Kasulu tumejenga Mnada wa Kimataifa wa Buhigwe na ningefikiri pengine moja ya mambo ambayo yangefanywa na Wizara ni kutusaidia kufanya *promotion* kubwa ya mnada huu ili pengine hata hawa wafugaji waweze kupunguza baadhi ya mifugo yao watakapoona inafaa waiuze kwenye mnada huo ili waweze kubaki na ng’ombe wachache ambao watahimili maeneo ya kufugia. Vinginevyo itakuwa ni matatizo.

Mnada huu ni mnada huu ni mkubwa na ni mdana wa kimataifa, umegharimu fedha nyingi. Ninaomba sana Wizara waweke kwenye programu yao ya *training* na *promotion* kwa ajili ya mnada huu iweze kukidhi pia mahitaji ya kuuza mifugo yetu kwa wananchi wa *DRC* Kongo na Burundi, Rwanda na hata nchi ya Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika nitoke kwenye eneo la ufugaji nije niende kwenye eneo la mabwawa ya asili. Nimesoma kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nimefurahishwa sana kwamba kuna mkakati mahsusi katika Wizara hii wa kuboresha ufugaji katika mabwawa ya asili na kwamba mwaka huu wa fedha Wizara imejipanga kuzalisha na kusambaza vifaranga wa samaki takribani milioni tatu. Kwa hiyo, naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri katika Mkakati huo yako mabwawa ya asili makubwa katika Wilaya ya Kasulu, mabwawa ya asili ambayo yamejaa viboko. Bwawa la asili la Kagaruka, bwawa kubwa sana limejaa viboko, bwawa la Nyang’hala ni kubwa sana limejaa viboko na bwawa la Lugoi huko Kasulu nalo limejaa viboko.

Ninaomba katika vifaranga hao au watoto wa samaki mtakaowapandikiza, basi vifaranga hao katika hao milioni tatu, ninaomba sana Wizara yako ishirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu tuweze kupata baadhi ya vifaranga kwa ajili ya kupandikiza katika maeneo haya asilia na sidhani kama anahitaji utafiti kwa sababu kuna

samaki kambale katika mabwawa hayo na viumbe wengine wa majini katika maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu, nizungumzie juu ya ushirika wa wafugaji. Nimesoma kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nimeona wanamkakati mzuri sana kwa ajili ya programu ya ushirika wa wafugaji. Ningeshauri tu kwa Mheshimiwa Waziri, Wizara yake, Tume ya Ushirika na Chuo Kikuu Kishiriki cha Moshi muandae mitaala kwa ajili ya ushirika wa wafugaji. Kuwe na programu maalum kabisa ambayo itasaidia kuendeleza elimu hii ya ushirika wa wafugaji katika maeneo husika na kama mnavyofahamu Chuo Kikuu cha Ushirika cha Moshi ndiyo mabingwa katika eneo hilo, lina wataalam wengi naomba Mheshimiwa Waziri atenge fedha kidogo. Hata hizi fedha za *SADP* tuweze kujiingiza vizuri katika eneo hili ili hatimaye programu hizi ziweze kusaidia kuimarisha vyama hivyo vya wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni ndorobo. Nimeona katika hotuba ya Waziri amezungumzia juu ya *remapping* ya maeneo ya ndorobo katika Mkoa wa Tabora na Kigoma hasa maeneo yenye miombo. Ni dhahiri katika maeneo ya Kasulu Mashariki hasa kwenye kitalu cha uwindaji kile cha Nyamloha Uvinza, kuna ndorobo wengi sana na kumekuwa na programu hii ya ndorobo ya muda mrefu. Ninaomba programu hii iendelezwe katika vijiji vya Mvinza na vijiji vya Kagera Nkhanda kwani ni vijiji ambavyo vimeathirika sana na ndorobo na ningeomba programu hii baada ya kuwa wamechora ramani zao mpya wajikite kwenye maeneo hayo ili kuweza kuhakikisha kwamba ndorobo hao tunawatokomeza katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ya kwangu yalikuwa ni hayo, mgogoro wa wafugaji, vijiji 266 katika Mkoa wa Kigoma tuvijue ni vijiji gani, mabwawa ya asili, ndorobo, *SACCOS* za wafugaji na mwisho nimemalizia kwamba Wizara itusaidie kufanya *promotion* kwa ajili ya mnada wa kimataifa ambao umejengwa katika Wilaya ya Kasulu kwenye mpaka wetu wa Burundi sehemu ya Buhigwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nasema tena nawashukuru sana, Wizara imefanya kazi kubwa na imekuja na kasi mpya na ari mpya inayostahili kabisa, hongereni sana na ni matumaini yetu kwamba kipindi kijacho cha utawala cha Serikali yetu, Wizara hii itakuwa ni Wizara kiongozi katika kuingiza fedha au kuwa chanzo kipya cha fedha zetu katika Hazina yetu ya Taifa. Nakushukuru sana, ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa namna ya pekee nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Naibu waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuwawezesha Watanzania kutumia rasilimali samaki na wanyama kuboresha maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina rasilimali kubwa sana ya samaki baharini. Tunathamini juhudi za Serikali kupitia *MACEMP* raslimali hii inakuwa endelevu kwa kupiga vita uvuvi haramu lakini bado Serikali haijafanya vizuri katika kubadilisha hali za

uvuvi wetu kutoka uvuvi wa kizamani wa kutumia vyomba vya zamani na utaaalam wa zamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiweza kuwapatia wavuvi wetu zana bora za uvuvi na utaalam, wa uvuvi wa kisasa tutaweza kubadilisha maisha ya Watanzania waishio katika ukanda mpana wa Pwani wa kilometa 64,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado samaki wetu wanaibiwa sana na meli za kigeni zinazovua bila haya katika ukanda wetu wa bahari kuu. Naishauri Serikali kuchukua hatua za dharura kukamata meli hizo ili bahari yetu isiwe shamba la bibi.

Napendekeza miradi ya *MACEMP* ikinge kumbadilisha mvuvi wetu afanane na karne ya 21, mwenye ustawi na taaluma ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua jitihada za Wizara kuboresha mifugo yetu ili iwe na tija zaidi kwa wafugaji. Hata hivyo, bado tunakumbana na changamoto kadhaa katika kufikia huko. Tuna tatizo la ukame ambalo linaua ng’ombe wengi kule Simanjiro na maeneo kadhaa nchini. Serikali inashindwa kuchimba mabwawa na malambo kunusuru maisha ya ng’ombe wetu wakati wa ukame. Nashauri kwamba, kwa kuwa maisha ya Watanzania wa maeneo hayo wanashughulika na ufugaji tu, Serikali haina budi kuchimba mabwawa na malambio ili sio tu kunusuru maisha ya ng’ombe lakini pia kunusuru maisha ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi za kuanzisha viwanda vya ngozi, maziwa/nyama zinaonekana. Kwa upande wa viwanda vya ngozi matatizo yamejitokeza kwa bidhaa zao kukosa soko kutokana na mtikisiko wa uchumi duniani. Nashauri viwanda vyetu vianze kutengeneza bidhaa za ngozi zinazoweza kuuzwa hapa nchini kwa mfano viatu, mikoba ya aina mbalimbali mikanda na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, usambazaji wa zao la maziwa kutoka viwandani bado haujakidhi kiu ya wanywaji sehemu mbalimbali nchini. Tunashauri juhudi zaidi zizidishwe katika usambazaji maziwa.

**MHE.SALIM YUSUF MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sina budi kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kuwa wazima na tukaweza kuendeleea na majukumu yetu vizuri. Nakushukuru na wewe Mheshimiwa Naibu Spika, Spika, pamoja na Wenyeviti wa Bunge hili kwa kuendesha vyema shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi shughuli za kiuchumi za kilimo na mifugo zinaathiri sana kutokana na ukosefu wa mvua na ukame katika baadhi ya maeneo. Hali hii ni tofauti sana na mazao ya uvuvi ambayo mara nyingi huwa yapo na baada ya kuzuia uharibifu wa mazalia ya samaki na mazingira mengine mazao hayo yanakuwepo kwa wingi. Kutokana na hali hiyo ya uendelevu wa mazao hayo, pato la Taifa linaweza kuongezeka haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi za makusudi zinahitajika ili kuona kuwa mazao hayo ya uvuvi yanazidi kuliingizia Taifa pato zuri. Mwaka 2009, doria 2,390 zaidi zilifanyika kuliko zile za mwaka 2008 ambazo zilikuwa 7,227. Ni lazima doria zizidishwe kwa ajili ya kulinda mazao haya ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, juhudi za makusudi za kutoa elimu kwa wavuvi ziendelezwe. Baada ya vilio vingi vilivyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa bajeti ya Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, alitoa kauli ambayo ilipunguza sana malalamiko ya waheshimiwa wabunge kuhusu unyanyasaji wa wavuvi wadogo wadogo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kauli yake hiyo, mheshimiwa Waziri alisema atakutana na wadau wote wa uvuvi ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge, Wakuu wa Wilaya na wavuvi wenyewe ili kuzungumzia na kupata suluhisho ya kadhia hiyo. Lakini kwa bahati mbaya Mkutano huo bado haujafanyika na hivyo bado wavuvi wanaendelea kupata taabu katika shughuli zao. Ni vyema Mheshimiwa Waziri aharakishe suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wavuvi wengi wa hapa nchini ni wavuvi wadogo wadogo na hivyo kipato chao ni kidogo na hivyo kukosa mitaji kwa ajili ya kupata zana bora za uvuvi zitakazopelekea kuendeleza kazi yao kwa ufanisi. Hivyo, Serikal iandae utaratibu wa makusudi kuwakopesha wavuvi hawa mitaji na zana za uvuvi bora na hivyo kuendeleza vyema maisha yao

Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante sana.

**MHE.RIZIKI OMAR JUMA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa umahiri wake na kuandaa hotuba hii pamoja na watendaji wa Wizara na namna wanavyoisimamia kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wangu ni ushauri kwamba Serikali ijikite zaidi katika suala la kutoa elimu kwa wafugaji ili wawe wafugaji wa kisasa na waondokane na ule mtindo wa kuhamahama ili kutafuta malisho kwa ajili ya mifugo yao.

Pili, Serikali iandae mazingira mazuri ya wafugaji katika maeneo ya jamii hizo ili waendelee kufuga kwa kutumia utaalam wa kileo ili wao wenyewe wafaidike na mifugo yao na sio kuendelea na kudhalilika na kuwa tajiri wa mifugo, lakini maskini wa maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini kwamba tukiimarisha miundombinu, tukiboresha mazingira na kutoa elimu stahili, basi tutawakomboa wafugaji na kulikomboa Taifa letu kupitia sekta ya ufugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tumejaliwa maziwa mengi na kuzungukwa na bahari pamoja na mito mikubwa ambayo yote hayo tungeyatumia vizuri, basi Tanzania tungeweza kujiendeleza kwa kutumia rasilimali hizo tu, kwani samaki waliomo kwenye bahari zetu mito na maziwa tusingekuwa na sababu leo hii Mtanzania wa kawaida

(mwenye kipato cha chini) hata samaki hawezi kumla kutokana na bei. Hii inasababishwa na Serikali kutokutoa kipaumbele kwa sekta hii ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maharamia wanavamia nchi yetu na kuvuna samaki wetu ambao kwa miaka kadhaa sisi wenyewe tumeshindwa kuwavuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ijitahidi kuboresha sekta ya uvuvi kwa kuhakikisha wanawapa wavuvi wetu zana za kisasa na kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahari mito na maziwa, sayansi hazihitaji umeme wala msimu ila zana ndio muhimu na masoko ya uhakika ili tukuze pato la Taifa letu.

**MHE. NURU A. BAFADHIL**: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa mchango wangu kwanza katika Uvuvi. Uvuvi ni sehemu ambayo kama itawekewa mkakati, utainua pato la nchi. Pato la nchi kupitia uvuvi linaweza kukua kwa kasi iwapo ubunifu utatumika. Kuna meli za kisasa ambazo zinavua katika mwambao wa bahari yetu na kodi wanayotozwa kwa mwaka ni ndogo mno ukilinganisha na kipato wanachopata wavuvi hao. Je, Serikali haioni huu ni wakati muafaka Watanzania wawekeze katika uvuvi? Bahari au maziwa ni kiwanda kisichohitaji vipuri wala matengenezo ya mara kwa mara, inahudumia jamii siku zote 365 au 366 za mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine linalohusu mazingira, kuna askari wanaofanya doria kwa ajili ya kuwasaka wavuvi haramu hawa, wanafanya vitendo ambavyo ni vya kiunyama hususan wavuvi wanaotumia bahari. Wao wanapiga wavuvi hadi kuwajeruhi kwa utashi wao tu. Ikiwa nyavu zinazotumika hazifai, kwa nini wasipewe nyavu mbadala?

Mheshimiwa Naibu Spika, wavuvi hao pia ili watende kazi zao vizuri hawana budi kupewa mafunzo ya mara kwa mara ili wawe na uelewa wa matumizi ya vyombo na vifaa vya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mifugo, Serikali iangalie jinsi gani wafugaji wanafaidika na mifugo yao. Mfugaji ana mifugo lakini utakuta mfugaji huyo hana nyumba bora ya kuishi, hanywi hata maziwa yeye na familia yake, hali kadhalika hata nyama pia hawapati. Naomba wafugaji wapewe elimu ya kutosha kuhusu ufugaji bora na wa kisasa. Mfugaji bora awe na ng’ombe wachache wenye tija kwake badala ya kuhesabu wingi wa ng’ombe mbuzi na kondoo alionao. Wafugaji wafundishwe njia za kisasa za ufugaji na umuhimu wa mfugaji kutumia mifugo yake kumnufaisha katika jamii yake.

**MHE. AZIZA S. ALLY**: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Napenda kuchangia katika maeneo ya majosho, utekelezaji wake ni mdogo sana, hivyo naomba Wizara ifanye utafiti kugundua kuna majosho mangapi katika nchi hii yaliyojengwa na yanayofanya kazi kwani ukweli ni kwamba wataalam wetu wanashauri na wananchi wanachangia na kuibua mradi huo na matokeo yake majosho hayafanyi kazi tena. Naomba kufahamu usimamizi wa majosho hayo unasimamiwa na nani? Kama hayafanyi

kazi, kuna uwajibikaji gani ambao umefanyika kwa wanaoshauri miradi ambayo haifanyi kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono.

**MHE.HEMED M. HEMED**: Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumshukuru mola kwa kunijalia kuamka salama mimi na wenzangu hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wake kwa kufanikisha hotuba hii ambayo imejaa matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Magufuli kwa kutoa picha za kuku na samaki katika kitabu chake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka Wizara husika ilipitisha sheria ya kuwalinda wanyama wakiwemo kuku kuwanyanyasa. Inavyoonekana, sheria ile imebaki katika maandishi tu kwani kuku hadi leo huchukuliwa kwa kushikwa miguu kwa kuninginizwa. Uchukuzi huu ni unyanyasaji kwa wanyama hawa. Serikali mpaka leo imeshindwa kusimamia uhalifu huu unaofanyiwa wanyama hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uvuvi, sekta ya uvuvi nchini ni miongoni mwa sekta muhimu katika kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi katika bahari kuu, ndio sehemu inayoweza kuiokoa nchi yetu katika dimbwi la umasikini, lakini ndio eneo lililo huru katika nchi yetu. Serikali inakosa utaratibu kabambe wa kusimamia kodi zinazolipwa na meli za wavuvi kutoka nje ya nchi. Mfano, mdogo ni pale Mheshimiwa Magufuli alipofanya kazi za ziada ya kuikamata meli ya kigeni ikivua samaki katika bahari yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii inakabiliwa na changamoto kadhaa zinazorejesha maendeleo ya uvuvi nchini petu. Kuna ukosefu wa mitaji na mikopo kwa ajili ya kuwekeza kwenye shughuli za uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wafugaji, mara nyingi tunapata matatizo yasio ya lazima, Serikali kuendeleza kupanua mbuga za wanyama, *"National Parks"* na mapori ya hifadhi *"GAMES RESERVES*"katika maeneo ambayo wafugaji huyatumia kwa wanyama wao. Kitendo hiki mara nyingi huleta ugomvi kati ya mwananchi na Serikali na hatimaye mfugaji huingizwa makosani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, nimpongeze Mheshimiwa Magufuli kwa umahiri wake katika kusimamia shughuli hizi. Ahsante.

**MHE. FELISTER A. BURA**: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa kazi yake nzuri ya utekelezaji wa ilani ya CCM ya uchaguzi ya mwaka 2005. Nampongeza Naibu Waziri Mheshimiwa

Dr. James Wanyancha, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kuifanya Wizara hii kuwa hai katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina utarjiri mkubwa wa mifugo na kwa utajiri huo tungeweza kukidhi mahitaji mengi ya wananchi wetu. Hivyo, sivyo ilivyo, kwani sekta hii haijachangia vilivyo katika pato la Taifa. Naipongeza Serikali kwa mikakati yake ya kuhakikisha kuwa sekta hii inakuwa kwa kasi kubwa ili iweze kuchangia pato la Taifa kwa asilimia kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ranchi za Taifa zina maeneo makubwa ya ardhi. Baadhi ya ranchi za Taifa hazina hatimiliki. Ninaishauri Serikali kuhakikisha kuwa ranchi zake zina hatimiliki na kwa ranchi kuwa na hatimiliki ni rahisi kupata wawekezaji au kuingia ubia na wawekezaji kupata mikopo kutoka taasisi mbalimbali za fedha kwa maendeleo ya ranchi za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Nyama cha *Tanganyika Packares* cha Kawe kilibinafsishwa zaidi ya miaka mitano iliyopita: Je, Serikali inaweza kuwaeleza wananchi sababu ya kiwanda kile kutofanya kazi mpaka sasa? Kama mwekezaji ameshindwa kuendeleza kiwanda kwa nini asinyang’anywe na kupewa mwingine mwenye uwezo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuanzisha Vituo vya Afya kwa ajili ya mifugo katika Halmashauri zetu. Tatizo lililopo ni vitendea kazi. Maafisa Ugani wachache waliopo wangeweza kufanya kazi zao vizuri iwapo wangekuwa na vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taarifa zisizo rasmi kuwa baadhi ya wafugaji wa kuku wa kisasa wasio waaminifu huwalisha mifugio yao (kuku) vidonge vya uzazi wa mpango na vidonge vya *ARV* kwa lengo la kuwakuza haraka na kuwanenepesha kwa kipindi kifupi: Je, taarifa hizi ni za kweli? Kama taarifa hizi ni za kweli Serikali inachukua hatua gani kukomesha ufugaji huo na je, watumiaji wa nyama ya kuku hao hawapati madhara?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KHADIJA S. AL-QASSMY**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uwezo wa Karima, leo hii nipo hapa na madhubuti kushika kalamu ili na mimi nitoe mchango na maoni yangu ili niweze kusaidia katika sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza Waziri, Naibu wake na Watendaji wote wa Wizara hii kwa maandalizi ya hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza wewe, Mheshimiwa Spika na Wenyeviti wote kwa umahiri wenu mkubwa kwa kuliendesha Bunge hili kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho na kwa umuhimu mkubwa, nampongeza Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa hotuba yake nzuri ambayo kama Serikali ina dhamira ya kweli, basi wanaweza wakachukua ushauri wa wapinzani, kwani Taifa hili ni letu sote na tunajenga nyumba moja, kwa nini mgombee fito?

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuchangia katika sekta ya uvuvi pamoja na Wizara kujipanga kuhakikisha wavuvi haramu, lakini bado Serikali haina mipango thabiti ya kuwasaidia wavuvi hao. Kama wananchi tumeshuhudia katika sehemu mbalimbali za karibuni wakichomewa nyavu haramu ambazo zinaharibu mazalio ya samaki, lakini la kujiuliza, hizi nyavu zimepitia wapi hata wananchi wa Chato wakazipata? Bila shaka hapa Serikali yetu ina mapungufu katika bandari zake na kuacha vitu ambavyo havikubaliki kupita na baadaye kuwatia hasara kubwa wavuvi mara nyingi ndio maskini wa kutosha kutokana na kukosa zana za kisasa na za kuvulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatukatai kuondoa zana haramu, lakini baadaye muwape zana mbadala ambazo zitawasaidia katika uvuvi wa kileo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kusikitisha zaidi, wavuvi wakishachomewa nyavu hizo wanapewa masanduku ya kufugia nyuki. Kweli hii ni haki kwa Serikali kuwafanyia usanii wavuvi? Kweli tuko *serious* na shughuli ambayo ni ya kuvuna tu kuwasaidia wananchi wakafanikiwa mnawapa masanduku ya kufuga nyuki wakati huo sio fani yao?.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani mara nyingi ilikuwa ikisema hapa Bungeni kwamba kuna nchi zinaiba rasilimali zetu, lakini hadharani Serikali ilikuwa inaona sio kweli, lakini bahati nzuri Mwenyezi mungu amejalia mmeona wezi wetu na leo wako Mahakamani. Je, Serikali ingekuwa inasikiliza Kambi ya Upinzani, sekta hii si ingechangia pato kubwa la Taifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ijitahidi sana kuwasaidia wavuvi kwa kuwakopesha zana za kisasa za kuvulia kwani kwenye sekta hii hakuna hasara, ni kuvuna matunda tu tofauti na kilimo ambacho kuvuna kwake ni kwa bahati kubwa mpaka utayarishe mashamba, upande, upalilie na uwe na mbolea halafu unategemea mvua ndio uweze kufanikiwa na mnakopesha zana zote hizo kwa mabilioni. Inakuwaje mshindwe kuwakopesha wavuvi na vile vile wenye mifugo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuruku sana.

**MHE. FETEH S. MGENI**: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nina heshima kubwa kukupongeza wewe binafsi kwa uwezo wako mkubwa, busara na hekima, katika kuongoza Bunge lako Tukufu. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wake wote kwa jinsi wanavyomudu Wizara na hotuba nzuri iliyotolewa na Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa mwanzo, ninaomba kuchangia juu ya uvuvi. Ninaiomba Wizara ijipange vizuri katika uvuvi wa Bahari Kuu tuondokane na uvuvi wa mwambao mwa bahari na sasa tuingie kwa nguvu kubwa katika bahari kuu. Ni vyema tukatafuta meli kubwa za uvuvi kwa njia za kuomba wawekezaji kwa njia yoyote

ya ubia. Eneo letu la Bahari ya Hindi ni kubwa mno na lina utajiri mkubwa wa samaki wa aina mbalimbali tena wenye thamani kubwa sana Duniani. Ni vyema tukajenga viwanda vya kutengeneza samaki wa makopo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufuagaji wa kuku, wanyama na nyuki, hivi sasa kumeingia au kumeenea ufugaji wa kuku wa aina hizo, lakini bado elimu muafaka ya ufugaji huo haijatolewa ipasanyo utakuta wafugaji wengi wanapata hasara kubwa kwa vifanga na hata kuku wenyewe kufa ovyo na mfugaji huyo kubaki na madeni na kurejea kwenye umasikini mkubwa. Aidha, madawa na vyakula vya mifugo kuwa na ubora na utaalam wa utumiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tuna utajiri mkubwa wa mifugo lakini bado Serikali haijajipata vizuri katika kusimamia na kuimarisha mifugo yetu. Kwanza mifugo yetu inahamishwa ovyo ovyo hasa kwa kutafuta malisho na zaidi wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani sasa umefika wakati wataalam wetu waandae utaratibu mzuri wa ufugaji na kupatiwa maeneo yao maalum kwa malisho, malambo, majosho na matibabu ya wanyama hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kwamba tukimudu kuweka maeneo maalum, yaani Maraji na Kadhali, hii itaepusha mgongano baina ya wafugaji na wakulima ambao hauishi kutokea kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu huu mdogo, kwa heshima kubwa, kwa niaba yangu na wananchi wa Jimbo langu la Bumbwini tunaiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante.

**MHE.GAUENTIA M. KABAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja hii mkono asilimia mia moja, nikiwa kama mtoto wa mfugaji na isingekuwa mifugo, nisingesoma kabisa. Hata hivyo, naunga mkono ufugaji wa kisasa kupunguza mifugo kwa kuuza/kuvuna ili kuboresha mazao ya mifugo hiyo.

Naomba mtaalam wa kunielekeza ili nichimbe bwawa la samaki sio nyumbani kwangu Sirari tu, bali kwa ndugu zangu wa Tarafa ya Inchugu na kwingineko. Kwa kawaida, Wakurya huogopa kuvua ziwani, lakini naamini watafurahi sana kuwa na mabwawa haya, maana sasa hivi ni walaji hodari wa sato kutoka Ziwa Victoria, lakini samaki hawa ni ghali sana.

Nawatakia nyote, Mheshimiwa Magufuli na kaka yangu Wanyancha ushindi wa kishindo kwenye Majimbo yenu. Ahsante.

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ugomvi kati ya wakulima na wafugaji hautakwisha mpaka pale maeneo ya wafugaji yatakapotengewa maeneo kwa uhakika. Naiomba Serikali iwatengee maeneo na kuweka miundombinu ya maji ili wamwagilie na kupata malisho na maji. Imetosha watu hawa kufika na mifugo na kubaki maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji wanapata shida hadi wanachungia mifugo katika hifadhi na kusababisha mifugo yao kuuawa na mabwana nyama, mfano ni ule wa Mpimbwe Mpanda ambako ng'ombe zaidi ya 30 walipigwa risasi kwa kuwa walichungiwa ndani ya hifadhi hapo mwaka wa 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, haipendezi mambo haya kutokea hapa Tanzania, kwani tuna ardhi ya kutosha ambayo wafugaji wakitengewa na kupewa miundombinu ya maji na malisho, mauji ya mifugo hayatatokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri wafugaji wasaidiwe kuunda *SACCOS* ili waweze kuweka na kukopa kwa maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu iende sambamba na huduma nyingine zote kwa wafugaji ili wawe wafugaji bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, soko kwa wafugaji iboreshwe ili waweze kuuza mazo yao ya mifugo kwa urahisi na kwa faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu kwa hotuba nzuri. Lakini niwapongeze sana kwa kazi kubwa na nzuri inayofanyika katika maeneo mnayoyasimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tumeshuhudia ukame mkubwa miaka miwili iliyopita,, mifugo mingi imeathirika, wanyama wamekufa wengi, wafugaji wamepoteza kipato na hivyo kuwa masikini zaidi. Je, katika bajeti hii, ni kitu gani/mkakati/programu gani ya makusudi iliyoandaliwa kutekelezwa ili ikitokea ukame tena wanyama wasiathirike kiasi kikubwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina mifugo mingi, bado wafugaji na mifugo yao wanahamahama. Ufugaji wa namna hii sio wa tija, hauwezi kuongeza Pato la Taifa kwa kiasi kikubwa. Je, ni lini sasa fedha nyingi zitatengewa Wizara hii na hawa wafugaji wakaelimishwa na kuwezeshwa kufuga kisasa, tupate mifugos bora, na kuongeza pato la mfugaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Magufuli na Wizara kwa juhudi zao za kupigana vita dhidi ya uvuvi haramu, matokeo ya vita hii tumeanza kuyaona sisi watu wa Bukoba, tumeanza kuwaona aina ya samaki waliokwishapotea. Kwa mamp Mboju au kitoga sasa hata wakubwa wanapatikana. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza, pamoja na vita dhidi ya uvuvi haramu, tungeanzisha misimu kwenye Ziwa Victoria kuwe na msimu wa kuvua na msimu wa kuachia samaki kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kagera wapo wanaotaka kufuga samaki. Je, wataalam wa kutufundisha wako wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote katika Wizara hii kwa upendo mkubwa wanaoonesha kwa mifugo, samaki na Taifa kwa ujumla. Kama tu mifugo na samaki wangekuwa na uwezo, hakika wangefanya sherehe ya kujipongeza kwa kupata hatimaye Waziri anayewatambua tena kwa idadi yao. Nawapongeza sana. Hotuba hii pia ni nzuri sana, inazidi kutia moyo wakulima na wafugaji kuendeleza mifugo yao na mifugo na samaki kuweza kuchangia zaidi katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi zangu kwa Wizara hii, ninayo maombi kadhaa kama mchango wangu. Maombi yangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na majanga ya mara kwa mara ya vifo vya mifugo katika maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu la tatu linahusiana na upatikanaji wa maji ya kutosha kwa mifugo na binadamu. Tatizo kubwa la wafugaji ni kuwa wengi wako katika maeneo yenye ukame, ni maeneo ambayo yanapata mvua kwa kiasi kidogo. Maeneo hayo yote yana makorongo na vijito ambayo hupitisha maji mengi wakati wa masika, maji ambayo baada ya muda mfupi huwa yamepotea yote. Naishauri Serikali kupitia Wizara hii itambue makorongo na vijito katika kila Kijijji ili kila Kijiji au Kata kijengewe makinga maji/mabwawa yatakayotumika kwa mifugo katika maeneo hayo kwa kipindi kirefu. Serikali inatakiwa kuamua kwa ajili ya mifugo na hata samaki kama ikiamuliwa hivyo. Jambo hili linawezekana, mbona kwa sekta ya elimu na sasa afya imewezekana? Tunatakiwa kujaribu ili tuanze. Bila kuanza hatuwezi kufaulu. Lengo letu kwa hiyo linatakiwa kuwa kufaulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kuwatakia Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake kheri na mfanikio kwa kila wakitarajiacho kwa siku za usoni, na kwa watumishi wote wa Wizara hii, Mwenyezi Mungu aendelee kuwalinda na kuwawezesha kuiendeleza Wizara hii. Njia muendelee nayo, inatia moyo. Mwenyezi Mungu awabariki. Ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye ufafanuzi wa kina kuhusu sekta ya mifugo na uvuvi. Pili naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ihakikishe kwamba majosho yote yanafanyiwa ukarabati ili mifugo iweze kuogeshwa, hii itasaidia sana kudhibiti magonjwa ya kupe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa gharama za dawa za mifugo ni kubwa nashauri gharama za dawa haya ipunguzwe ili wafugaji waweze kumudu kuyanunua na kutibu mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ina mpango wa kufanya sensa ya mifugo, je, ni lini sensa hii itafanyika ili tuwe na takwimu sahihi za mifugo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini sheria ya kuanzishwa taasisi ya utafiti wa mifugo ya Taifa italetwa Bungeni ili taasisi itambulike kisheria? Kwa kuwa Mheshimiwa Rais alipotembelea Wiaya ya Mpwapwa mwaka 2008 aliagiza kwamba wanafunzi/wanachuo wote wanaosomea mafunzo ya mifugo (Vyuo vya *LITI*) kikiwemo Chuo cha Mifugo cha Mpwapwa waajiriwe moja kwa moja. Je, mpango huo unatekelezwa kwa wanachuo wa *Diploma* na vyeti?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nakushukuru sana kwa kutenga fedha kwa ajili ya kuimarisha Chuo cha Mifugo *(LITI)* Mpwapwa, kituo cha uchunguzi wa magonjwa ya mifugo *(V.I.C* Mpwapwa) na taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo Mpwapwa. Je, mwaka huu wa fedha wametengewa kiasi gani kila kituo kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshmiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wakuu wa Wizara hii.

Kuhusu suala la uhamasishaji juu ufugaji bora na utunzaji wa ngozi za wanyama ili tuongeze zao la ngozi, usindikaji wa bidhaa za ngozi ni jambo muhimu, tunahitaji kuwa na wataalum na mitambo ili tusindike ngozi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hamasa ya matumizi ya bidhaa za ngozi zinazotengenezwa Tanzania kwani sasa viwango vya bidhaa za ngozi Tanzania ni viwango bora sana hasa mabegi, viatu, mikanda na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza Wizara kuanzisha siku ya maziwa na hamasa kwa watu kunywa maziwa kwani taratibu tatasonga mbele. Naomba msisitizo mkubwa juu ya mabwawa ya samaki ya Luhila, Songea wananchi wamehamasishwa sana juu ya ufugaji samaki hivyo Bajeti katika kitengo cha ufugaji samaki ikiongezwa itasaidia kutekeleza mipango ya ufugaji wa samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napongeza sana Wizara hii imepata Waziri makini, Naibu Waziri msikivu, Katibu Mkuu mwenye upeo mkubwa, watendaji wengine wote waelewa. Mungu awabariki muendeleze Wizara hii vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wake wote kwa kuandaa hotuba hii na kuileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutenga maeneo kwa ajili ya mifugo kwa kila mkoa, wilaya na kwa kila kijiji, jedwali namba tano limeainisha maeneo yaliyotengwa kwa baadhi ya mkoa/wilaya. Hizi ni takwimu za kwenye karatasi siyo hali halisi iliyopo vijijini. Haya maeneo hayapo, wafugaji wanahangaika, wanatangatanga bila kutulia. Migogoro inaendelea kati ya wafugaji na wakulima. Naiomba Serikali ipeleke wataalam wake huko kwenye halmashauri kuhakikisha maeneo ya wafugaji yanatengwa na yanatambulika kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kutoa elimu ya ufugaji wa kisasa vijini ni ndogo sana, kwani wataalum hao wa mifugo ni wachache na hata waliopo hawana zana/vifaa vya usafiri hivyo kazi haionekani. Takwimu nyingine hapa zinategemewa ofisini na sivyo hali halisi. Sisi tupo huko vijijini tunajua matatizo ya wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatakiwa kujiwekea malengo kwa muda fulani. Elimu ya ufugaji wa kisasa inaweza kuenea maeneo yote ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufugaji utaweza kuleta tija kwa wananchi wetu pale tutakapoweza kubadili hali ya ufugaji wa sasa ambapo wapo wafugaji wanaotumikishwa na mifugo bila kunufaika na kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya usindikaji wa mazao ya mifugo bado havikidhi mahitaji, tuna mifugo mingi sana mikoa mbalimbali, cha ajabu eneo ambalo mifugo ni mingi viwanda ni vichache au hakuna kabisa. Wote tunajua Kaskazini mwa Tanzania ni wafugaji sana lakini viwanda viko ukanda mwingine. Hizo gharama za kusafirisha mifugo kupeleka huko atalipa nani? Sivyo kuongeza gharama za bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ng'ombe, mbuzi wa Arusha wanakwenda Kenya ambapo ni jirani, Wakenya wana-*process*, wanarudisha hapa nchini tunauziwa ghali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, maziwa yanakwenda Kenya wanapata wanaleta hapa kuuza hii ni haki?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uendelezaji viwanda vya ngozi hapa nchini, Serikali inachangia kwa asilimia mia moja kwa kuua viwanda vya ngozi hapa nchini. Kwa kupata soko zuri la ngozi za mifugo tungeweza kuinua kipato cha wafugaji wetu. Viwanda vyetu vinashindwa kujiendesha kwa sababu pamoja na kukosa utaalam wa kutosha uwezo mdogo wa mtaji hata zile nchi zinazozalishwa hazina soko zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Serikali imeruhusu bidhaa za ngozi kutoka nje. Viatu, mabegi, pochi za akinamama, mikanda ya suruali vyote vinatoka Dubai, China na kwingineko. Tena ngozi iliyotengeneza bidhaa hizo ni feki wakati hapa tuna ngozi halisi

*(original).* Nchi zote zinalinda viwanda vyake vya ndani kwetu ni tofauti! Hii ni aibu kwa Taifa.

Mheshimia Naibu Spika, tungeamua kwa dhati kwamba viatu vya wanafunzi mashuleni tu (msingi na sekondari) tutengeneze wenyewe hapa nchini tungesaidia sana zao hili kupata soko la uhakika. Tunatoa soko kwa bidhaa za nchi za nje huku bidaa zetu zikikosa soko. Tuamke kumekucha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Hali ya Uchumi ya Taifa 2009 imeeleza kwamba mauzo ya samaki yanapungua kutoka *USD* 141.6 mwaka 2008 hadi *USD* 127.6 mwaka 2009. Hii inathibitisha wazi ni kwa jinsi gani Serikali imeshindwa kusimamia vizuri mazao haya ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezungukwa na bahari na maziwa kona zote. Hakuna gharama za malisho kwa samaki ni mali iliyotayari, gharama ni kuvua tu na kufikisha kwenye masoko. Samaki wengi wanavuliwa na watu kutoka nje bila kulipa hata senti wala ushuru wowote. Wanakuja na meli zao wanavua na kuondoka zao huku sisi tunalia umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ufugaji wa samaki, bado nchi yetu haijaweza kutoa elimu ya kutosha na kueneza utaalamu wa ufugaji wa samaki. Tunazo fursa zote za kutuwezesha kunufaika na ufugaji wa samaki kwani tunayo mito mingi sana, tumezungukwa na maziwa tatizo ni utaalam. Leo Vietnam na China wanaongoza kwa ku-*export*samaki wanaofugwa kitaaalamu sisi tunashindwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashuikuru sana. Ahsante.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuitekeleza Ilani ya Chama ili kuwapunguzia wananchi umaskini na kuongeza pato katika uchumi wa Taifa kwa kupitia sekta hii ya mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri, hongera sana. Nawapongeza kwa juhudi mlizochukua ili kupambana na uvuvi haramu katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Hata hivyo kuna baadhi ya maeneo uvuvi haramu bado unaendelea. Elimu iendelee kutolewa kwa wavuvi, watumie zana bora za uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na migogoro baina ya wafugaji na watumiaji ardhi. Elimu zaidi itolewe juu ya ufugaji wa kisasa, pia watengewe maeneo kwa ajili ya mifugo yao kuondoa migogoro na wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kuwapongeza kwa mara nyingine kwa kazi nzuri.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Hata hivyo nichangie machache katika hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, uingizwaji ng'ombe holela kutoka mikoa ya Tabora, Rukwa na Shinyanga. Hali si shwari katika Wilaya ya Kasulu. Ng'ombe wengi kwa maelfu wameingizwa katika maeneo yetu. Bila shaka sheria tulizotunga ikiwemo ya utambuzi na usajili itatekelezwa vizuri. Ng'ombe wasiachwe wazurure nchini bila utaratibu. Ukurasa wa 19 wa hotuba "J" unasema ili kupunguza migogoro, Serikali imetenga hekta milioni 1.4 na katika vijiji 266 katika mikoa tajwa ikiwemo Kigoma. Je, ni vijiji gani hivyo katika Mkoa wa Kigoma na Wilaya ya Kasulu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumbuka mifugo hii sasa inatishia *scheme* zetu za umwagiliaji za Titye na Rungwe mpya kwa sababu zimevamia mabonde yetu tena ambayo ni *source of water,* kwenye *scheme* zetu nilizozitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzisha kituo cha kuzalisha mitamba Wilaya ya Kasulu na hasa uwanda wa juu ambao sasa ni wilaya mpya ya Buhigwe. Ninashauri *strongly* kuanzisha/kurejesha kituo sehemu ya Mwayaya na Itevu Juu. Miaka ya 1980 na 1990 tulikuwa na kituo hicho sehemu ya Manyovu – kituo cha Mwayaya na kuanzisha kituo kipya pale Itevu Juu. Aidha, kituo hiki/hivi vitasaidia wafugaji wa asili kuboresha mifugo yao na kujipatia kipato zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vyama vya ushirika vya wafugaji, nashauri sana Wizara yako, ishirikiane na halmashuri ya wilaya kuanzisha programu za ushirika huu. Halmashauri za wilaya hazina *capacity* ya kuanzisha programu za aina hii. Wizara ishirikiane kitaalam na halmashauri/idara za mifugo kuanzisha programu za aina hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu minada ya mifugo halmashauri ya Wilaya ya Kasulu tumejenga mnada wa Kitaifa pale Bakigwe, Wilayani Kasulu, Wizara yako iisaidie halmashauri ya Wilaya kutangaza mnada huu kwa nchi jirani za Burundi, Rwanda na *Congo DRC.* Bila shaka *promotion strategics* zinahitajika ili minada hii iwe na manufaa mapana ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uvuvi kwenye mabwawa ya asili, pale Kasulu tuna mabwawa makubwa matatu ya asili. Nashauri Wizara hii, itume mtaalamu wa uvuvi washirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ili kufanya utafiti wa kina kwenye bwawa la asili la Kaguruka ambalo pia lina viboko wengi. Pamoja na bwawa la Nyankara, ninaamini utafiti wa kina ukifanyika maeneo hayo yanaweza kuwa na fursa mpya za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri mtoa hoja, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, wavuvi kata ya Mazinga, Muleba Kusini wanahitaji msaada maalum wa zana za kuvulia samaki. Je, Serikali ina mpango gani mahsusi kutusaidia katika sekta hii ambayo inatoa ajira kwa vijana wengi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni maelezo ya nyongeza katika sekta ya migofu. Muleba tumepata majosho mengi, tunashukuru. Tatizo letu ni maeneo ya kufugia na hasa kuchungia. Wizara ishirikiane na Wizara ya Ardhi ili maeneo yatengwe kwa ajili ya wananchi wanaochunga wapate maeneo ya kuchungia/kulishwa mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufugaji, ujukite zaidi kwa kuku wa kienyeji pia kwa sababu ya urahisi na unafuu wa chakula. Kuku anataga kwa kula pumba na kupata maji. Kuku wa kienyeji wana bei nzuri. Naushauri wataalam wa ugani wawafikie wananchi wafugaji wa ng'ombe, kuku, mbuzi/kondoo na kadhalika ili tuwe na mifugo bora ambayo itatoa mazao bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nirudie kushukuru jitihada za makusudi zinazoendelea kufanywa na Serikali ili kuwepo amani katika ranchi ya Kagoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza na kumshukuru Mheshsimiwa Dr. John Magufuli, kwa jinsi alivyosimamia suala hili. Nampongeza pia Mkuu wa Mkoa Kagera, Mheshimiwa Babu alivyolipokea na kutekeleza maagizo ya Rais kwamba iwepo amani na migogoro idhibitiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa ipo amani kwa kiasi fulani. Hata hivyo, Serikali iangalie kama waliopewa maeneo ya kuwekeza hawajafanya vizuri, wanyang'anywe. Pia wale wanaoleta leta vurugu kama *Block 3* wadhibitiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia heri katika siku ya leo. Nawasilisha.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE**: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uvuvi katika Bwawa la Mtera, Mheshimiwa Waziri utakumbuka ulitembelea Jimbo langu la Kibakwe na ukapambana na uvuvi haramu na hasa matumizi ya nyavu ndogo zisizoruhusiwa (makokoro) katika vijiji vya Mtera, Kibwegere, Chamsisiri, Chamdumbwei A & B. Nakupongeza sana kwa kazi nzuri uliyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini dhamira hiyo nzuri haitafanikiwa kama hakutakuwa na mpango maalumu wa Wizara yako au halmashauri zinazozunguka Bwawa la Mtera na sehemu zote ambako wanafanya uvuvi haramu, hazitatoa vifaa (zana) mbadala baada ya kuwanyang'anya zana haramu wavuvi hao, iwe kwa kuwakopesha au kwa kuwauzia kwa bei nafuu, ili waondokane na uvuvi haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wavuvi hawa au kundi hili ni la wavuvi wa hali ya chini hivyo kuteketeza zana zao bila kuwapa zana mbadala kwa wao wanaona kama Serikali ni wanyang'anyi na wasiopenda maendeleo yao na hivyo kujenga chuki na Chama kinachounda Serikali badala ya kuachana na uvuvi huo haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uvuvi katika Ziwa Tanganyika ni hafifu sana, ziwa hili ni *under utilized* kwani wavuvi hawana vifaa madhubuti vya uvuvi, hakuna meli hata moja ya uvuvi, wanatumia viboti vidogo vinavyoitwa *"vipe"*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba bado ziwa ni *under utilized* hii kazi ambayo inasaidia kipato cha wavuvi wadogo wadogo na vile vile kitoeo kwa wananchi wa Mkoa wa Kigoma. Lakini sasa wavuvi wamepewa masharti ya kuvua wakati miaka yote walikuwa wanavua bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi wa Ziwa Tanganyika ni wa aina tatu, uvuvi wa dagaa, hawa hawakui ni aina ya samaki wadogo sana na nyavu zake lazima ziwe za vitundu vidogo. Je, Serikali inapokataza nyavu hizo wavuvi watumie nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi wa samaki aina migebuka, hawa ni wa *size* ya kati ambao mmoja anaweza kuwa na nusu kilo au kilo moja. Hawa wanavuliwa na nyavu kubwa kidogo. Sasa Serikali imetoa nyavu gani mbadala kama hawaruhusiwi kuzitumia tena?

Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi wa sangara, ziwa hili lina sangara pia na zana zinazotumika ni tofauti na wao wanapatikana kwenye maji marefu ambapo si rahisi kwa mvuvi mdogo mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo samaki aina nyingi lakini hao ndio maarufu. Hivi sasa wavuvi wanakatazwa kuvua kama walivyozoea basi, Serikali ioneshe zana bora ni zipi ili waendeleze ajira zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, usalama wa wavuvi wa Ziwa Tanganyika ni mdogo sana, wanavamiwa na maharamia wa Congo. Mbaya zaidi polisi wanadai Bajeti yao ni ndogo hivyo, wavuvi inawabidi wachangie mafuta ya *diesel* kwa ajili ya boti ya polisi ya doria. Lita mia moja kila usiku wa kipindi cha uvuvi, wanachangia kwa zamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie jinsi gani watawasaidia mvuvi wa Kigoma hasa katika ulinzi ili kumpunguzia ukali wa maisha, kwani ameweza kuchangia mafuta na bado siku hiyo asipate samaki wa kutosha ukizingatia vifaa vyao ni dhaifu na hawana meli za uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba Serikali iangalie uwezekano wa kupata meli ya uvuvi Kigoma na vile vile kiwanda cha samaki, bila kusahau ulinzi wa wavuvi.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naiunga mkono hoja hii. Naomba sana sheria ya kuogesha mifugo itumike ili kupunguza magonjwa yanayosababisha ng'ombe kufa na pia kuharibu ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, malambo ikiwezekana kila kata kuwe na lambo la kunywesha mifugo. Pia kila kata ya kijiji kuwe na josho la kuongesha mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya kujua faida ya ngozi, namna ya kuchuna, visu vya kuchunia vipatikane kila kijiji. Pia kuwe na sehemu maalumu ya kuanikia ngozi kila kijiji au kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimuulize Waziri, *TAFICO* hivi sasa kunafanyika nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono.

**MHE. DR. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalamu wote kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Hanang ina wafugaji wengi. Wafugaji hao wanakabiliwa na miundombinu hafifu kama vile kutokuwa na mabwawa na malambo, majosho na maeneo ya kutolea chanjo, matokeo yake ni ng'ombe wengi kufa. Vifo vingi vya ng'ombe husababisha wafugaji kuhamahama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maelezo hayo ni muhimu kwa wilaya kuwekwa miundombinu hiyo hususan malambo. Kutokana na mahitaji (gharama) makubwa ya fedha, Bajeti ya Halmashauri haitoshi kujenga hata lambo moja acha mbali mabwawa makubwa.

Mhehimiwa Naibu Spika, je, Wilaya ya Hanang imepewa fedha kiasi gani za kujenga malambo hasa ikizingatiwa kuwa ni moja ya wilaya yenye mifugo mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri aone umuhimu wa kusaidia wilaya ili kupunguza vifo vya ng'ombe au mifugo kwa ujumla na kuzuia uhamaji wa wafugaji kwenda maeneo ambayo ni tofauti na yale waliyozuia.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ombi ni kuwa Serikali iendelee kutoa ruzuku kwa dawa za kuongesha mifugo, *(Dips* – majosho), pamoja na zile za chanjo hususan *ECT, Foot and Mouth, CBPP* (Orkipyei), dawa ya ndigana kali, ndorobo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu Makadirio ya Matumizi ya ofisi yake, alikiri kuwepo kwa tatizo la ukame ambao siyo tu limesababisha njaa kali katika baadhi ya mikoa ikiwemo Mkoa wa Arusha Wilaya za

Longido, Ngorongoro na Monduli, lakini pia imeua mifugo katika maeneo hayo kwa asilimia zaidi ya 80.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji wa maeneo hayo wanategemea mifugo kwa kipato na chakula kwa asilimia mia moja. Waziri Mkuu kwa kutambua athari hiyo kwa wafugaji alisema Serikali italifanyia kazi suala hilo ili ione namna ambavyo Serikali itasaidia wafugaji hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara yenye dhamana ya mifugo itoe mapendekezo kwa Waziri Mkuu ya namna ya kuwasaidia wafugaji walioathirika na ukame ikiwa ni pamoja na kununua mifugo na kuwapa *restocking*.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Mifugo na Uvuvi pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kuwasilisha hotuba yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa Tanzania ni nchi ya pili kwa kuwa na wingi wa mifugo katika Bara la Afrika lakini bado mchango wa mifugo ni mdogo sana katika Pato la Taifa. Serikali inasema nini kuhusu hali hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya mifugo ina matatizo mengi ikiwa ni pamoja na mfumo mzima wa ufugaji pamoja na mipango bora itakayoleta mahusiano mazuri baina ya wafugaji na wakulima. Kuna migogoro baina ya wakulima na wafugaji hasa katika maeneo ya malisho jambo linalopelekea mapigano na hata kusababisha watu kufa au kuumizana vibaya sana. Serikali ina mipango gani ya uhakika kuondoa tatizo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, kila unapotokea ukame mifugo mingi hupoteza maisha kwa kukosa malisho pamoja na maji ya kutosha jambo linalowafanya wafugaji kuhama kama kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine na hivyo kusababisha mapambano baina ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji wapatiwe elimu kuhusu ufugaji bora na wenye tija badala ya kuwaachia wafugaji wakikusanya ng'ombe wengi lakini wanashindwa hata kupata makazi bora yaani kujenga nyumba bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ihamasishe viwanda vya kusindika ngozi ili ngozi zisiuzwe kama malighafi jambo ambalo linalikosesha Taifa pato kubwa pamoja na wafugaji wenyewe. Tukiwa na viwanda vya kutengeneza viatu vya kutosha tutaingiza pato kubwa la ndani hasa viatu vikiuzwa kwa wanafunzi mashuleni na katika vyuo vikuu, watumishi katika sekta mbalimbali za Serikali na za watu binafsi, askari na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ihamasishe wananchi kutumia maziwa, nyama, samaki na vitu vingine vitokanavyo na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, samaki katika bahari yetu ni wengi lakini bado hakuna mipango madhubuti ya kuvuna mazao ya baharini hasa hao samaki ambao wananufaisha zaidi watu wa nje kuliko sisi wenyewe.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza Bajeti nzuri ya Wizara hii. Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara hii. Pia nampongeza Naibu Waziri kwa kujibu maswali vizuri hapa Bungeni. Pongezi zangu pia zimuendee Katibu Mkuu wa Wizara hii yeye binafsi na watendaji wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nigusie machache. Kwanza ni kuhusu chanjo za mifugo, Serikali ianzishe kitengo maalum katika Wizara cha chanjo za mifugo kama ilivyo katika Wizara ya Afya. Pia chanjo ya ugonjwa wa miguu na midomo ya ng'ombe, mbuzi na kondoo. Chanjo hii ni ghali sana na inapatikana nje ya nchi. Kwa Karagwe chanjo hii imefikia shilingi 2,000/=. Nashauri chanjo hii itengenezwe hapa hapa nchini na itolewe bure au ikiuzwa isizidi shilingi mia moja. Mifugo yetu ikichanjwa bure wafugaji wengi watachanja mifugo yao na kuwezesha mifugo yetu ikubalike katika soko la nje. Hili eneo la chanjo ni muhimu sana. Pia chanjo zote zitolewe bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa kutoa ruzuku dawa ya kuoshea mifugo, tatizo dawa hizi hazikuwafikia wafugaji wengi hasa walioko vijijini. Naomba Serikali iliangalie suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda cha kusindika nyama, Serikali imekuwa ikiahidi kujenga kiwanda cha kusindika nyama mkoani Kagera. Je, ni kwa nini kiwanda hicho hakijajengwa. Ninaomba kijengwe haraka ili kisaidie kutoa soko zuri la mifugo ya Mkoa wa Kagera na mikoa jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhamasishaji ndiyo njia pekee ya kuongeza uzalishaji wa mifugo iliyo bora, Serikali imelihamasisha vizuri lakini bado halijafanikiwa vizuri. Tatizo mojawapo ni kwamba mbegu za *NIC Arusha* hazina nguvu *(fertility rate)* iko chini kati ya 40% - 60%. Hivyo mifugo inapopandishwa kwa mbegu za *NIC Arusha* matokeo ni mabaya sana. Wananchi wangu wanahangaika kwenda Uganda na Kenya kutafuta mbegu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maeneo ya malisho katika Ranchi ya Kitengule. Ranchi ya Kitengule iliyoko Wilayani Karagwe iligaiwa kwa wafugaji wadogo wadogo na kampuni ya *Kagera Sugar*. Baadhi ya wananchi waliopewa maeneo hayo hawana mifugo bali wanakodisha maeneo hayo kwa wahamiaji haramu kutoka nje ambao ndio wanaolisha mifugo yao humo. Vile vile kampuni ya *Kagera Sugar* ilipewa eneo kubwa sana ambalo hawalitumii kwa kilimo cha miwa wala ufugaji. Tatizo la maeneo ya malisho Wilayani Karagwe ni kubwa sana. Je, ni kwa nini Serikali isimege maeneo waliyopewa kampuni ya *Kagera Sugar* na kuwapatia wananchi wanaohitaji ardhi ya malisho. Pia nashauri wale wanaokodisha ardhi kwa watu toka nje ya nchi wanyang'anywe na kuwapatia wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nakushukuru sana na naunga mkono hoja.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Dr. John Magufuli, Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi/ushauri, kiwanda cha kusindika mazima cha Mkoani Tabora katika Manispaa ya Tabora kuna kiwanda ambacho kinafanya kazi hiyo kwa mazingira magumu sana, kwani uwezo nao ni mdogo. Hivyo basi, ningeshauri wawekezaji wa kizalendo wapewe mikopo ili angalau waweze kuinua kipato cha wafugaji wa Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo pia ningeomba elimu itolewe zaidi kwa wafugaji wajue umuhimu wa kuuza maziwa bora kwenye viwanda hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, itolewe elimu kwa utunzaji wa ngozi bora kwani kumekuwa na mifugo mingi ambayo kuna alama za uharibifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuongeza majosho na malambo kwa Mkoa wa Tabora, kwani kuna mifugo mingi na wafugaji wengi wamehamia kwenye maeneo yenye malisho mengi ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vitendea kazi, maafisa mifugo wakopeshwe vitendea kazi kama vile pikipiki ili angalau waweze kufikia maeneo mengi hapa nchini kwani jiografia ya Tanzania, kata zetu ziko mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa wataalamu ni mkubwa, wapewe motisha ya kazi hasa ambao wako pembezoni ya wilaya pia nyumba bora. Hawana ofisi za uhakika na kama zipo haziridhishi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la uvuvi, bwawa la Igombe lipatiwe mbegu bora ya samaki, angalau tupate kitoweo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tabora, ipewe maabara ya mifugo kama nilivyotangulia kuomba kwamba nayo ina mifugo mingi (Zahanati za Mifugo).

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU**: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja *good job*. Hongera.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa hotuba nzuri ya bajeti walivyoiandaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo nina maoni au ushauri kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuwe na programu maalum itakayohusisha usimamizi na ukopeshaji wa zana za uvuvi kwa Wavuvi wetu kama Boti, Nyavu na zana zingine zihusuzo uvuvi wa kisasa.

Pili, Ukanda wa Pwani kama (Dar es Salaam, Pwani, Mtwara, Lindi, Bagamoyo na Tanga) ziwe na utaratibu maalum wa kuboresha, kuwezesha miradi ya Wavuvi wadogo wadogo wa uvuaji wa mazao ya baharini yakiwemo kamba koche (*prowns*) na uhifadhi wa mazalia yake. Kwa sababu hiyo itasadia kuboresha maisha ya Wavuvi walioko ukanda wa Pwani.

Tatu, kuwe na Boti za doria ili kudhibiti uvuvi haramu.

Nne, Serikali iwekeze au itafute mwekezaji wa kuanzisha Viwanda vya Ngozi hapa nchini ili ngozi zetu ziongezewe thamani na kuweza kuboresha maisha ya wafugaji.

Tano, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Ushirika zifanye jitihada mahususi za kuanzisha *SACCOS* za uvuvi ili ziweze kupata mikopo kwa urahisi.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara chini ya usimamizi wa Waziri na Naibu Waziri wake na Watendaji wake wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili mifugo yetu iwe bora kunahitajika elimu ya uhakika ya ufugaji na miundo mbinu yake. Je, Wizara ina maelezo gani kwa maeneo ambayo walipeleka ng’ombe waliotoka Ihefu na maeneo hayo hayakuwa na miundombinu ya mifugo, mfano malambo hususan kwa Mkoa wa Pwani.

Je, Wizara ina mkakati gani wa kutoa mikopo kwa vikundi vidogo vidogo vya uvuvi hususanikwa akinamama? Vile vile, wanatoa msaada gani kwa wavuvi wana Mwani.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba nipatiwe majibu na naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Dr. Magufuli kwa kuwahakikishia Umma wa Tanzania uwezo wake mkubwa katika uchapaji kazi. Dr. Magufuli kama mtoto wa Mfugaji na Mvuvi akishirikiana na timu yake wamefanya mengi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Naibu Waziri Dr. Wanyancha ambaye pia ni mtoto wa mfugaji, nampongeza Katibu Mkuu ambaye pia ni mtoto wa mfugaji na mvuvi. Nawapongeza Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, naomba nichangie eneo moja muhimu linalotatiza wafugaji wa Wilaya ya Rorya na Wafugaji wa Mkoa wa Mara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Rorya ina jumla ya Ng'ombe 223,839, Mbuzi 145,883 na Kondoo 48,586 ikiwa ni jumla ya Mifugo 418,308. Ng'ombe wanapelekwa Kenya kwa njia ya wizi na minada kwa kuwa upande wa Kenya kuna Viwanda na machinjio karibu na mpaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kutoa maoni au nashauri Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu watoto wa wafugaji waanze mchakato wa kujenga Kiwanda cha Nyama, Mkoa wa Mara hususan Rorya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu nzima ya Wakurugenzi kwa maandalizi mazuri ya bajeti ambayo imefafanua vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, utendaji wa Waziri kwa kipindi chote ambacho Waziri ameonyesha kujali wafugaji sekta ambayo imekuwa nyuma kwa muda mrefu. Kazi nzuri ni suala la kuwakumbuka wafugaji katika suala la uchimbaji wa malambo kwenye maeneo ya wafugaji suala hilo limewapa faraja kubwa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kupatiwa madawa ya ruzuku limeonyesha usikivu mkubwa wa Serikali kuwaona wafugaji kuwa ni wahusika wakuu katika ukuzaji wa uchumi nchini. Ombi langu kwa Serikali, iongeze ruzuku zaidi kwa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zinazotakiwa zifanyiwe kazi ni masoko ya mazao ya mifugo. Juhudi zimeonyeshwa kwa Serikali kuanza ujenzi wa machinjio kubwa na ya kisasa eneo la Ruvu. Niishukuru Serikali bajeti ya mwaka jana ilitenga shilingi bilioni tatu, mwaka huu katika bajeti hii kuna shilingi bilioni mbili, jambo ambalo linatia shaka ujenzi unaoendelea hasa ukizingatia mikataba ambayo kampuni ya Ranchi za Taifa na JKT na kushuhudiwa na Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Mifugo na kushuhudia uwekaji wa jiwe la msingi ambalo Mheshimiwa Rais alitoa ushauri mbalimbali na kuahidi kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali ikumbuke kutokamilisha ujenzi huo kwa kuzingatia mikataba, hasara kubwa itajitokeza ikiwemo vifaa kupanda bei na mambo mengine. Natoa ombi kwa Serikali, iangalie sana katika bejeti ili ujenzi huo ukamilike ndani ya wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi katika Wizara hii imeonekana hasa katika juhudi za uvuvi na mfano tumeona jinsi udhibiti wa maliasili ukisimamiwa pato la Taifa litaongezeka toka sekta ya uvuvi. Kwa hiyo, Serikali iongeze msukumo katika sekta hii ikiwa ni pamoja na kutoa mikopo kwa wavuvi wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika,niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Tanzania inayo mifugo mingi Ng'ombe, Mbuzi, Kondoo. Miundo mbinu ya Minada, Majosho na Malambo si ya kutosha ukilinganisha na wingi wa mifugo hiyo. Malisho ili kupata mifugo bora nayo ni matatizo.

- Je, Wizara ina mpango gani wa kupiga marufuku uuzwaji wa mifugo kwa bei ya ulanguzi na haraka sana mifugo iuzwe kwa kilo. Iwekwe mizani kila mnada ili mifugo iuzwe kwa thamani halisi

- Uchimbaji wa Malambo ya kupata maji ya mifugo ningependekeza ifanywe pia na Wizara ya Mifugo badala ya kuachia kwenye Wizara zingine.

- Je, Sheria ya Mifugo iliyotungwa na Bunge hivi majuzi imeshafasiriwa kwa lugha ya Kiswahili?

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio makubwa ambayo yanaonekana katika takwimu hakipaswi kutazamwa kama ndio hali ilivyo, taarifa na takwimu na hali ilivyo ipo tofauti kubwa hata hayo mafanikio hayaonekani kwa maana hali za wafugaji na wavuvi nchini hazijabadilika wala hizo rasilimali hazijabadilika, hali zao za maisha ni duni na wameendelea kubaki kuwa maskini au walalamikaji wakubwa, dhuluma na unyanyasaji kwa wafugaji na wavuvi bado unaendelea bila kujali kilio cha wafugaji na wavuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wavuvi ambao wananunua nyavu katika maduka, nyavu ambazo hawatengenezi wao wanachomewa kila siku kwa sababu ni maskini, nyavu zilizokamatwa kiwandani kwa matajiri hatujaona zinachomwa hadharani kama Wizara inavyofanya kwa watu maskini. Hakuna udhibiti wa uingizaji wa nyavu nchini, anaadhibiwa mvuvi maskini, lazima jitihada zifanyike katika eneo hili. Aidha, hakuna mpango wa kuwasaidia wavuvi wa Ziwa Tanganyika na hususan Mkoa wa Rukwa kama jinsi Wizara inavyoimarisha na kuendeleza uvuvi katika Bahari. Ziwa Tanganyika lina kina kirefu, wanahitaji zana bora na za kisasa zaidi, Wizara ina mpango gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji wengi waliathirika na *operation* mbalimbali nchini, Tume nyingi zimeundwa taarifa zake zimekua siri kubwa, lakini wafugaji hawa wamepoteza mali na mifugo yao, Serikali imekaa kimya haitaki kusema kama wafugaji hawa watalipwa hasara waliyopata au laa! Kimsingi wafugaji hawa walipoingia katika maeneo mbalimbali walikuwa wanaonekana na hakukuwa na hatua za kuwazuia na wakati wote walipata vibali toka kwa Watendaji wa Serikali hii hii ya CCM, leo

wanaadhibiwa wao badala ya Watendaji walioruhusu watu hawa wafugaji kuwepo katika maeneo hayo.

Hii ni dhahiri mfumo wa Serikali hii umekufa wanashindwa kusimamia Sheria na maagizo mbalimbali matokeo yake wanawatesa wananchi wafugaji katika nchi yao. Wafugaji walipwe haki zao mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, aliye na macho haambiwi ona. Napongeza juhudi kubwa zilizofanywa na Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wote kwa kazi nzuri inayofanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uvuvi haramu, juhudi zimeanza kuonyesha mafanikio, Samaki wameanza kuongezeka na wananchi wenyewe wameanza kuwa askari wa kulinda maeneo yao ili yasiathirike na uvuvi haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo yameanza kuonekana katika ongezeko la Viwanda vya Maziwa na ongezeko la unywaji wa maziwa ni dhahiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza juhudi hizi zote kwa sababu nchi yetu inaweza kuendelea na kupata mapato makubwa ya Serikali na kufuta umaskini nchini kama rasilimali ya mifugo uvuvi na mazao yake yangetumiwa vizuri. Ziko nchi ambazo uchumi wao unategemea mifugo tu, sisi tuna kila kitu. Tanzania imebarikiwa sana. Endeleeni na kazi vizuri na mbarikiwe sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba, uvuvi wa kwenye Maziwa utiliwe maanani kama Ziwa Nyasa, Mto Ruaha, Mtera Dam kama utaratibu wa Uvuvi wa Baharini. Aidha, maeneo ya uvuvi mengine yaanzishwe na kutunzwa kama eneo la Ipogoro, Iringa Mto Ruaha, the Little Ruaha na Mto Ruhuhu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mifugo. Ufugaji wa kuku wa kienyeji utiliwe mkazo kwa kutoa dawa ya chanjo ya kuku na elimu kwani gharama yake ni ndogo. Aidha, ufugaji wa *Zero Grazing* ufikiriwe zaidi na kutolewa maelekezo.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kukupongeza wewe mwenyewe kwa kazi kubwa ya kuliongoza Bunge.

Pili, napenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dr. Jakaya Kikwete kwa kuwapatia wana Mbinga Wilaya mpya ya Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue pia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri John Pombe Magufuli na Naibu wake Mheshimiwa James Wanyancha kwa kazi nzuri na hususani katika maendeleo ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya mpya ya Ziwa Nyasa ni miongoni mwa Wilaya ambazo wakazi wake ni maskini sana kwani sehemu kubwa ya watu waishio huko hutegemea mazao ya majini tu kama vile Samaki na Dagaa. Kugawika kwa Wilaya hiyo ni mtego mkubwa kwenu kwani hakuna *income* nyingine zaidi ya mazao ya Ziwa hilo na Kahawa kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo imejitokeza katika mwelekeo wa Ilani upande wa Zanzibar, ni vema ijitokeze wazi jinsi ambavyo Wizara yako itawasaidia wavuvi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Wakulima wanapata ruzuku ya mbolea, kwani kuna kigugumizi gani kutoa ruzuku ya maboti katika Ziwa hilo? Wiki iliyopita kulikuwa na dhoruba na mtu akafa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha Maboti yale ya dawa, wavuvi wa Ziwa Nyasa hawatafaidika kama hakutakuwa na *deliberative efforts* za kuwasaidia. Leo sitawaunga mkono kwa kuchangia kwa kusema kwa vile nina kikao cha Chama (CCM). Hata hivyo, juhudi zenu zimetambuliwa na Mungu awabariki na awarudishe tena. Pongezi pia kwa Watendaji wenu hususan Katibu Mkuu na wenzake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi Dr. John Pombe Magufuli kwa hotuba yake nzuri na endelevu. Pia nampongeza sana Mhe. Dr. Wanyancha kwa jinsi alivyo mchapa kazi akisaidiana na Waziri wake pamoja na Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ninayochangia ni juu ya ufufuaji wa Viwanda vya Ngozi, Kiwanda cha Nozi cha Moshi kilichobinafsishwa bado matumizi yake ni kidogo sana. Natoa ushauri kuwa Kiwanda hicho kingeboreshwa sana ikiwezekana kipelekwe kwenye maeneo ya mifugo kama vile Mwanza, Shinyanga, Rukwa, Iringa au Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na kupongeza sana kwa Wizara yako kwa kutupatia majosho na malambo kwenye Jimbo la Njombe Magharibi. Majosho hayo ni Kanamalenga, Mpululu, Visuka, Mambegu na Saji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile machinjio ya kisasa ya Ilembula nayo nakupongeza sana. Ombi, tunaomba gari la kubebea nyama kutoka machinjio hayo ya kisasa hadi Kwamalaji pale Ilembula mjini machinjio yako umbali wa kilomita tatu hivi. Pia machinjio hayo hakuna maji na umeme.

Umoja wa Wenyebucha wanaomba wawekewe umeme, maji na gari la kisasa ili kulinda usalama wa walaji, mpaka sasa vifaa vinavyotumika ni mikokoteni michakavu na haina ubora kabisa. Tunaomba Wizara yako ishirikiane na Halmashauri ya Njombe sasa Halmashauri ya Wanging'ombe, Umoja huo uko Ilembula.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi zingine kwa kiwanda cha machinjio cha Ruvu kuanzishwa kitasaidia sana wafugaji kupata mapato mazuri kwa Serikali na wafugaji.

Mwisho, nashauri vyuo vya Mifugo na Semina mbalimbali zitiliwe mkazo wa kutosha. Tukiwa na wataalam wengi wafugaji watafuga kwa faida na kuongeza pato la Taifa.

**MHE. RAJAB HAMAD JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa hotuba yake nzuri aliyoiwasilisha hapa Bungeni leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipochangia hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira juu ya suala la *MACEMP* kuwa haitoi nyavu za kutosha kwa wavuvi wanaobahatika kupata nyavu. Aidha, maboti wanayopewa ni mepesi hayahimili uvuvi wa bahari ya mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Kilimo ya Zanzibar wafanye mapitio ya mafanikio na matatizo ya mradi wa *MACEMP* na wawashirikishe viongozi wataalam wa Uvuvi na Mazingira. Mradi wa *MACEMP* kwa Zanzibar umetoa vifaa vingi lakini vinalalamikiwa kwa mapungufu yake ya kutokuwa bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa bajeti nzuri na kuiwasilisha vilivyo. Lakini zaidi nawapongeza kwa utendaji wao mzuri katika kuendesha Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu samaki Dar es Salaam. Ni matokeo ya sisi wananchi kutojibidiisha kwani kuna shida ya Samaki na wakipatikana ni wa ghali kupindukia, hii ni kwas ababu, pamoja na kuwa na bahari hatujibidiishi kuvuna Samaki wa kutumia sisi hata kuuza nje. Nashauri Serikali iweke msukumo kuwahamasisha wananchi kujihusisha na uvuvi wa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu dawa za Mifugo. Dawa hizi ni za ghali sana na hasa chanjo. Serikali iangalie njia ya kuongeza msaada. Kuna dawa zinazosambazwa na wakati mwingine siyo *"very effective"'* hasa zile za kuosha. Tunaomba Serikali iongeze ufuatiliaji.

**MHE. SAMUEL M. CHITALILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri na Naibu kwa kuandaa hotuba nzuri na yenye kukidhi mahitaji ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo nina ushauri kama ifuatavyo:-

Kwanza, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii ya kuhakikisha uvuvi haramu unakomeshwa hasa kwa kuwasaka wavuvi haramu wanaovua kwa sumu na nyavu haramu, kwa kuwa wanaolengwa ni watu wenye mitaji midogo midogo walio na uwezo wa kununua nyavu moja moja tu au kokoro moja watu hawa hunyang'anywa nyavu na kuziteketeza, kwanini wasiwe wanafuatiliwa matajiri wakubwa wanaoagiza toka nje?

Pili, pia mradi huu wa kusaka nyavu haramu maeneo mengi imekuwa ni miradi ya baadhi ya Maafisa Uvuvi hasa wale wa Kata kwa kushirikiana na Maafisa Uvuvi wa Wilaya, wanakubaliana na wenye nyavu haramu, wanawaruhusu kufanya kazi hiyo kwa makubaliano ya posho, hiyo yote inakuwa rushwa. Je, hili Wizara inalifahamu au na kama linafahamika linashughulikiwaje?

Tatu, kwa nini Boti za uvuvi haziruhusiwi kufanya shughuli ya uvuvi katika Ziwa Victoria? Kufanya hivi kunaendeleza uvuvi ambao ni wa kienyeji sana na hivyo wavuvi kwa kuwa wanavua Samaki kwa kutumia mitumbwi ambayo haiwezi kwenda mbali sana husababisha kufanya kazi ya uvuvi katika maeneo yale yale kila siku na hii husababisha samaki kuhama.

Nne, kuna Samaki aina ya Njegere ametoweka kabisa katika Ziwa Victoria. Je, kuna jitihada ipi ya kuhakikisha samaki aina hii anapatikana tena katika Ziwa Victoria?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ametueleza kwamba Serikali inajenga Machinjio ya Ng'ombe eneo la Ruvu, Mkoa wa Pwani. Aidha, machinjio kama haya yamejengwa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba ujenzi wa Viwanda vya nyama na machinjio ni kichocheo kikubwa kwa wafugaji kuweza kuzalisha zaidi, lakini pia kuwaletea urahisi wafugaji kuweza kuvuna mifugo yao na kuifikisha kwenye viwanda pasipo na gharama kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuona kwamba machinjio yanayojengwa na viwanda vilivyopo vimejengwa katika maeneo ambayo idadi ya mifugo sio kubwa

ukilinganisha na maeneo mengine.  Sote tunafahamu kwamba idadi kubwa ya ng'ombe ipo katika maeneo ya Mikoa ya Kanda ya Ziwa, Arusha na Manyara.  Lakini la kusikitisha ni kwamba, maeneo hayo hayana machinjio ya kisasa ya kuweza kuhudumia wafugaji wa maeneo hayo.  Aidha, viwanda vya kusindika maziwa navyo ni vichache mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ituarifu ni lini Serikali itajenga viwanda vya kutosha vya kusindika maziwa na machinjio ya kisasa yenye uwezo wa kusindika nyama.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika,nampongeza Mheshimiwa Dr. John Pombe Magufuli, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Mheshimiwa Dr. James Mnanka Wanyancha, Naibu Waziri; Katibu Mkuu wa Wizara na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri ya kuandaa bajeti hii ya 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo maeneo kadhaa ya kutoa mchango ili kuboresha utendaji wa Wizara hii. Maeneo hayo ni haya yafuatayo:-

Kwanza, Wataalam wa Mifugo, (ufugaji), uvuvi bado hawatoshelezi kwa kuwa sasa tunatoka katika ufugaji wa kizamani kwenda ufugaji wa kisasa, hivyo Wataalam wa Sekta hii (*Extention Officers*) wanahitajika wa kutosha kwa kutoa elimu kwa wafugaji na wavuvi ili waendane na dhana ya mabadiliko ili kufanya shughuli zao kwa tija, wafugaji na wakulima wa Iramba Magharibi wanategemeana hivyo katika kuwatengea maeneo wakulima ni vema pia wafugaji wakipewa maeneo, mfano mzuri kama inavyotenganishwa kwa maeneo ya Iramba Magharibi yale ya hifadhi (Ndobido), mashamba ya wakulima na maeneo maalum ya malisho ya wanyama.

Pili, kuhusu uvuvi.  Sekta hii ni muhimu sana kwa kuongeza pato la Taifa, uvuvi holela unanyima mapato Taifa. Ziwa Kitangiri bado kuna uvuvi haramu, kwa kutumia makokolo, ukataji wa makuruili  na kutumia mabomu.  Udhibiti kwa kuwa na doria katika kudhibiti hali ya uharibifu wa mazalio na kuvua samaki wachanga haupo, ahadi ya Serikali kuleta boti la Doria hadi sasa bado hawaoni umuhimu.  Naomba Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho atoe ufafanuzi juu ya kuboresha uvuvi na hasa hatua za kumlinda mvuvi wa Ziwa Kitangiri.

Tatu, ujenzi wa nyumba za Maafisa Samaki na Kituo cha Wavuvi, pamoja na ahadi ya Serikali juu ya kutekeleza ujenzi wa nyumba za Maafisa Uvuvi Kitangiri, inasikitisha hatua hiyo hadi sasa haijafanyika bado, naomba Serikali kuona umuhimu wa kukamilisha hatua hiyo ili kuondoa adha kwa jamii ya wavuvi wa Ziwa Kitangiri.

Nne, kuhusu ujenzi na uboreshaji wa Minada.  Wizara ione umuhimu wa kujenga mnada wa Malendi uliopo Kata ya Shelui, nyumba ya Afisa Mifugo wa Mtekente, kadhalika kuboresha maboma ya kuhifadhia ng'ombe, mbuzi na kondoo katika minada yote ya Iramba Magharibi ili kuondoa uholela wa mifugo kusambaa hovyo kabla ya kunadiwa kwa wanunuzi.

Tano, kuhusiana na ufugaji kuku. Elimu itolewe katika kuongeza tija ya ufugaji kuku wa kienyeji kisasa kuondoa hatua ya kuwa na kuku wa kienyeji huria wanaojitafutia chakula bila udhibiti. Dawa za chanjo kwa ugonjwa wa kideli na kadhalika, ni muhimu ili wafugaji kuongeza pato kwani bei ya kuku inaongezeka siku hadi siku hivyo ukiwezeshwa ufugaji makini na wa kisasa idadi ya pato litaongezeka.

Sita, Kiwanda cha Ukataji Nyama. Naomba Serikali kutafuta mwekezaji ili kuanzisha kiwanda cha ukataji nyama Mkoani Singida. Kiwanda hiki kitasaidia mfugaji kuuza mifugo kwa bei nzuri na kuepuka usafirishaji kwa umbali mrefu kutafuta soko na hivyo kuingia gharama kubwa na mnyama kupunguza kilo nyingi kwa umbali wa safari. Saba, ni kuhusu ng'ombe wa kisasa. Bado mbegu ya ng'ombe wa kisasa haijaenea katika Jimbo la Iramba Magharibi. Naomba Serikali itoe kipaumbele ili kuwa na ng'ombe wa kisasa Iramba Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kituo cha Maksai kilichopo Mkulu naomba kiwezeshwe vya kutosha ili kuendelea kutoa mafunzo kwa wananchi katika maandalizi ya wanyama kazi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majosho ya kuogeshea mifugo yajengwe kila kijiji ili kuondoa misongamano kwa eneo linalojumuisha zaidi ya vijiji vitano hadi kumi kutumia josho moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza Wizara kwa kazi nzuri na kwa ubunifu. Ni muhimu sana kulinda haki za wakulima na wafugaji kwa kuendelea kugawa maeneo ya shughuli zao ili kuepuka migogoro kati yao kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dokta Magufuli (Mb), Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, hongera kwa kupata Mikoa, mawasilisho ya hotuba yako na uchapakazi wako. Ombi langu ni kutaka msiondoe shilingi, niambieni nitapata wapi majogoo ya kisasa? Wananchi wangu wameathirika sana na *HIV/AIDS,* sasa wataka kuanzisha miradi yao ya kufuga kuku kwa ajili ya kupata lishe na mbolea ya kuku kwa ajili ya bustani za mboga na fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakieni mafanikio huko kwenye Majimbo yenu.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE – SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ninayokusudia kuchangia inaitwa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Ili Wizara hii ipate uhakika wa kuitwa ya Maendeleo ya Mifugo, ni lazima ijielekeze kufanya kazi kwa namna ambayo itawaondoa wafugaji kutoka hali yao ya sasa na kuwa wafugaji wenye tija zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kuwa ili kufikia ufugaji wenye tija zaidi zipo hatua za makusudi zinazotakiwa kuchukuliwa kwa haraka sana ambazo ni:-

(1) Kutenga na kulinda maeneo ya malisho yasivamiwe na shughuli nyingine kama vile kilimo, madini, uhifadhi wa wanyamapori na shughuli zingine zinazoathiri ufugaji. Hii ni pamoja na kumaliza mgogoro wa mpaka kati ya *Mkungunero Game Reserve* na Wilaya ya Simanjiro na Kiteto;

(2) Kwa kuwa wafugaji wengi wanaishi na kufuga katika maeneo ya nyanda kama zenye tatizo kubwa la maji, ni dhahiri Serikali inatakiwa kutenga fedha za kutosha kuchimba visima vya kina kirefu pamoja na kuchimba mabwawa. Hatua hii itazuia uhamaji wa mara kwa mara wakati wa kiangazi;

(3) Wizara ihakikishe inatenga fedha katika bajeti hii kwa ajili ya kutoa ruzuku ya chanjo ya *ECF, East Coast Fever* (Ndigana), hatua ambayo itajenga kinga kwa ndama watakaozaliwa katika msimu huu;

(4) Haiwezekani Serikali hii itoe ruzuku kwa athari za mtikisiko wa kiuchumi duniani na kwa majanga yatokanayo na mvua lakini ikakaa kimya kwa janga la ukame uliopelekea baadhi ya wafugaji (ambao ni wengi) kufikia umaskini uliotopea. Tunaomba kauli ya Waziri Mkuu ya Serikali kusaidia wafugaji walioathirika na janga la ukame sasa liwekwe katika utekelezaji;

(5) Serikali sasa itumie Ranchi za Taifa kutoa madume wa Mbegu walio bora kwa njia ya ruzuku ili kuleta mapinduzi katika sekta nzima ya ufugaji;

(6) Ifike sasa wakati ambapo Serikali yetu itamke na kuchukua hatua madhubuti za kushughulikia ustawi wa Watanzania wa Jamii ya Wafugaji kwa kuboresha miundombinu yake. Tumechoka na fedheha ya kuhamahama kufuata maji wakati tuna malisho ya kutosha isipokuwa maji;

(7) Ranchi ziwezeshwe kumudu changamoto hiyo ya kutoa madume bora;

(8) Wafugaji wanaoishi katika Mikoa ya Morogoro, Pwani, Iringa, Mbeya na Rukwa, sasa watengewe maeneo yao ya kudumu ili kuepusha migogoro kati yao na wakulima;

(9) Haieleweki ni kwa nini hadi sasa ng’ombe na mbuzi wauzwe kwa bei ya kukisia wakati nyama inauzwa kwa mizani; na

(10) Dawa ya kuogesha mifugo inayopata ruzuku sasa iwe ni pamoja na chanjo ya *ECF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Naibu Waziri na Maafisa wa Wizara kwa kuiongoza Wizara kwa ufanisi, utaalamu na ari ya hali ya juu. Mheshimiwa Magufuli ni mmojawapo wa MaWaziri wa Serikali ya Awamu ya

Nne, anayestahili pongezi za hali ya juu na ni mfano wa kuigwa kwa viongozi wote hususani MaWaziri. Ninamwombea Mungu ashinde Jimboni kwake na kurudi tena kipindi cha Awamu ya Tano kuongeza nguvu ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali kwa kupitia Wizara, wawasaidie wanawake kupata mafunzo ya ufugaji bora wa mifugo na kuwawezesha kuanzisha makundi ya wafugaji wa Kuku, Bata, Kanga, Sungura, Mbuzi, Ng'ombe na Samaki kibiashara zaidi kuliko ilivyo sasa. Wanawake wamekuwa wakinufaika sana na ufugaji lakini wanahitaji kujengewa uwezo wa kufanya hivyo kitaalam zaidi na kuongeza thamani kwa kusindika na kuuza bidhaa za ufugaji huo kwa tija zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili, napendekeza Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendelo ya Makazi, Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Jinsia, Maji na Umwagiliaji ili waweke mkakati wa pamoja kusaidia kina mama katika vijiji na mijini kwa kufanikisha suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE.CHARLES. N. MWERA**: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Watendaji wote wa Wizara, kwa hotuba nzuri, kwa namna ya pekee kabisa bila unafiki, nimshukuru sana na kumpongeza Waziri, kwa utendaji wake wa kazi, amekuwa mtendaji mzuri kwa kila Wizara aliyopangiwa. Namtakia kila la kheri na Mungu azidi kumpa hekima na busara. Natambua na Watanzania wenzangu kwa namna alivyoongoza Wizara ya Miundombinu na Wizara zingine kwa makini, hekima na busara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi, nimwombe Waziri na Serikali kutoa idadi ya mifugo hasa ng'ombe ambayo ni sahihi. Ninalisema hili kwa sababu kwa sasa katika Jimbo la Tarime, wananchi wangu wameibiwa ng'ombe wengi sana na kwenda nchi jirani ya Kenya. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Jeshi la Polisi ya kupambana na wezi wa mifugo, namwomba Waziri wa Mifugo na Waziri wa Mambo ya Ndani washirikiane ili mifugo ya wananchi isiishie Kenya. Kama leo atatoa idadi ya ng'ombe, ni vema Bunge na Watanzania wajue ni ng'ombe wangapi wameibiwa kutoka Tarime na kwenda nchi jirani ya Kenya?

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo (ng'ombe, mbuzi, kondoo, punda) wamekufa, baada ya kunywa maji yanayosemekana yana sumu katika Mto Tigite, sumu inayotoka katika Mgodi wa North Mara unaomilikiwa na kampuni ya Barrick. Wizara ya Mifugo ilichukua sampuli za damu na vipimo vingine kubaini nini tatizo la kufa ng'ombe, mbuzi, kondoo na punda. Namwomba Waziri anijulishe ni lini matokeo ya vipimo hivyo yatatolewa kwa wananchi na ni nini matokeo yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ina mpango wa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ili kupunguza vifo kwa mifugo ambayo ni rasilimali kubwa kwa wananchi. Katika maeneo ya vijijini, wagani ni wale wa fani ya ukulima *(Crops)*, Serikali ipeleke vijijini wataalamu wa mifugo *(Livestock)* ili waweze kufanya kazi kulingana na fani

husika na hao ambao wapo vijiji wachache kazi yao ni kukagua nyama buchani tu, ni vema wapewe majukumu yao ya kufanya ya kila siku. Mkurugenzi ahakikishe anafuatilia utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni ya muhimu sana, naishauri Serikali kuongeza bajeti ya kutosha. Naomba Serikali kusaidiana na mimi Mbunge kutafuta mwekezaji wa kujenga Kiwanda cha Nyama maana Wilaya ya Tarime na Mara kwa jumla, tuna idadi kubwa ya ng'ombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana, Mungu ibariki Tanzania.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo iliyohamishiwa kwenye Bonde la Songwe, imesababisha uharibifu mkubwa wa mazingira sehemu hiyo kwani Ziwa Rukwa limejaa matope kiasi cha kupungua kina, Ziwa limeendelea kukauka na ugomvi na mafarakano yasiyoisha kati ya wakulima na wafugaji. Je, Serikali haiwezi ikaisaidia Halmashauri ya Chunya kufanikisha uchimbaji wa marambo na majosho?

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwa maandishi hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara hii kwa kazi kubwa inayofanyika ya maendeleo ya mifugo na mvuvi, kwa kutoa elimu ufugaji na uvuvi lakini suala la uvuvi baada ya kuchoma nyenzo za uvuvi haramu, je, ni hatua gani zimechukuliwa kuwapatia nyavu zinazostahili ambazo haziharibu mazalia na mazingira?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Wizara hii imefanikiwa kukamata meli ambayo ilifanya uvuvi haramu na kugundua Serikali inakosa fedha nyingi kutokana na uvamizi huo. Sasa Serikali itoe ufafanuzi mpaka sasa imejipanga vipi? Inasemekana maeneo ya bahari ya Pemba maeneo ya mbali zinaonekana meli zinatia nanga kwa muda mrefu na ongezeko la meli za uvuvi zilizosajiliwa limepiga hatua kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya mifugo, naiomba Serikali ifuatilie kwa karibu majosho kwa sababu katika baadhi ya Halmashauri yamegeuka mapori. Ni majosho mazuri lakini hayafanyi kazi kwa kuwapatia ng'ombe dawa za majosho. Ni vema basi pamoja na kuwa Halmashauri zipo chini ya TAMISEMI, basi Wizara ifuatilie kwa karibu ili kuhakikisha inanusuru hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukielezwa katika Bunge hili kuwa ng'ombe na mifugo mengine haiopo kwenye kiwango kinachotakiwa kimataifa, je, kwa sasa hali ya mifugo ikoje ili nasi tuuze mifugo nje?

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naunga mkono hotuba hii. Napenda kuipongeza hotuba hii kwa maelezo yaliyojaa takwimu kwa

maana ya kujua tulikotoka, tulipo na tunaelekea au tumepiga hatua angalau kiasi gani ndani ya Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe hoja zangu kwanza, uchomaji wa mkokoro. Nampongeza sana sana Waziri kwa taratibu za uchomaji makokoro kwa sababu walikuwa tayari wamesababisha kupungua kwa samaki Ziwani na Baharini na kukosekana kwa samaki wakubwa majini. Swali la kujiuliza, je, nyavu hizi haramu zinapokamatwa kuna ufuatiliaji gani kuhakikisha kuwa hatapata tena popote nyavu hizi haramu toka viwanda au maduka yanayouza nyavu hizi?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, elimu endelevu kwa wavuvi na wafugaji, katika suala zima la wavuvi na wafugaji ndani ya jamii hizi mbili inahitajika sana. Inawezekana mvuvi huyu haelewi kabisa ni kwa nini nyavu zake zinakamatwa na baadaye kuchomwa moto. Ifike mahala Taifa ilipe kipaumbele suala hili katika mpango kazi wake kwamba tukielimisha jamii tutapunguza tatizo. Wafugaji pia wanahitaji elimu ya ufugaji bora, nini maana ya ufugaji bora? Lakini ufugaji uliopo sasa hauna tija yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Viwanda vya Maziwa, naishauri Serikali kuongeza kasi ya kuvifufua viwanda hivi vya maziwa. Inaposhauri ufugaji bora maana yake unamwandaa mfugaji huyu kupata mazao mengi na bora. Je, Serikali imejiandaa vipi kumpokea mfugaji huyu?

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa mchango wangu kuhusu Wizara hii ambayo imekuwa kero, je, ni kiwanda kipi ambacho kinatengeneza zana haramu za uvuvi? Je, Serikali pamoja na Wizara ina mikakati gani kudhibiti kiwanda hicho au kukifunga, ili wavuvi wakose mahali pa kununua zana hizo na wenyewe kutokana na umasikini watazinunua, mwenye kosa ni nani kiwanda au anayenunua?

Naomba ufafanuzi wa tatizo hili ambalo limekuwa kero katika Ziwa Victoria, wanatuuliza sisi wawakilishi tunakosa majibu. Je, ni kiwanda kipi kinachotengeneza zana halali ili tuelekeze wavuvi wetu pamoja na maduka ambayo yanauza zana hizo wakanunue ili waondokane na kukamatwa hovyo na kuchomewa zana zao na tupunguze uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo matatizo, kuna sehemu ambazo mifugo jadi yao kwa mfano Umasaini, Mkoani Kagera nilishalalamikia walioshika ardhi kubwa ya *Kitengure Ranch*, wanaojifanya wafugaji na uwezo wao ni mdogo sana na kwa kuwa tuna Kilimio Kwanza, je, ni kwa nini wasipuguziwe ardhi, tukawagawia wakulima kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kuliko kufuga majambazi? Je, Wizara ina mkakati gani kupunguza migogoro ya mara kwa mara? Pamoja na kila mtu kujua mipaka yake, mara kwa mara ya Wilaya ya Misenye wafugaji bado wananyanyasika sana, wananyang’anywa na wakulima, hawana sehemu za malisho, je, Wizara inawasaidiaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, Viwanda vya Maziwa vilivyo Mkoani Kagera hasa cha mifugo kilichoko Bukoba mjini, usindikaji wake unasuasua, je, Serikali inakisaidia vipi

ili wafugaji wa vijiji vilivyo karibu wapate pa kuuza maziwa yao? Kwa sasa wafugaji wanakosa pa kuuza maziwa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa mzima hatuna kiwanda hata kimoja cha nyama pamoja na machinjio ya kisasa pamoja na kiwanda cha nyama na wafugaji wapo. Pale mjini hatuna machinjio ya kisasa, je, tutapata lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kagera hasa Wilaya ambazo wana ng'ombe, mbuzi wengi hawana utaalamu wa kutengeneza ngozi pamoja na utunzaji wa ngozi. Kwa sasa kuna ufugaji wa Shamba Darasa bila kuwazungukia kuwapa utaalamu, hawataifadika na ufugaji wa Shamba Darasa ambao ni muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kuna viwanda vya samaki lakini sio vya kisasa, tunaomba tupate viwanda vya kisasa ili wavuvi wapate pa kupeleka samakio wao. Biashara ya mapanki imekuwa kero, hakuna sehemu ambayo ni safi, pawepo na kiwanda maalum, viwe na heshima maana sasa ubanikaji wake unakuwa ni uchafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ziwa Victoria ni lini tutakuwa na boti inayokaa hasa pale Bukoba, izunguke Kemondo hasa (Miaro) ya Uganda Rubafu ndiko wanakotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati tulitembelea Kigamboni, Jeshini wanatengeneza boti, je, Wizara inasemaje kuhusu hilo ili Mkoa huu uwe na boti yao ya kujitegemea?

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru viongozi BIEMU, kwa kazi nzuri wanayoifanya, je, Wizara pamoja na Serikali mnawasaidiaje kuwapa nguvu wanaojitosa kupambana na wavuvi haramu? Kuna vijana wa Miharo ya Kifungwa Kastamu, wakiongozwa na kijana mmoja Joramu anayepambana sana, naomba wakubukwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji ufugaji wa samaki, elimu itolewe hasa Mkoani Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndio mchango wangu, naomba nijibiwe, naomba kuwasilisha.

**MHE. BRIG. JEN. HASSAN A. NGWILIZI**: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba yako inajibu hoja zote nilizokuwa nazo. Hata hivyo, bado ipo haja ya kuongeza juhudi katika udhibiti wa nchi zinazoendesha uvuvi haramu katika eneo la Bahari ya Tanzania *(EEZ)*. Katika kulitekeleza hili, JWTZ lihusishwe zaidi katika doria na ukamataji wa meli za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hongera sana, naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii, kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dr. John Pombe Magufuli (Mb), Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha (Mb), Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii ambayo imeonyesha kuongezeka kwa kiwango kikubwa ukusanyaji wa mapato kupitia vyanzo mbalimbali ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiofichika kuwa Mheshimiwa Dr. Magufuli, ameonyesha umakini wa juu katika kuchapa kazi, akishirikiana na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Wanyancha kwani Wizara hii sasa iko juu kuliko miaka iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi kwa zana zisizotakiwa, ninaipongeza sana Serikali kwa kuwa makini katika kuwagundua wavuvi wanaovua samaki kwa kutumia nyavu zisizostahili mfano Makorokoro kwani Serikali huzikamata na kuzichoma moto kukomesha tabia hiyo. Naomba pamoja na kuchoma moto nyavu hizo, ni vema Serikali ingetoa elimu kwa wavuvi hao ili kupata zana sahihi kwa uvuvi ili kulinda samaki wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kutoa ushauri kwa wafugaji kupunguza mifugo yao ili waweze kuwa na mifugo michache watakayoweza kuwapa malisho vizuri pamoja huduma zote muhimu mpango ambao ukifuatwa, wafugaji watakuwa na mifugo yenye afya safi na uzito ambao utampa bei nzuri mnyama huyo. Ni vema soko lenye tija la kuuza wanyama hao mfano ng'ombe, kondoo, mbuzi n.k. Ni vema uuzaji wa mifugo itumike mizani ili mfugaji asipunjike na wawepo Mabwana Mifugo kwa kila Kata kutoa elimu ya ufugaji bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu kuwa katika Mikoa mitano ya kwanza yenye mifugo mingi ni pamoja na Mkoa wa Singida ingawa Mkoa una mifugo mingi lakini bado Manispaa ya Singida haina machinjio ya kisasa. Kutokana na Maamuzi ya Kikao cha Ushauri cha Mkoa *(RCC)* chini ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Parseko Konne, kiliagiza Manispaa ya Singida kuwa na machinjio ya kisasa. Kupitia maamuzi haya, tayari Baraza la Madiwani walishafanya ziara kwenye Mikoa jirani yenye machinjio ya kisasa kuona ama kujifunza jinsi ya kujenga machinjio ya kisasa Manispaa ya Singida. Ninapenda kujua kama Serikali itakuwa tayari kuunga mkono mpango huu wa ujenzi wa machinjio ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufugaji wa kuku Singida, vile vile nitakuwa mchoyo wa fadhila kwa wananchi wa Singida, kwa kazi kubwa wanayofanya kuzalisha kuku wengi wa asili na kulisha kuku hao Mikoa mingi nchini hususani Dar es Salaam. Ninaiomba Serikali kutoa elimu zaidi ili uzalishaji uongezeke na kuboresha afya za kuku hao kwa lengo la kuongeza pato la wafugaji wa kuku. Ninaiomba Serikali kutoa agizo kwa Halmashauri za Mkoa wa Singida kuweka kumbukumbu ya takwimu za uuzaji wa kuku hata mifugo yote kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo kupitishwa kwenye barabara, bado kuna wafanyabiashara bahili ambao hupitisha ng'ombe zao kwa miguu kuwapeleka Dar es Salaam kwa kutumia barabara na kuharibu barabara. Ninaomba Serikali itoe adhabu kali kwa yeyote anayepatikana na kosa hili la kupitisha ng'ombe kwa miguu barabarani na kusababisha uharibifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimalizie mchango wangu kwa kuiomba Serikali kuhakikisha kila Kijiji kina maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya wafugaji kuchungia mifugo yao ili kuondokana tabia ya mifugo kuharibu mashamba yenye mimea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kwa pongezi kubwa kwa Serikali kwa kuinua pato la Taifa kupitia mifugo na samaki. Ninaiomba Serikali kuajiri Bwana Samaki ili kusaidia kupandikiza samaki wa aina mbalimbali katika maziwa yaliyopo Singida mfano Ziwa Kitangiri, Kindai, Singida Mjini n.k. ili wananchi wa Singida wapate kitoweo cha samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimalizie kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia nikitegemea kuwa hoja zangu zitajibiwa ili nisimsumbue Waziri wakati wa vifungu.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Dr. John Pombe Magufuli (Mb), Mheshimiwa Dr. Wanyancha (Mb), Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara, kwa hotuba nzuri na kutekeleza vema majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma kulikuwa na mpango wa kuuza mifugo na mazao yake katika Soko la Kimataifa baada ya kuboresha afya za mifugo yetu. Uboreshaji wa afya ya mifugo ulilenga kuanzisha Ukanda usio na Maradhi ya Mifugo yaani *Disease Free Zone (DFZ).* Je, mpango huu mzuri uliishia wapi hasa ukizingatia ujenzi wa machinjio mapya ya kisasa yanayoendelea kujengwa nchini?

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nitoe pongezi nyingi sana kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, na Maofisa wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya ufugaji ni muhimu sana kwa jamii ila pamoja na mafanikio mengi, yapo matatizo mengi yanayowakatisha tama wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa kutujengea Kiwanda cha Machinjio ya Nyama katika Wilaya ya Bagamoyo, pia naishukuru Serikali kwa kutujengea minada na majosho katika vijiji vya Chemakwezo, Mindutulieni na kadhalika, wafugaji wamefurahi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji wanalalamikia sana bei ya madawa ya mifugo. Kama Serikali inataka kumjadili mfugaji itazame upya kuhusu bei na usambazaji au ugawaji wa madawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo sekta nyingi ambazo hupewa kipaumbele kama kilimo, chakula maji na kadhalika, kuna misamaha inawafikia wananchi moja kwa moja , kwa nini inapofikia suala la mifugo kunakuwa na utata? Kwa nini mfugaji hapati msamaha kama alivyo mkulima, mwanafunzi, kwani jamii ya wafugaji wanayo maombi ya jamii na kimaendeleo, tegemeo lake ni mifugo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inasaidia zaidi taasisi kuliko mfugaji wa kawaida kwani ng'ombe kwenye *Ranch* ni tija kuliko ng'ombe wa mfugaji wa kawaida? Pamoja na kuwa wafugaji huenda hawafugi kisasa, je, Serikali itamuokoa lini huyu mfugaji na je mna uhakika kama mnatoa elimu ya kutosha au mnaweka umuhimu wakati wa ugonjwa? Bila hayo umakini wa kuwasaidia wafugaji ni ndoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Ranch* ya Ruvu inamiliki eneo kubwa kuliko ng'ombe au mifugo waliyokuwa nayo na wao wanashindwa kulilinda kiasi wananchi wa kawaida, wakulima na wafugaji kuingia kwenye hilo eneo na kusababisha migogoro isiyo na lazima. Eneo hili limeanzia Chamakweza, Mbala hadi Ruvu. Ikiwezekana mtazame upya ili kuepuka matatizo kwani wapo wafugaji wamelalamika kuwa mifugo yao inapoingia kwenye *Ranch* hukamatwa na hutozwa fidia, naomba mlifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba usafiri wa Pikipiki kwa watumishi wa mifugo waliopo katika Jimbo la Chalinze.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo heshima kuwasilisha mchango wangu wa maandishi katika hoja ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Kwanza kabisa, naomba nitumie fursa hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Dr. John P. Magufuli, Waziri wa Wizara hii, kwa kazi nzuri na bidii kubwa anayoionyesha katika uchapaji kazi pia Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Wanyancha, wote wawili wameonyesha juhudi kubwa kwa maendeleo ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nampongeza Katibu Mkuu Ndg. Nyamurunda pamoja na watendaji wote, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuhakikisha Watanzania tunatumia rasilimalli ya mifugo na samaki kwa ajili ya kupunguza umaskini wa kipato na kuongeza pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuelekeza mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, *Tanganyika Ranch* – Mbeya. Eneo hili lilikuwa ni mashamba ya wananchi, waliamua yachukuliwe kwa ajili ya kupisha maendeleo ya ujenzi wa Kiwanda cha Nyama cha Mbeya. Mpaka sasa ujenzi wa kiwanda hiki umesimama, tunaelezwa kuwa Serikali bado inatafuta wawekezaji kupitia *Consolidated Holding Company*

ambayo kusema ukweli hatuoni juhudi za makusudi za kukinadi kiwanda hiki ili kizalishe na kutoa ajira kwa wote.

Mbaya zaidi, eneo hili linatumika kama mashamba ya Mahindi, lakini linakodishwa kwa watu wanaotoka nje ya maeneo yale. Ni kwa nini mashamba haya wasipewe wananchi hawa ambao ndio waliotoa kwa kiwanda? Nashauri wakati tunapoendelea kutafuta wawekezaji, Serikali ichukue hatua za kuwapatia wanavijiji wa maeneo haya, wayatumie mashamba hayo badala ya watu kutoka nje ya vijiji hivyo.

Pili, juhudi za kukiendeleza Kiwanda cha Nyama Mbeya, sioni juhudi ya dhati kabisa inayofanywa na *Consolidated Holdings* katika kupata wawekezaji. Aidha, *Consolidated Holdings* imeleta ukiritimba wa kuhodhi rasilimali hii bila jasho. Ni kwa nini Serikali isibebe jukumu kwa kupitia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi katika kutafuta wawekezaji? Aidha, nini mantiki ya Serikali kujenga Kiwanda cha Nyama, Ruvu, wakati huo wameshindwa kukianzisha Kiwanda cha Mbeya ambacho tayari mashine/mitumbwi ipo? Serikali iepuke kuwa na maamuzi ya utatanishi, *Consolidated Holdings* wameshindwa kabisa kufanya kazi iliyokusudiwa. Aidha, urasimu ni mkubwa kwa sababu ya kutafuta 10%, kwa taarifa za wawekezaji. Ninashangaa kwa nini Serikali imenyamaza bila kutoa taarifa hasa baada ya Wizara hii kuomba rasmi kupewa kiwanda hiki ili watafute wawekezaji kwa karibu zaidi kuliko ilivyo sasa. Serikali itoe uamuzi sasa ili kiwanda hiki kianze kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI**: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itoe elimu kwa wanaochunga ng’ombe kwamba wanatakiwa wafuge ng’ombe. Kufuga ng’ombe kukiwa na maana ya kuwa na idadi ya ng’ombe inayokubalika kulingana na mazingira wanayofugia na miundombinu. Kama wafugaji ni matajiri kwa kuwa na ng’ombe wengi, basi wawe matajiri pia kwa kuwa na fedha ndani ya mabenki ili mifugo itakapopata maradhi basi fedha ya benki iweze kuwasaidia kuishi au kupata mifugo mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa BMUs uangaliwe vizuri ili usiwe kero kwa wananchi na wavuvi wadogo wadogo kwa ujumla. Mifano ya kero hizi nimeshuhudia katika Ziwa Victoria, Jimbo la Katoro, katika Kata ambazo Ziwa Victoria linapita. Hivi sasa tunatarajia kuona katika maeneo ya Wilaya zinazozungukwa na Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge orodha ya wachangiaji walioomba imekamilika na wote wamepata nafasi lakini ninafurahi kwamba leo tuna wageni wengi wafugaji katika ukumbi huu na itakuwa nafasi yao nzuri sana kuweza kumsikiliza Waziri atakavyojaribu kufafanua hoja mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge wametoa.

Bahati mbaya tu, sisi kipindi chetu kimekuwa kimebana kwa sababu Waziri na Naibu wake watakuwa na dakika arobaini za kujibu. Lakini nadhani watajibu kwa

ufasaha na sifa hizi mlizowapa watakwenda kwa mambo yale makubwa sana. Lakini umoja wa nchi hii bado upo, wafugaji, wakulima na wavuvi wote ni jamii moja ya Watanzania ila kazi mbalimbali. Nadhani tuendelee kuwa na umoja huo mpaka mwisho. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha hapa nilipo nikiwa na afya njema, nguvu na uwezo wa kuendelea kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na kuwa na imani nami katika utendaji wangu wa kazi.

Napenda pia kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kwa umahiri wake wa kuliongoza Taifa letu na kusimamia maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika Serikali ya Awamu ya Nne. Namwomba Mola azidi kumjalia afya njema, maarifa na hekima ili aweze kuchaguliwa tena kwa kipindi cha pili kuongoza nchi yetu kwa amani na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa uongozi wake mzuri wa shughuli za Serikali. Napenda kukupongeza wewe na Spika, kwa namna mlivyoongoza Bunge letu Tukufu kwa kipindi chote cha miaka mitano. Kwa kweli tumefanya mambo mengi sana ambayo yalikuwa ni mapinduzi. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano walionipa katika kipindi chote nilipokuwa Naibu Waziri na nawaombea kwa Mola waweze kuchaguliwa tena na kurejea Bungeni katika uchaguzi ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru sana Waziri wangu Mheshimiwa Dr. John Pombe Magufuli kwa kunishirikisha kwa karibu sana katika majukumu ya kuongoza Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa kipindi chote nilichokuwa naye. Kwa kweli kwa sakafu ya moyo wangu namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wangu, amenisaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Wizara yetu chini ya uongozi wa Dr. Charles Nyamrunda. Pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa wapigakura wangu wa Jimbo la Serengeti kwa ushirikiano wanaondelea kunipa na uvumilivu wao kwangu na hasa wanaponikosa kwa shughuli mbalimbali za kiserikali na za Kibunge. Naomba waendelee na moyo huo, nami naahidi kuendelea kushirikiana nao kwa karibu. Kwa heshima na taadhima natarajia kuwaomba ridhaa yao tena ili waweze kunichagua tena kwa kipindi cha uchaguzi ujao ili tuendelee kushirikiana kutekeleza miradi ya maendeleo na kuboresha hali ya maisha ya wananchi wote wa Serengeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru sana Serikali ya Awamu ya Nne kwa kutimiza ahadi ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 – 2009 katika Wilaya yetu ya Serengeti. Katika kipindi hiki, miradi muhimu ifuatayo ilitekelezwa:-

Kwanza kabisa, ilikuwa kuvuta umeme kutoka Bunda hadi Mugumu. Hii tulikuwa hatutarajii kupata umeme na tumeupata, tunashukuru sana.

Pili, kukamilisha bwawa la Manchira na kuvuta maji hadi Mugumu; Tatu, kuchimba malambo ya mifugo takribani Kata zote. Sisi tuna malambo 60 hatuna Wilaya inayotuzidi. Nne, tumejenga shule za sekondari, tumejenga *hostel* za wasichana, tumeanza ujenzi wa Hospitali ya Kisasa pale Serengeti, tumeanza matayarisho ya ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Kimataifa pale Mugumu na kufanya matayarisho ya kujenga barabara ya lami toka Nanta hadi Mto wa Mbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *last but not least* napenda kumshukuru sana mke wangu Sara Wanyancha na watoto wangu wote kwa kunipa moyo, kunivumilia na kuniombea dua ili niweze kulitumikia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huu, sasa naomba nichangie hoja ya bajeti ya Wizara ya Mifugo kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, naomba nitamke kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kuwa muda niliopewa ni mfupi ambao ni wa dakika kumi. Nitajibu tu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge na zitakazobaki zitajibiwa kwa maandishi na zaidi sana zitatolewa na Mheshimiwa Waziri wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja iliyotolewa ni kwamba, elimu itolewe kwa wafugaji ili waweze kufuga kisasa na kibiashara. Napenda kusema kwamba hii kazi imeanza na katika mwaka wa 2009/2010. Wafugaji 8,865 wanaume na 5,910 wanawake wa Mikoa ya Mwanza, Kagera, Shinyanga Arusha, Mwanza, Tanga na Ruvuma wamepata mafunzo kuhusu ufugaji wa kisasa na kibiashara.

Pia mafunzo yanaendelea kutolewa na mashirika yasiyo ya kiserikali yakiwemo *HPI, Farm Africa VetAid* na *World Vision* katika maeneo mbalimbali. Nia ya Serikali ni kuhakikisha wananchi wanapatiwa elimu ya ufugaji bora na hiyo itaendelea kwa kasi namna siku zinavyokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kwamba Maofisa Ugani wa Mifugo na Uvuvi waongezwe ili ufugaji wa kisasa uboreshwe. Takribani miaka mitatu iliyoanza tulifungua vyuo vyetu vya Liti na kwa sasa hivi vyuo hivyo vinapelekewa wanafunzi, kwa mfano mwaka huu wanafunzi 1,500 watadahiliwa kwa upande wa ufugaji na upande wa uvuvi watadahiliwa 300, hivyo kufikisha wanafunzi 1,800. Wengine wameshamaliza.

Mfano, kupitia mpango maalum wa kutoa mafunzo ya ngazi ya stashahada na astashahada jumla ya wataalam wa ugani 140 wamehitimu ambapo kati ya mwaka 2009/2010 wataalam 357 wameajiriwa katika Halmashauri, hivyo kupunguza pengo la wagani. Hii kazi itaendelea na nia ni kuhakikisha kwamba baada ya muda mchache tuwe na Maafisa Ugani 16,500 ili waweze kuwafikia wafugaji na kuwapa elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba kuimarisha maeneo ya malisho ya mifugo. Ni kweli kwamba kumekuwa na matatizo ya malisho ya mifugo na juzi tumeleta Sheria ambayo tunataka wafugaji watengewe maeneo. Mpaka sasa jumla ya hekta 32,095 zilipimwa mwaka jana kufikisha hekta milioni 1.4. Maeneo haya yamepimwa, kinachotakiwa sasa ni kufanyiwa *land use plan* ili kuonesha mifugo ikae wapi, kilimo kiwe wapi na hivyo kazi hiyo inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine kilikuwa ni masoko na mauzo ya mifugo. Wabunge wengi wamelalamika kwamba watu wanapeleka ng'ombe wanamuuza tu bila kutumia kilo. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Wizara imepanga kuanza kutumia mizani kuanzia mwaka huu wa fedha katika baadhi ya minada.

Vilevile imeandaa kanuni za kuwabana wafanyabiashara wanaokwepa kutumia mizani minadani. Kwa kweli ni lazima tuhakikishe kwamba wafugaji wetu wanapata bei nzuri na tatizo hili litatatuliwa kutumia mizani. Napenda kuwahakikishia kwamba hili tutaliwekea maanani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine lilihusu miundombinu ya mifugo. Wameomba kwamba mlambo, mabwawa, majosho na vituo vya afya vya mifugo vijengwe. Napenda kuwaambia Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa wajumla.

Tatizo la kuchimba sio la Wizara tena lakini fedha zinakuja kwa kupitia *DADP's* na tatizo lililopo ni kwamba sehemu nyingi sana hazielekezwi kwenye malambo na majosho. Tunaomba Wilaya zote zichukue hizi hasa zile ambazo ziko kwenye maeneo ya ukame watumie hizo hela.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine lilikuwa ni kwamba sensa ya mifugo ifanyike. Serikali ifanye sensa ya mifugo nchi nzima, kwani haijafanyika zaidi ya miaka 20. Hili tumeliona na Serikali imedhamiria kufanya sensa kamili ya mifugo kwa nchi nzima kwa mwaka wa fedha 2011/2012, sasa hivi tunaendelea na maandalizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine ambayo Waheshimiwa Wabunge wameelekeza ni kwamba ujenzi wa machinjio ya kisasa yafanyike katika maeneo yenye mifugo mingi. Mpango wa Serikali ni kuhakikisha sehemu kama za Arusha kule

Musoma, Shinyanga, Rukwa tunapata machinjio ya kisasa na tunachofanya hivi sasa ni kutafuta wawekezaji katika sehemu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru tena kwa kupata nafasi hii ya kuweza kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Hoja ni nyingi sana na jumla ya waliochangia ni Waheshimiwa Wabunge 91 na kati ya hao waliochangia kwa maandishi ni 60, walioongea ni 18 na waliochangia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu pamoja na Waziri wa Fedha na Uchumi ni 13 jumla ya wachangiaji ni 91. Sasa kwa dakika 30 ambazo umenipa sifahamu kama zitatosha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Utakapowaita majina hatutahesabu muda.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa huruma yako hiyo takatifu na Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

Sasa ninaanza kwa kutaja waliochangia katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri Mkuu wameshatajwa tayari katika Hotuba zilizotangulia lakini waliochangia katika Hotuba yangu kwa kuzungumza humu Bungeni ni Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Tedddy Kasella–Bantu, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko na Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Anna Makinda, Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mheshimiwa Janeth Masaburi, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Samuel Chitalilo, Mheshimiwa Mkiwa Kimwaga, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Brigedia Jenerali Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Salim Salum Mohamed, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed,

Mheshimiwa Felista Bura, Mheshimiwa Elietta Switi, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa George Simbachawene na Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Usisikilize.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, unajua majina ya Wagogo yana matatizo sana angetamka vizuri hili jina Mheshimiwa Malecela. Mheshimiwa Richard Ndasa, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Nuru Bafadhil, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir na Mheshimiwa Mussa Azan Zungu. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Endelea tu wanajifahamu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru sana lakini niseme kwa dhati kabisa kuwa ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia kwa dhati kabisa katika hoja tuliyoileta hapa inayohusu Wizara yangu. Kwa ujumla tu masuala yote yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wote wa Upinzani na wa Chama Tawala ni ya msingi na bahati nzuri wa Upinzani nao walikuwa wanajaribu kufafanua na kama wangeleta haya mapema tungeweza tukaya-*cooperate* humu kwenye Bajeti, lakini bahati yao mbaya huwa wanachelewa kila mara kama ambavyo wanavyochelewa katika kupiga kura saa nyingine sisi tunawashinda tunakuwa tunaongoza CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutoa ushauri kwa Waheshimiwa Wabunge wa Kambi ya Upinzani michango yao ni mizuri sana. Katika Bajeti inayokuja wailete mapema ili kusudi tuweze kuifanyia kazi katika kuboresha hili suala la Mifugo na Uvuvi, lakini kama nilivyosema michango iliyotolewa pia katika upande wa Chama Tawala ni mizuri sana kwa sababu wao walikuwa wakitekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, na bahati nzuri Waheshimiwa Wabunge wametekeleza sana lakini ninachotaka kusema hoja zote ni nzuri, muda wa kuzijibu zote ni vigumu lakini tutazijibu baadaye kabla ya Bunge hili halijaisha hoja zote na tutawagawia Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kaika Telele ambaye ni Msemaji kwa niaba ya Kamati ametoa pongezi amesema Bajeti ni ndogo na sisi tunasema kwa kweli Bajeti ni ndogo. Lakini Rais Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ameahidi wakati anachukua fomu kuwa katika sekta zitakazowekewa umuhimu mkubwa sana ni sekta ya kilimo, sekta ya uvuvi, sekta ya mifugo na sekta ya maji, katika sekta hizi nne ambazo zitatiliwa umuhimu sana sekta mbili ziko kwenye Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi, ninaamini kabisa Watanzania wote wa vyama vyote watampa kura nyingi sana na ninashangaa wanajitokeza tokeza kutaka kugombea hawa wa Vyama vya Upinzani

wangemuachia tu Rais Mheshimiwa Jakaya Kikwete akapita bila kupingwa ili hii ari ambayo ameianzisha katika kusaidia Wizara hii na hasa kwa kusema kwamba Bajeti itakuwa kubwa iweze kutekelezwa mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Kilimo Kwanza ni pamoja na Uvuvi na Mifugo, nakubaliana kabisa na Kamati. Uhaba wa wataalamu hasa Maafisa Ugani tumeanza kulishughulikia katika Bajeti ya mwaka huu, tutapeleka wananchi karibu 2,000 katika vyuo mbalimbali, tuna vyuo saba vya mifugo na tuna vyuo viwili vinavyohusika na uvuvi, ninaamini vitakuwa vinaendelea kupunguza lakini pia kwa sasa hivi wapo wanachuo zaidi ya 1,800 ambao wame-*graduate* na bahati nzuri wamegawanywa katika Halmashauri mbalimbali kwa ajili ya kufanya kazi, ninaamini kwamba kutokana na huu mwanzo mzuri wa ku-*produce* maafisa ugani siku moja tataizo la Maafisa Ugani litakuwa limepungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi za Utafiti ziongezewe fedha na hili ninakubaliana nalo lakini bahati nzuri katika Bajeti ya Wizara ya Fedha na Uchumi zimetengwa shilingi bilioni 30 ambapo katika Taasisi za Utafiti zote zinazohusika na Mifugo na Uvuvi zitaomba fedha huko katika kuongeza pesa katika masuala yanayohusu utafiti unaohusu uvuvi na mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi wasiachiwe Halmashauri tu, unywaji wa maziwa uhamasishwe na tumeendelea kufanya hivyo na katika mwaka huu sherehe za unywaji wa maziwa zilifanyika kule Lindi na bahati nzuri sasa unywaji wa maziwa umeanza kuongezeka kutoka lita 41 kwa kila Mtanzania kwa mwaka sasa imeongezeka lita 43 kwa kila Mtanzania kwa mwaka na leo Waheshimiwa Wabunge wamekunywa wengi sana maziwa na hata kule kwa watani zangu Wafipa kule nako sasa wameanza kuongeza unywaji wa maziwa kwa mwaka huu, kwa hiyo, unywaji wa maziwa umeanza kuongezeka na sasa utaongezeka zaidi baada ya kufutwa ushuru wote unaohusika na masuala ya maziwa ninaamini hili ni juhudi nzuri zinazofanywa na Serikali ya Chama cha Mapainduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda vya nyama Serikali ijenge malichinjio ya mifugo tumeanza na juzi juzi Mheshimiwa Rais aliweka jiwe la msingi la machinjio ya kisasa pale Ruvu ambayo yatakuwa yanachinja zaidi ya ng’ombe 800, mbuzi na kondoo 400 kwa siku. Tunaamini kuwa machinjio haya na machinjio mengine ambayo yamekuwa yapo kwa mfano haya ya hapa Dodoma sasa hivi yameanza kuongezeka na yameanza kuzalisha fedha nyingi, kuna machinjio ya Sumbawanga, yapo mengine Manyara na sehemu zingine ninaamini sasa wawekezaji wataanza kujenga viwanda vyao vingi vya machinjio, tatizo kubwa lilikuwa ni Sheria zetu lakini napenda nichuke nafasi hii kulipongeza sana Bunge lako Tukufu kwa kupitisha Sheria ya *Traceability* pamoja na ya mazao ya mifugo iliyopitishwa hapa ambayo kwa bahati nzuri Mheshimiwa Rais ameishaisaini, ile itakuwa motisha kwa wawekezaji mbalimbali kuja kujenga viwanda vikubwa katika nchi yetu na nina uhakika sasa sekta ya mifugo inaweza ikachangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wamefanya hivyo kwa mfano Ethiopia michango ya sekta ya mifugo katika *GDP* ni zaidi ya 18.8% pamoja na kwamba Ethiopia ni wapili kuwa na mifugo mingi katika Afrika. Lakini Sudan mchango wao katika sekta ya mifugo kwenye *GDP* ni 20.8 wao wana ng'ombe karibia milioni 35, Ethiopia wana ng'ombe karibu milioni ishirini na kitu na sisi tuna ng'ombe zaidi ya milioni 19 lakini *contribution* yetu imekuwa ni chini sana, ninaamini sasa kwa kubadilisha Sheria tulizonazo sasa wawekezaji watakuja wengi na huo ni mwanzo mzuri na mimi napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa kupitisha Miswada yote tuliyoileta hapa inayohusu sekta ya mifugo na uvuvi na ninaamini kwa njia moja au nyingine tutaweza kuboresha masuala haya yanayohusu mifugo, amezungumzia pia mradi wa *MACEMP* ambao unaenda vizuri mpaka sasa hivi tumeshagawa zaidi ya shilingi bilioni 5.7 katika Halmashauri zaidi ya 16 zilizoko upande wa Pwani kuanzia Moa hadi Msimbati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kwamba miradi hii itasaidia na itawawezesha wananchi wengi kufaidika katika masuala yanayohusu uvuvi. Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha wa Kambi ya Upinzani mchango wake kwenye sekta ya mifugo na uvuvi amesema Serikali inaongeza mapori kwa ajili ya wanyama haiongezi kwa ajili wa mifugo, sasa sielewi ni mapori gani yameongezwa na kadhalika lakini nataka kusema tu kuwa hii ni *challenge* na amesema maeneo ya madini yanachukuliwa yanawekwa mifugo, upinzani wakichukua uongozi wataandaa sera nzuri kwa ajili ya wafugaji. Sasa nilifikiri wameshaandaa hiyo sera, watupe tuifanyie kazi kumbe wataandaa sasa kwa maana nyingine hawatachukua nchi na sera hawataandaa kwa hiyo, tutaendelea kutekeleza sera ya mifugo ambayo ipi na Sheria zipo na tunedelea kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua kupinga saa nyingine huwa ni rahisi sana unaweza ukawa umesimama hapo ukasema hata michezo unaweza kusema kuwa mchezo huu ningekuwepo mimi ningefunga na saa nyingine unaweza ukawa unatingisha mguu peke yako ukijua kuwa utashinda ukiingia mle ndipo unaweza kuziona *challenge,* kwa hiyo, wenzetu wa upinzani wana bahati ya kuzungumza unaeleza wewe hapa halafu wao wanasema ningekuwa mimi ningefanya hivi, ningekuwa mimi ningeruka hivi, ningekuwa mimi ningeruka hivi, ningekuwa mimi ningegeuka hivi, wananchi wanafahamu yaliyofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni makubwa sana na ndiyo maana Chama cha Mapinduzi kitaendelea kupeta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningemshauri Mheshimiwa tuendelee kujifunza kutoka kwenye Ilani hii ya uchaguzi ambayo utekelezaji wake umekuwa ukiendelea. Wafugaji watapewa mikopo yenye nafuu, tuna benki 33 katika masuala ambayo yamekuwa yakizungumzwa ambapo kwa bahati nzuri mkutano uliosimamiwa chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ulifanyika hapa Dodoma na mwingine ulifanyika Dar es Salaam na mwingine ulifanyika Mwanza akiwa yeye ni Mwenyekiti, ni mara chache sana kuwa Mwenyekiti ambaye ni Waziri Mkuu asimame siku tatu kuzungumza na wadau wanaohusu sekta ya mifugo na uvuvi na mimi napenda sana kwa nafasi ya pekee nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri aliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala yaliyozungumzwa ni pamoja na kuwa mikopo nafuu kwa wakulima, wafugaji na wavuvi suala hili linafanyiwa kazi na hivi karibuni tu

kutapatikana Benki kwa ajili ya wakulima na haya masuala ambayo amezungumza yatajitokeza. Kuandaa utaratibu mzuri wa uwekezaji tumepitisha Sheria huwezi kuandaa utaratibu kwa kuzungumza tu, ni lazima ubadilishe Sheria, tumebadilisha Sheria tuna Sheria ya Ngozi namba 18, tuna Sheria ya Ustawi wa Wanyama namba 19, tuna Sheria ya Magonjwa ya Mifugo namba 17, tuna Sheria ya Nyama namba 10, tuna Sheria ya Maziwa namba 4 na Sheria zingine nyingi na Sheria ya Usyawi wa Wanyama na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ubadilishaji wa Sheria huu ndiyo utatuwezesha kuwafanya wawekezaji waje. Kutochanja mifugo kwa dawa zinazotengenezwa hapa nchini badala kutegemea dawa ya nje, tumeshaanza katika kituo cha Temeke pale dawa za mdondo wa kuku zinatengenezwa hapa na sasa hivi tunafanya mpango wa kuwa na kiwanda kabisa cha kuanza kutengeneza dawa kwa hiyo, bahati nzuri nafikiri Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha ameyaona haya ambayo yameanza kutengenezwa na Wizara akaona achomekee pale pale aone na yeye angefanya hivyo lakini ukweli ni kuwa Serikali imeshaanza kufanya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Wanasema umechanganya siyo kutengeneza magonjwa ni kutengeneza dawa. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:**Mheshimiwa Naibu Spika, sawa uvuvi katika Bahari Kuu uangaliwe vizuri, tumeshaanza kuchukua hatua, tumebadilisha Sheria ya *Deep Sea Fishing Authority,* tumekamata watu waliokuwa wanavua kiharamu na baada ya kuanza kuchukua hizo hatua na wengine wako mahabusu sasa zaidi ya mwaka mzima na sitaki kulizungumzia sana kwa sababu hili suala liko Mahakamani, hawa waliokuwa wanatuibia sasa wameanza kuogopa, sasa hivi kuna meli zaidi ya 20 kutoka Spain, Ufaransa, Shelisheli na Watanzania wamekuja kujisajili na kuvua kihalali na wameshalipa zaidi ya dola 650,000 lakini hata wale samaki waliokuwa wanaingia kiharamu tumeanza kuwatoza ushuru kwa dola 0.25 nimeandika katika hotuba yangu na tumeshakusanya sasa karibia milioni 600. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata samaki tunaosafirisha yaani Pweza na Ngisi ambao walikuwa hawatozwi ushuru, sasa hivi tunatoza kwa dola 0.25 tumeshaingiza zaidi ya shilingi milioni 900 kwa hiyo, mwanzo ni mgumu, nilifikiri Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha atatupongeza kwa hili lakini bado anatuponda tu, tunaomba hata kwa haya machache basi utupongeze lakini ninafahamu ni changamoto kubwa sana ambazo Mheshimiwa mwadini Abbas Jecha anatakiwa kutupa na sisi tunazichukua kama changamoto katika hatua nyingine nina uhakika katika Bajeti tunazozifanya tutayaangalia vizuri haya ili tuone ni namna gani tunaweza kuya- *cooperate*.

Mheshimiwa Job Ndugai ametoa pongezi kwa kazi nzuri, yeye ni mwakilishi wa Chuo Kikuu ameeleza ukurasa wa 10 kuwaelimisha wananchi kuuza mifugo, anasema sasa tuwaeleze watumie neno kuvuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuvuna na kuuza yote kwa msukuma mimi naona yanafanana tu kwa sababu tumezoea kuvuna maji, mimi ukisema kuvuna maji, lakini

kuvuna na kuuza bado ni masuala mazuri lakini sasa kwa sababu Mheshimiwa Job Ndugai anasema niwaeleze watani zangu Wagogo kuwa neno kuvuna ndiyo wanalielewa kuliko kuuza, nawashauri Waheshimiwa Wagogo watani zangu wa Jimbo la Mheshimiwa Job Ndugai sasa wavune mifugo yao ili ipungue kwa ajili ya kupata faida nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji, pametengwa eneo la hekta milioni 1.4 tu, hili halitoshi nakubaliana kabisa na Mheshimiwa. Ni kweli kabisa eneo kwa ajili ya wafugaji hekta milioni 1.4 halitoshi lakini tumeanza kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Ardhi nina uhakika eneo litakuwa linaendelea kutengwa mwaka hadi mwaka na katika Bajeti ya mwaka huu mtaona fedha nyingi zimepelekwa pia Wizara ya Ardhi kwa ajili ya kuanza kutenga na kupima maeneo kwa ajili ya kupunguza migogoro kati ya wakulima na wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili suala linashughulikiwa ili kusudi kupunguza migogoro kati ya wakulima na wafugaji *(marine packer)* liko Wizara ya Mifugo ni vyema likapekwa Wizara nyingine. Sasa hili ni suala la kuzungumza kwa sababu katika *instrument* tulizopewa *marine packer* ambayo inasimamiwa na Sheria namba 29 ya mwaka 1994 iko chini ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Kutafuta wawekezaji nje kwa ajili ya Kongwa ni vizuri wananchi wa maeneo ya Kongwa nao wakahusishwa, hili Mheshimiwa Job Ndugai nakubaliana na wewe kabisa kwamba kama patatokea wawekezaji wazuri hata wewe Mheshimiwa Job Ndugai na wengine ambao wanataka kuingia ubia na Ranchi zetu zikiwepo za Kongwa wanakaribishwa kwa mikono miwili na hili ndilo suala zuri la kuwaendeleza wananchi na Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Michael Laizer anasema kilio cha wafugaji kuwa wamekuwa kama watoto yatima na kadhalika. Mheshimiwa Laizer sasa hivi tumepitisha Sheria nzuri za kuweza kuwalinda hawa wafugaji dawa za mifugo nalo tumelizungumza na bahati nzuri mwaka huu tumegawa dawa zenye thamani ya zaidi ya bilioni 13 ambayo tumeyagawa katika Halmashauri zote, ningependa tu nitoe wito kwa Wakurugenzi wote na Maafisa Mifugo walioko katika Halmashauri zetu wahakikishe dawa hizi zinafika kwa wafugaji, wafugaji wanalipa 60% na 40% imeshalipiwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekezaji wapatikane kwa ajili ya soko na mimi nasema wawekezaji sasa watapatikana kwa sababu Sheria tumeshazipitisha na Mheshimiwa Lekule Laizer alihusika pia kuzipitisha. Mifugo ipimwe kwenye mizani, hili ni ombi zuri na sisi tutaanza, tutatoa waraka baadaye baada ya Bunge hili kwamba mifugo yote inayouzwa kwenye mnada sasa ianze kupimwa badala ya kukadiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Lekule Laizer pia alizungumza kuwa Serikali ingetoa tamko kwa maeneo ya wafugaji hayana maji na kadhalika. Haya yote tunayachukua kama changamoto na tutashirikiana na wenzetu na Wizara zinazohusika Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Wizara ya Tawala za Mikoa na Seriklai za Mitaa katika kuhakikisha kuwa malambo mengi yanapatikana lakini pia ningependa kutoa wito pia kwa Wakurugenzi

kuwa miradi ya *DADPS* ihusishwe pia katika kuchimba malambo mengi yatakayowahususisha wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Longido mifugo inakufa kila siku Magufuli yeye anazungumzia nyavu, nyavu tu na kadhalika, nimelipokea hili ni *challenge* na tutalifanyia kazi kama Wizara kuhakikisha kwamba tunafanya nini katika Jimbo la Longido katika kuwaelimisha wananchi na kufanya wajue kwamba mifugo ni muhimu. Lakini Serikali kwa ujumla inatambua mifugo, uvuvi na kilimo vyote ni muhimu katika kuleta maendeleo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Yono Kevela amesema pongezi kwa Wizara tunachapa kazi, kijiji kimepata mabirika ya ng'ombe wanashukuru, kuku wa kienyeji wanataka hili lishughulikiwe vizuri, na mimi naunga mkono katika Wilaya ya Njombe bahati nzuri pamoja na kwamba wana mbwa wengi kule lakini pia ni wafugaji wazuri wa kuku, kwa hiyo, tutajipanga vizuri. Nimeshatoa maelekezo kwenye Wizara yangu tuangalie ni namna gani tutaweza ku-*promote* suala la ufugaji wa kuku na hili ni suala zuri kulipata kwa mtu ambaye walizoea kufuga wanyama wa aina fulani na sasa wanataka kufuga kuku. Masoko ya kuku wa kienyeji nayo yapatikane, hili pia tutalifanyia kazi. Suala la minada, ni vyema minada iimarishwe. Huu ni wito na sisi tunauzingatia wito na maelekezo ya Mheshimiwa Yono Kevela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma anazungumzia kuhusu Waraka wa Mkurugenzi wa kupiga vita uvuvi haramu, anazungumzia pia mkutano maalum wa wadau mbona hajawahi kuuona?

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumweleza Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, mkutano uliokuwa unahusu wadau wa sekta ya uvuvi, ulifanyika Mwanza na ulikuwa chini ya Uenyekiti wa Waziri Mkuu kwa siku tatu mfululizo. Napenda nimshukuru sana Waziri Mkuu kwa sababu matatizo mengi ya uvuvi yaliweza kujitokeza. Lakini pia kuhusu suala la watu kushikwa wengine wakiwa wana mitungi na kadhalika na wanapelekwa Mahakamani. Hapa tunazingatia Sheria namba 22 ya mwaka 2003 na *regulation* za mwaka 2005, lakini *regulation* hizo pia zimepitiwa na kuna *regulation* mpya ambazo nitampatia Mheshimiwa Shoka Khamis Juma za mwaka 2009 ambazo zinazungumzia Kanuni kuhusu masuala ya ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tatizo ambalo linajitokeza katika ukanda wa Pwani, ukitumia mtungi wa gesi kujiokolea au kwenda kushika samaki wa mapambo huna kosa. Lakini ukitumia mtungi wa gesi ya *oxygen* kwa ajili ya kwenda kutega mabomu, lile ni kosa. Ni kama mtu ukimshika na shoka anakata miti hana kosa, lakini ukimshika na shoka ana kata binadamu ana kesi ya jinai. Kwa hiyo, ni namna tu ya kile kitu kinatumikaje na ningependa nimweleze Mheshimiwa Shoka Khamis Juma kwamba shoka ukishikwa nalo linakata miti huna makosa, lakini ukishikwa na shoka unakata mtu una kosa. Ni suala la kuangalia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo watu wanatumia mitungi hii ya *oxygen* kwenda kutega mabomu, wanatumia mitungi ya *oxygen* kwenda kuwaua na kuwashika pweza

kwa ajili ya kwenda kuwauza, wanatumia mitungi ya *oxygen* kwenda kushika majongoo na nchi iliyobaki na majongoo katika ukanda wa pwani ni Tanzania tu, nchi nyingine zinazotuzunguka zote majongoo bahari yamekwisha. Kwa hiyo, unaposhikwa na mtungi wa gesi huku umebeba baruti ni lazima utapelekwa mahakamani na mtungi wako na baruti yako na vitu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kinaweza kikawa kizuri ukikitumia mahali pazuri, ukikitumia mahali pabaya ni lazima sheria namba 22 ya mwaka 2003 itakushughulikia na *regulation* zake za mwaka 2005 ambazo zimefanyiwa *amendment* mwaka 2009. Lakini ukiwa upande wa Zanzibar utashughulikiwa na sheria namba 8 ya mwaka 1988 ambayo pia imefanyiwa *amendment* mwaka 2010. Kwa hiyo, sheria ni msumeno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro amesema Bajeti ya mifugo ni kidogo na mimi nakubaliana naye, lakini kutokana na ahadi ya Serikali hasa Mheshimiwa Rais aliyoitoa nina uhakika kuanzia mwaka kesho Bajeti itakuwa nzuri. Tatizo la magonjwa ya mifugo tumelizingatia, tutaliangalia ni namna gani tutaweza kulishughulikia. Maeneo ya mifugo watumiaji wengine wasiingie mle, hili nakubaliana naye kabisa na ndiyo maana tulipitisha sheria ya *Traceability* kwamba eneo litakalotengwa kwa ajili ya wafugaji, wakulima au wavuvi na watu wengine wasiingie kwenye eneo hilo na ndiyo maana ya sheria hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mhehsimiwa Ole-Nangoro pia amezungumzia suala la tafiti kufanyika ili kuongeza thamani kwa mazao, yote ni michango mizuri tu. Suala la ukame katika maeneo ya Kaskazini pia amenielezea. Kwa ujumla michango yote ya Waheshimiwa Wabunge leo ni mizuri tu. *(Makofi)*

Mhehsimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Teddy Bajeti-Bantu naye ametoa pongezi kubwa na akasema kwamba kilimo ni pamoja na mifugo, na amezungumza itatumika vizuri katika kutoendeleza migogoro hata katika sheria ambazo tumezipitisha, lakini pia amezungumza kwamba katika mabwawa yake ambayo bahati nzuri yamekuwepo tangu siku nyingi, mabwawa madogo madogo tuyatumie katika kutuma watu kwa ajili ya kuanza kufuga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kukuhakikishia Mheshimiwa Kasella-Bantu nitatuma watalaamu wangu siku yoyote utakapotaka uende nao mpaka Jimbo la Bukene wakaanze kufuga samaki, lakini pia hata maeneo mengine ambapo Waheshimiwa Wabunge wanataka kuanza kufuga samaki tutaoa vifaranga vile kwa kuanzia hata bure ili kusudi wananchi wengi waweze kufuga vifaranga na kutoa mchango mkubwa katika sekta ya mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kasella-Bantu anasema watalaamu wetu mishahara yao ni midogo, hilo pia linashughulikiwa na Ofisi ya Utumishi, anasema boti ya Mbegani itengenezwe, bahati nzuri tumepata msaada kutoka kwa Wajapan wataikarabati, watalaamu wetu waende Bukene wananchi wanakofuga samaki, wataenda. Amezungumzia kuhusu Bwawa la Itobo la Mwaisela liwekewe samaki, nataka kukuhakikishia kwamba litawekewa samaki.

Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha amesema wanaofuga si Wasukuma tu, bali hata wao pamoja na kwamba amesahau kwamba na yeye ni Msukuma ndiyo maana ni mrefu kuliko hata mimi, lakini anaunga mkono, anazungumzia juu ya mabwawa ya Jimbo lake, nasema pale ni karibu tutaangalia ni namna gani tutayashughulikia. Amezungumzia suala la majosho kwa Kata zake hili nalo tutalizingatia. Amezungumzia pia wafugaji wa kuku katika Wilaya ya Kibaha, kuku wa kienyeji na kuku wa kisasa, tatizo la upatikanaji wa vifaranga. Zote hizi ni *challenges* na ndiyo maana nimesema muda ni mfupi sana wa kuweza kujibu hoja zote lakini nataka kumhakikishia Mheshimiwa Dr. Msabaha kwamba tutalifuatilia na tuone ni namna gani tutamtatulia.

Kuhusu dawa za kuku na vyakula, navyo bei yake imekuwa kubwa, naungana na yeye kwa sababu siku za nyuma hatukuwa na sheria ya vyakula vya mifugo. Sasa kwa kupitia ile sheria ya vyakula vya mifugo ambayo tayari imeshasainiwa na itakuwa Sheria namba 13 nina uhakika masuala haya ya vyakula vya mifugo yataweza kuzingatiwa vizuri zaidi. Kwa ujumla michango ya Mheshimiwa Dr. Msabaha ni mizuri na tutaangalia ni kwa namna gani tutaweza kumsaidia mtu anayesema ni baba wa Wasukuma wakati ameshindwa kukumbuka kwamba yeye ndiye mtoto wa Msukuma kwa sababu Wasukuma wengi walikuwa wanatoka Tabora na Wanyamwezi kuja Pwani na wengine walipitia pale Kibaha akazaliwa yeye, nampongeza sana kwa kuzaliwa na Wasukuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ruth Msafiri ametoa pongezi, amesema kazi nyingi zinafanyika kwenye sekta ya uvuvi, upande wa Pwani, kazi hizo ni vizuri zikafanyika pia katika upande wa maziwa ikiwemo Ziwa Victoria. Nakubaliana na Dada yangu Mheshimiwa Ruth Msafiri kwamba ni kweli kazi nyingi zimefanyika upande wa Pwani kwa sababu palikuwa na mradi wa *MACEMP* ambao umekuwa ukitumika kule kwa kipindi cha miaka mitano. Lakini kazi pia katika maziwa mengine umeanza kufanyika. Kwa mfano hivi karibuni zaidi ya shilingi bilioni 3.3 zimetumika katika kuimarisha mialo, kuna mradi wa *Lake Victoria Fisheries* ambao unafanyika katika Ziwa Victoria, lakini kuna mradi pia wa *Lake Tanganyika* ambao upo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais utakuwa Ziwa Tanganyika na kadhalika. *(Makofi)*

Naamini kwa pamoja tutaweza kufanikiwa. Amezungumzia pia BMU ziimarishwe, wafugaji wa samaki wa Muleba anawapongeza na mimi nawapongeza sana kwa sababu nimeyaona hayo mabwawa, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge pamoja na mwenzake Mheshimiwa Wilson Masilingi kwa kusimamia haya mabwawa naomba waendelee hivyo hivyo na wananchi wa Muleba waendelee kuwarudisha ili mabwawa mengi yaweze kufuga samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumzia juu ya utafiti lakini pia amezungumzia wananchi waliopo kwenye Ranchi. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Ruth Msafiri kwamba wale wananchi hawataondolewa, wataendelea kukaa pale mpaka matatizo haya yatakapokuwa yametatuliwa na kuhakikisha haki inatendeka katika pande zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi ametoa pongezi, yeye ni mfugaji ameeleza mambo mengi na kengele nimeshagongewa, amesema uvuvi kila mahali, nampongeza

sana na mimi nashukuru. Mheshimiwa Benson Mpesya amezungumzia kuhusu Kiwanda cha Mbeya, *challenge* alizozitoa ni za kweli na kweli ni kwamba sisi tumeshaandika barua kwa Wizara ya Fedha ili kusudi kile kiwanda kirudishwe Wizarani tuweze kukitangaza, napenda kuchukua nafasi hii kumwambia Mheshimiwa Benson Mpesya kwamba tutazungumza na mwenzangu Waziri wa Fedha ili watupe kibali haraka kile kiwanda kirudishwe Wizarani na sisi tuweze kukitangaza ili kusudi kiweze kupata wawekezaji. Hata kama ni wawekezaji wa ndani ili kiwanda kile kisiendelee kuharibika. Kwa hiyo, ombi la Mheshimiwa Benson Mpesya ni zuri tu na nina uhakika sasa wananchi wa Mbeya watamrudisha vizuri ili kusudi aje alishughulikie vizuri hili katika kuhakikisha kwamba kiwanda hiki kinafufuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa ametoa pongezi kwa Serikali kwa kutoa ushuru kwenye sekta ya maziwa, anasema viwanda vya maziwa viimarishwe na napongeza kiwanda cha maziwa kimoja kitakachoanzishwa na Askofu Barina kule Shinyanga na mimi nachukua nafasi hii kumpongeza sana Askofu Barina kwa kuanzisha kiwanda cha maziwa Shinyanga na hiki nafikiri kitasaidia sana wananchi wa maeneo yote. Sekta ndogo ya nyama nayo amezungumzia, amezungumzia pia kiwanda cha *Triple S*. Ningeomba kiwanda cha *Triple S* muda wao uta-*expire* tarehe 01 Januari, 2011 basi wahakikishe kwamba kiwanda hiki kinafanya kazi mapema kabla hawajanyang'anywa kulingana na makubaliano ya mkataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Maria Hewa naye ametoa shukrani nyingi, kwanza naomba nimpe pole kwa kufiwa na Mzee wetu Mzee Hewa, Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. Amina. Bahati nzuri yule Mzee nilimfahamu sana na Mungu azidi kumuimarisha Mama Hewa, amesema Wizara hii inafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Magdalena Sakaya amezungumzia pongezi, nashukuru sana kwa kupata pongezi kutoka kwako dada yangu, unajua ni wachache kutoka Kambi ya Upinzani kukupongeza na mimi nimepongezwa na wewe, najisikia raha kweli na leo nitalala vizuri sana. Nataka kusema hoja zako zote ulizozizungumza na ndiyo maana ulianza na pongezi. Kuhusu suala la ekari milioni 1.4 hazitoshi ni kweli na sisi tunasema hazitoshi lakini tunashirikiana na wenzetu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuongeza ekari zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa John Cheyo anasema tuwasikilize wafugaji na mimi nasema tutawasikiliza, na nafikiri hilo ni suala zuri tu kwa sababu Serikali ya CCM ni sikivu huwa inawasikiliza na ndiyo maana tunasikiliza wapinzani, tutawasikiliza wafugaji, tutawasikiliza wavuvi, tutawasikiliza watu wa aina yoyote, hiyo ndiyo Sera ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, hao wafugaji nao tutawasikiliza na tutawashauri ili kusudi waanze kufuga kisasa kwa kuzingatia sheria tulizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Daniel Nsanzungwako amezungumzia masuala mengi, amezungumzia Bwawa la Lugoi, mabwawa haya yawekewe samaki, ushirika wa wafugaji, ndorobo. Bahati nzuri kule Kigoma kuna kituo cha ndorobo tutalizingatia hili suala katika vijiji vya Mvinza na Kagerankanda kuhakikisha kwamba tunapambana na ndorobo na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, muda ni mfupi masuala ya mifugo na uvuvi ni mengi, nataka kukuthibitishia kwamba hoja zote zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge tutazijibu kwa ufasaha ili tuwagawie Waheshimiwa Wabunge, michango yao ni mizuri sana na sisi tunaamini katika Bajeti inayokuja itakuwa nzuri sana kwa sababu tutajumlisha michango iliyotolewa na Wabunge katika pande zote, upande wa Upinzani na Upande wa Chama Tawala katika kuhakikisha sasa tunaimarisha sekta hii ya mifugo na uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, muda umeisha na ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 99 - Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi**

Kifungu 1001 *Admnistration and General*.............sh. 2,954,985,500/=

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili kuomba ufafanuzi. Katika mchango wangu wa maandishi nilielezea jinsi Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa jinsi ambavyo yapo *under utilized*, nilitaka kujua mikakati. Lakini pamoja na hilo jambo kubwa sana nilitaka kujua…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa umeanzaje?

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Katika mchango wangu wa maandishi…

**MWENYEKITI**: Hapana, tupo kwenye Kamati ya Matumizi.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti samahani, *Vote 99, programme 10,* mshahara wa Waziri.

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nilielezea jinsi Ziwa Tanganyika lilivyo *under utilized* pamoja na Ziwa Nyasa na nikataka kujua mikakati ya Serikali ni ipi, lakini jambo kubwa ambalo nilitaka kujua Serikali inapochoma nyavu za wavuvi ambao wengi wao ni maskini bado haijatoa njia mbadala. Kile kiwanda ambacho kinatengeneza zile nyavu hakijafungwa, nilikuwa naomba kujua kwa nini Serikali isitoe maelekezo au ikatoa nyavu za mkopo kwa wale wavuvi ili wasiweze kuendelea kutumia nyavu ambazo hazitakiwi na kiwanda ambacho kinatengeneza nyavu ambazo hazitakiwi kwa nini kisielekezwe

kutengeneza nyavu ambazo zinatakiwa ili kuwaondolea adha wavuvi. Naomba ufafanuzi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sikuweza kujibu hoja zote kwa sababu ya muda. Waliochangia kwa maandishi ni watu 60 na waliozungumza hapa nao ni wengi tu. Kwa hiyo, kwa dakika 30 nisingeweza kujibu hoja zote. Ndiyo maana niliahidi kwamba nitatoa maelezo yote kwa hoja zote zilizochangiwa na Waheshimiwa Wabunge kwa maandishi na Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Ziwa Tanganyika, nimeeleza hapa mwishoni kwamba kuna mradi unaohusisha Ziwa Tanganyika ambapo kuna fedha zimetengwa ambazo zitahusisha nchi tano, nchi ya Tanzania, Burundi, *DRC,* Zambia na nchi zote zinazozunguka Ziwa Tanganyika na bahati nzuri mradi huu upo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Kwa hiyo, nina uhakika haya masuala yatazingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuchoma nyavu hilo ni suala la sheria ambayo ipo chini ya Sheria namba 22 ya mwaka 2003 na *regulations* za mwaka 2005 ambazo zimefanyiwa mabadiliko mwaka 2009 na wale wanaochomewa nyavu huwa wanapelekwa mahakamani na mahakama ndiyo inatoa hicho kibali cha kuchoma nyavu, kwa hiyo, kama kuna matatizo aende aka-*appeal* mahakamani ili wananchi wasichomewe nyavu. Lakini sisi tunazingatia sheria na sheria ni msumeno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda vinavyotengeneza nyavu ambazo hazikubaliki, sina habari ya kiwanda chochote kinachotengeneza nyavu ambazo hazikubaliki, ninamuomba Mhehsimiwa Mhonga atusaidie ni kiwanda gani ambacho kinatengeneza nyavu ambazo hazikubaliki ili tutume askari waende wakafanye kazi zao. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Wizara hii imefanyakazi nzuri sana kuimarisha Kituo cha Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo pamoja na kuimarisha Chuo cha Mifugo Mpwapwa, nawashukuru sana. Sasa swali langu ni kwamba je, hawa wanafunzi wote wanaomaliza Vyuo vya Mifugo ngazi ya *Diploma* pamoja na vyeti je, wote wanapata ajira? Kama hawapati ajira wengine kwa mfano wa vyeti kuna sababu gani za kutowaajiri kwa sababu Mheshimiwa Rais alipotembelea Wilaya ya Mpwapwa mwaka 2008 alitoa maelekezo pale pale kwamba wanafunzi wote wanaomaliza vyuo vya mifugo wapate ajira moja kwa moja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa George Lubeleje kwa kutupongeza. Kituo chake cha Mpwapwa cha Utafiti kimekuwa kikiongezewa fedha kila mwaka na mwaka huu wameongezewa fedha tena nyingi zaidi. *(Makofi)*

Kuhusu suala la wanaomaliza chuo ngazi ya vyeti na *Diploma* katika vyuo mbalimbali katika taarifa yangu hapa nimeeleza mwaka jana walimaliza wanafunzi 1,800 na wote wameajiriwa kwenye Halmashauri za Wilaya. Wale ambao hawataki kuajiriwa ni

wale ambao wamepangiwa maeneo yao na hawataki kwenda. Wengine wanachagua maeneo wanataka wafanye Dar es Salaam wakati mifugo haipo, anataka afanye maeneo mengine labda ya ufugaji.

Kwa hiyo, watu wote wanaomaliza vyuo kwa sababu tuna upungufu na Maofisa Ugani, Maofisa Ugani wanaotakiwa katika nchi hii ni 16,000 waliopo ni 3,500 kwa hiyo, kila wanaomaliza sisi tunawapangia *direct.* Katika kazi nzuri ambazo huhangaiki hata kutafuta ni Maofisi Ugani. Kwa hiyo, ambao wameng'ang'ania kukaa huko Mpwapwa nimshauri Mheshimiwa Lubeleje akawaeleze kwamba ajira zipo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Zaidi ya hapo wawe wavumilivu maana unafanyakazi mazingira hayo utahamishwa. Unataka siku ya kwanza tu uhamishiwe mahali haiwezekani.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, programu hiyo hiyo ya 10, *sub vote 1001*. Wakati nachangia japokuwa najua Mheshimiwa Waziri hakupata muda wa kujibu maswali yote ambayo tumemuuliza ningependa Serikali itolee maamuzi au itolee tamko suala hili kwamba nimeomba sasa kutokana na kwamba tunayo maziwa na viwanda vimeanza kufanyakazi lakini yameanza kukosa masoko kutokana na kwamba bado maziwa yanatoka nje yanaingia ndani, ni kwamba Serikali izuie maziwa yanayotoka nje ili tuweze kusaidia soko la ndani. Serikali inasema nini kuhusiana na hilo?

**MWENYEKITI:** Hiyo ndiyo inavyotakiwa.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana nilimpongeza sana Mheshimiwa Magdalena Sakaya kwa kutupongeza. Serikali imeshachukua hatua, maziwa yote yanayotoka nje yanapigwa *VAT* ya 18%. Kuna kitu kingine mazao ya ngozi yanayotoka nje nayo yanapigwa *VAT* kwa asilimia 40. Ile ni ku-*discourage* kwamba maziwa yanayotoka nje yawe ya gharama kubwa na watu wasiyanywe kwa sababu tuna maziwa ya kutosha. Kwa hiyo, Serikali imeanza kufanyakazi zake.

Lakini pia haiwezi ikapiga marufuku kabisa kwa sababu mtu mwingine hii napo tutakuwa tunajizuia kitu kikubwa ni kupiga *VAT* kubwa badala ya kuzuia na hicho ndicho tulichofanya. Naamini kwa Serikali kutoa ushuru wote wa masuala ya maziwa, vifaa vya maziwa, kontena na kadhalika sasa uzalishaji wa maziwa utakuwa *cheap* na Watanzania watakunywa maziwa mengi badala ya sasa hivi tunavyokunjwa lita 43 kwa kila Mtanzania kwa mwaka badala ya kunywa lita 200 kwa kila Mtanzania kwa mwaka. Kwa hiyo, hilo limezingatiwa Mheshimiwa Sakaya. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema sana juu ya viwanda vya maziwa, amesema vile vile juu ya viwanda vya nyama na pia amesema kwamba ifikapo mwakani bei ya mifugo itakuwa kwa kilo. Lakini kwa bahati mbaya sana sijamsikia akisema juu ya viwanda vya ngozi. Wakati najua kuna viwanda vya ngozi vimekuwepo kwa mfano Kiwanda cha Mwanza, Morogoro, ni hatua gani ambayo inachukuliwa juu ya viwanda hivyo vya ngozi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri jibu, wote wanang'ang'ania mshahara wako.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa hata Mheshimiwa Selelii hataki nilipwe mshahara kwa siku zilizobaki hizi ndogo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tulichofanya pamepitishwa Sheria ya Ngozi namba 18 ya mwaka 2008. Kitu kikubwa ni kubadilisha sheria zetu. Baada ya kubadilisha ile sheria kwa bahati nzuri kwa sasa hivi viwanda saba tulivyokuwa navyo vya ngozi vimeanza kufanyakazi. Kiwanda cha Himo - Kilimanjaro, Kiwanda cha Morogoro kinafanyakazi na viwanda vingine vimeanza kufufuka. *(Makofi)*

Napenda kutoa wito kwa wale wote waliobahatika kumilikishwa viwanda vya ngozi sasa wavifufue ili viwezi kutoa *product* nzuri kwa Watanzania. Lakini pia katika *factor* hiyo hiyo ya kuzuia bidhaa za ngozi zinazotoka nje kuingia nchini bidhaa za ngozi zilizokuwa zikitoka sasa zinapigwa *VAT* ya asilimia 40. Hii itasaidia ngozi zetu kuwa na *value*. Kwa sababu katika miaka yote ngozi zetu tumekuwa tukiziuza kama *raw materials* asilimia 80 na ndio maana tumekuwa tukipata fedha kidogo ukilinganisha na nchi nyingine kama Ethiopia ambayo zao la ngozi limekuwa liki-*contribute* kwa kiasi kikubwa katika uchumi wao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wito wangu pia ningependa kutoa kwa Watanzania waanze sasa kupenda bidhaa za ngozi zinazotengenezwa na Tanzania. Kama Wabunge wote tungekuwa tumevaa viatu vya ngozi za Tanzania na nina hakika hata Mheshimiwa Lucas Selelii hajavaa viatu vilivyotengenezwa Tanzania vya ngozi ya Tanzania, nina uhakika bidhaa za ngozi zingeweza zikazaa faida na vikaleta faida kubwa. Ngozi moja inatengeneza *pair* kumi za viatu. Kwa hiyo, kama kila *pair* inauzwa shilingi laki moja maana yake ngozi itatoa shilingi milioni moja. Ni vizuri Watanzania wote tukaanza kupenda bidhaa zetu za Tanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya ngozi ya ng'ombe na ya mbuzi sawa sawa.

**MHE. DR. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi niko kwenye mshahara wa Waziri *vote 99, sub vote 1001* na sitegemei ya kwamba atashindwa kujibu swali langu akose mshahara.

Swali langu linahusu namna ya kutoa kipaumbele kwa uvuvi, nahitaji ufafanuzi hasa katika maeneo ambayo ndiyo maisha yao huwezi kuondoa umaskini kama hujaboresha uvuvi kama Ukerewe. Nataka nijue kwa nini Bajeti hii kwa mkokotoo wote niliouona hatukupewa *priority* maji ni asilimia 90, ardhi ni asilimia 10 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wataondokaje kwenye umaskini kama Waziri anayepaswa kutuenzi anapata kigugumizi kusukuma maendeleo katika eneo hilo katika sekta ya uvuvi katika Wilaya ya Ukerewe?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti hii imezingatia masuala yote kwa ujumla. Lakini pia imeangalia kwa undani masuala yanayohusu uvuvi katika sekta mbalimbali na ndiyo maana nimeeleza katika masuala mengi ambayo yamepangwa ni pamoja na kuboresha sekta ya uvuvi na kwa bahati nzuri kwa Ziwa Victoria kuna mradi ambao ni wa *Lake Victoria Fisheries Organization* ambao unahusisha wavuvi katika maeneo hayo.

Lakini labda ningependa wito kwa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe kama wanafahamu kwamba asilimia 90 ni maji na asilimia 10 ndiyo ardhi nitawashangaa sana Halmashauri hiyo kama itaagiza ma-*power tillers* mia moja ya kwenda kulima badala ya kuagiza mitego kwa ajili ya kuvua kwa sababu haya ni masuala ya kupanga katika Halmashauri. Huo ndiyo wito ambao ulitolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba Halmashauri ziangalie ni kipaumbele gani kitakachofanyika katika maeneo. Kwa mfano kama ni eneo la wafugaji ni vizuri wakaangalia miradi inayoshughulikiwa kwa wafugaji kwa mfano katika miradi ya *DADPs* na miradi ya *ASDP* kwa hiyo, nina uhakika kwa vile miradi ya *DADPs* na miradi ya *ASDP* ipo katika Wilaya ya Ukerewe, Halmashauri husika na Madiwani husika wataweka vipaumbele katika sekta inayohusu wavuvi na kuwaendeleza wavuvi katika kupanga mikakati yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawashangaa Halmashauri ya Ukerewe kuweka Bajeti kubwa katika miradi ya *DADPs* na *ASDP* katika ufugaji au katika kilimo badala ya kuzingatia katika masuala ya uvuvi ambayo ndiyo yanaajiri wananchi wengi katika eneo la Ukerewe. Lakini *otherwise* mimi ninampongeza sana Mheshimiwa Dr. Getrude Mongella ambaye amekuwa mstari wa mbele katika kushughulikia masuala ya wananchi wa Ukerewe na hasa wavuvi. Kwa bahati nzuri ninaamini kabisa wananchi wa Ukerewe wanafahamu na wataendelea kulizingatia hili ili wamrudishe ili aendelee kulishughulikia vizuri hili katika kipindi cha miaka mitano ijayo. *(Makofi)*

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi niko kwenye programu hiyo hiyo wenzangu wanayozungumzia ya mshahara wa Mheshimiwa wa Waziri. Niliongea kwa kirefu juu ya kauli ya Serikali ambayo alitoa Mheshimiwa Waziri hapa. Nimezungumzia mambo mengi lakini nataka niulizie mambo mawili tu.

**MWENYEKITI:** Unauliza moja tu.
**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Niulize moja tu?

**MWENYEKITI:** Ndio utaratibu.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Haya nitauliza moja, Mheshimiwa Waziri katika kauli yake alisema kuwa Wabunge, Wakuu wa Wilaya pamoja na Wakurugenzi wa Halmashauri ambao katika sehemu zao zina wavuvi watapewa semina. Sasa leo amezungumza hapa katika majibu yake kuwa semina hiyo ilifanywa Mwanza. Sasa katika semina hiyo iliyofanywa Mwanza hawa watu aliowataja Wabunge ambao katika

maeneo yao yana wavuvi kulikuwa na Wabunge wangapi ambao walishiriki katika semina hiyo? Nataka kufahamu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu Mheshimiwa Shoka Khamis Juma kuwa nilipotoa tamko hapa kwanza nataka kumueleza kwamba sikutaja tarehe gani nitafanya hiyo semina, hilo sikulitaja katika tamko langu. Lakini nimetoa maelezo mazuri tu kwamba katika kikao ambacho kilifanyika chini ya Uenyekiti Mheshimiwa Waziri Mkuu katika siku tatu mfululizo ulifanyika Mwanza, ulihusisha Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, baadhi Waheshimiwa Wabunge wa Kamati inayohusika na hili suala walikaa na wavuvi kujadili masuala ya uvuvi tu siku tatu mfululizo. Mheshimiwa Waziri Mkuu aliacha kazi zake zote kushughulikia suala la uvuvi tu. Waliitwa wadau wengine mbalimbali katika nchi nzima. *(Makofi)*

Lakini katika suala lile linalohusu wavuvi wa upande wa Pwani tuna mradi *MACEMP* ambao nimeeleza katika hotuba yangu pale zimeshatumika mpaka sasa hivi shilingi bilioni 5.7. Baada ya kikao tulipotoa ile taarifa hapa tuliwaita Wakurugenzi wote na kuweka nao mkataba namna nzuri ya kuweza kuzitumia hizi fedha za *MACEMP*. Halmashauri zote 16 zimeshasaini makubaliano hayo. Kuanzia Moa hadi Msimbati ambapo ni zaidi ya kilomita 1,422 lakini mbali ya hivyo mimi nimezunguka na hivi karibuni nilikuwa Mtwara, nimekwenda mpaka Msimbati, Lindi nimekwenda sehemu nyingine sikuweza kwenda kwa Jimbo la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma kwa sababu Sheria namba 22 ya mwaka 2003 haihusiki kule kwenye Jimbo lake. Jimbo lake anatawaliwa na Sheria namba 8 ya mwaka 1988 ambayo pia imefanyiwa mabadiliko kwenye mwaka 2010. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sheria ya Baraza la Wawakilishi.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimezungumzia kuhusu mradi unaoendeshwa na Halmashauri ya Manispaa ya Singida wa ujenzi wa machinjio ya kisasa. Ujenzi huo ni mkubwa sana, Halmashauri imetenga fedha kupitia vyanzo vya mapato vya kwao na watalaam wa Halmashauri na Madiwani walishafanya ziara ya kwenda kujifunza. Nilikuwa nataka nijue nguvu ya Serikali ya ku-*support* mradi huu mkubwa kupitia Bajeti hii ni kiasi gani?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawapongeza sana Halmashauri ya Wilaya ya Singida kwa kuanza kujenga machinjio ya kisasa. Ningependa nitoe *solution* mbili labda huo mradi wao wauandike kupitia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili waangalie ni kwa namna gani wanaweza kutoa fedha kupitia mradi wa *DADPs* katika kuimarisha yale machinjio. Lakini pia wanaweza kupitia Mkuu wa Mkoa wakaandika barua moja kwa moja kwa Waziri wa Fedha na Uchumi katika miradi ambayo itahusika kwenye Kilimo Kwanza. Kwa sababu kwenye Kilimo Kwanza kuna fedha shilingi bilioni 145 ambazo zimewekwa *pending* kwa ajili ya miradi itakayohusika na kilimo, miradi mizuri itakayohusika na

uvuvi, miradi itakayohusika na mifugo. Kwa hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Singida ichangamkie hizo fedha kwa kuandaa *write up* nzuri itakayokubalika. *(Makofi)*

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote 99,* programu 10 katika mchango wangu wa maandishi ambao kama alivyoeleza Mtoa Hoja kwamba hakuweza kujibu hoja zetu zote nilizungumzia juu ya wavuvi na wafugaji hasa katika maeneo ya Mkoa wa Rukwa. Lakini nalazimika sasa nipate maelezo ya ziada baada ya Mheshimiwa Waziri kutoa changamoto katika kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya kwamba amtajie kiwanda chochote kile.

Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri aliyoiwasilisha leo ukurasa wa 98 kuna Kiwanda cha *Imara Fishnet* ambao walikamatwa na nyavu 101,290 mpaka sasa nyavu hizi hazijachomwa. Ni kwa nini wavuvi maskini ambao nyavu zao zinakamatwa asubuhi wanapelekwa mahakamani na siku inayofuata wanaitwa waandishi wa habari na *television* na zinachomwa nyavu zao na za *Imara Fishnet* hazijachomwa mpaka sasa hivi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nimueleze kwamba hiyo kesi ya *Imara Fishnet* iko mahakamani na kwa mujibu wa sheria siruhusiwi kuzungumza kitu chochote kilichoko mahakamani. Kwa hiyo, tulishika tukapeleka mahakamani. Sasa si vizuri nikaanza kuzungumza ni mahakama ndiyo itakayotoa uamuzi wa kuchoma au kutokuchoma.

**MHE. *ENG.* STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu hicho hicho kwa kuwa Mheshimiwa Waziri hivi karibuni alijipatia umaarufu wa kukamata meli ambayo pia ina kesi mahakamani, sitaki kuizungumzia. Kwa kuwa Ziwa Nyasa kuna wavuvi ambao pia wanavua kwenye Ziwa ambalo mipaka yake ina utata jambo ambalo pia nafahamu linashughulikiwa na Wizara ya Mambo ya Nje kwa siku nyingi. Je, wewe kwa kuwa una nia ya wavuvi wako kufanyakazi zao kwa utulivu na amani, una mikakati gani ya kusaidia kulifuatilia jambo ili likamilike mapema?

**MWENYEKITI:** Nadhani umelielewa.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza samaki hawana mipaka ndiyo maana katika makubaliano ndani ya *Mtwara Development Corridor* ambayo yalisainiwa kwenye mwezi wa 12 kule Lilongwe, Malawi suala la uvuvi lilizingatiwa kuhusu Ziwa Nyasa. Kwa hiyo, ninaamini lile linashughulikiwa ndani ya *Mtwara Development Corridor*. Lakini kwa upande wa Serikali tumepanga mikakati ambayo tunajua kwamba itaweza kusaidia katika Ziwa Nyasa na uvuvi wake. Hivi karibuni tulitoa boti ambazo zitasaidia kule, lakini pia kuna utafiti unaofanywa ndani ya *TAFIRI* katika kujua ni kwa namna gani samaki wengi wako upande wa Malawi wakati upande wa kwetu ni wachache ni hii ni kutokana na *difference* ya kina kule upande wetu kina ni kirefu upande mwingine ni kina kifupi. Lakini pia kuna utafiti mkubwa umefanyika wa kuweza kuanza kuvua dagaa wakati wa mchana na kadhalika. Haya yote yamezingatiwa na napenda nimhakikishie Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya kwamba Ziwa Nyasa limezingatiwa katika Bajeti hii na tunawapongeza

sana wananchi wa Ziwa Nyasa kwa kazi nzuri wanazozifanya na ushirikiano mzuri tunaopata kutoka kwa Mheshimiwa Manyanya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka ameleta wageni wake kibao kwa hiyo, ndiyo nimemuweka wa mwisho sasa. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote 99, program* 10 mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

Katika mchango wa maandishi nilimshauri sana Mheshimiwa Waziri, kwa niaba ya kuishauri Serikali kwamba namna bora ya Wizara yake kuweza kujenga uhalali wa kubeba jina hili zuri la kuitwa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ni kwa kuwezeshwa na kutenda kwa namna ambayo itamtoa mfugaji kutoka katika hali yake ya sasa na kumpeleka katika hali ya ufugaji wenye tija. *(Makofi)*

Nilimshauri kwamba safari ya kuelekea kwenye ufugaji wenye tija inaanzia pale ambapo maeneo ya wafugaji yanapaswa kutengwa hasa katika maeneo yenye migogoro kama Morogoro, Pwani na maeneo mengine. Lakini nikasema inakuwa ni dhambi kubwa sana eneo la ufugaji kama lile la Kimotoroko katika Wilaya ya Simanjiro mpakani mwa *Mkungunero Game Reserve* linakuwa kwamba mvamizi wa eneo la malisho ya mifugo ni Serikali yenyewe. Nikisema Serikali ni pale ambapo *establishment* ya *Mkungunero Game Reserve* inatamka bayana kwamba *Mkungunero Game Reserve* itakuwa katika eneo la Wilaya Kondoa katika Mkoa wa Dodoma.

Lakini kwa bahati mbaya sana wapimaji kwa kutokujua maeneo wamevuka wamechukua eneo la Kiushiboro katika Wilaya ya Simanjiro pamoja na vitendo vya fedheha wanavyowafanyia wafugaji pale, lakini sasa eneo la ufugaji limeporwa. Ushauri wangu ni kwamba Waziri atakubaliana nami kwamba kuna haja ya yeye kukutana kama Waziri wa Mifugo na Waziri wa Maliasili pamoja na Waziri wa Ardhi ili kwa pamoja wabainishe utata huu wa mpaka na wananchi wa Kimotoroko waweze kuwa huru na kufuga katika maeneo yao ya malisho. Ningependa Waziri afafanue jambo hili ili kuondoa adha hii kubwa sana kwa wafugaji wa eneo hilo na iwe mfano kwa maeneo mengine ambayo Hifadhi za Taifa zimeingilia maeneo ya malisho na maeneo ya wananchi. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa mchango wa Mheshimiwa Ole-Sendeka aliuleta lakini kutokana na ile sababu tu ya msingi kwamba muda, sikuweza kujibu hoja zote za Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Michango inapotolewa kwa Serikali *whether* imetolewa kwenye Wizara ya Maendeleo ya Mifugo au imetolewa kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, imetolewa kwenye Serikali. Kwa sababu hili suala linahusika na mipaka na masuala ya mipaka huwa yanashughulikiwa na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, tutalipeleka hili suala kwenye Wizara zinazohusika ili wakalifanyie kazi. Kwa sababu sisi kazi zetu ni kushughulikia mifugo na

mifugo haina mipaka hata ingechungiwa Kenya sisi inachunga tu, sasa hili la mipaka wapo wahusika watakaolishughulikia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, maandishi yake aliyoyatoa Mheshimiwa Ole-Sendeka tutayapeleka kwenye Wizara zinazohusika ili wakayafanyie kazi na sisi tutashirikiana nao katika kutoa michango na baadaye Serikali inaweza kumjibu Mheshimiwa Ole-Sendeka kwa ukamilifu zaidi. Lakini kwa sasa hivi, sina jibu la kuzungumzia Kimo, kwanza jina lenyewe ni gumu hata kulitamka kwa hiyo, kwa sababu ni majina ya ndugu zangu Wamasai, kwa hiyo, naomba tu Mheshimiwa Ole-Sendeka avumilie kwa sababu suala hili sasa ni la Serikali na amelitoa humu kwa Serikali, Serikali italifanyia kazi ili kusudi litafutiwe ufumbuzi ili wananchi hawa wafugaji wasipate shida na lengo la Serikali sio kuwapa shida wafugaji, tunataka wafugaji waishi kwa amani katika nchi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, naridhika kwamba Waziri amejibu vizuri.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya madailiko yoyote)*

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts*…………….sh. 673,943,000/=
Kifungu 1003 – *Policy and Planning*…………………...sh. 784,126,000/=
Kifungu 1004 – *Livestock Research and*
*Training Inst.* …............................................................ sh. 6,486,847,600/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bil aya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1005 - *Information, Communication*
*and Education* ………….....................................………sh. 174,165,000/=

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kifungu hicho 1005 na kifungu kidogo 22, *1200- Communication and Information,* ambacho kimetengewa shilingi milioni 33. Wakati nachangia nilizungumzia jambo la mahusiano na wafugaji kwa njia ya uzito sana, najua Mheshimiwa Waziri hakuwa na nafasi ya kulitafakari vizuri, lakini mimi nafikiri kwamba sasa hivi kuna watu hata hawaelewi hata kati ya Wabunge wenzetu, mtu unakutana na ng'ombe laki nane ambao ni sawa sawa na shilingi bilioni 160 ambazo ni sawa sawa na Bajeti yako mara tano, unafikiri huu sio utajiri?

Kwa hiyo, unahitaji pia kutufundisha hata sisi Wabunge tuelewe Waheshimiwa wanaofuga kuna sheria mpya ambayo ina mambo mengi ambayo sio ya asili unahitaji kutufundisha. Sasa mimi nilikuwa nashangaa ni wapi hizo fedha ambazo umepewa Mheshimiwa Waziri ambazo zitakusaidia wewe kuweza kujenga mahusiano mazuri na kuwaeleza watu wote kuamini mifugo na watu wote waweze kuishi kwa salama na usalimini bila kuwa na ugomvi kama ambavyo tumeona ugomvi hivi karibuni?

**MWENYEKITI:** Yaani unachouliza ni kwamba hizi hela zitafanya kazi gani, tutakifikia *stage* hiyo ndio tunauliza maswali ya namna hiyo.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najua Mheshimiwa John Cheyo anaona kama hizi fedha ni kidogo kwa ku-*communicate* na mimi najua ni kidogo lakini kidogo ukikitumia vizuri kinazaa matunda mazuri na katika Idara zote utaona hata kwenye kile kifungu tulichopitisha cha 1004 cha *Livestock Research and Training* nacho kina kifungu cha *Communication* na tutakapoenda kwenye *Policy* napo kuna kifungu la *Communication*. Kwa hiyo, katika kifungu hiki *Information, Communication and Education* ambacho ni kitengo kidogo pale Wizarazni, tumeona hizi shilingi milioni 32 kutokana na hiki kidogo tulichokipata cha sungura kitafaa kwa ku-*communicate* na hiyo ndio hali halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa tupate fedha nyingi lakini tumepata hizi. Kwa hiyo, sungura mdogo ni lazima tumtumie kwa uangalifu na mimi nataka kukuhakikishia Mheshimiwa John Cheyo, tutatumia vizuri katika ku-*communicate* na hata sasa hivi tuna *communicate*, watu wana *TV* wanaangalia na wamekuona Mheshimiwa John Cheyo uki-*communicate* na sisi, ukiwapigia debe wananchi wale wenye matatizo ya mifugo na mimi nimekubali nita-*communicate* nao hapa hapa wala hapatahitajika nauli kama watakuwa wapo hapa *that is communication.* Kwa hiyo, naomba tu Mheshimiwa usituzuie kupata hata hiki kidogo kwa ku-*communicate*, utupitishie hiki kifungu ili tuweze ku-*communicate* hata kwa hiki kidogo tulichokipata. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1006 – *National Livestock Institute*
*– Mpwapwa*………………………………………………….sh. 1,403,960,000/=
Kifungu 1007 – *Internal Audit* ………………………..sh. 200,681,000/=
Kifungu 1008 – *Procurement Management Unit*...sh. 302,474,000/=
Kifungu 1009- *Legal Services Unit*…………………sh. 148,460,000/=
Kifungu 7001 – *Veterinary Services*………………sh. 5,057,673,500/=
Kifungu 7002 – *Livestock Identification*
*Registration & Traceable Unit*…………………..sh. 325,091,000/=
Kifungu 7003 - *Pastoral System Development*…….sh. 525,610,000/=
Kifungu 7004 – *Central Veterinary Lab*..................sh. 3,613,785,000/=
Kifungu 7005 - *Veterinary Council of Tanzania*……sh. 340, 374,000/=
Kifungu 8001 - *Animal Production*…..……………..sh. 4,132,550,300/=
Kifungu 9001 – *Fisheries Development Division*...sh. 5,842,899,100/=
Kifungu 9002 - *Aquaculture Development*
*Division*..........................................................................sh. 1,073,615,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 99- Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi**

Kifungu 1001 – *Administration and General*...............................sh. 0/=
Kifungu 1003 – *Policy and Planning*……………….sh. 1,180,672,500/=
Kifungu 1004 – *Livestock Resarch and*
*Training Institute*.........................................................sh. 2,865,139,600/=
Kifungu 1006 – *National Livestock*
*Institute- Mpwapwa*…...............................................sh. 2,156,583,600/=
Kifungu 7001 – *Veterinary Services*…………....….sh. 3,066,767,500/=
Kifungu 7002 – *Livestock and Identification,*
*Registration & Traceable Unit* …........................……sh. 309,336,500/=
Kifungu 7003 – *Pastoral System Development*……sh. 712,388,700/=
Kifungu 7004 - *Central Veterinary Laboratories*....sh.1,423,196,200/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 7005 - *Veterinary and Council*
*of Tanzania*........................................................................sh. 216,857,100/=

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWAKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni kama naomba mwongozo wako, mimi nilikuwa naangalia sioni lile eneo la *Tsetse fly control*. Sasa kule kwangu kuna maeneo ambayo kuna tatizo kubwa sana la *tsetse,* (mbungo) na mwaka jana nilipata vifo. Sasa nilikuwa naangalia kwenye hii ya *development* sioni mahali popote penye hii *control* chini ya kituo kilichopo Kigoma cha *Tsetse fly*.

Sasa nilikuwa naomba tu mwongozo wako nijue maana mwaka jana kituo kile kilipata fedha kwa kusuasua na katika vile vijiji vya Kagera Nganda na Mvinza ile programu kwa kweli ili suasua sana. Nataka kuwa na hakika tu ni wapi *Tsetse fly control* imewekwa. Naomba mwongozo wako maana nimepotea sioni kifungu chochote kwenye *development*. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri una majibu? Sisi tunaona kifungu cha *sub-vote 7001 Veterinary Services*, *4540, Livestock Diseases Control*, lakini Waziri hebu eleza.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hapo hapo lakini pia kuna fedha nyingine ambazo zimewekwa kwene *National Livestock Institute* – Mpwapwa ambazo ziko kwenye kitabu kile cha *Volume II* ambapo walitengewa zaidi shilingi bilioni moja zile pia zinahusisha na ile inayohusika na *Tsetse fly control* ya Kigoma. Kwa sababu kuna *Tsetse fly control* mbili tu ambayo kituo kimoja kiko Tanga na kingine kiko Kigoma. Ni viwili tu katika Tanzania nzima na *head office* yao iko kule. Kwa hiyo, vyote hivyo vimeahidiwa katika…

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, ipo kwenye *recurrent?*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *yes.*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 8001 – *Animal Product*……………………sh. 3,060,880,000/=
Kifungu 8002 – *Fisheries and Development Division*..........................................................................sh. 9,175,071,600/=
Kifungu 9001 – *Aquaculture Development Division*….........................................................................sh. 584,487,700/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*
*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ya mwaka wa fedha 2010/2011 kifungu kwa kifungu na kuyapitia bila mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja sasa kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe makadirio hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2010/2011 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, tunampongeza Mheshimiwa Waziri na Wizara yake na mazingatio ya hoja zilizoletwa na Wabunge mbalimbali nadhani yatafanyiwa kazi na kama ulivyoahidi kwamba majibu mengine yatakuja kwa maandishi itakuwa vizuri kwa ajili ya kuweka *records* sahihi.

Waheshimiwa Wabunge tunalo tangazo moja tu kabla hatujaahirisha shughuli za Bunge. Tutakuwa na mabadiliko ya tarehe za kusoma hotuba za Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa sababu ambazo haziwezi kuzuilika, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko wamebadilishana

na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto tarehe za kuwasilisha Bajeti zao kama ifuatavyo:-

Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko itawasilisha Bajeti yake tarehe 01 Julai, 2010 badala ya tarehe 9 Julai, 2010 ni vizuri mkazingatia hilo na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto itawasilisha Bajeti yake tarehe 9 Julai, 2010 badala ya tarehe 01 Julai, 2010. Kwa hiyo, Wizara hizi mbili wamebadilishana tarehe.

Kwa hiyo, mtakaposoma kwenye mwongozo wetu ule mtabadilisha tarehe ya Viwanda itasomwa siku ya Maendeleo ya Jamii na siku ya Maendeleo ya Jamii itasomwa siku ya Viwanda. Hilo ndio badiliko ambalo lilitolewa.

Waheshimiwa Wabunge, shughuli tulizopanga leo zimekwisha kwa hiyo, hatuna matangazo zaidi ya hayo. Naomba niwashukuru sana kwa siku nzima tuliyofanya kazi na tuwapongeze wenzetu wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa kazi nzuri wanazofanya na sifa zote hizi tuone baadae Wizara hii inaonesha mafanikio kwa wakulima, wafugaji na wavuvi na maendeleo kwa wananchi kwa ujumla. Kwa hiyo, nawatakia jioni njema mwende mkaangalie mpira, sasa naahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 1.20 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 25 Juni, 2010 saa tatu asubuhi)*